

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Kumi na Saba - Tarehe 11 Mei, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI: Hati za kuwasilisha mezani.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia , Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka fedha 2016/2017.

MHE. GRACE V. TENDEGA – K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, swali letu la kwanza linaenda Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Tebweta Omary.

Na.140

Asilimia Tano ya Fedha kwa Ajili ya Vijana na Kina Mama kwa kila Halmashauri

MHE. OMARY T. MGUMBA aliuliza:-

Sera ya Serikali ni kuzitaka Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Akina Mama kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu; lakini Halmashauri nyingi ikiwemo Morogoro Vijijini haitoi mikopo hiyo kwa makundi hayo kama ilivyokusudiwa:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuzibana na kuziamuru Halmashauri zote ikiwemo ya Morogoro Vijijini kutenga asilimia tano ya fedha za mapato ya ndani kwa vijana na asilimia tano kwa ajili ya akina mama ili waweze kupata mikopo yenye riba nafuu na kutimiza lengo lililokusudiwa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro imewezesha vikundi 39 vya wanawake na vijana vyenye wanachama 295 ambavyo vimepata mikopo ya shilingi milioni 23.8 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, zimetengwa

shilingi milioni 175, kwa ajili ya wanawake na vijana kutokana na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mkakati wa Serikali hivi sasa ni kuimarisha makusanyo ya mapato ili kujenga uwezo wa kutenga fedha zaidi.

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, sharti la kupitisha makisio ya bajeti ya kila Halmashauri lilikuwa ni kuonesha asilimia kumi zilizotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Kutokana na mapato ya ndani Halmashauri zote zimeagizwa kuhakikisha fedha hizo zilizopelekwa kwenye vikundi husika ikijumuisha walemavu na kusimamia marejesho yake ili vikundi vingine viweze kunufaika.

MWENYEKITI: Swali la nyongeza.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba vikundi 39 vya vijana na akina mama wamepata shilingi 23,800,000. Nataka kujua je, fedha hizi ni kwa muda wa fedha wa miaka mingapi?

Swali la pili; fedha hizi shilingi 23,800,000 zimekwenda katika Vijiji vipi na vikundi vipi katika Halmashauri ya Morogoro vijijini? Ahsante

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linasema pesa hizi zimeenda kwa vikundi vingapi. Ninaomba nifanye mrejeo swali hili nadhani nilijibu katika Bunge lililopita. Niliainisha vikundi hivi na nilikiri wazi nikasema kwamba pesa hizi zilizotengwa kwa Halmashauri ya Morogoro Kusini ni chache sana ukilinganisha na mahitaji halisi yaliyotakiwa kupelekwa. Nikatoa msisitizo hata katika *wind up* ya bajeti yetu ya Wizara ya TAMISEMI, nikasema ndugu zangu hizi pesa *own source* Wabunge ndiyo wenye jukumu ya kwenda kuzisimamia. Kwa sababu pesa hizi haziendi kwa Waziri wa Fedha wala haziji TAMISEMI, pesa hizi zinabakia katika Halmashauri na vikao vya Kamati ya Fedha za Halmashauri ndiyo vinavyopanga maamuzi ya mgawanyo wa pesa hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana katika bajeti yetu ya mwaka huu tukasema Halmashauri yoyote haiwezi ikapitishwa bajeti yake lazima kuonyesha mchanganuo kwa sababu hata hizi zilizopelekwa ni chache hazitoshelezi. Kipindi kilichopita nimesema hata Mkaguzi wa Hesabu za Serikali *outstanding payment* ambayo wapeleke karibu shilingi bilioni 39 hazijakwenda

kwa wanawake na vijana. Mwaka huu peke yake tunatarajia kwamba kutokana na bajeti ya mwaka huu tumepisha shilingi bilioni 64.12 zinatakiwa ziende katika mgawanyiko huo. Lengo langu ni nini? Ni kwamba kila mwananchi, kila Mbunge atahakikisha kwamba hizo bilioni 64 tukija kujihakiki mwaka unapita katika Jimbo lake amesimamia katika vikao vyake pesa hizo zimewafikia wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ni vikundi vingapi kwamba nivitaje kwa jina naomba niseme kwamba kwa takwimu nitampatia ile orodha ya mchanganuo wote wa vikundi vyote katika Jimbo la Morogoro Kusini.

MWENYEKITI: Dakika sita zimekwisha tunaendelea na swali lingine Mheshimiwa Mwakang'ata.

Na.141

Hitaji la Wodi ya Akina Mama na Watoto Kituo cha Afya Kirando

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Kituo cha Afya cha Kirando katika Wilaya ya Nkasi kinatoa huduma kwa vijiji zaidi ya ishirini katika mwambao wa Ziwa Tanganyika na katika kituo hicho wodi za watoto na akina mama zimekuwa ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya watoto na akina mama wanaohudumiwa katika kituo hicho.

Je, ni lini Serikali itajenga wodi hizo ili kuondoa kero kwa akina mama na watoto wanaohudumiwa katika kituo hicho?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha wodi ya akina mama na watoto katika kituo cha afya cha Kirando, tathmini ya awali imefanyika na kubaini kuwa zinahitajika shilingi milioni 250 ili kukamilisha ujenzi huo. Baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo Serikali itaweka katika mpango na bajeti wa Halmashauri ili kuanza ujenzi wa wodi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umbali wa kituo hicho kutoka Makao Makuu, Serikali imepeleka gari la wagonjwa ili kuboresha huduma za Rufaa kwa akina mama na watoto. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2016/2017,

Halmashauri imeweka kipaumbele katika ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Kabwe ili kiweze kuhudumia wananchi wa Korongwe na Kabwe ambao wanahudumiwa na kituo cha afya cha Kirando.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakang'ata.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa tatizo hili limeikumba pia hospitali ya Namanye - Nkasi Kusini na kwa bahati nzuri Serikali imejenga majengo ya wodi. Je, ni lini sasa Serikali itakabidhi na kufungua majengo haya?

Swali la pili, azma ya Serikali ni kuwa kila kata kuwa na kituo cha afya na kila kijiji kuwa na zahanati, je, ni lini vijiji hivi vinavyotegemea hospitali ya Kirando vitapatiwa zahanati? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kushukuru kama *facilities* zimekamilika, sasa bado kuweza kufunguliwa nadhani kikubwa zaidi tutawasiliana na uongozi wa mkoa kuangalia utaratibu tukishirikiana na wenzetu wa Wizara ya Afya, vifaa hivyo vikishakamilika basi hospitali hiyo iweze kufunguliwa. Hilo ni jambo ambalo tunasema kama Serikali tunalichukua kwa ajili ya kwenda kulifanyia kazi ili wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda ya pili ni jinsi mchakato wa ujenzi wa vituo vya afya ya zahanati ni kweli sasa hivi tuna karibuni ya kata 3390, lakini vituo vya afya tulivyonavyo ni vituo 484 maana yake tuna *gap* kubwa sana ya kufanya. Ndiyo maana leo hii Waziri wa Afya ata-*table* bajeti yake hapa ikionyesha mikakati mipana kwa ajili ya kufikia maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijua wazi kwamba katika hao wenzetu wa eneo hili wanachagamoto kubwa sana na nikifanya rejea ya Mheshimiwa Keissy hapa alishasema mara nyingi sana. Hiki hasa kituo chako cha Kirando na yeye alikuwa akiomba ikiwezekana iwe Hospitali ya Wilaya kwa mtazamo wake. Lakini alikuwa akifanya hivi ni kwa sababu wenzetu wa kule wa pembezoni wakati mwingine wanapata wagonjwa wengine mpaka kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Serikali naomba tuseme wazi kwamba tutashirikiana vya kutosha na mimi naomba nikiri kwamba katika maeneo yangu ya mchakato wa kuanza kutembelea nina mpango baada ya Bunge hili

I Bajeti kutembelea katika mkoa huu ili kuangalia changamoto zinazowakabili ili kwa pamoja tuweze kuzitatua tukiwa katika *ground* pale tuone ni lipi linalowakabili wananchi wetu. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, sema na jina lako.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naitwa Bobali, Mbunge wa Mchinga.

Kwa kuwa matatizo yaliyopo katika Mkoa wa Katavi yanafanana kabisa na matatizo ya kituo cha afya ya Chalutamba katika Jimbo la Mchinga kumekuwa na kuharibika mara kwa mara kwa gari ya kituo kile.

Je, Wizara haioni kwamba kuna haja sasa ya yale magari yaliyochakaa kuya-compensate katika vituo vyote ambavyo vina magari yaliyochakaa wakapewa magari mapya? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelisikia suala la Mheshimiwa Bobali, lakini mimi nikijua kwamba hapa tulivyokuwa tunapitisha bajeti tuliona vipaumbele vya kila Halmashauri, wengine walitenga gari, wengine wakatenga vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa sababu yale magari yamechakaa lakini nadhani tutaangalia jambo kubwa ni kwamba kama Halmashauri tunapokaa katika *priority* zake katika mpango wa bajeti ni vema zaidi kuona kwamba kama gari limechaka basi tutenge bajeti maalum kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata gari jipya ili kuondoa gharama za matengenezo ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tumelisikia hilo, niwahamasishe sasa katika maeneo ya vipaumbele tuangalie lipi hasa ni kipaumbele cha wananchi katika eneo letu husika ili wananchi wapate huduma bora. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea, Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo.

Na. 142

Hitaji la Gari la Wagonjwa- Hospitali ya Tunduru

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Tunduru inayohudumia majimbo mawili ina tatizo la gari kubebea wagonjwa ambapo gari lililopo ni moja na linaharibika mara kwa mara.

Je, ni lini Serikali itapeleka gari jipya katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imetenga shilingi milioni 141 kutokana na mapato ya ndani ili kununua gari la wagonjwa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Tunduru. Vilevile katika mwaka huo zimeombewa shilingi milioni 300 kupitia maombi maalum ili kununua magari mawili kwa ajili ya vituo vya afya, ili kuboresha mfumo wa rufaa kwa wagonjwa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa azma ya Serikali ni kuhakikisha magari hayo yanapatikana kwa ajili ya huduma za afya.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Chikabo.

MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Chikambo siyo Chikabo.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ikumbuke kwamba Wilaya ya Tunduru tumeendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi kwa kutoa kura nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikumbuke kwamba wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2014 alitoa ahadi za kutoa magari ya *ambulance* katika vituo vya afya vya Nalarasi, Nakapanya na Matemanga. Kwa hali ile ile ya kuendelea kukiamini Chama cha Mapinduzi. Naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie ni lini sasa ahadi hiyo itatekelezwa? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba ahadi hii imetolewa na Mheshimiwa Rais aliyepita na ahadi hii ni ahadi ya Serikali na ndiyo maana nimesema katika mchakato huu sasa hivi kuna gari la wagonjwa, bajeti imetengwa kwa ajili ya kupelekwa. Umesema maeneo mbalimbali ambayo Mheshimiwa Rais mstaafu alitoa ahadi hiyo, hii ni ahadi ya Serikali na ninajua wazi katika mkoa ule kwa sababu una vipaumbele vingi sana. Siyo ahadi hiyo peke yake, Mheshimiwa Mbunge ameniambia kwamba mpaka walikuwa na ahadi ya Mkoa mpya wa Selous tunayajua hii kama Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa sababu maeneo haya yana vipaumbele maalum naomba nikwambie kwamba ahadi ya Serikali iko palepale katika mchakato tulioondoka nao tutahakikisha kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais inatekeleza ili mradi wananchi wapate huduma bora. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Profesa.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa tatizo la Tunduru huko linalingana kabisa na Korogwe Mjini. Ni lini Serikali itaifanya Hospitali ya Magunga iwe Hospitali Teule?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Hospitali ya Korogwe Mjini, juzi nilipita pale katika ziara yangu wakati naenda Arusha nilitembelea Hospitali ile na nikaona kwamba *congestion* ya watu wa pale na mahitaji yake na kwamba Wilaya iko barabarani, bahati nzuri Naibu Waziri wa Afya juzi alifika pale hali kadhalika Waziri wa Afya alifika pale, naona kwamba haya yote nimeona ni kipaumbele hospitali ile kuwa Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa ili mradi kufanya hivyo. Ninaamini mchakato unaohitajika ukamilika na mahitaji yote hasa yanayotakiwa kwamba kuifanya hospitali ya Mkoa kukamilika basi nadhani Serikali haitosita kuhakikisha hospitali ile inakuwa Hospitali ya Mkoa kwa vigezo vitakavyokamilika na kutokana na maelekezo kutoka Wizara ya Afya. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea Mheshimiwa Kanyasu Constantine.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti kwanza naomba shule ya ...

MWENYEKITI: Samahani, subiri Mheshimiwa Waziri TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri Jafo nataka kuongezea kwenye suala la muundo na mgawanyo na set up kwa kuzingatia maeneo katika utoaji wa huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea na Waziri wa Afya, tumeona liko tatizo la *catchment areas* namna zilivyowekwa na uwiano wa vituo vya afya, hospitali za Wilaya, hospitali za Mikoa na ziko nyingine ambazo maombi yako mengi sana wakiomba zipandishwe madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa utaratibu unaanzia huko chini kuanzia kwenye Kata, kwenye Wilaya, kwa maana ya Halmashauri, hata hivyo tunaona haja ya Serikali kukaa na kufanya sensa maalum ya kuweka mfumo wa utaratibu mzuri ili tuende kwa utekelezaji ambao utastahiki. Kwa mfano, haiwezekani ukakuta *catchment area* ya kata karibu nne kukawa hakuna kituo cha afya, lakini kituo cha afya kimeelekea upande mmoja. (Makofi)

Kwa kuwa tuna uchache wa rasilimali lakini iko haja ya kufanya sensa hiyo ili baadaye tuje na mpango kazi maalum kwa kushirikiana na Wizara ya Afya tutakapopanga mpangilio mzuri wa vituo vya afya, Hospitali za Wilaya na Hospitali za Mikoa kulingana na mahitaji ya wananchi. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea Mheshimiwa Kanyasu.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanza naomba shule ijulikane ni Shule ya Wasichana Nyankumbu siyo Nyankumbo.

Na.143

Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Wasichana Nyankumbu ilijengwa na mradi wa GGM kusaidia kundi kubwa la wasichana wasome Wilayani Geita, shule hii ina hosteli za kutosha na nyumba za walimu.

Je, ni kwa nini shule hiyo imebaki kuwa shule ya kutwa wakati mazingira yake yanafaa kuwa sekondari ya bweni?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kanyasu Constantine John, Mbunge wa Jimbo la Geita Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Wasichana Nyankumbu ilijengwa chini ya mradi wa *Geita Gold Mining* na kupata usajili Na. S. 1942 mwaka 2006 ikiwa ni shule ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne. Aidha, mwaka 2012 iliongezewa kidato cha tano na sita. Hivyo shule hiyo imesajiliwa kuwa ya kutwa kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na bweni kwa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zinazotumika ili kuisajili shule kuwa ya bweni, ni Halmashauri yenyewe kupeleka maombi Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi ili kupata kibali.

Aidha, kabla ya kupata usajili huo, Kamishna wa Elimu atatuma timu ya wataalam katika shule husika kwa ajili ya kuhakiki uwepo wa miundombinu inayohitajika ili shule iweze kusajiliwa kuwa ya bweni.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa amejibu kwamba ni jukumu la Mkurugenzi kuandika na kuomba shule hii iwe ya bweni; ni lini sasa ofisi yake itamuagiza Mkurugenzi huyo ambaye anaonekana hafahamu kama yeye ndiyo anawajibika ili aweze kuandika barua na kuomba? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa mwezi huu au mwisho wa mwezi ujao, Serikali itaajiri walimu wapya na uchunguzi wangu shule nyingi za Jimbo la Geita za Vijijini hazina walimu; ni maagizo gani Serikali itatoa kwa walimu wapya ili waelekezwe zaidi Vijijini badala ya Mjini? Nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini nitamwagiza Mkurugenzi, nadhani huu mchakato unaanza kwenu ninyi katika Baraza la Halmashauri, kwa sababau hii ni *need* ambayo ninyi mnahitaji. Kama Baraza la Madiwani mtaona kwamba ninyi mnahitaji hilo, baadaye Mkurugenzi ataandika barua, akishaandika barua maana yake ikifika katika Wizara ya Elimu, Wizara ya Elimu inatuma wataalamu

chini ya Kamishna wake, wataenda kufanya uhakiki, baadaye vigezo vikishapita ndiyo shule hiyo itasajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliache suala hili katika Baraza lenu la Madiwani, maana inawezekana Mkurugenzi akaandika halafu Madiwani wakamgeukia kwa nini umegeuza shule hii kwa mahitaji yako bila kutaka maelekezo kutoka katika Baraza la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba niache jambo hili katika mchakato wa Baraza la Madiwani litaamua kumwelekeza Mkurugenzi aweze kufanya haraka kupeleka Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuhusu suala la upelekaji wa walimu. Ni kweli hivi sasa tupo katika mchakato siyo muda mrefu sana tutaajiri walimu wapya. Katika kuajiri, kuna Mikoa ambayo inabidi ipewe kipaumbele, tuna Mikoa takribani sita ambayo ina changamoto kubwa sana ya walimu ikiwepo ni pamoja na Mkoa wa Kigoma, Rukwa, Katavi na Geita. Kwa hiyo, katika maeneo hayo yote tutaangalia walimu watakaopatikana basi tutawapa maelekezo maalum. Wakifika pale lazima waende maeneo ambayo wananchi wanataka huduma, bahati mbaya wakati mwingine inajitokeza walimu tukiwaajiri, tukiwapeleka kule inawezekana wengine sisi Waheshimiwa tunapeleka vi-memo ili yule mwalimu arudi mjini, tunasababisha maeneo ya vijijini yanakosa walimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Ofisi ya Rais TAMISEMI tunaelekeza walimu watakaopangwa lazima waende kufanya kazi katika maeneo husika.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii.

Kwa kuwa, hili suala la Geita linafanana sana na tatizo lililoko Wilaya ya Kakonko, Jimbo la Buyungu kutokuwa na sekondari kabisa ya *A-level* na tunayo shule moja ya sekondari Kakonko ambayo ikiwekewa miundombinu mizuri yafaa kuwa na *A-level*.

Je, Waziri yuko tayari kuweka kipaumbele katika shule ya sekondari Kakonko ili ipewe hadhi ya kuwa na *A-level* itakayokuwa ya kwanza katika Wilaya ya Kakonko?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba Serikali kutoa kipaumbele, nadhani hili tumetoa maagizo katika maeneo mbalimbali, kwa sababu tuna shule nyingi sana za kata. Shule hizi za kata watoto wakifaulu lazima waende *Advance*

Level. Tunapokuwa na shule za kata wanafunzi wanishia *form four* maana yake wakikosa nafasi za kwenda *advance*, shule zikiwa chache vijana inawezekana wakafaulu lakini wakakosa nafasi.

Kwa hiyo, haya ni maelelekezo ya maeneo yote, ndiyo maana mwaka huu hata ukiangalia bajeti yetu tumezungumza, tunakarabati zile shule kongwe, hali kadhalika kuhamasisha maeneo mbalimbali kujenga shule. Kwa sababu tunajua eneo lile jiografia yake ni ngumu tutaangalia jinsi gani ya kufanya maeneo ambayo hayana shule za Kata tuyape msukumo shule za *advance level* ili kwamba watoto wakifaulu katika shule a *O level* waende *advance level* katika maeneo husika.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga.

Na. 144

Shirika la NAFCO Magamba

MHE. PASCAL Y. HAONGA aliuliza:-

Shirika la NAFCO Magamba limeshindwa kuyaendesha mashamba yaliyochukuliwa kutoka kwa wananchi na kuwakosesha maeneo ya kulima na mara nyingine kuwakodishia kwa gharama kubwa.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka wa kuyarejesha mashamba hayo kwa wananchi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Yohana Haonga, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maslahi mapana ya Taifa, kwa sasa Serikali haiwezi kulirejesha shamba hilo kwa wananchi kwa kuwa lipo kimkakati kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa mbegu za kutosha ili kukidhi mahitaji ya mbegu nchini. Vilevile kupitia shughuli za uzalishaji mbegu, wakulima hupata elimu kuhusu matumizi sahihi ya mbolea na madawa ya kilimo na utunzani wa shamba, pia kusambazia teknolojia mpya za kilimo bora.

Aidha, tayari Serikali ilichukua hatua za kurejesha mashamba nane ya kahawa ya Ngamba, Shishiwanda, Ihanda, Ndugu I, Ndugu II, Tukumbi, Ruanda na Ishera ambayo yalikabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ili

kuyagawa au kuyauza kwa wananchi kwa shughuli za kiuchumi na kijamii ambapo baadhi yao wamepatiwa hati miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi, tayari alishatembelea shamba hilo, akiwa pamoja na Mkuu wa Mkoa, Mbunge wa Mbozi mwenyewe, wataalam wa ASA na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi. Katika ziara hiyo, wataalam wa ASA na Halmashauri walitoa maelezo kuwa kuna kipindi cha kupumzisha shamba kwa mwaka mmoja au miwili ili kuongeza rutuba ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu hizo za kitaalam zinaweza kutafsiriwa kuwa shamba hilo halitumiki ipasavyo. Aidha, baada ya ASA kukabidhiwa shamba hilo na Shirika Hodhi la *CHC*, hakuna wakulima waliowahi kukodishwa shamba hilo, bali ASA imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu kwenye shamba hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati uliopo wa kuzalisha mbegu ni pamoja na kupanua wigo wa ushirikiano ili Kampuni zaidi zishiriki katika uzalishaji wa mbegu kwa kutumia shamba hili. Vilevile kuhamasisha vikundi vya vijana ili washirikiane na ASA katika uzalishaji wa mbegu. Mwisho, kuweka miundombinu muhimu iliyohitajika katika uzalishaji ikiwemo kuunganisha umeme wa gridi na kujenga miundombinu ya umwagiliaji.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa shamba hili ni kubwa sana takribani ekari 12,000; na wazalishaji wa mbegu hata ekari 1000 hazijafika katika kuzalisha mbegu kwenye shamba hili. Wananchi wamehangaika kwa muda mrefu wanaharibu mazingira wanatafuta maeneo mapya ya kulima.

Je, Waziri sasa yuko tayari kwenda kuyapitia upya yale maeneo angalau kuwarudishia wananchi eneo angalau hata kidogo ili waendeleo kulima kwa maana wanaharibu mazingira hawana maeneo ya kulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, *NFRA* walipokuwa wananunua mahindi msimu wa mwaka 2015; Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi inawadai ushuru wa shilingi milioni 420, hawajalipa fedha hizo.

Je, Serikali ipo tayari kupeleka fedha hizo Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, shilingi milioni 420 ambazo hazijapelekwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri mhusika!

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Wabunge wa Mbeya kwa kufuatilia suala hili, nakumbuka tuliambatana na Mbunge wa Mbozi pamoja na pacha wake Mheshimiwa Hasunga, Mbunge wa Vwawa. Niseme tu maeneo ya aina hii yapo, ambayo yamekuwa yakivutia wananchi kutaka wagawiwe. Nakumbuka hata suala la Bugaga ambalo Mheshimiwa Nsanzugwanko amekuwa akilihangaikia, naelewa *concern* ya Wabunge kutaka wananchi wapate maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wabunge tukubaliane kwamba zoezi la kuwagawia wananchi mashamba ya Serikali siyo endelevu kwa sababu uhitaji wao ni mkubwa kuliko ukubwa wa maeneo yanayopatikana. Kwa hiyo leo hii hata tungenema tunatoa ekari 2000, kwa sababu hatutoi kwenye shamba la ujamaa, ni dhahiri kwamba wale vijana hawataweza kupata wote eneo hilo ambalo litakuwa tunaligawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, utaratibu endelevu ni kuwaweka vijana kwenye vikundi, halafu washirikiane na taasisi na Serikali, kutimiza lengo lile la kupata mbegu kutoka katika eneo hilo, huku wakisimamiwa na kutimiza vigezo ambavyo vinatakiwa katika suala hilo la mbegu. Nimeelekeza wataalam wangu wanipe mashamba yote ambayo yalishageuka kama mapori ambayo yanatamanisha wananchi kuona hayatumiki ili tuweze kutengeneza ushirika wa vijana wanaotaka kwenda kwenye kilimo waweze kuyatumia na Serikali itimize lengo lake la kupata mbegu kutoka katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kulipa fedha zile ambazo hazikuwa zimelipwa, nimelipokea na nitawaelekeza wataalam wangu wa *NFRA* waweze kutimiza jambo hili, kwa kulipa deni hilo ili Halmashauri iweze kutekeleza miradi yake ya maendeleo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Gekul, jiandae Mheshimiwa Keissy.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Haya mashamba ya *NAFCO* hata kwa Babati yapo, yaka-*transform* kwenda *RIVACU*. Hivi karibuni mwaka jana, Waziri wa Ardhi alitaka Ofisi ya *DC* katika Wilaya ya Babati, shamba la *RIVACU* - Dareda lirudishwe kwa wananchi ambalo wanalihitaji kwa kilimo. Lakini hadi leo jambo hilo halifanyiki ilihali wananchi hao wamekuwa wakihangaika sana. Naomba nifahamu kupitia kwa Waziri wa Kilimo, je, uko tayari sasa kushirikiana na Waziri wa Ardhi, kuhakikisha mashamba ya *RIVACU* Babati yanarudi kwa wakulima wa Babati?

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya ardhi katika Mkoa wa Manyara yamekuwa yakipigiwa kelele sana na Waheshimiwa Wabunge akiwepo Mama Mary Nagu upande wa Hanang na Mheshimiwa Jitu Soni.

Kwa hiyo, kwa jambo hili alilolisema *schoolmate* wangu, Mheshimiwa Gekul, Serikali tunafanya kazi kwa pamoja, na ndugu zangu wa Manyara ni majirani zangu, nitazungukia kuona maeneo hayo kama ratiba itaweza kwenda sambamba tutaweza kupata fursa hata ya kuwa na wenzentu wa Ardhi ili tuweze kuamua kama Serikali tukiwa wote tuko na taarifa sahihi ambalo zinahusu eneo hilo ili tuweze kuwa na jawabu la kudumu la maeneo hayo. Kwa hiyo, kwa sababu si mbali sana Manyara, tutapangilia utaratibu tuweze kufika katika maeneo hayo, na mimi sioni taabu kwenda kuwasalamia watani zangu japo tu sitaenda na nyama ya punda. (Kicheko/Makofi)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Nkasi, kuna Ranchi ya Kalambo ambayo iligawiwa kwa wafugaji *block* kama kumi, kila *block* heka 3000 mpaka 2500 kila mfugaji, *block* kumi. Lakini hizo *block* kumi hakuna ng'ombe zilizopelekwa baadhi ya *blocks* na baadhi ya waliochukua hizo *block* ni wajanja hawana mfugo hata mmoja wanakaa wanakodishia wafugaji.

Je, Serikali iko tayari kupitia upya Ranchi ya Kalambo ili kugawa upya kwa wafugaji ili kuondoa matatizo ya wafugaji na wakulima nchini?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba kuna changamoto kubwa sana katika *ranch* ya Kalambo na *ranch* nyingine ambazo zinamilikiwa na NAFCO, hasa zile ambazo zimegawiwa kwa Wawekezaji.

Nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa sasa Wizara inafanya tathmini ya kuangalia namna uwekezaji ule ulivyofanywa ili ikigundulika kwamba kuna wawekezaji walipewa ranchi za NAFCO lakini hawatumi ipasavyo wanyang'anywe na kupewa kwa wafugaji na wawekezaji wengine ambao watatumia inavyotakiwa.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Jesca David Kishoa.

Na. 145

Uingizaji wa Mafuta ya Kula Nchini

MHE. JESCA D. KISHOA aliuliza:-

Moja ya njia ya kuimarisha uchumi ni kupunguza uagizaji wa bidhaa nje ya nchi, Taifa linatumia fedha nyingi za kigeni kuingiza mafuta ya kula wakati kuna vyanzo vingi vya mafuta kama vile alizeti - Singida na Michikichi – Kigoma.

Je, ni lini Serikali itaweka msukumo kwa mazao haya katika mikoa hii kwa faida ya nchi na wakazi wa mikoa hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvivi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta ya kula wakati kuna vyanzo vingi vya mafuta kama alizeti na michikichi kwa sababu mbalimbali. Ili kukabiliana na changamoto hii Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeandaa mikakati inayolenga kuongeza tija na uzalishaji wa mbegu za mazao ya mafuta hususani alizeti ambazo uzalishaji wake umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka.

Aidha, katika Mkoa wa Singida vikundi mbalimbali vimeundwa na taasisi mbalimbali za Serikali na zile zisizo za kiserikali. Mojawapo ya malengo ya vikundi hivyo ni kuongezea thamani kwa maana ya *value addition* ya zao la alizeti na upatikanaji wa pembejeo ili kukuza tija na uhakika wa masoko kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma ni mkoa pekee nchini unaolima zao la mchikichi kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na maeneo mengine nchini. Hadi sasa mkoa una zaidi ya hekta 18,924 za michikichi zenye tija ya tani 1.6 kwa hekta. Uzalishaji huu bado ni mdogo sana ikilinganishwa na tani 4.0 kwa hekta zinazoweza kuzalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza tija, mkoa kupitia Halmashauri zake unaendelea kuhamasisha wananchi kufufua mashamba ya zamani ya mchikichi kwa kuyapalilia, kuondoa majina yaliyozeeka na kuanzisha mashamba mapya yatakayokuwa yanapandwa mbegu bora. Vilevile Mkoa kwa kushirikiana na wadau wengine umeshaanza kuzalisha miche bora ya michikichi ambayo itasambazwa kwa wakulima kwa gharama nafuu ili kila mkulima apande miche 137 inayotosha hekari moja.

Pia wajasiriamali wanawezeshwa kupata mashine bora za kusindika michikichi; Serikali Kuu na Serikali ya Mkoa tunakaribisha wawekezaji zaidi kuwekeza katika uzalishaji mkubwa na viwanda vya kati na vikubwa vya kukamua mafuta na bidhaa nyingine zitokanazo na michikichi.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa kutoka Benki Kuu inaonesha kwamba kuanzia mwaka 2006 mpaka 2015 takribani miaka kumi kila mwaka nchi imekuwa ikitumia gharama ya takribani wastani wa dola milioni 900 ambayo ni sawa sawa na shilingi trilioni mbili katika fedha hizi zinatumika kwa ajili ya kununulia bidhaa kutoka nje. Katika fedha hizi, fedha dola milioni 120...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca uliza swali.

MHE. JESCA D. KISHOA: Nauliza swali Mheshimiwa Mwenyekiti, dola milioni 120 zinatumika kununulia mafuta ambayo ni sawa na takribani shilingi bilioni 250.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali iliyoko madarakani itawakumbuka wananchi wa Singida ambao wamepuuzwa wametelekezwa, lakini wamesahaulika hata katika hili la mafuta? Ninaomba Waziri aje anipe majibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca hujauliza swali.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Waziri...

WABUNGE FULANI: Swali.

MHE. JESCA D. KISHOA: Tulieni ninyi.

MWENYEKITI: *Order*, mwacheni. Mheshimiwa Jesca zungumza na Kiti.

MHE. JESCA D. KISHOA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaona kuna ulazima wa mafuta kuundiwa bodi kama ilivyoundwa kwanye pamba, kama...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa Jesca.

MHE. JESCA D. KISHOA: Kama ambavyo kwenye...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jesca hutakiwi kuchangia unatakiwa uulize swali.

MHE. JESCA D. KISHOA: Ni lini bodi itaundwa kwa ajili ya mafuta?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri majibu?

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitambue umuhimu wa maswali haya kwa *logic*, kwa maana ya kwamba Wizara na Serikali, tukishirikiana na Wizara ya Viwanda, tumedhamiria kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunajitegemea kwenye sekta hii ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Mheshimiwa Mwijage, ameshazindua mkakati ambao utatuondoa katika tatizo hilo. Mheshimiwa Jesca mdogo wangu ambaye tuligombea naye Jimbo moja, wananchi wa Mkoa wa Singida hawajapuuzwa, isipokuwa tunalotaka kufanya kama Serikali na Wabunge wote wanaotokea mikoa hii tuwahamasishe na sisi tulisema kwenye hotuba yetu kila familia iwe angalau na ekari moja ya alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kigoma na Mheshimiwa Jesca amewagusa watu wake wote, kaanzia Singida kwa wazazi wake halafu kaenda swali la michikichi kwa wakwe zake alipoolewa kule na Mheshimiwa Kafulila. Tuwahamasishe, hamasa hii ambayo inatoka kwenye alizeti ambayo Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Kingu na Mheshimiwa Mlata na Aisharose wanafanya pamoja na akina Mheshimiwa Nkamia na Mheshimiwa Ashatu, tuhamasishe walime alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kule Kigoma, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu ya michikichi 137 kwa kila ekari tuwahamasishe walime, baada ya hapo hatua zitakazofuata za Serikali zitakuwa zile za kisera za kuhakikisha kwamba tuna-discourage mafuta kutoka nje na yatumike yale yanayotoka ndani. Tukianza kwanza kwa ku-discourage mafuta ya nje kabla hatujahamasisha watu kulima kitakachofuata bei zitapanda na watu watakosa hiyo bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili linalohusu bodi na lenyewe sasa hivi alizeti itakuwepo kwenye Bodi ya Mazao Mchanganyiko kwa sababu uzalishaji wake haujawa mkubwa, wananchi hawa tusije tukawawekea mzigo ambao wamekuwa wakibeba wengine kwa ajili ya kuhudumia bodi hizi ile hali wao hawajajitosheleza na kuvutiwa zaidi kwa ajili ya zao hilo.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Nchambi kwa kifupi sana.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wabeja sana. Kwa kuwa Wilaya ya Kishapu imebarikiwa kuwa na ukame hata nyakati za masika na kwa kuwa Wilaya hiyo hiyo ya Kishapu imebarikiwa kuwa na mito mingi sana ambayo inatiririsha maji mengi....

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nchambi swali please.

MHE. SULEIMAN M. NCHAMBI: Namuomba sasa Mheshimiwa Mwiguli na Naibu wake Mawaziri hawa shapu wanaofanya mambo kwa ushapu watumie neema hiyo kwa kutengeneza mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji wa mazao ambayo yatawakomboa wana Kishapu.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea wazo la Mbunge shapu wa Jimbo shapu la Kishapu, ambaye kwa kweli kwa ushapu wake ndiyo maana amekuwa akichaguliwa. Tayari tumeshaandika barua kwa Waziri pacha ambaye kwa leo yupo na heshima kubwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri umeshapokea ombi lake hebu kaa.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Kwa hiyo tutatengeneza hilo ili tuweze kutumia mabwawa hayo.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mattar Ali Salum.

Na. 146

Kuboresha Makazi ya Askari

MHE. MATTAR ALI SALUM aliuliza:-

Makazi ya askari yamekuwa ya zamani pia mengine yamekuwa mabovu sana, mfano nyumba za Ziwani Zanzibar, Wete, Pemba na Chakechake Pemba hazikaliki kabisa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia marekebisho nyumba hizo?

(b) Je, ni gharama gani Serikali itatumia kwa marekebisho ya nyumba hizo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mattar Ali Salum, Mbunge wa Shaurimoyo lenye sehemu (a), na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nyumba nyingi za makazi ya askari hazijafanywa ukarabati zikiwemo za Ziwani Zanzibar, Wete na Chakechake. Serikali ina mpango wa kuzifanyia marekebisho nyumba zote za polisi Unguja na Pemba kwa kadri uwezo wa fedha utakavyoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama halisi za ukarabati wa nyumba zote za polisi Unguja na Pemba ni bilioni 1.5.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri Mheshimiwa Masauni, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini Serikali au Wizara yake itaanza kufanya ukarabati wa nyumba hizo?

Swali la pili, nafahamu Wizara ina mpango mzuri wa kulinda raia na mali zake, kuna kituo cha Shaurimoyo, kuna kituo kidogo cha Mwembeladu lakini vituo hivi vimefungwa kwa muda mrefu sasa.

Je, ni lini Wizara yake itavifungua vituo hivi na kuendelea na kazi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, anauliza ni lini ukarabati huo utaanza. Kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi kwamba pale tu ambapo tutaweza kupata fedha tuaanza huo ukarabati. Kwa hiyo, siwezi kusema *exactly* ni siku gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia swali lake la pili alikuwa alitaka kujua kwa ni nini kituo cha Shaurimoyo pamoja na kituo cha Mwembeladu havitumiki. Kituo cha Shaurimoyo hakitumiki kwa sababu kwanza, takwimu zinaonyesha kwamba eneo hilo la Shaurimoyo halina uhalifu.

Lakini pili kuna vituo vingi sana ambavyo vipo karibu na kituo cha Shaurimoyo ikiwemo kituo cha Ng'ambo, kituo cha Mwembemakumbi na Makadara ambapo imezidi maili moja kutokea kituo kilichopo kituo cha Shaurimoyo. Kwa hiyo, kwa kutilia maanani kwamba hali ya kituo hicho siyo nzuri kituo kimechakaa sana tumeamua kituo hicho kwa sasa hivi kitumike kwa ajili ya matumizi ya Polisi Jamii na wananchi wanaendelea kutumia vituo vilivyo karibu na kituo cha Shaurimoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na kituo cha Mwembeladu ambapo kipo mpakani mwa Jimbo langu vilevile, kituo hiki kilijengwa kwa ajili ya matumizi ya *traffic*, lakini kutokana na mkakati wa kipolisi wa matumizi ya shughuli za *ki-traffic* Wilaya, uratibu huo unafanyika katika kituo cha Malindi ambacho nacho hakipo mbali sana na eneo hilo. Pia miundombinu ya kituo cha Mwembeladu haikidhi haja ya kufanya shughuli za *traffic* kwani hata ukikamata magari siyo zaidi ya gari moja linaweza kukaa katika eneo hilo. Kwa hiyo, kwa kutilia maanani hoja hizo kwa sasa hivi tunaangalia uwezekano wa kubadilisha matumizi ya eneo ili tuweze kupata maeneo mengine ya kuweze kuimarisha shughuli za *traffic* badala ya kutumia kituo cha Mwembeladu.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Catherine jiandae Mheshimiwa Mariam.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la makazi ya polisi yamekuwa makubwa sana haswa katika Mkoa wangu wa Arusha, polisi wamekuwa wakiishi katika nyumba mbovu na chafu na wengine kuishi uraiani. Kwa kuwa tuna ekari 30 tulizopewa na Magereza kwa ajili ya makazi haya ya polisi. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kutumia zile ekari 30 tulizopewa na Magereza kwa ajili ya kujenga makazi haya ya polisi Mkoa wa Arusha? (Makofi)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali. Nilizungumza jana kwamba tuna mpango wa kujenga nyumba 4136 kwa awamu ya kwanza katika mikoa 17 ikiwemo Arusha. Lakini wazo lake la kutumia eneo la Magereza basi tutalichukua tuone tunalifanyia kazi kwa kiasi gani. (Makofi)

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na mimi naomba kumuuliza Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya vituo vingi Zanzibar ni vibovu na majengo ni chakavu na askari hawana vitendea kazi wanapokamata wahalifu kama wino wa kuchapisha barua na mahitaji mengine muhimu na hata wahalifu wale hawapati hata mkate kwa sababu siyo wahalifu wote wana jamaa wa kwenda kuwaangalia kwenye vituo vya polisi wanapokuwa mahabusu.

Je, ni lini Serikali itahakikisha vituo vyote vinapatiwa huduma stahiki za kuendesha kazi zao kwa wakati muafaka. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ni lini tu anataka kujua, hataki kujua mengine.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo Serikali itapata uwezo wa kifedha.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Khatibu.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri mbona waondoka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri bado kuna swali dogo.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Rudi hapo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatibu endelea na swali.

MHE. MOHAMMED JUMA KHATIB: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri, jana ulipoulizwa swali hili la nyongeza kuhusu kituo cha Shaurimoyo ulisema hakuna askari wa kutosha, leo umejibu unasema eneo hilo hilo halina uhalifu. Mheshimiwa Rais alikuteua ili umsaidie huoni kwamba kuwa Waziri kwako imekuwa ni mzigo, ni lini utamwandikia Mheshimiwa Rais akufute kazi kwa sababu umeshindwa kumsaidia? (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa.

Na. 147

Serikali Kuwaunga Mkono Wananchi wa Busiri katika Uchimbaji Mdogo Mdogo

MHE. OSCAR R. MUKASA aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Busiri, Wilayani Biharamulo ni miongoni mwa Watanzania wanaoendesha maisha yao kwa shughuli za uchimbaji mdogo mdogo ambazo zinahitaji kuungwa mkono na Serikali kimkakati.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwaunga mkono wachimbaji wadogo wadogo wa Busiri?

Je, Serikali iko tayari kuwatembelea wananchi wa Busiri na kuwaelewesha ni namna gani na ni lini itaanza kutekeleza mkakati huo wa kuwaunga mkono wachimbaji wadogo wadogo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati ambayo Serikali imechukua kwa wachimbaji wadogo wa madini hasa katika eneo la Busiri ni kuwatafutia maeneo ya uchimbaji wa madini. Wizara imetenga eneo lenye ukubwa wa takribani hekta 11,031 lililoko chini ya leseni za utafutaji wa madini namba 3220 ya mwaka 2005 iliyokuwa inamilikiwa na Ndugu Daudi Mbagu. Kadhalika katika eneo hilo la leseni ya utafutaji wa madini namba 5853 ya mwaka 2009 iliyokuwa chini ya kampuni *Meru Resource Limited* ambazo zote zimemaliza muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwisho wa mwezi Machi mwaka jana na mwisho wa mwezi Machi mwaka huu Wizara imegawa kwa wananchi wa Busiri leseni 81 zenye uchimbaji mdogo wa madini ambazo kwa ujumla wake zinachukua hekta 810 kati ya hekta 11,031 za eneo hilo. Aidha, Wizara imegawa leseni nyingine 30 za uchimbaji mdogo katika eneo lililoko katika karibu na eneo hilo takribani kilometa moja tu kutoka eneo la uchimbaji mdogo wa madini la Busiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati mwingine ni kuendelea kuitumia eneo la Shirika la STAMICO kutoa huduma za ugani kwa wachimbaji madini wadogo hasa wa kijiji cha Busiri na maeneo mengine nchini. Mkakati mwingine ni kuwapatia ruzuku pamoja na kuwapatia elimu endelevu itakayoendelea kutolewa pamoja na shirika la STAMICO.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwatembelea wachimbaji hawa mara kwa mara hasa kwa kutumia Maafisa na wataalam wa ofisi ya Kanda ya Ziwa Victoria Magharibi na Afisi Madini Mkazi wa ofisi ya Bukoba. Tarehe 11 Machi, 2016 Afisa Madini Mkazi wa Bukoba alifika na kufanya mkutano na kikundi cha *Busiri Mining Co-operative Society Limited* chenye leseni ya uchimbaji mdogo. Aidha, ili kutekeleza sasa ombi la Mheshimiwa Mbunge Wizara yangu itamtuma tena Afisa Madini kutembelea eneo hilo na kuwaelimisha wananchi juu ya uchimbaji mzuri mdogo wa madini katika eneo hilo.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja; eneo la Karukwete lina wachimbaji wadogo na lipo jirani kabisa na Kijiji cha Busiri kinachazungumziwa kwenye swali la msingi. Waziri yupo tayari kulijumuisha kwenye mkakati wa kuwawezesha kielimu na uwezesaji?

Swali la pili; naomba kujua orodha ya mambo ya kiuwezesaji yatakayofanyika kwa wananchi wa Karukwete na Busiri na lini tutawenda kuzungumza nao kuwafahamisha? Nashukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mukasa kwamba eneo la Karukwete nalo litaongezwa kwenye maeneo ya kufikiriwa kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu langu la pili kwenye orodha ya huduma zitakazotolewa kwa msaada huu ni pamoja na kuwapatia ruzuku wachimbaji wadogo. Mwaka huu kwenye bajeti yetu mtaona tumetenga takribani shilingi milioni tisa za Tanzania pamoja na dola bilioni nne kwa ajili ya kuwawezesha

wachimbaji wadogo. Pia tutaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo ili waweze kuwa na uchimbaji wenye tija.

Pamoja na hayo bado Wizara yetu itatuma wataalam wa GST iyafanyie tathmini maeneo yote yatakayotengwa ili wachimbaji wawe na uhakika wa uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kuongeza kwa manufaa ya wengine kwamba maeneo ambayo tutayatenga yapo mengi tunategemea kutenga eneo la Kasubwiya hekta 495, eneo la Nyaluyeye hekta 658, eneo la Matabe hekta 659 na maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutaendelea kuwawezesha. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri amejibu na maeneo mengine yote. Tunaendelea na Mheshimiwa Musukuma Joseph, kwa niaba yake Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 148

Umeme wa REA - Sengerema

MHE. COSTANTINE J. KANYASU (K.n.y MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA) aliuliza:-

Mkandarasi wa REA anayefunga umeme katika Jimbo la Geita Vijijini amemaliza tatizo na yule anayeunganisha kutoka Sengerema yupo pole pole sana.

Je, ni lini sasa Serikali itamsimamia kikamilifu mkandarasi huyo ili aweze kumaliza kazi hiyo na umeme uweze kuwashwa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Musukuma Joseph Kasheku, Mbunge wa Geita Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa REA Awamu ya II katika Mkoa wa Geita likiwemo Jimbo la Geita Vijijini unatekelezwa na mkandarasi *Nakuroi Investment Company Limited*. Kazi ya kupeleka umeme Geita inajumuisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 161.5; ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 119.2; ufungaji wa *transfoma* 49 za ukubwa mbalimbali. Pamoja na hayo pia kuunganisha umeme wateja wa awali 2,560 na kazi za mradi zimekamilika kwa

asilimia 94 ambapo ujenzi wa laini kubwa umekamilika kwa asilimia 100 na ujenzi wa laini ndogo umekamilika kwa asilimia 84. Kadhalika ufungaji wa *transfoma* 29 zimefungwa na wateja 846 wameunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, umeme umeshafika Nyamadoke kutoka Sengerema Mkandarasi ameelekezwa sasa kuhakikisha kwamba, kazi zote za kuunganisha zinakamilika ifikapo mwezi June mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, REA pamoja na TANESCO wameongeza kasi sasa ya kumsimamia Mkandarasi huyu ili kuhakikisha kwamba kazi za ujenzi zinakamilika ifikapo Juni mwaka huu.

MHE. COSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika REA Second Phase ambayo ilikuwa inaendelea ni robo tu ya vijiji vya Jimbo la Geita na Geita Mjini ambavyo vimepata umeme, vijiji kama Nyawilimilwa, Kagu, Senga, Bulela bado havijafikiwa; naomba kujua ananipa uhakika gani kwamba Vijiji hivi ambavyo bado havijapata umeme vitapata umeme kwenye Awamu ya Tatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Mji wa Geita tumekuwa na tatizo la umeme kukatika katika kila siku kutokana na umeme mdogo ambao tunatoka Mwanza. Hata mji wenyewe wa Geita pale Mjini umeme unakuta upo lakini sehemu nyingine hauwaki. Ni lini Mheshimiwa Waziri atahakikisha Geita inapata umeme wa uhakika?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, anataka *commitment* tu basi.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza kuhusu kujumuisha vijiji vya Nyawilie na Bulila nimhakikishie kwamba vijiji hivyo vyote vitaingia kwenye REA Awamu ya Tatu inayoanza Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kukatika katika kwa umeme nichukue fursa hii kuwataarifu kwamba ni kweli kabisa karibu nchi nzima siyo Geita tu umeme bado unakatika katika na suluhisho la kukatika kwa umeme kama tulivyosema miji ya Geita na maeneo ya Kanda ya Ziwa pamoja na maeneo mengine, itapata sasa umeme wenye kilovoti 400 unaotoka North West Grid unaotoka Mbeya unaopita Sumbawanga, unaopita Mpanda, unaokuja Kigoma unakwenda mpaka Nyakanazi na baadaye Geita na umeme huo utatoka Geita kwenda Bulyanhulu na utatoka Bulyanhulu kwenda maeneo ya Biharamulo. Umeme huu utakuwa na nguvu kubwa ya kilovolt 400 na unatembewa kwa takribani ya kilometa 1148.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nassari ajiandae Mheshimiwa Shangazi.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linafanana sana na swali la muuliza swali Mbunge wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua jitihada ambazo zilifanywa na Serikali hapo nyuma kwa baadhi ya maeneo na vijiji kupata umeme kupitia Wakala wa Umeme vijijini kwa maana ya REA, lakini pia tunatambua mapungufu makubwa ambayo yameonekana kwenye miradi hii. Vipo baadhi ya vijiji ambavyo wananchi walipitiwa, ramani ikapitishwa, Serikali ikawaagiza wakakata mazao yao, wakakata kahawa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nassari uliza swali.

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Wakachimba mashimo na mashimo yakachimbwa na Serikali kupitia Wakandarasi waliopewa kazi kwa ajili ya kuwapa umeme, lakini badala yake Wakandarasi wameondoka watu hawajapata umeme, mashimo yamebaki, mazao yao yameanguka, ng'ombe wanaanguka kwenye mashimo. Sasa ningetaka kauli ya Serikali kwamba ni kwa nini unamnawisha mtu unamuweka mezani halafu kama huwezi kumpa chakula, kwa hivyo ni lini wananchi hawa ambao tayari ramani zimeshapita kwao na mashimo yakachimbwa halafu yakaachwa na mazao yao yakakatwa, ni lini wanakwenda kufungiwa umeme? Vijiji hivyo ikiwa ni pamoja na Mulala, Kilinga pamoja na baadhi ya maeneo mengine?

MWENYEKITI: Ahsante inatosha Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuna maeneo mengine mkandarasi ameendelea kuchimba mashimo na kuweka nguzo.

Sasa ni lini maeneo haya yatapatiwa umeme, jibu la uhakika kabisa ambapo Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiwaambia kwamba REA Awamu ya Tatu inakuja kusambaza umeme kwenye vijiji vyote, REA Awamu ya Tatu inaanza mwezi Julai baada ya bajeti yetu kupita mwaka huu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ni kuanzia mwezi Julai miezi inayofuata maeneo yenye mashimo yatapatiwa umeme kuanzia mwezi wa saba mwaka huu mara baada ya bajeti yetu kupita.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dhumuni la *REA Phase One* ilikuwa ni kupekeka umeme kwenye kila makao makuu ya kata na kwa kuwa Kata ya Hemtoye, Mbaramo, Mbaru pamoja na kata ya Shagayu bado hazina umeme.

Je, ni lini Serikali itapelekea umeme katika maeneo hayo? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge anataka *commitment* ya tarehe tu, kama bajeti ikipita mwambie.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nisahihisha kidogo, siyo kweli kama *Phase One* ya *REA* ilikuwa inapeleka kata zote ni Kata chache. *REA II* pia ilichagua Mikoa na Kata na maeneo ya kati. Jibu la uhakika sasa kama alivyosema ni lini sasa atapewa, *REA* ya Awamu ya Tatu inayoanza mwezi wa saba ndiyo itakayopeleka umeme kwenye Vijiji vyote pamoja na vya Mheshimiwa Mbunge ambavyo havijapata umeme hadi sasa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Savelina Mwijage.

Na. 149

Viwanda vingi kuwa Chakavu na Kufanya Kazi kwa Kusuasua

MHE. SVELINA S. MWIJAGE aliuliza:-

Viwanda vingi nchini vimekuwa vya kizamani, vingine vimetekelezwa na wawekezaji na baadhi hufanya kazi kwa kusuasua hasa katika Mkoa wa Kagera.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuviboresha viwanda hivyo ili viweze kufanya kazi vizuri kwa faida ya nchi yetu?

WAZIRI WAVIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi vinavyotumia teknolojia ya zamani ambavyo havifanyi kazi au kuzalisha kwa kusuasua vingi ni vile vilivyobinafsishwa. Tathmini iliyofanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina inaonesha kuwa kati ya viwanda vilivyobinafsishwa, viwanda 24 vinafanya kazi kwa kusuasua na viwanda 37 vimefungwa kote nchini.

Aidha, katika Mkoa wa Kagera kiwanda cha *NMC Old Rice Milling* kimefungwa wakati kiwanda cha *Kagera Tea Co. Ltd* (MARUKU) kinafanya kazi kwa kusuasua. Kusuasua kwa kiwanda hiki na vingine vyote nchini kutokana na uchakavu wa mitambo katika baadhi ya viwanda, ushindani katika soko, kupungua kwa mtaji na kutopatikana kwa malighafi nikizungumzia kiwanda changu cha MARUKU.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashauriana na wawekezaji wa viwanda vinavyofanya kazi kwa kusuasua na vile vilivyofungwa ili kuviwezesha viwanda hivi kufanyakazi. Aidha, majadiliano yanayoendelea pia tunawahimiza kutumia teknolojia ya kisasa katika uzalishaji ili kuongeza tija na kupunguza athari za mazingira zinazohusiana na uzalishaji viwandani. Vilevile tunawashauri wawekezaji walioshindwa kuendesha ipasavyo viwanda vyao kuingia ubia na wawekezaji wengine wenye uwezo wa kuviendesha kwa tija ili tuongeze ajira, tuzalishe bidhaa kwa ajili ya soko la ndani lakini na zaidi walipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na mamlaka nyingine itaendelea kulinda viwanda vya ndani kwa kuhakikisha bidhaa zote ziingiazo zinakidhi viwango na zinatozwa tozo stahiki. Aidha, tutahakikisha tunaboresha wepesi wa kufanya biashara kwa kuondoa tozo kero na kuhakikisha kuna umeme wa uhakika kama alivyosema Naibu Waziri wa Nishati.

MHE. SABELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Kwa kuwa, viwanda vilivyopo Mkoa wa Kagera hasa ukiangalia Kiwanda cha *TANICA* kimejengwa mwaka 1967, kiwanda cha *BUCOP* 1967 na *Kagera Sugar* 1990. Viwanda vyote vimekuwa chakavu na viwanda vyote havifanyi kazi vizuri, tukitegemea Serikali au kutegemea wawekezaji ili waweze kuvitengeneza au kuviboresha tutakuwa tunaenda sehemu ambayo siyo nzuri.

Je, ni lini Serikali itaviboresha angalau vikawa viwanda vya kati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Kagera tuna wazalishaji wengi wa matunda na wazalishaji wengi wa maziwa, Mkoa wa Kagera hatuna hata *SIDO* angalau ya kuweza kujumuisha Mkoa mzima, je, ni lini Serikali itaweka viwanda vya kuzalisha matunda na kuweka viwanda vya *SIDO* ili vijana wapate ajira? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uboreshaji wa viwanda vilivyopo na mfano wake aliotolea ni *Kagera Sugar*, mmiliki wa *Kagera Sugar* anaweza kisasa kutoka tani 60,000 za sukari

anazozalisha akilenga tani 120,000. Nimefanikiwa kuongea na Waziri wa Uwekezaji wa Oman ambako kutoka tani 120,000 *Kagera Sugar* atazalisha tani 180,000 ili kusudi *Kagera Sugar* izalishe tani 300,000 tutosheleze soko la ndani na kupeleka Oman.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maziwa na matunda, Kagera ni eneo lenye fursa nzuri ya kuwekeza kwenye maziwa. Mkakati tulionao nawasiliana na wajasiriamali wenye Kampuni ya *GESAPU Agro Farming* ambao watawekeza pesa karibu bilioni 14, watatengeneza mtandao wa kukusanya maziwa kuanzia Chato kwenda Geita mpaka Kagera na wataweka kiwanda Misenyi na mimi niko tayari kupambana nao ili wafanikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *SIDO* Mheshimiwa Mwijage nitahakikisha *SIDO* inaanzia Kagera na inasambaa nchi nzima kwa nguvu zaidi. (Makofi)

MWENYEKITI: Muda wetu ni mchache nampa Mheshimiwa Ndassa ajiandae Mheshimiwa Sugu na Mheshimiwa Chegeni.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mwanza hapo awali kulikuwa na zaidi vinu 15 vya kuchambulia pamba, kikiwepo na cha *Nyambiti Ginnery*, Ngasamo. Mheshimiwa Waziri kwa sababu nilishaongea na Mheshimiwa Waziri Marehemu Abdallah Kigoda, pia niliongea na Waziri aliyekuwepo wakati huo Mheshimiwa Mama Nagu; ni lini sasa angalau *Nyambiti Ginnery* iweze kutengeneza pamba nyuzi? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pamba limekuwa na hoja kubwa kwenye bajeti yangu, majibu niliyotoa ni kwamba tarehe 02 Mei, nilizindua mkakati namna ya kuboresha pamba kusudi iendane na ujenzi wa uchumi wa viwanda. Ijumaa mikoa yote inayolima pamba, tunakutana Mwanza na mimi nitakuwepo niwapitisha kwenye mkakati na nitahakikisha kwamba Kiwanda cha *Nyambiti* kiweze kuingizwa katika mchakato wa kuchambua pamba na kutengeneza kiwanda ikiwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo siku ya Ijumaa shughuli nzima inafanyika Mwanza mimi nitakuwepo pale, tuchambue suala la pamba ili ule mkakati wangu wa nguo uweze kutekekezwa.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Sugu kwa kifupi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba amewashauri walionunua viwanda ambao wameshindwa kuviendeleza chini ya sera ya ubinafsishaji watafute wabia, lakini wote tunakumbuka Serikali hii wakati wa kampeni na hata baada ya kampeni mara kadhaa imetoa matamko kwamba itawapa muda wawekezaji walioshindwa kuviendeleza viwanda wavirudishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nijue Kiwanda cha ZZK Mbeya, Kiwanda cha Chai Katumba na Mbeya Textile, ni lini vitarudishwa kama ambavyo mliahidi kwenye kampeni na baada ya uchaguzi au hizi ndiyo siasa za *flip flap*?

MWENYEKITI: Ahsante, majibu Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbilinyi, *Chief Lumanyika* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma hotuba yangu haya maneno mengine mimi siyo mtu wa rahisi rahisi siwezi kuteka mtu nyara. Kuna mambo mawili, kiwanda ulichopewa natumia lugha viwanda vilivyobinafsishwa havikuuzwa, walipewa. Kwa sababu ile pesa waliolipa ilikuwa na masharti kwamba ukiendeleze kizae bidhaa, uzalishe bidhaa, utoe ajira na ulipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la Mheshimiwa Mwijage nimezungumza lazima mtu alipe kodi, sasa habari yenyewe ndiyo hii, tamko la Serikali ni hili. Aliyepewa kiwanda kwa utaratibu huo, ama kiendeshwe ama atapewa mtu mwingine akiendeleze, mambo ya kujadiliana hayo hayapo, na imeandikwa kwenye hotuba yangu. Nimekuwa nikilisema nimeliandika kwenye hotuba yangu nitakuwa kwenye *position* ya kuwaeleza kabla ya nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha unaoanza kwamba hizi ni mbivu, hizi ni mbichi, lakini lakini viwanda vyote viwe vinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaeleze tu kwamba wote waliochukua viwanda wanakuja kwa Msajili wa Hazina na wametoa programu namna ya kutengeneza, programu siyo moja. Hili suala ni la kimakataba, wanamikataba tunahakikisha kwamba tunakwenda kwa mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vingine vilishindwa kufanyakazi kwa sababu ya ushindani usio sawa, ndiyo maana tunaweka mazingira wezeshi kwa kuzuia watu waliokuwa wana-*dump* bidhaa hapa. Ni kama maswali mnayolalamikia kwamba kuna *uplifting*, *uplifting* zitaendela ili kuwazuia watu wanao-*dump* vitu hapa kusudi viwanda vyangu vifanye kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri inatosha, Mheshimiwa Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimwia Mwenyekiti, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwanza nimpongeze amekuwa anatoa majibu marefu na mazuri.

Kwa kuwa viwanda vya pamba au vinu vya pamba katika Wilaya ya Busega vingi havifanyi kazi kwa mfano, kule Ngasamo na Nasa; na kwa sababu Waziri amesema kwamba, ana mkakati wa kuvifufua viwanda hivi, Je, kupitia sera hii mpya ya viwanda kwa Serikali ya Awamu ya Tano, viwanda hivi vitakuwa ni sehemu ya mkakati huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana muda wetu umekwisha.

WAZIRI WAVIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 02 Mei nimezindua mkakati unaitwa *C to C (cotton cloth)*; ukiusoma ule mkakati unaanzia kwa mzalishaji wa pamba, azalishe kwa tija. Pamba ikiwepo *ginnery* zitafufuka, *ginnery* zilikufa kwa sababu pamba haikuwepo, kwa hiyo ni mchakato mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudie kama alivyosema hapa Mheshimiwa Ndassa. Ijumaa nitakuwa na wadau wenyewe wa pamba Mwanza ambapo Wakuu wa Mikoa wote watashiriki na Bodi ya Mazao itashiriki, tutayajadili yote hayo. Nipeni *information* zote zinazotakiwa kwa siku ya leo kesho naanza safari nitakuwa Mwanza yote hayo nitayafanya tu, ningependa viwanda vyote vifanye kazi ikiwemo kile cha Mzee Gulamali cha Manonga.

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na sasa nitatangaza wageni.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo ukumbi wa Spika, wageni wa Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu, Mbunge, Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao ni Dkt. Mpoki Ulisubisya - Katibu Mkuu Afya, Ndugu Sihaba Nkinga - Katibu Mkuu, Maendeleo ya Jamii, pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo, Wakurugenzi na watendaji wengine. (Makofi)

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni wageni sita toka zahanati ya Uturo iliyoko Wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya, wakiongozwa na Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Dkt. Seif B. Mhina, zahanati hii ya Uturo imefanikiwa kuzuia vifo vya mama na mtoto kuanzia mwaka 1998 hadi sasa, hongereni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia timu ya pamoja ya upasuaji wa kikuchwa kikubwa na mgongo wazi ya hospitali ya *MOI* na *GSM Foundation* ikiongozwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa *MOI* ambaye ni Dkt. Othman Kiloloma na ndugu Halfan Kiwamba kutoka *GSM Foundation*, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wawakilishi na wadau wa maendeleo wanaofanya kazi na kusaidia sekta ya afya hapa nchini wakiongozwa na mwakilishi kutoka Shirika la Afya Duniani (*WHO*). (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla Mbunge, Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wakiongozwa na mke wake Dkt. Bayoum Kigwangalla ameambatana pia na marafiki zake tisa, karibuni Dodoma.

Pia wapo wanafunzi 33 kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM* na *St. John* wanaosoma mafunzo ya udaktari, uuguzi na ukunga. Karibuni (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, tunaye pia Bi. Aneth David Balozi wa Wanasayansi wachanga ambao pia ni mshindi wa tuzo ya *Next Eistern Forum* ameongozana na kaka yake, karibu. Pia kuna wageni kumi wa Mheshimiwa Flatei Massay Mbunge, ambao ni wanafunzi wa *St. John University* kutoka Mkoa wa Manyara. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wageni watatu wa Mheshimiwa Khadija Salum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye ni ndugu Hania Omar Sultan, ndugu Ayoub Haji Ame na ndugu Abdallah Ally Juma. Pia tunao wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge, ambaye ni wajukuu zake wawili, Ndugu Steven Herman na Ndugu Angel Sekumbi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wageni sita wa Mheshimiwa Peter Serukamba, Mbunge Jimbo la Kigoma Mjini ambaye ni viongozi wa *Mkapa Foundation* kutoka Mkoa wa Dar es salaam wakiongozwa na Dkt. Hellen M. Senkoro, Afisa Mtendaji Mkuu, karibuni mnafanya kazi nzuri. (Makofi)

Wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni ambao ni wafugaji kutoka Jimbo la Busega Mwanza wakiongozwa na Mzee Malale Mchele ambaye ni Kiongozi wa Wazee Jimbo la Busega - Lamadi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo kwa ajili ya ziara ya mafunzo wanafunzi 49 wa Mheshimiwa Oscar Mukasa, Mbunge kutoka shule ya *St. Peter Clever High School* kidato cha tatu Mkoa wa Dodoma. Wengine ni wanafunzi 30 na walezi watatu kutoka shule ya msingi ya kiingereza ya *St. Pius* iliyopo

Tarekea Mkoa wa Kilimanjaro, pia wanafunzi 40 na walezi watatu kutoka *St. Joseph English Medium Primary School* ya Rombo Kilimanjaro, karibuni. (Makofi)

Viongozi wawili kutoka Baptist Taifa na kiongozi mmoja wa jumuiya ndogo ya Baptist Dodoma ambaye ni Michael Honya, Makamu Mwenyekiti Taifa, Atupile Banda Kyando, Makamu Mweka Hazina Taifa, Anthony Maria Simba Mwenyekiti wa Jumuiya ndogo ya Dodoma. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, leo Jumatano tarehe 11, mara baada ya Bunge kuahirishwa saa saba mchana, kutakuwa na Ibada ya misa mtakatifu katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili karibuni katika kumwabudu Mungu, tangazo hilo limeletwa na Cecilia Paresso, Katibu wa Jumuiya ya St. Thomas - Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mnaalikwa na taasisi ya NGO ambayo inashughulika na masuala binafsi ya ujasiriamali kutoka Zanzibar iliyoshughulikia na kirutubisho kinachoitwa *Trevo* Wabunge wote wanaombwa siku ya Jumapili wenye nia ya kutaka kujua aina ya kirutubisho hicho kuanzia saa nne asubuhi mpaka saa nane mchana katika ukumbi wa VETA, Mjini Dodoma.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo nyongeza ya wageni waliopo Bungeni ambao ni wageni wanne wa Mheshimiwa Juma Kombo Hamad, Mbunge Jimbo la Wingwi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali, Hoja ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017- Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Kama Ilivyosomwa Bungeni

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na kwa ridhaa yako kutokana na ukubwa na umuhimu wa hotuba yangu naomba iingie yote kwenye *Hansard* kama tulivyoiweka mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya

Bunge lako Tukufu ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2015/2016 na Mipango ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2016/2017. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo wa Wizara yangu kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunikabidhi majukumu ya kusimamia Wizara hii. Wajibu ulio mbele yangu ni kukidhi matarajio ya Mheshimiwa Rais, matarajio ya Watanzania hasa wanawake wa Tanzania kwa kufanya kazi kwa kasi na ufanisi mkubwa ili kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma bora za afya, sambamba na kujenga jamii inayojali usawa wa jinsia, haki za wazee na watoto.

Aidha, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake imara na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu. Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa huduma za afya na usafi wa mazingira zinaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri wake wa dhati katika kuboresha huduma za afya hasa afya ya mama na mtoto na masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Akiwa ndiyo Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya Tanzania, Wizara yangu itaendelea kutumia taswira yake, itatumia ushawishi wake, itatumia uzoefu wake ili kujenga jamii ya Watanzania inayowajali, kuwaheshimu na kuwaendeleza wanawake na wasichana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze wewe kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge, naamini Waheshimiwa Wabunge wote wamefurahi kukuona umerudi tena katika kiti hiki na Bunge sasa litachangamka na litaenda kwa kasi ile ambayo tunaijua ya Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, nakupongeza sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kwa kuaminiwa kuwa sehemu ya uongozi wa Bunge. Kipekee niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, kwa ushauri na maelekezo yake waliyoyotoa wakati wa maandalizi ya Bajeti yangu. Namshukuru sana Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel ambaye tumefanya naye kazi kwa karibu sana na ametupa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize katika awamu hii ya kupongeza, kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuaminiwa na wananchi katika majimbo yenu. Lakini naomba mkumbuke wapiga kura wengi wenu ni wanawake, naamini mtafanya kazi kwa ajili kutatua changamoto zinazowakabili wanawake katika majimbo yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo ya vipaumbele vya Wizara katika bajeti ya 2016/2017 pamoja na utekelezaji wa kazi za Wizara kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 na maombi ya fedha kwa mwaka 2016/2017. Vipaumbele vya Wizara ni vingi lakini katika mwaka 2016/2017 tutajikita katika masuala makubwa yafuatayo:-

Kwanza, kuimarisha huduma za kinga, tiba, kuongeza usawa katika utoaji wa huduma za afya na kupunguza vifo vya wanawake wajawazito. Tutaimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya. Tutaimarisha miundombinu kwenye vituo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu.

Pia kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Hospitali ya Benjamin Mkapa - UDOM, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto pamoja na Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, KCMC, Mbeya na Mtwara.

Kuhamasisha wananchi kujiunga na Mifuko ya Bima za Afya, kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, ikiwemo kupambana na mimba na ndoa za utotoni. Pia kuimarisha na kupanua juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuhamasisha uanzishwaji wa SACCOS na VICOBA vya wanawake, kuwapatia elimu ya ujasiriamali, biashara na kuwaunganisha na vyombo vya fedha. Kuimarisha miundombinu ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi ili

kuwapatia maarifa na stadi za kuwajengea uwezo wa kujitegemea na kuinua hali za maisha yao na Taifa kwa ujumla.

Kuwajengea uwezo watumishi wa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ili waweze kuchochea ari na mwamko wa wananchi wa kutumia rasilimali zilizopo katika kuongeza kipato kwa jamii hasa vijana na wanawake. Kuimarisha haki, ulinzi na usalama wa wazee na kuwezesha mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazokinzana na haki za wanawake na watoto ikiwemo Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipitie ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2015/2016 na malengo ya mwaka 2016/2017. Kama nilivyosema kwa sababu mambo ni mengi, nitajikita katika maeneo makubwa matatu, kwanza ni huduma za kinga, pili ni huduma za tiba na tatu ni upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa mapato na matumizi ya fedha, Wizara yangu kupitia Fungu 52 - Afya, hukusanya mapato yake kupitia Bodi na Mabaraza mbalimbali, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi na vyanzo vingine.

Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 122.9. Katika kipindi cha robo tatu za kwanza, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 92.2 hadi kufikia mwezi Machi 2016, Wizara imekusanya jumla ya shilingi bilioni 87.1 ikiwa ni asilimia 94.4 ya lengo la kipindi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara inatarajia kukusanya shilingi bilioni 163.7 kupitia Fungu 52 ambalo ni Afya. Katika mwaka 2015/2016 jumla ya shilingi bilioni 780.7 ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 340 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 440.6 za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2016 jumla ya shilingi bilioni 604.5 zilipokelewa ikiwa ni asilimia 77.4 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi bilioni 269.2 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 335.3 ni fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016 Wizara yangu kupitia Fungu 53, ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 2.7 kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, Wizara iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 27.5 ambapo kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi bilioni 18.6 yakijumuisha shilingi bilioni 11.03 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 7.58 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Matumizi ya Miradi kupitia Fungu 53 iliyoidhinishwa ni shilingi bilioni 8.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi 2016, makusanyo yalifikia shilingi bilioni 1.8 sawa na asilimia 66.9 ya lengo. Fedha za Matumizi Mengineyo shilingi bilioni 3.8 zilipokelewa sawa na asilimia 51 ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi bilioni 4.1 za mishahara zilipokelewa sawa na asilimia 37 ya bajeti iliyoidhinishwa. Vilevile bajeti ya Miradi ya Maendeleo, shilingi milioni 827 fedha za nje sawa na asilimia 28 ya fedha za nje zilizoidhinishwa zilipokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, kwa upande wa rasilimali watu katika sekta ya afya, Wizara wangu iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) kwa kuongeza idadi ya wanafunzi wa tarajali wa ngazi ya kati waliodahiliwa katika vyuo vya Afya nchini na kufikia 11,192 kwa mwaka na hivyo, kuvuka lengo la kudahili wanafunzi 10,000 kwa mwaka. Aidha, Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi 295, wanaochukua mafunzo ya Uzamili katika vyuo mbalimbali, lengo ni wanafunzi 350.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu imepunguza pengo la upungufu wa watumishi wa afya kutoka asilimia 58 hadi kufikia asilimia 51 mwaka 2015/2016. Haya ni mafanikio makubwa kwetu ingawa bado iko changamoto ya uhaba wa rasilimali watu lakini hii ni kutokana na utekelezaji wa mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa.

Aidha, Wizara imeongeza uwiano wa Kitaifa kati ya madaktari na watu wanaowahudumiwa kutoka madaktari 7.74 mwaka 2014/2015 hadi 9.03 mwaka 2015/2016 kwa watu 10,000. Katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kuongeza idadi ya watumishi wa afya pamoja na kuendesha mafunzo ya afya na kuongeza idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa katika ngazi mbalimbali. Aidha, Wizara itatoa kipaumbele cha kufadhili mafunzo ya uzamili kwa watumishi ambao maombi yao yatawasilishwa na Taasisi, Hospitali kwa kuzingatia mahitaji kama yalivyoanishwa katika ikama 2014/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisistize tu hapa, udhamini kwa ajili ya mafunzo ya uzamili na uzamivu sasa hivi yatakayotolewa ni yale ambayo hospitali husika au taaasisi husika itasema ndiyo yanayohitajika katika kuboresha utoaji wa huduma za afya. Kwa hiyo, hatutamdhamini mtu yeyote kwasaabibu tu anafanya kufanya *Masters* au anataka kufanya *Ph.D*, tutazingatia vipaumbele vya taasisi na hospitali husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kinga; Wizara imeendelea kudhibiti magonjwa ya mlipuko ikiwemo Kipindupindu na Homa ya Bonde la Ufa na katika mwaka huu Wizara imefanya kazi katika Mikoa tisa na katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo wa magonjwa ya mlipuko ikiwemo kipindupindu, na itapanua utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya

simu kwa kutumia mfumo wa kieletroniki kwa kuongeza mikoa minne ya Kigoma, Mbeya, Katavi na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa malaria; Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kutekeleza afua mbalimbali. Wizara imenunua katika mwaka huu wa 2015/2016, Wizara imenunua na kusambaza vitendanishi milioni 17.5 vinavyotoa majibu ya haraka na dawa mseto dozi milioni 19 kwa ajili ya vituo vya umma vya kutolea huduma za afya na jumla ya chupa milioni 1.1 za dawa ya sindano zilisambazwa kwa ajili ya kutibu wagonjwa wenye malaria kali.

Vilevile Wizara imetekeleza kampeni ya usambazaji wa vyandarua vyenye dawa 20.5 katika mikoa 18 nchini. Katika mwaka 2016/2017 Wizara itaendelea na ugawaji wa vyandarua kupitia wanafunzi shuleni na kliniki za afya ya uzazi na mtoto katika Mikoa ya Mwanza na Mtwara kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kudhibiti ugonjwa wa kifua kikuu na ukoma, pia kudhibiti UKIMWI kwa kutoa elimu, ushauri nasaha na kupima. Jumla ya Watu wanaoishi na VVU 743,773 walianzishiwa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI sawa na asilimia 84 ya lengo la kuwafikia watu wenye virusi vya UKIMWI 880,681 ifikapo Juni, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa ambalo tumepata mafanikio katika mwaka huu ni kuboresha vituo 5,540 vya mpango wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kwa kuviwezesha kutoa ARV kwa wajawazito na wanaonyonyesha na kufanya idadi ya wajawazito na wanawake wanaonyonyesha wanaopata tiba ya ARV kuongezeka kutoka asilimia 75 hadi asilimia 90 mwaka 2015. Kwetu sisi haya ni mafanikio makubwa sana na tunaamini kwamba tutaweza kuwafiki wanawake wote wajawazito na wanaonyonyesha ili kuwakinga watoto wao na maambukizi ya VVU. Jumla ya wanaume 444,900 wamefanyiwa tohara na kufikia wanaume milioni 1.9 waliokwisha kupata huduma hiyo tangu kuzinduliwa kwa kampeni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeratibu utekelezaji wa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, kwa mfano, trakoma, usubi, mabusha, kichocho na minyoo ya tumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya afya ya uzazi na mtoto, Wizara imeendelea kuboresha huduma hizi kwa kuwajengea uwezo watoa huduma kutoka katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi jinsi ya kumhudumia mtoto aliyezaliwa na uzito pungufu kwa njia ya mwambatano wa ngozi kwa ngozi kati ya mama na mtoto au *Kangaroo Mother Care*. Aidha, hadi Machi, 2016, jumla ya vituo 54 vilivyopo katika mikoa 22 ya Tanzania Bara vilitoa

huduma hiyo. Katika mwaka 2016/2017 Wizara itaanzisha vituo 20 vya Kangaroo Mother Care katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la vifo vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto kubwa katika Nchi yetu. Kwa mujibu wa taarifa ya umoja wa Mataifa, vifo hivyo vimepungua kutoka 454 mwaka 2010 hadi vifo 398 mwaka 2015 katika kila vizazi hai laki moja. Katika kuendelea kupunguza vifo vya wajawazito, Wizara imetoa mafunzo kwa watoa huduma kutoka vituo mbalimbali vya afya Nchini lakini pia vituo vya afya vimeendelea kuboreshwa na kupandishwa ngazi na kuanza kufanya upasuaji wa kutoa mtoto kutokana na uzazi pingamizi. Hivi sasa vituo vyetu vya afya vya Serikali 159 vinatoa huduma za kutoa mtoto kutokana na uzazi pingamizi. Halmashauri zimeendelea kuhamasishwa kununua magari ya kubebea wagonjwa lakini pia kuhakikisha wanaweka utaratibu mzuri wa vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma kutoa huduma za dharura kwa wanawake wajawazito, kuhimiza Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye uzazi salama na kushirikisha wananchi na jamii. Wizara itaanza kutoa taarifa kila baada ya robo mwaka ya vifo vitokanavyo na uzazi vilivyotokea katika kila Halmashauri ili kuongeza uwajibikaji katika Halmashauri na jamii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo tutaweka nguvu kwa pamoja tutaweza kushinda vita hii na kuwahakikishia wanawake usalama wao na wa vichanga vyao wakati wanapotekeleza haki yao ya msingi ya uzazi. Ndiyo maana leo nimeialika Serikali ya Kijiji cha Uturo, Halmashauri ya Mbarali kwa sababu wameweka mikakati thabiti ya kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga toka mwaka 1998, Kijiji cha Uturo kupitia zahanati yake, hakuna mwanamke mjamzito aliyefariki kwa sababu tu ya kutimiza haki yake ya msingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba iwapo wote tutawajibika, tutaweza kupunguza vifo vya kina mama wajawazito. Nitumie Bunge lako Tukufu kuipongeza Serikali ya Uturo na kuwaambia kwamba Serikali tunatambua jitihada zao na niombe kupitia Bunge lako Tukufu Waheshimiwa Wabunge, wapeleke Mabaraza yao ya Madiwani katika Kijiji cha Uturo wakajifunze ni mikakati gani wameweka ya kupunguza vifo vya kina mama wajawazito. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la chanjo, tumeweza kutoa chanjo za kuinga watoto na makundi mbalimbali dhidi ya magonjwa ya kuambukiza na napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba, mwezi Novemba 2015, Shirika la afya Duniani liliipatia Tanzania cheti cha kuitambua kuwa moja ya nchi zisizokuwa na virusi vya ugonjwa wa polio. Katika mwaka

2016/2017 Wizara itaendelea kuongeza kiwango cha chanjo hadi kufikia asilimia 95.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yangu nimezungumzia usafi wa mazingira na hasa jitihada za Mheshimiwa Rais za kuweka msisitizo katika usafi wa mazingira lakini pia kutambua jitihada za Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Paul Makonda kwa kuzindua kampeni ya usafi katika mkoa wa Dar es Salaam. Nizihimiza Halmashauri, inawezekana Majiji yetu na Wilaya zetu kuwa safi iwapo tutatekeleza mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia suala la huduma za lishe lakini sasa niruhusu tu niingie katika eneo linalohusu huduma za tiba. Katika mwaka 2015/2016 Wizara yangu imetoa huduma za matibabu ikiwemo matibabu ya kibingwa kupitia hospitali zetu kuu tano, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa - MOI, Taasisi ya Jakaya Kikwete ya Moyo, *Benjamin Mkapa Hospital – UDOM* na Taasisi ya Saratani - *Ocean Road*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara itaongeza idadi ya vitanda vya wagonjwa mahututi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kutoka vitanda 21 hadi vitanda 75. Tutanunua vifaa tiba vya upasuaji na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka 13 hadi vyumba 18. Lakini pia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili itapanua huduma za kusafisha figo kwa kuongeza vitanda kutoka vitanda 15 hadi vitanda 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutarajie maboresho makubwa katika utoaji wa huduma za afya hasa matibabu ya kibingwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Taasisi ya mifupa ya Muhimbili itaongeza nafasi ya wagonjwa wanaolazwa kutoka vitanda 150 hadi vitanda 340 lakini pia tutaongeza chumba cha wagonjwa mahututi kutoka vitanda nane hadi vitanda 32. Tutaijengea uwezo Taasisi ya MOI kwa kununua mashine mpya za uchunguzi ikiwa ni pamoja na mitambo ya *MRI, CT Scan* na *Digital X-ray*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete imeendelea kuwahudumia wagonjwa mbalimbali wa moyo, na katika mwaka huu wa 2015/2016 jumla ya wagonjwa 207 wamefanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo hapa nchini na kati yao watoto chini ya umri wa miaka 18 walikuwa 178.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kukuthibitishia katika upasuaji uliofanywa ni kifo kimoja tu kilichotokea katika Taasisi, kwa hiyo tunataka kutumia fursa hii kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ya Awamu ya Tano itaboresha huduma za upasuaji pamoja na huduma za matibabu ya moyo katika kuhakikisha kwamba tunatoa huduma hizo nchini badala ya kuwapeleka Watanzania nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ilifanya uchunguzi kwa wagonjwa wa moyo 451 kwa kutumia mashine ya kisasa ya *Cath Lab*, mashine hiyo inamuwezesha daktari kuweka vyuma maalum ndani ya mishipa ya moyo, kuziba matundu bila kupasua kifua. Kutokana na upasuaji ambao umefanyika katika nchi yetu, Serikali imeweza kuokoa zaidi ya shilingi bilioni nne ambazo zingeweza kutumika kupata huduma hii nje ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Taasisi itaendelea kuboresha huduma na kuifanya kuwa kituo cha mafunzo kwa wataalam wa upasuaji wa moyo Afrika Mashariki na Kati. Aidha, Wizara itaijengea uwezo taasisi hii kwa kuweka vifaa ili chumba cha upasuaji cha tatu kianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaboresha huduma katika hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa, Taasisi ya saratani ya *Ocean Road* kwa kununua vifaa vya uchunguzi na matibabu ikiwa ni pamoja na *PET*, *CT Scan*, *LINAC* na *MRI*. Tunatambua changamoto kubwa ya upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani nchini. Katika mwaka huu wa fedha asilimia 13 ya fedha za dawa zitatumika kununua dawa za saratani ili kupunguza mzigo kwa wagonjwa wa saratani ambao wengi ni wanawake hasa wa kipato cha chini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mirembe, hospitali ya Kibong'oto, Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, *KCMC* na Mbeya tumeonesha katika taarifa zao ni kazi gani wameteteleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za tiba nchini ikiwa ni pamoja na kufuatilia Hospitali zetu za Mikoa, hospitali zetu za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Wilaya, zahanati na vituo vya Afya. Mheshimiwa Naibu Waziri ametembea zaidi ya Mikoa 20 na mimi nimetembelea takriban mikoa saba na kubwa tulilolikuta ni uhaba wa dawa, vifaa, vifaatiba lakini pia wananchi wamelalamika kuhusu ubora wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshatoa maelekezo kwa viongozi wote ngazi ya Mkoa na Wilaya kuweka utaratibu mwepesi kwa wananchi kufikisha malalamiko yao pindi wanapoona kwamba hawakupatiwa huduma za afya kwa kiwango stahiki. Kwa upande wetu katika Wizara ya Afya kwa mwaka 2016/2017 tutaanzisha madawati maalum ya Kanda ambayo yatasimamia kwa karibu malalamiko yanayotolewa na wananchi ili yaweze kuyafanyiwa kazi. Tutaigawa nchi katika Kanda tisa ikiwemo Dar es Salaam, Kusini, Mashariki, Magharibi, Nyanda za Juu Kusini, Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Ziwa, Kanda ya Kati na Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeamua kutumia namba ya Bima ya Afya ambayo wananchi wataweza kutoa malalamiko yao pale ambapo watakuwa

wamepata huduma za afya zisizoridhisha. Namba hiyo ya simu ya bure ambayo nawaomba wananchi waitumie kutoa malalamiko ni 08001163.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matibabu ya wazee, Wizara imeendelea kuratibu utolewaji wa huduma za matibabu bure kwa wazee, na katika kutekeleza azma hiyo tumeelekeza kila kituo cha afya cha umma kuanzisha au kutenga dirisha maalum kwa ajili ya matibabu ya wazee. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya madirisha ya wazee 24 katika Hospitali za Mikoa yameanzishwa na madirisha 133 yameanzishwa katika Hospitali za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Februari 2016, Wizara yangu kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilizindua kampeni ya “Mzee Kwanza” ili kuhamasisha jamii kutoa umuhimu na kipaumbele kwa wazee. Kauli mbiu yetu inasema; “Mzee alikuwa kama wewe na wewe utakuwa kama yeye tutoe kipaumbele cha huduma kwa wazee”. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara yangu italeta mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria.

Pia Wizara yangu itaendelea kuboresha huduma za afya kwa wazee na kuhakikisha kuwa dawa zinazotakiwa kutibu magonjwa yanayowasibu wazee mara kwa mara zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeandika katika hotuba yangu kuhusu huduma za uchunguzi ambazo zimefanywa katika maabara zetu 18 lakini pia tumeonesha ni jinsi gani Wizara imenunua vifaa vya kisasa vya radiolojia ambavyo vimefungwa katika hospitali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu huduma za damu salama. Katika mwaka 2015/2016 Wizara imekusanya jumla ya chupa za damu salama 71,600 ikilinganishwa na chupa 100,040 za damu salama zilizokusudiwa. Katika mwaka 2016/2017 Wizara itaendelea kuhamasisha uchangiaji na uhifadhi wa damu nchini pamoja na kukamilisha ujenzi wa vituo vya kukusanya damu salama katika mikoa ya Iringa, Simiyu, Mara, Geita na Mwanza. Nitoe rai kwa wananchi kuchangia damu, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha na kuwahimiza wananchi kuchangia damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kuhusu huduma za dawa. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika suala zima la upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Katika kufanikisha hilo, Serikali imefanya mapitio ya kina ya mfumo wa ununuzi, utunzaji na usambazaji dawa katika bohari ya dawa kwa lengo la kuimaisha upatikanaji wa dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua bado zipo changamoto katika upatikanaji wa dawa. Katika mwaka wa 2016/2017 Bohari ya Dawa itaendelea kuhakikisha kwamba dawa hizo zinatumika kwa kufanya ukaguzi hasa upotevu wa dawa. Lakini pia tutaendesha na kufungua maduka ya dawa katika hospitali kumi nchini kwa kushirikiana na hospitali husika. Vilevile Bohari ya Dawa itanunua dawa, vifaa, vifaatiba na vitendanishi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji badala ya kununua kutoka kwa wafanyabiashara walio Dar es Salaam. Tunaamini hatua hii itawezesha upatikanaji wa dawa nyingi zaidi kwa wananchi na kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma za ukunga na uuguzi; Wizara imeendelea kuratibu huduma za uuguzi na ukunga ikiwemo kutayarisha mpango mkakati kwa ajili ya huduma za uuguzi na ukunga. Katika mwaka 2016/2017 tutaendelea kusimamia suala hili ikiwemo kuandaa mwongozo utakaotekeleza mahitaji halisi ya wauguzi na wakunga kwa kila aina ya kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia uhakiki wa ubora na huduma za afya, uratibu na ufuatiliaji wa huduma za afya, lakini kubwa katika hili ni kwamba sasa hivi tumeboresha upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa. Taarifa za afya sasa hivi zinapatikana mitandaoni.

Kuhusu ugharamiaji wa huduma za afya ni kwamba tumeongeza wigo wa wanufaika wa Bima ya Afya, hadi kufikia Disemba 2015 mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa unahudumia jumla ya wanufaika milioni 11.7 sawa na asilimia 27 ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 tutaendelea kuwahamasisha wananchi wajiunge na Mfuko wa Bima ya Afya lakini pia Mfuko wa Bima ya Afya utanza kugharamia huduma za matibabu kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18, bila kuangalia uhusiano uliopo kati ya mtoto na mchangiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikiliza vilio vya Waheshimiwa Wabunge na vilio vya wananchi kwamba Watanzania hawatazamiki kwa sababu ni mtoto wa kumzaa, kwa hiyo tutaangalia watoto wote wa chini ya miaka 18. Yule mchangiaji atakaporidhika atakapotuambia kwamba yuko chini ya mikono yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la udhibiti wa kemikali nchini lakini pia udhibiti wa ubora wa chakula, dawa na vipodozi, kazi mbalimbali zimefanyika ikiwemo utafiti wa magonjwa ya binadamu. Lakini kwa sababu ya

muda niruhusu nizungumzie sekta ya maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu inalo jukumu ya kujenga hamasa na kuchochea hali ya wananchi kujitea maendeleo yao na ya Taifa. Hii ni pamoja na kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ya kujenga utamaduni kwa Watanzania siyo tu kupenda kufanya kazi bali pia kufanya kazi kwa bidii. Katika mwaka 2015/2016 Wizara yangu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii imetoa elimu na kuhamasisha jamii katika shughuli mbalimbali za maendeleo. Bado tuna changamoto ya upungufu wa wataalam wa maendeleo ya jamii katika ngazi ya Halmashauri na Kata. Katika mwaka 2016/2017 Wizara yangu itaendelea kutoa hamasa kwa wananchi na jamii kwa ujumla kuhusu kupenda kufanya kazi ili kujitea maendeleo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya jinsia nataka kulithibitisha Bunge lako Tukufu kwamba bado Serikali ya Awamu ya Tano inathamini na kutaka kuhakikisha kwamba usawa wa kijinsia unafikiwa hapa nchini. Kwa hiyo, katika mwaka 2015/2016 kazi mbalimbali zimefanyika ikiwemo kuratibu Madawati ya Jinsia katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali.

Lakini pia Wizara yangu imeshirikiana na wadau kutoa elimu katika jamii dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia. Waathirika wakubwa wa ukatili huu mara nyingi ni wanawake na watoto na tumeweka pale takwimu kuanzia Januari hadi Disemba 2015 matukio 22,876 yameripotiwa, hii ni sawa wa wastani wa matukio 63 kwa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016/2017 Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika kusimamia sheria na kutoa elimu kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia.

Kuhusu kuwawezesha wanawake kiuchumi, Wizara imeendelea kuratibu utendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake. Benki ya Wanawake imetoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo kwa wananchi takriban 13,000. Wizara pia iliendelea kuratibu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ambapo jumla ya shilingi 54,000,000 zilitolewa katika Halmashauri saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Benki ya Wanawake Tanzania inatarajia kufungua dirisha maalum la kutoa mikopo yenye riba nafuu ili kuwafikia wanawake wengi zaidi hasa walio vijijini. Vilevile Wizara itaimarisha usimamizi na uratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama

Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Ban Ki-Moon kuwa Mjumbe wa jopo la ngazi ya juu la Umoja wa Mataifa la kuwawezesha wanawake kiuchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uteuzi huu unakuja wakati tafiti za matumizi ya huduma za kifedha hapa nchini zinaonesha kwamba wanawake wachache sawa na asilimia 51.2 wanatumia huduma rasmi za kifedha ikilinganishwa na wanaume asilimia 63.

Aidha, tafiti zinabainisha kuwa wanawake wanaomiliki simu za kiganjani ni asilimia 53.2 ikilinganishwa na wanaume wanaomiliki simu za kiganjani ambao ni asilimia 70.5. Katika mkwa wa 2016/2017 Wizara yangu itashirikiana na Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kuendesha kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha na kuwawezesha wanawake kufungua akaunti za benki na kutumia benki mtandao. Tunaamini kwamba kwa kufanya hivi wanawake wengi wataweza kutumia benki mtandao kupata huduma mbalimbali ikiwemo huduma za VICOBA na SACCOS.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ya mtoto tuliendelea kuratibu masuala mbalimbali juu ya haki na ustawi wa mtoto na tulipeleka taarifa kwa Kamati ya Umoja wa Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto. Tatizo kubwa lilibainishwa katika taarifa zetu ni tatizo la mimba na ndoa za utotoni hasa katika Mikoa ya Mara, Singida, Dodoma, Shinyanga na Geita. Katika mwaka 2016/2017 Wizara itaendelea kuinua uelewa na uwezo wa jamii kushiriki kikamilifu katika kutokomeza na kuzuia mimba na ndoa za utotoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara pia itaendelea kuhamasisha jamii kuachana na mila na desturi kandamizi kwa mtoto wa kike ikiwemo ukeketaji katika mikoa ya Iringa, Njombe, Dodoma, Singida, Kilimanjaro, Mara, Morogoro, Tabora na Dar es Salaam. Vilevile jamii itahamasishwa kuhusu kuboresha mazingira rafiki kwa elimu ya mtoto wa kike na kuwezesha kuanzishwa kwa klabu za wasichana shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabaraza ya watoto ni muhimu. Katika kuwajengea uwezo, mabaraza ya watoto matano yalianzishwa na hivyo kufanya Halmashauri zenye Mabaraza ya Watoto kufikia 122. Katika mabaraza haya mwaka 2015/2016 Mjumbe wake mtoto Getrude Clement mwenye umri wa miaka 16 aliweza kushiriki na kuhutubia kwa kujiamini Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi uliofanyika Marekani chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Mheshimiwa Ban Ki-Moon. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza mtoto Getrude Clement na kuwahamasisha wazazi, walezi, kuwaruhusu watoto wao kujiunga

na kushiriki katika Mabaraza ya watoto. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Wizara itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa Mabaraza ya Watoto pamoja na kuhamasisha Halmashauri kuyaanzisha na kuyatengea fedha za kuyaendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo na ustawi wa wazee, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ulinzi, matunzo na usalama wa wazee. Katika mwaka wa 2015/2016 jumla ya wazee 167 wameuawa kwa sababu tu ya imani potofu. Jambo hili halikubaliki!

Wizara yangu itaendelea kuhakikisha inatoa elimu ya kuwalinda na kuwatunza na kuhakikisha usalama wa wazee unazingatiwa. Katika mwaka wa 2016/2017, Wizara inatarajia kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Wazee ili kuhakikisha kwamba haki za wazee zinalindwa. Lakini pia tutaendelea kutoa huduma ya chakula, malazi na matibabu katika makazi ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ustawi wa jamii, shughuli mbalimbali zimetetelezwa ikiwemo kutoa huduma za malezi ya kambo na kuasili na pia kuendelea kuzalisha wataalam wa ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza kuhusu mashirika ya Kiserikali ambapo kazi mbalimbali zimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie sasa fursa hii kusema nawashukuru wadau wote, mashirika yasiyo ya Kiserikali, mashirika ya kitaifa na sekta nyingine zinazosaidia na kuchangia katika huduma za afya, maendeleo ya jamii, jinsia wazee na watoto.

Napenda kuzishukuru nchi zinazochangia mfuko wa pamoja wa kugharamia huduma za afya (*Health Sector Basket Fund*), aidha, nazishukuru nchi rafiki zinazochangia katika huduma za afya na maendeleo ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika hotuba yangu nimeainisha wadau wote ambao wamekuwa wakishirikiana nasi kuanzia aya ya 156 katika ukurasa wa 102 hadi aya ya 161 ukurasa wa 107.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika kipindi cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri nimepata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Hamis Andrea Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua Wizara hii ni ya afya, ina-deal na masuala ya matibabu, mimi siyo mtaalam wa afya, mimi ni Mwanasheria lakini

Naibu Waziri amekuwa akinisaidia sana kunisaidia katika masuala ya kitaalam yanayohusu masuala ya afya, nakushukuru sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya anayeshughulikia afya, Dkt. Mpoki Ulusubisya na Katibu Mkuu Bibi Sihaba Nkinga ambaye anashughulikia maendeleo ya jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata pia ushirikiano kutoka kwa Profesa Mohamed Bakari, Mganga Mkuu wa Serikali, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara yangu. Nawashukuru pia Mkurugenzi wa Taifa wa Hospitali ya Muhimbili Profesa Mseru, Kaimu Mkurugenzi wa Moi Dkt. Othman Kiloloma, Kaimu Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Dkt. Mohamed Janabi na Wakurugenzi wa Hospitali Maalum na za Rufaa za Kanda na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri mbele ya Bunge lako Tukufu nimepata ushirikiano mkubwa sana na kuniwezesha kuifahamu Wizara haraka sana na hivyo sasa kuwa tayari kuweza kukabiliana na changamoto mbalimbali. Niwashukuru pia Waganga Wakuu wa Mikoa wote, Waganga Wakuu wa Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Taasisi na Wakuu wa Vyu vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara yangu. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niishukuru sana familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu. Nimshukuru sana mume wangu mpenzi Paskali Kasi Richard naamini kesho atakuwa na sisi hapa, lakini amenitia moyo. Kwa mwanamke kufanya kazi huonekani nyumbani siyo jambo rahisi, namshukuru sana.

Kwa wananchi na hasa wanawake wa Mkoa wa Tanga, nawashukuru sana kwa kunirudisha tena Bungeni. Lakini nawashukuru kwa kunipa ushirikiano. Nataka kuwaahidi wanawake wa Tanga na hasa kupitia Jumuiya ya Wanawake wa Mkoa wa Tanga, tutaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Mkoa wetu wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niruhusu niombe fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 na Mheshimiwa Mwigulu anasema ukiomba fedha inabidi upunguze sauti kidogo iwe taratibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 52 - Afya katika mwaka 2016/2017 Wizara inakadiria kukusanya mapato ya shilingi 163,755,679,857. Kati ya fedha hizo,

shilingi 146,968,868,000 zitakusanywa katika Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 16,786,811,875 ni kutoka katika vyanzo vya Makao Makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na mabaraza ya kitaaluma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida kwa mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Fungu 52 inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 277,604,173,000 na kati ya fedha hizo shilingi 58,151,377,000 zitatumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 219,452,796,000 zitatumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara, shilingi 41,198,490,000 ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara Makao Makuu na shilingi 178,254,387,000 ni kwa ajili ya watumishi wa taasisi, mashirika na wakala zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara inakadiria kutumia shilingi 518,511,683,780 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 320,134,600,000 na fedha za nje ni shilingi bilioni 198,377,083,780.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto mapato; Wizara inatarajia kukusanya shilingi 2,382,679,000 kutokana na ada za wanafunzi kutoka vyuo nane vya maendeleo ya jamii, ada ya usajili wa mashirika yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha shilingi 40,148,480,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 21,479,351,200 zitatumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 18,669,128,800 zitatumika kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo kupitia Fungu 53 katika mwaka 2016/2017 Wizara inakadiria kutumia shilingi 8,848,583,276 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,365,400,000 ni fedha za ndani na shilingi 3,483,183,276 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa muda. Hotuba yangu pia hii inapatikana katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.
(Makofi)

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono.

HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO, MHESHIMIWA UMMY A. MWALIMU (MBUNGE) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka 2015/16 na Mipango ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa mwaka 2016/17.

2. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuchukua fursa hii kwa heshima na unyenyekevu mkubwa kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunikabidhi majukumu ya kusimamia Wizara hii. Wajibu ulio mbele yangu ni kukidhi matarajio yake na matarajio ya Watanzania kwa kufanya kazi kwa kasi na ufanisi mkubwa ili kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma bora za afya na kujenga jamii inayojali usawa wa jinsia pamoja na kuimarisha haki za wazee na watoto. Aidha, namshukuru na kumpongeza pia kwa uongozi wake imara na maelekezo yake ambayo yamekuwa dira sahihi katika utendaji wangu na kuimarisha huduma za Afya, maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto. **Mheshimiwa Rais** amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa huduma za afya na usafi wa mazingira zinaboreshwa. Vilevile, **Mheshimiwa Rais** ametoa kipaumbele kwa kuweka misingi inayoweza kusimamia na kuendeleza haki za makundi maalum ikiwemo haki ya watoto kupata elimu kupitia mpango wake wa elimu bure ngazi ya msingi na sekondari. Kwa jinsi hiyo Wizara itaendelea kuelimisha na kuhimiza umma wa Watanzania kuhusu usafi wa mazingira, haki za wazee na watoto.

3. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa miongozo na ushauri wake wa dhati katika kuboresha huduma za Afya hasa afya ya mama na mtoto na masuala ya kuwawezesha wanawake kiuchumi. Akiwa ndiyo Makamu wa Rais wa kwanza mwanamke katika historia ya Tanzania, Wizara yangu itaendelea kutumia taswira, ushawishi na uzoefu wake ili kujenga jamii ya watanzania inayowajali kuwaheshimu na kuwaendeleza wanawake na wasichana kwa ajili ya kuwa na maendeleo ya kweli endelevu katika nchi yetu

4. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake ambao umesaidia kuongeza ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa na Wizara yangu. Aidha, naomba nimpungeze kwa hotuba yake aliyoivasilisha kwenye Bunge hili ambayo ni dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka 2016/17.

5. Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inadhihirisha jinsi Waheshimiwa Wabunge walivyo na imani kubwa kwako katika kuliongoza Bunge letu tukufu. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge hili. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa kuaminiwa kuwa sehemu ya uongozi wa Bunge hasa katika kusimamia mijadala ndani ya Bunge.

6. Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru **Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki (Mb)** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na **Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb)** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao uliowezesha kusimamia na kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini. Pia, nawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote ambazo ushirikiano wao na Wizara yangu umechangia katika utoaji wa huduma za afya.

7. Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb)**, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, namshukuru Waziri Kivuli wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto **Mheshimiwa Dkt. Godwin Aloyce Mollel (Mb)** kwa ushirikiano mkubwa anaotupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hotuba zilizotangulia. Michango yao imesaidia kuboresha hotuba yangu. Nawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao na ninaahidi kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zilizopangwa.

8. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali. Ninawaahidi kuwapa ushirikiano ili tuendelee kuwatumikia wananchi kwa pamoja. Aidha napenda kuwapongeza Wabunge wote kwa kuaminiwa na wananchi katika majimbo yao. Ni Imani yangu kuwa watatimiza wajibu wao kikamilifu kwa wapiga kura wao ambao wengi ni wanawake.

9. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu na jamaa zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali. Vilevile, natoa pole kwa wagonjwa na majeruhi wa ajali waliopo hospitalini na majumbani pamoja na wahanga wa vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka, ili waweze kuendelea na ujenzi wa Taifa.

10. Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo, ninapenda sasa kutoa maelezo ya vipaumbele vya Wizara katika bajeti ya 2016/17 pamoja na utekelezaji wa kazi za wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2015/16 pamoja na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2016/17.

VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KATIKA BAJETI YA MWAKA 2016/17

11. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika bajeti ya mwaka 2016/17 ni kama ifuatavyo:

i. Kuimarisha Huduma za Kinga, Tiba, kuongeza usawa katika utoaji wa huduma za afya na kupunguza vifo vya wanawake wajawazito,

ii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya,

iii. Kuimarisha miundombinu kwenye vyuo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kuongeza udahili na upatikanaji wa rasilimali watu,

iv. Kuendeleza ujenzi, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Hospitali ya Benjamini Mkapa - Dodoma, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali Maalum za Mirembe na Kibong'oto; pia Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, KCMC, Mbeya na Mtwara,

v. Kuimarisha mazingira ya ubia na ushirikiano kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP) katika utoaji wa huduma za afya,

vi. Kuimarisha huduma za lishe na upatikanaji wake katika jamii na vituo vya kutolea Huduma za Afya,

vii. Uimarishaji wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kuboresha huduma za afya,

viii. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa katika Sekta ya Afya,

ix. Kuhamasisha wananchi kwa nia ya kuongeza idadi ya wanaojunga na Mifuko ya Bima za Afya,

x. Kuzuia na kukabiliana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto ikiwemo kupambana na mimba na ndoa za utotoni;

xi. Kuimarisha na kupanua juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi kwa kuhamasisha uanzishwaji wa SACCOS na VICOBA vya wanawake, kuwapatia elimu ya ujasiriamali, biashara na kuwaunganisha na vyombo vya fedha ikiwemo Benki ya Wanawake Tanzania na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake;

xii. kuimarisha miundombinu ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi ili kuwapatia maarifa na stadi za kuwajengea uwezo wa kujitegemea na kuinua hali za maisha yao na taifa kwa ujumla,

xiii. Kuwajengea uwezo watumishi wa maendeleo ya jamii wa Halmashauri ili kuchochea ari na mwamko wa wananchi wa kutumia rasilimali zilizopo katika kuongeza kipato kwa jamii hasa vijana na wanawake;

xiv. Kuimarisha haki, ulinzi na usalama wa wazee pamoja na kukarabati makazi ya wazee, shule za maadilisho na mahabusi za watoto na kuwapatia chakula; na

xv. Kuwezesha mapitio ya sheria na kanuni mbalimbali zinazokinzana na haki za wanawake na watoto ambazo ni: Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, Sura ya 29 na marekebisho yake ya mwaka 2002; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004; Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009; na Kanuni za Mirathi Na. 279 za mwaka 1963.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA 2015/16 NA MALENGO YA MWAKA 2016/17

Mapato na Matumizi ya Fedha Fungu 52 – Afya

12. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Fungu 52 (Afya) hukusanya mapato yake kupitia Bodi na Mabaraza mbalimbali, ada za uchangiaji wa gharama za mafunzo, marejesho ya masurufu, malipo ya ununuzi wa vitabu vya maombi ya zabuni, pamoja na makusanyo yatokanayo na utoaji wa huduma katika Taasisi na Mashirikayaliyochini ya Wizara. Hadikufikia mwezi Machi 2016 Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 87,117,583,604** ikilinganishwa na makadirio ya **Shilingi 122,998,941,500.00** yaliyoidhinishwa kwa mwaka 2015/16. Hii ni asilimia **70.8** ya makadirio ya makusanyo ambayo yamevuka lengo kutokana na usimamizi thabiti na matumizi ya TEHAMA. Katika mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kukusanya **Shilingi 163,755,679,857.00**.

13. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, jumla ya **Shilingi 780,740,723,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 340,098,271,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 440,642,452,000.00** za Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2016 jumla ya **Shilingi 604,547,066,537.00** zilipokelewa ikiwa ni **asilimia 77.4** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **Shilingi 269,205,005,123.00** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 335,342,061,414.00** ni fedha za Miradi ya Maendeleo. Vilevile, kati ya fedha zilizopokelewa kutoka kwa wadau wa maendeleo kiasi cha **Shilingi 309,409,703,350.00** ni thamani ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyo pokelewa kutoka Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Fungu 53 - Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara yangu kupitia Fungu 53, iliendelea kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kulingana na malengo na shabaha zilizopangwa. Katika bajeti ya mwaka huo, Wizara ilitarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 2,712,550,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, Wizara iliidhinishwa jumla ya **Shilingi 27,501,007,000** ambapo kati ya hizo, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 18,627,587,000** yakijumuisha **Shilingi 11,038,075,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 7,589,512,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishwa ni **Shilingi 8,873,420,000**

15. Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2016, makusanyo yalifikia **Shilingi 1,815,145,600** sawa na **asilimia 66.9** ya lengo. Fedha za Matumizi Mengineyo **Shilingi 3,870,651,121** zilipokelewa sawa na **asilimia 51** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Shilingi 4,138,691,435** za Mishahara zilipokelewa sawa

na **asilimia 37** ya bajeti iliyoidhinishwa. Vilevile, bajeti ya miradi ya Maendeleo, **Shilingi 827,087,080** fedha za nje sawa na **asilimia 28** ya fedha za nje zilizoidhinishwa zilipokelewa.

UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA MWAKA 2015/16 NA MALENGO YA MWAKA 2016/17

A: AFYA

16. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inazingatia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21), Sera ya Afya (2007), Mpango Mkakati wa IV wa Sekta ya Afya (2016 -2020) na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007 – 2017). Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015.

17. Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni taarifa ya sekta ya afya ya kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha Julai 2015 hadi Machi 2016 na mpango wa mwaka 2016/17.

RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

18. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa kuongeza idadi ya wanafunzi watarajali wa ngazi ya kati waliodahiliwa katika vyuo vya Afya na kufikia **11,192** kwa mwaka. Hivyo, kuvuka lengo la kudahili wanafunzi **10,000** kwa mwaka waliolengwa kudahiliwa ifikapo mwaka 2017. Aidha, Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi **295**, wanaochukua mafunzo ya uzamili katika vyuo mbalimbali ya ndani (**275**) na nje (**20**) ya nchi, lengo ni kufadhili wanafunzi 350.

19. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imepunguza pengo la upungufu wa watumishi kutoka asilimia 58 mwaka 2011/12 hadi kufikia asilimia 51 mwaka 2015/16. Hii imetokana na utekelezaji wa Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa. Aidha, Wizara imeongeza uwiano wa kitaifa kati ya madaktari na watu wanowahudumia, kutoka Madaktari **7.74** mwaka 2014/15 hadi **9.03** mwaka 2015/16 kwa watu **10,000**. Vilevile, Wizara imetoa mafunzo kwa timu za usimamizi wa uendeshaji wa huduma za afya kwa mikoa ya Dodoma na Ruvuma pamoja na halmashauri zake zote juu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki unaotumika kubaini mahitaji halisi ya watumishi

kulingana na uzozi wa kazi wa kituo husika (Workload Indicators of Staffing Needs) ili kuweza kufahamu mahitaji halisi ya watumishi katika mikoa hiyo na halmashauri zake.

20. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka 2015/16, Wizara imeongeza vyuo vinavyoendesha mafunzo kwa njia ya masafa kwa kada ya Tabibu Wasaidizi wanaojiendeleza kuwa Tabibu, kutoka vyuo **3** hadi **8**. Hivyo kufanya ongezeko la wanafunzi wanaochukua mafunzo kwa njia hiyo kufikia **238** kwa mwaka 2015 kutoka **54** kwa mwaka 2012. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya awali juu ya mfumo wa ukusanyaji taarifa za vyuo vya Afya na Ustawi wa Jamii (TIIS) kwa maafisa **4** wa Wizara makao makuu, **24** kutoka vyuo **12** vinavyoendesha mafunzo ya Ustawi wa Jamii nchini.

21. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya maandalizi ya mtaala wa mafunzo ya afya makazini (Occupational Health) na kuendelea na maandalizi ya mtaala wa Radiografia kwa kufuata mfumo wa tuzo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi. Aidha, Wizara itatoa kipaumbele cha kufadhili mafunzo ya uzamili/uzamivu kwa watumishi ambao maombi yao yatawasilishwa na Taasisi/Hospitali kwa kuzingatia mahitaji kama ilivyoainishwa kwenye ikama (2014-2019). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), itaendesha mafunzo yatakayolenga kuziwezesha Kanda za mafunzo ya Afya, kufuatilia na kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika vyuo vyote vya Afya nchini.

22. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa afya, Wizara imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa nyumba **480** za watumishi wa kada ya afya katika maeneo yaliyo katika mazingira magumu kufikika. Mradi huo unatekelezwa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilihusu nyumba **310** katika mikoa ya Mtwara, Rukwa/Katavi, Ruvuma, Singida, Pwani, Morogoro, Lindi, Arusha na Manyara. Kati ya nyumba **310**, nyumba **250** zimekamiliika na kukabidhiwa kwa halmashauri husika na ujenzi wa nyumba **60** katika mikoa ya Arusha, Manyara na Pwani zipo katika hatua za ukamilishwaji. Awamu ya pili ilihusu nyumba **170** katika mikoa ya Tanga, Pwani, Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera, Simiyu na Kigoma. Ujenzi wa nyumba hizo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji na unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa kwa halmashauri husika mwezi Juni, 2016.

23. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa uimarishaji wa vyuo vya mafunzo ya Sekta ya Afya, Wizara imekarabati na kupanua hospitali na vyuo mbalimbali. Vyuo vilivyofanyiwa ukarabati wa majengo na kukamilika ni Chuo cha Matabibu Lindi na Chuo cha Uguzi Nzega – Tabora. Aidha, ukarabati wa Taasisi ya

Afya ya Msingi Iringa na Vyuo vya Uuguzi vya Songea, Njombe, Rukwa, Mpanda, Kigoma na Ujenzi wa Vyuo vya Uuguzi vya Musoma na Morogoro unaendelea. Ukarabati wa vyuo hivyo unakwenda sambamba na ukarabati wa majengo ya hospitali za rufaa za mikoa husika.

24. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea na upanuzi na ukarabati wa vyuo vya afya vya Mtwara, Tanga, Mirembe na Mvumi. Ujenzi na ukarabati huo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishwaji. Katika mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha upanuzi na ukarabati wa vyuo hivyo na kuiwezesha Wizara kuongeza idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa.

HUDUMA ZA KINGA

Udhibiti wa Magonjwa ya Milipuko

25. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa yanayotolewa taarifa kitaifa na kimataifa ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko. Aidha, utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki umesambazwa na kufikia mikoa **10** ikilinganishwa na mikoa **mitatu** mwaka 2014/15. Vilevile, mafunzo ya utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki yalitolewa kwa jumla ya wataalam **2,315** wa ngazi zote katika Mikoa ya Mwanza (**361**), Geita (**290**), Arusha (**296**), Dodoma (**490**), Singida (**214**), Manyara (**190**), Dar es Salaam – Ilala (**184**) na Kinondoni (**290**). Teknolojia hiyo imerahisisha upatikanaji wa taarifa za magonjwa kwa haraka na hivyo kufanikisha udhibiti wa magonjwa ya milipuko kwa wakati. Utoaji wa taarifa kwa wakati umeongezeka kutoka **asilimia 60** mwaka 2013 hadi **asilimia 75** mwaka 2015.

26. Mheshimiwa Spika, kufuatia tishio la homa ya Zika lililotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) mwezi Februari 2016, Wizara imeandaa Mpango Mkakati wa namna ya kudhibiti ugonjwa huo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya magonjwa ya milipuko ikiwemo Kipindupindu na itapanua utoaji wa taarifa za magonjwa kwa njia ya simu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kwa kuongeza mikoa minne ya Kigoma, Mbeya, Katavi na Rukwa. Aidha, Wizara itaendelea kuchukua tahadhari ya homa ya bonde la ufa (RVF) kufuatia utabiri wa hali ya hewa unaoonesha kuwa, kutakuwa na mvua kubwa.

27. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege katika vituo sita

maalumu vilivyopo sehemu mbalimbali nchini (sentinel surveillance sites). Vituo hivyo ni pamoja na Hospitali za Mikoa ya Dodoma na Mwanza; Hospitali ya Rufaa Ngazi ya Mkoa ya Hydrom (Manyara) na Mwananyamala (Dar es Salaam); Hospitali ya Wilaya ya Kibondo na Kliniki ya 'International School of Tanganyika' ya jijini Dar es Salaam. Katika kipindi hicho, wastani wa sampuli **3,714** zilichukuliwa na vipimo vya maabara vilionyesha kutokuwepo kwa vimelea vinavyoweza kusababisha mlipuko wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufanya ufuatiliaji katika vituo **6** vilivyopo na inatarajia kuongeza vituo vingine **viwili (2)** katika mikoa ya Mtwara na Kilimanjaro, iliyo mpakani na nchi jirani ili kuweza kutambua ugonjwa huo kwa haraka na kudhibiti uwezekano wa ugonjwa huo kuingia nchini.

Udhibiti wa Malaria

28. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kutekeleza afua mbalimbali. Katika mwaka 2015/16, Wizara ilitekeleza zoezi la kunyunyizia viuatilifu ukoko aina ya *actellic* ndani ya nyumba katika mikoa ya kanda ya ziwa na kufikia nyumba **358,989** ambapo wananchi **1,794,945** walikingwa dhidi ya malaria. Aidha, Wizara imeboresha upatikanaji wa vitendanishi vya kupima malaria na dawa ya mseto kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa malaria isiyo kali katika vituo vyote vya huduma za afya nchini. Jumla ya vitendanishi **17,566,750** vinavyotoa majibu ya haraka (mRDT) na dawa mseto dozi **19,084,230** zilinunuliwa na kutumika katika vituo vya umma vya kutolea huduma za afya. Jumla ya chupa **1,150,000** za dawa ya sindano zilisambazwa kwa ajili ya kutibu wagonjwa wenye malaria kali. Vilevile, uhamasishaji juu ya utekelezaji wa Mkakati wa kuangamiza mazalia ya mbu umefanyika kwa Timu za mikoa na halmashauri saba (7) za Manispaa za Ilemela, Nyamagana, Musoma, Bukoba na Shinyanga, na Miji ya Kibaha na Geita.

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imetekeleza kampeni ya usambazaji wa vyandarua **20,547,849** vyenye viuatilifu vya muda mrefu (LLITNs) katika mikoa **18** ya Mara, Mwanza, Katavi, Tabora, Kigoma, Kagera, Geita, Mbeya, Njombe, Rukwa, Simiyu, Shinyanga, Singida, Iringa, Dodoma, Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Vilevile, usajili katika kaya unaendelea katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Tanga, ikiwa ni maandalizi kwa ajili ya ugawaji wa vyandarua.

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na ugawaji wa vyandarua kupitia wanafunzi shuleni na kliniki za afya ya uzazi na mtoto katika mikoa ya Mwanza na Mtwara kwa awamu ya kwanza. Pia, itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi (mRDT) kwa ajili ya kupima uwepo wa vimelea vya malaria na kununua na kusambaza dawa kwa

ajili ya matibabu katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na sekta binafsi.

Udhibiti wa Kifua Kikuu na Ukoma

31. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za kifua kikuu na kifua kikuu sugu kwa kuboresha huduma za vipimo na kuzisogeza karibu na wananchi. Hivi sasa, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha maabara nne za Kanda za Mbeya (Hospitali ya Rufaa), Mwanza (Bugando), Dodoma (Hospitali ya Rufaa ya Mkoa) na Kilimanjaro (Hospitali ya Kibong'oto) ambazo zinatarajia kuanza kutoa huduma hivi karibuni. Aidha, Wizara itaendelea na ugatuzi wa matibabu ya kifua kikuu sugu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Bugando. Vilevile, katika kuimarisha huduma shirikishi za kifua kikuu na UKIMWI nchini, Wizara imefanikiwa kufikia idadi ya vituo **547** vinavyotoa huduma hiyo chini ya mfumo mmoja. Huduma hiyo inapunguza usumbufu kwa mgonjwa mwenye maambukizi mseto ya Kifua Kikuu na UKIMWI kwa kupata huduma sehemu moja. Jumla ya Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) **692,642** walipata huduma ya kubainisha uwepo au kutokuwepo kwa maambukizi ya kifua kikuu miongoni mwao. Kati ya waliopata huduma hiyo, **26,218** waligundulika kuwa na maambukizi ya kifua kikuu na walipatiwa matibabu.

32. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kufanya kampeni maalum ya utoaji elimu kwa jamii kuhusu dalili za ukoma na namna ya kutambua mapema wagonjwa katika hatua za awali za ugonjwa. Kampeni hiyo, imetekelezwa katika wilaya za Kilombero (110), Nanyumbu (30) na Liwale (130) na kusaidia kuibua na kuwaweka katika matibabu jumla ya wagonjwa wapya **270** mwaka 2015.

33. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kugatua huduma za kifua kikuu sugu kufikia hospitali kumi za mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Dodoma, Morogoro, Mtwara, Tanga, Shinyanga, Geita na Mara. Aidha, Wizara itaiongezea uwezo mikoa 16 yenye viwango vya chini kabisa vya uibuaji wagonjwa wa kifua kikuu ili kuongeza kasi ya kudhibiti ugonjwa huo nchini. Vilevile, Wizara itaendelea kufanya kampeni maalum za uchunguzi na uibuaji wa wagonjwa wapya wa ukoma katika wilaya zenye viwango vikubwa vya maambukizi zikiwemo wilaya za Liwale, Kilombero, Chato, Nanyumbu, Mkinga na Muheza.

Udhibiti wa UKIMWI

34. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na juhudi za kudhibiti UKIMWI kwa kutoa ushauri nasaha na kupima. Kutoka mwezi

Januari hadi Desemba, 2015 jumla ya wateja wapya **3,474,780** walipata ushauri nasaha na kupima VVU. Idadi hiyo inajumuisha pia waliopata huduma kupitia mpango wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Aidha, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watu wanaoishi na VVU kwa kutoa dawa za kupunguza makali ya UKIMWI. Hadi kufikia Desemba, 2015, jumla ya Watu Wanaoishi na VVU (WAVIU) **743,773** walikuwa wameanzishiwa dawa sawa na asilimia **84** ya lengo la kuwafikia WAVIU **880,681** ifikapo Juni, 2016. Vilevile, Wizara imepanua wigo wa utoaji huduma hizo kwa kuongeza idadi ya vituo zaidi na kufikia vituo **1,677** Desemba, 2015 ikilinganishwa na vituo **1,235** Desemba, 2014.

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kutekeleza afua ya tohara kwa wanaume kama mojawapo ya afua ya kupambana na maambukizi ya VVU. Kufikia Desemba, 2015 jumla ya wanaume **444,900** kati ya **492,842** waliolengwa, wamefanyiwa tohara na kufikisha jumla ya wanaume **1,997,000** waliokwisha kupata huduma hiyo tangu ilipozinduliwa nchini mwaka 2010. Idadi hiyo ni sawa na asilimia **71** ya wanaume **2,800,000** wanaopaswa kufikiwa ifikapo mwaka 2017.

36. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuboresha upatikanaji wa vifaa tiba, vitendanishi na mashine za kupimia wingi wa virusi vya UKIMWI kwenye damu kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa matibabu. Lengo ni kupima **asilimia 50** ya WAVIU wanaotumia dawa za kupunguza makali ya VVU ifikapo mwezi Juni, 2017. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa watoa huduma **674** kutoka vituo vya kutolea huduma za afya vya mikoa ya Njombe, Dodoma, Lindi, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Singida, Tabora na Iringa kuhusu kupimawingi wa virusi vya UKIMWI kwenye damu. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutoa huduma ya upimaji VVU na dawa za kupunguza makali ya VVU kwa kuyafikia makundi yaliyo katika hatari zaidi ya maambukizi ya VVU. Vilevile, Wizara itafunga mashine mpya **10** za kupima uwingi wa virusi vya UKIMWI katika damu katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mtwara, Dodoma, Tabora, Iringa, St. Francis Ifakara, Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Bugando, KCMC, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Maabara ya Taifa ya Viwango na Ubora. Mashine hizo zitasaidiana na mashine **11** zilizofungwa katika hospitali zote za rufaa za kanda. Ongezeko hilo la mashine katika hospitali za rufaa za mikoa litaleta ufanisi katika kutoa vipimo na upatikanaji wa majibu ya vipimo hivyo.

37. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutekeleza Afua za Kutokomezwa Maambukizi ya VVU toka kwa Mama kwenda kwa Mtoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara iliviboresha vituo vya Mpango

wa kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) kwa kuviwezesha kutoa ARV kwa wajawazito na wanaonyonyesha ili kuinga maambukizi mapya ya VVU kwa watoto na kwa ajili ya kuboresha afya zao. Hadi kufikia Desemba, 2015, kati ya vituo **5,540** vinavyotoa huduma za upimaji wa VVU na ushauri nasaha, vituo **5,057** vilipata wateja walio na VVU na kuwapa dawa za ARV ili kuzuia maambukizi. Kati ya vituo **5,540**, vituo **4,538** vinatoa huduma ya utambuzi wa mapema wa hali ya maambukizo ya VVU kwa watoto wenye umri wa kati ya wiki 4 hadi 6. Aidha, katika kipindi hicho cha utekelezaji, idadi ya wajawazito na wanawake wanaonyonyesha wanaopata tiba ya ARV imeongezeka kutoka **asilimia 75** mwaka 2013 hadi **asilimia 90** mwaka 2015. Vilevile, watumishi **10,862** walipatiwa mafunzo na stadi husika ili waweze kutoa huduma hizo kwa weledi.

38. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/17, Wizara itakamilisha Mpango Mkakati wa kutokomeza maambukizi wa VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto (2016-2020). Aidha, Wizara itaendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT). Vilevile, huduma ya utambuzi wa mapema wa hali ya maambukizo ya VVU kwa watoto wenye umri wa kati ya wiki 4 hadi 6 itaongezeka toka vituo **4,538** vilivyopo hadi **5,068** ifikapo Juni 2017. Pia, Mfumo wa ufuatiliaji wa watoto wanaozaliwa na wanawake wenye VVU ndani ya kipindi cha mwezi mmoja, wanaoandikishwa katika huduma za PMTCT, utasambazwa kutoka mikoa 6 na kufikia mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele.

39. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, ambapo katika mwaka 2015/16, dawa za Kinga-Tiba za magonjwa ya matende na mabusha, usubi, trakoma, kichocho na minyoo ya tumbo ziligawiwa kwa wananchi **28,935,520** walio na umri kati ya miaka **mitano** na kuendelea katika Halmashauri **169** zilizo na viwango vya juu vya maambukizi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na ugawaji wa dawa za kinga tiba katika wilaya zote nchini kulingana na maambukizi ya magonjwa husika. Vilevile, itaendelea na tathmini ya matokeo ya zoezi la kinga tiba mbalimbali ili kufahamu kiwango cha maambukizi husasan ya ugonjwa wa usubi kwa binadamu na wadudu waenezao ugonjwa huo (nzi weusi wadogo) katika wilaya za Muheza, Lushoto, Korogwe, Rungwe na Kyela.

Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto

40. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto. Katika mwaka 2015/16, Wizara

imewajengea uwezo watoa huduma **284** jinsi ya kumhudumia mtoto aliyezaliwa na uzito pungufu kwa njia ya mwambatano wa ngozi kwa ngozi kati ya mama na mtoto (Kangaroo Mother Care- KMC) katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Kanda ya Magharibi. Kufikia Machi, 2016 jumla ya vituo **54** vya KMC vinatoa huduma katika mikoa mbalimbali ya Njombe (**1**), Kigoma (**1**), Mwanza (**1**), Ruvuma (**1**), Kagera (**14**), Pwani (**3**), Dar es Salaam (**2**), Mara (**11**), Lindi (**2**), Mbeya (**4**), Morogoro (**1**), Shinyanga (**1**), Iringa (**1**), Rukwa (**1**), Mtwara (**2**), Tabora (**1**), Tanga (**1**), Kilimanjaro (**2**), Arusha (**1**), Singida (**1**), Dodoma (**1**) na Manyara (**1**).

41. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma namna ya kumhudumia mtoto mgonjwa mwenye umri chini ya miaka mitano kwa uwiano na kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kutibu Nimonia na kuharisha. Aidha, Wizara itaanzisha vituo **20** vya KMC katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Vilevile, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma wa jinsi ya kumhudumia mtoto mchanga katika vituo vya kutolea huduma vilivyopo katika Kanda ya Ziwa, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini.

42. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma ya afya kwa watoto chini ya umri wa miaka **mitano**, hususan kudhibiti magonjwa ya Nimonia na Kuhara, Wizara ilifanya uzinduzi wa matumizi ya dawa ya Amoxycilin myeyuko na Zinki ORS zilizofungashwa pamoja. Faida za ufungashaji wa Zinki ORS ni kuboresha upatikanaji, kutolewa kwa pamoja kwa mtoto anayeharisha ili kurudisha maji na chumvichumvi mwilini, kupunguza kiwango cha kuharisha na idadi ya kuharisha kwa siku na kisha kumkinga mtoto na kuharisha kwa kipindi cha miezi 2 au 3. Aidha, Mafunzo elekezi ya matumizi ya dawa hizi mpya yalitolewa kwa Waganga Wakuu, Wafamasia waganga wafawidhi wa hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati katika mikoa na wilaya zote. Hadi kufikia Machi, 2016 jumla ya washiriki **2,800** kutoka halmashauri zote **182** walipatiwa mafunzo.

43. Mheshimiwa Spika, suala la vifo vitokanavyo na uzazi bado limekuwa changamoto. Kutokana na Taarifa ya Umoja wa Mataifa imeeleza kuwa tumeweza kupunguza vifo hivyo kutoka **454** mwaka 2010 hadi vifo **398** mwaka 2015. Ili kuhakikisha vifo hivi vinaendelea kupungua kwa kasi zaidi Wizara imehakikisha, watoa huduma wa afya **2,087** wamejengewa uwezo kwa kuwapatia mafunzo ya huduma muhimu wakati wa ujuzito, stadi za kuokoa maisha kwa matatizo ya dharura yatokanayo na uzazi na mtoto mchanga, baada ya kujifungua na huduma muhimu baada ya mimba kuharibika. Aidha, ili kuhakikisha huduma ya afya ya uzazi inakuwa endelevu hadi kufikia jamii, wahudumu wa afya ngazi ya jamii **917** walipatiwa mafunzo jumuishi ya afya ya uzazi na mtoto. Vilevile, jamii imeendelea kuelimishwa kupitia luinga na redio kwa

programu ya “Wazazi Nipendeni”, kupitia simu ya kiganjani ambapo wanawake wajawazito hujisajili kwa namba 15001 na kuweka neno “mimba” ili kupata taarifa ya huduma anazostahili kupatiwa kulingana na umri wa mimba katika vituo vya kutolea huduma za afya. Pia, jamii inaweza kujisajili kwa namba hiyohiyo na kuweka neno “mtoto” ili kupatiwa elimu ya masuala ya uzazi. Aidha, vituo vya afya vimeendelea kuboreshwa na kupandishwa ngazi kwa kuanza kufanya upasuaji wa kutoa mtoto kutokana na uzazi pingamizi. Hadi sasa viko vituo **159** vinavyotoa huduma hizo. Vilevile, jamii imeendelewa kuhamasishwa kuhusu kujitolea kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wanawake kwa matatizo yatoakanayo na uzazi. Aidha, Halmashauri zimeendelea kuhamasishwa kuhakikisha magari ya kubebea wagonjwa yanapatikana katika vituo vya kutolea huduma ili kutoa rufaa mapema endapo itahitajika katika kuokoa maisha.

44. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma kutoa huduma za dharura kwa wanawake wajawazito, kuhimiza Halmashauri kuweka kipaumbele kwenye uzazi salama na kushirikisha wananchi na jamii kwa ujumla juu ya kutokomeza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi. Sote tuwajibike, tuweke nguvu kwa pamoja tutaweza kushinda vita hii na kuwahakikishia wanawake usalama wao na wa watoto wao wanapotekeleza haki yao ya msingi ya uzazi. Wizara itaanza kutoa taarifa kila baada ya robo mwaka ya vifo vitokanavyo na uzazi vilivyotokea katika kila Halmashauri ili kuongeza uwajibikaji katika Halmashauri na jamii husika. Tuwajibike kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Aidha, Wizara inaipongeza Serikali ya kijiji cha Utulo, Halmashauri ya Mbarali kwa kuweka mkakati wa kudhibiti vifo katika jamii yao ambapo toka mwaka 1998 hakuna vifo vya uzazi vilivyoripotiwa katika zahanati ya kijiji cha Utulo.

45. Mheshimiwa Spika, Katika kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi, Wizara pia imeendelea kuimarisha huduma za uzazi wa mpango kwa kusambaza dawa na vifaa pamoja na kuwajengea uwezo watoa huduma. Hadi kufikia Machi, 2016, Wizara imenunua kondomu za kiume **9,000,000**; Dawa ya sindano (Depo provera) vichupa **2,908,043**; Vipandikizi (Implants) **1,313,004**; Vitanzi (IUDs) **211,500** na Dawa za vidonge mizunguko (cycles) **544,320**. Aidha, watoa huduma **989** wamejengewa uwezo ikilinganishwa na lengo la watoa huduma **780** ili waweze kutoa huduma za uzazi wa mpango kwa ufanisi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kusimamia upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango. Aidha, tathmini ya utekelezaji wa mpango mkakati wa huduma za uzazi wa mpango uliothaminiwa kwa kipindi cha miaka mitano (2010- 2015) itafanyika. Matokeo ya tathmini hiyo yatatoa mwelekeo wa mambo muhimu yatakayotekelezwa kwa kipindi cha mwaka 2016-2021.

46. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau wengine kukabiliana na kuhudumia wahanga wa ukatili wa kijinsia kwa kuwapatia mafunzo watoa huduma. Hadi Machi, 2016, jumla ya watoa huduma **316** wamejengewa uwezo. Vilevile, jumla ya wahanga **42,390** ambao wanawake ni **32,103** sawa na **asilimia 76** na watoto wenye umri chini ya miaka 18 ni **3,985** sawa na **asilimia 9.4** walipatiwa huduma za matibabu na uchunguzi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaongeza vituo vya kutoa huduma toshelezi katika mikoa ya Simiyu (Maswa), Shinyanga (Kahama) na Pwani (Kibaha). Vilevile, Wizara itaendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa, kuboresha mfumo wa rufaa na ukusanyaji wa ushahidi wa kimahakama kwa waliofanyiwa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto.

47. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi. Kufikia Machi, 2016, vimeanzishwa vituo vipya **12** vya uchunguzi na matibabu katika mikoa ya Arusha, Shinyanga, Lindi, Morogoro na Mwanza hivyo kufanya jumla ya vituo **298** vilivyopo katika Mikoa 26 ya Tanzania bara (**Kiambatisho Na. 1**). Jumla ya wanawake **120,011** walipimwa ambapo **2,060** waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na walipatiwa matibabu. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi na matibabu ya mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi.

Huduma za Chanjo

48. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kutoa huduma za Chanjo kulingana na Sera na Miongozo. Aidha, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa chanjo, imehakikisha kuwepo kwa chanjo za kutosha kwa ajili ya huduma za chanjo nchini kwa watoto na makundi mengine kwa kununua na kusambaza chanjo katika mikoa na halmashauri zote nchini. Mnamo Novemba, 2015 Tanzania ilipata cheti cha kuwa mojawapo ya nchi isiyokuwa na virusi vya ugonjwa wa polio. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutoa chanjo ya polio ili kuendelea kuhakikisha uwepo wa kinga dhidi ya virusi vya polio katika jamii. Vilevile, Wizara ilinunua magari **58** ambayo yaligawanywa katika halmashauri zilizokuwa na uhaba mkubwa wa magari zikiwemo halmashauri mpya. Pia, pikipiki **40** ziligawanywa katika baadhi ya Halmashauri ili kuboresha ufuatiliaji wa magonjwa kwa lengo la kudhibiti milipuko ya magonjwa yanayokingwa kwa chanjo.

49. Mheshimiwa Spika, Wizara ilinunua na kusambaza baiskeli **968** katika halmashauri zote kwa ajili ya kuimarisha huduma za mkoba katika vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa chanjo, ili kuwafikia watoto wote na kuwapatia chanjo (**Kiambatisho Na. 2**). Aidha, vituo **37** vya mikoa ya Geita, Njombe, Tabora, Iringa, Mwanza, Arusha, Dodoma,

Lindi na Manyara vilifungiwa majokofu ya umeme-jua sambamba na utoaji wa mafunzo ya utumiaji wa majokofu hayo, utunzaji wa chanjo na vifaa vya kutolea chanjo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuongeza kiwango cha chanjo hadi kufikia **asilimia 95** na kuongeza kiwango cha utunzaji chanjo kwa kununua majokofu ya kutunzia chanjo hadi **asilimia 90** ya mahitaji kwenye ngazi ya Halmashauri.

Usafi wa Mazingira

50. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira kwa lengo la kuhimiza jamii kujenga na kutumia vyoo bora. Kufuatia uhamasishaji huo, jumla ya kaya **479,011** kati ya kaya **554,000** sawa na asilimia **86.4** ya lengo zimejenga vyoo bora. Idadi hiyo inafanya jumla ya vyoo vyote vilivyojengwa tangu kuanza kwa utekelezaji wa kampeni ya usafi wa mazingira mwaka 2013 kufikia **1,030,817**. Vyoo bora vilivyojengwa mashuleni ni **1,630** na kuvuka lengo la vyoo **812**.

51. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendesha zoezi la usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira ili kuimarisha utekelezaji wa afya katika Mikoa na Halmashauri zote nchini. Katika mwaka 2015/16, zoezi la ufuatiliaji wa Kampeni hiyo lilitokelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza Mikoa 15 ya Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Shinyanga, Geita, Simiyu na Halmashauri zote katika mikoa hiyo ilitembelewa. Awamu ya pili ilihusisha Mikoa mingine iliyobakia ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Mwanza, Kagera na Mara. Aidha, Wizara imeanza hatua za manunuzi ya pikipiki **100** ili kuimarisha ufuatiliaji ngazi ya halmashauri. Vilevile, utekelezaji wa Mfumo wa uhifadhi taarifa za usafi wa mazingira wa kielektroniki umeshaanza kutumika katika mikoa 13 ya majaribio ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Iringa, Njombe, Mbeya, Mwanza, Kagera, Dar es Salaam, Pwani, Dodoma, Mara na Tabora. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira katika mikoa na halmashauri zote nchini. Ni wajibu wa kila halmashauri kuweka mikakati madhubuti ya usafi wa mazingira katika maeneo yake. Wizara inapongeza jitihada za Mheshimiwa Rais, wa awamu ya tano kwa kuweka msisitizo katika usafi wa mazingira. Aidha Wizara inatambua kazi nzuri ya **Mheshimiwa Paul Makonda** Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam kwa kuzindua kampeni ya usafi katika mkoa wa Dar es Salaam.

52. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara iliwahamasisha viongozi wa ngazi ya Mkoa kwa Mikoa ya Kigoma na Dodoma na Halmashauri za Manispaa ya Kigoma na Wilaya ya Kongwa juu ya athari za

kiafya zitokanazo na mabadiliko ya Tabia nchi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendesha mafunzo kwa Watendaji wa Mamlaka ya Maji safi na maji taka Manispaa ya Kigoma na Kikundi cha watumia maji cha Mbande kilichopo katika Wilaya ya Kongwa. Mafunzo hayo yatajenga uwezo wa mamlaka hizo ili ziweze kuchukua hatua stahiki zitakazowezesha upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yao kutokana na athari zinazoweza kutokea na mabadiliko ya mara kwa mara ya Tabia nchi.

53. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuvijengea uwezo vituo vyake vya mipakani **10** kwa madhumuni ya kujikinga na magonjwa yanayotolewa taarifa kimataifa na athari nyingine za kiafya pamoja na kudhibiti wasafiri kuwa na chanjo ya homa ya manjano pale inapotakiwa. Aidha, katika mwaka 2016/17, Wizara itaimarisha udhibiti wa magonjwa mipakani kwa kuhakikisha kuwa chanjo ya homa ya manjano inasimamiwa na pale msafiri anapokutwa hajachanja ipasavyo atachanjwa na siyo kugongewa kitabu. Wizara itaweka adhabu kali kwa wote watoa huduma na wasafiri ambao watakiuka utaratibu huu.

Elimu ya Afya kwa Umma

54. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2015/16, Wizara iliendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kutunza afya zao dhidi ya magonjwa na kufanya uchunguzi wa afya ikiwemo saratani ya tezi dume. Aidha, Wizara ilitayarisha na kusambaza vielelezo vya kuelimisha jamii kuhusu saratani ya tezi dume (vipeperushi **100,000**) na ugonjwa wa kipindupindu (mabango **267,000**; bango kitita **7,000**; vipeperushi **640,000**; DVDs **7000**; CDs **2,000**). Vilevile, kutokana na ugonjwa wa kipindupindu kuathiri takriban nchi nzima, Wizara ilitumia njia za ziada ili kuifikia sehemu kubwa ya jamii zikiwemo mitandao ya kijamii, matangazo kwa njia ya radio (**29**) na televisheni (**7**); huduma za simu bila malipo kupitia nambari 17554 kwa kutuma neno kipindupindu au kupiga simu nambari 117 kuelimishwa au kuongea na mtaalamu. Pia, wahudumu wa afya ngazi ya jamii wapatao **1,070** walijengewa uwezo wa kuhamasisha jamii nyumba hadi nyumba kwa kutumia bango kitita. Wizara ilihakiki vielelezo mbalimbali vilivyotayarishwa na wadau ili kuona iwapo vina ubora unaotakiwa na iwapo vimezingatia Sera na Miongozo ya Wizara. Vielelezo hivyo ni pamoja na vile vya uzazi wa mpango, afya ya uzazi, mama na mtoto, lishe, chanjo, UKIMWI, kifua kikuu, afya ya mazingira, magonjwa yanayoambukiza na yasiyo ya kuambukiza, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, malaria, afya ya kinywa na macho.

55. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya kiafya

kupitia njia zote za mawasiliano ili kuifikia jamii, ikiwemo machapisho, vyombo vya habari, simu za mkononi, njia za asili, mitandao ya kijamii na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ngazi ya jamii ili waweze kufanya uhamashishaji wa nyumba hadi nyumba.

Huduma za Lishe

56. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2015/16, Serikali imevuka lengo la kuhamasisha viwanda vinavyosindika vyakula ili kuongeza virutubishi aina ya vitamini na madini kufikia 21 ikilinganishwa na viwanda 13 mwaka 2014/15. Viwanda vilivyoongezeka ni *Basic Elements Ltd* (DSM), *Sunkist Group Ltd* (Arusha), Mount Meru (Arusha), VOIL Mwanza (Mwanza), GM Medol (DSM) pamoja na viwanda vitatu vya kati vya kusindika mafuta na kuongeza vitamini A vilivyopo Babati na Singida. Serikali pia imeanza kupanua wigo wa kuongeza virutubishi kupitia vinu vya kusagisha unga wa mahindi ngazi ya vijiji, ambapo jumla ya vinu **290** katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Morogoro, Dodoma na Arusha vinasaga mahindi na kuongeza virutubishi vya madini na vitamini.

57. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imenunua tani **93** za virutubishi (Premix) katika mwezi Agosti na mwezi Novemba, 2015. Virutubishi hivyo vilisambazwa kupitia Bohari ya Dawa kwenda wilaya sita zenye mradi wa majaribio wa kuongeza virutubishi katika unga wa mahindi zilizopo Mikoa ya Njombe (Njombe Mji), Iringa (Iringa Vijijini na Kilolo) na Arusha (Meru, Monduli na Karatu). Vilevile, **katoni 805** zenye jumla ya vipaketi **milioni 4.8** zilinunuliwa kwa ajili ya watoto walio na umri chini ya miaka mitano na tayari pakiti **milioni 1.52** zimesambazwa **(Kiambatisho Na. 3)**. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kushirikiana na asasi zisizo za serikali kuhakikisha virutubishi muhimu kwa ukuaji na ufanisi wa mwili vinaendelea kupatikana na kufikia wilaya nyingine nchini.

HUDUMA ZA TIBA

Huduma za Tiba katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda

58. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Taifa Muhimbili** imehudumia jumla ya wagonjwa **299,769**. Kati yao, **256,888** walikuwa wagonjwa wa nje na **42,881** ni wagonjwa waliolazwa. Vilevile, katika kutekeleza mkakati wa Serikali wa kupambana na tezi dume, hospitali iliwafanyia uchunguzi jumla ya wagonjwa **4,054**. Wagonjwawanjewaliopatiwatibaya upasuaji walikuwa **6,021**, mishipa ya fahamu walikuwa **3,855** na waliopatiwa matibabu ya figo walikuwa **10,040**, ikiwemo mizunguko **6,292** ya kusafisha figo. Vitanda vya kulaza wagonjwa vimeongezeka kutoka **1,354** mwaka

2014/15 hadi **1,643** mwaka 2015/16. Aidha, katika mwaka 2016/17, hospitali itaongeza idadi ya vitanda vya wagonjwa mahututi (ICU) kutoka vitanda **21** vya sasa hadi vitanda **75**, itanunua vifaa tiba vya upasuaji na kuongeza vyumba vya upasuaji kutoka **13** vya sasa hadi **18**, itapanua huduma za kusafisha figo kwa kuongeza vitanda kutoka vitanda **15** vya sasa hadi vitanda **50** na kuanza kusafisha figo kwa watu wenye maambukizi ya virusi vya UKIMWI na virusi vya ini. Aidha, hospitali itaanzisha huduma mpya za upandikizaji wa figo (*renal transplant*) na upandikizaji wa “*cochlea*” kwa wagonjwa ambao ni viziwi. Vilevile, hospitali itaboresha huduma za kulaza wagonjwa binafsi na kujenga jengo la kisasa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa binafsi na viongozi wa kitaifa na watu mashuhuri litakalokuwa na jumla ya vitanda **170** na kuongeza mapato ya ndani kutoka shilingi **bilioni 2.6** za sasa hadi shilingi **bilioni tano** kwa mwezi.

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeanzisha **Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete**. Aidha, Taasisi hiyo iliwahudumia wagonjwa **24,570** wa nje na wagonjwa **2,134** waliolazwa. Jumla ya wagonjwa **207** walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo ambapo kati yao, watoto chini ya umri wa miaka 18 walikuwa **178**. Kwa kufanya upasuaji huo hapa nchini, Taasisi imeweza kuhudumia wagonjwa wengi zaidi kuliko ambavyo huduma hii ingepatikana nje ya nchi na kuokoa zaidi ya **shilingi bilioni nne** za Serikali. Vilevile, Taasisi imeanza kupokea wagonjwa kutoka nchi mbalimbali zikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Nigeria na Comoro.

60. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ilifanya uchunguzi kwa wagonjwa wa magonjwa ya moyo **451** kwa kutumia mashine ya kisasa (Cath Lab.). Mashine hiyo inamuwezesha daktari kuweka vyuma maalum ndani ya mishipa ya moyo “*stents*”, mashine za kuendesha moyo (*pacemarkers*) na kuziba matundu bila kupasua kifua. Kati ya wagonjwa **451** waliotibiwa, ni kifo kimoja tu kilitokea. Aidha, Taasisi iliongeza uwezo na uzoefu kwa wataalam wake kupitia kambi zilizohusisha wataalam toka taasisi za nje ya nchi zenye uzoefu wa miaka mingi zaidi katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa moyo na mishipa ya damu. Katika mwaka 2016/17, Taasisi itaendelea kuboresha huduma na kuifanya kuwa kituo cha mafunzo kwa wataalam wa upasuaji wa moyo Afrika Mashariki na Kati. Aidha, Taasisi itaongeza idadi ya kambi za upasuaji wa kibingwa kwa kushirikiana na wataalamu kutoka nje ya nchi. Hii itatoa fursa kwa wataalam wa Taasisi kujifunza zaidi. Katika mwaka 2016/17, Wizara itajengea uwezo Taasisi kwa kuweka vifaa ili chumba cha upasuaji cha 3 kianze kufanya kazi.

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Serikali imeanzisha **Hospitali ya Rufaa Benjamin Mkapa** iliyopo Chuo Kikuu cha Dodoma. Kuanzia Oktoba, 2015 hadi Machi, 2016, Hospitali hiyo iliyopewa

hadhi ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati imehudumia wagonjwa **6,450**. Kati yao, **1,747** ni wagonjwa waliolazwa na **4,520** ni wagonjwa wa nje. Aidha, wagonjwa **183** waliopata huduma ya upasuaji na wanawake **102** waliojifungua.

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, **Taasisi ya Mifupa Muhimbili** (MOI) imehudumia Wagonjwa **81,106**. Katiyaowagonjwa **74,711** walikuwawagonjwa wa nje na **6,395** wagonjwa wa kulazwa. Aidha, Taasisi ilifanya upasuaji mkubwa kwa wagonjwa katika maeneo yafuatayo; ubongo (**278**), uti wa mgongo (**101**), nyonga (**278**), goti (**25**), mifupa mikubwa (**5,827**), vichwa vikubwa kwa watoto (**855**) na pia kuwawekea viungo bandia wahitaji. Taasisi imeweza kushinda tuzo ya mwaka ya utafiti bora Duniani kuhusu upasuaji wa mfupa wa paja kwa mwaka 2015 inayotolewa na Orthopaedic and Trauma Association (OTA) ya San Diego, Marekani.

63. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Taasisi ya MOI itaongeza nafasi ya wagonjwa wanaolazwa kutoka vitanda **150** hadi **340** ambapo katika chumba cha wagonjwa mahututi (ICU) vitaongezeka kutoka vitanda **8** hadi **32**. Katika kujengea uwezo Taasisi, Serikali itanunua mashine mpya za uchunguzi ikiwa ni pamoja na MRI, CT Scan na Digital Xrays. Aidha, Taasisi itatoa mafunzo na upasuaji wa marejeo kwa nyonga na goti. Vilevile, mfumo mpya wa kieletroniki utafungwa ili kuboresha huduma na makusanyo ya maduhuri. Pia, huduma za kibingwa za mkoba (outreach services) zitatolewa katika hospitali za Temeke, Amana - Ilala, Mwananyamala - Kinondoni, Tumbi - Kibaha na Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Morogoro.

64. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Saratani Ocean Road ilihudumia jumla ya wagonjwa **31,075**, kati yao wagonjwa wa saratani walikuwa **17,819** na wagonjwa wa kawaida ni **13,256**. Taasisi iliwafanyia uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti wanawake **5,367**, kati yao **435** waligundulika kuwa na dalili za awali za saratani ya mlango wa kizazi na **149** waligundulika kuwa na dalili za awali za saratani ya matiti.

65. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Saratani kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa mafunzo ya Shahada ya Kwanza ya Tiba ya Saratani kwa Mionzi kwa wanafunzi **27** na Shahada ya Uzamili katika Sayansi ya Tiba ya Saratani kwa wataalamu **13** kwa lengo la kuongeza wataalamu wa kuchunguza, kupima na kutibu saratani nchini. Aidha, Taasisi iliendelea na ujenzi wa "bunkers" kwa ajili ya kuweka mashine mpya za kisasa za kutibu saratani. Utaratibu wa kununua mashine moja ya LINAC unaendelea.

Lengo ni kupunguza mrundikano wa wagonjwa wanaosubiri kwa kipindi cha muda mrefu kupata matibabu ya mionzi.

66. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itaimarisha huduma za kinga na uchunguzi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, kwa kuipatia vifaa vya kisasa vya uchunguzi na matibabu ikiwa ni pamoja na PET/CT Scan, LINAC na MRI. Aidha, Taasisi itaimarisha huduma za mkoba hasa katika maeneo ambayo yanaonekana kuwa na idadi kubwa ya watu waliogundulika kuwa na saratani. Vilevile, Wizara itaimarisha upatikanaji wa dawa kwa wagonjwa wa saratani ambapo asilimia 13 ya fedha za dawa itatumika kununua dawa za saratani ili kupunguza mzigo kwa wagonjwa hasa wa kipato cha chini.

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Mirembe** ilihudumia jumla ya wagonjwa **33,900**, kati yao wagonjwa wa akili **1,926** walilazwa na wengine **31,772** walihudumiwa na kurudi nyumbani. Aidha, wagonjwa wa akili wahalifu wapya **211** walipokelewa na kuhudumiwa kwa mujibu wa sheria katika Taasisi ya Isanga. Vilevile, watumishi wapatao **55** walipatiwa mafunzo ya huduma ya tiba kwa waathirika wa madawa ya kulevya ili waweze kuboresha huduma kwa wagonjwa hao.

68. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa na Hospitali ya Mirembe. Itakarabati miundombinu ya kutolea huduma pamoja na kuweka mfumo wa kieletroniki wa Hospitali kwa awamu ya pili wa WEBERP. Aidha, mafunzo yatatolewa kwa watumishi ili kukidhi mahitaji ya kutoa huduma kwa waathirika wa madawa ya kulevya.

69. Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Kibong'oto ilihudumia jumla ya wagonjwa wa nje **22,348** na wagonjwa **575** wa kifua kikuu walilazwa. Kati ya waliolazwa, waliokuwa na Kifua Kikuu Sugu walikuwa **114** na wagonjwa wa UKIMWI **130**. Aidha, hospitali iliendelea kutoa huduma za usimamizi shirikishi kwa wagonjwa **140** wa Kifua Kikuu Sugu kwa vikoba kutoka katika Mikoa 18. Vilevile, Hospitali ilitoa mafunzo ya kuwahudumia Wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu kwa wataalamu **50** wanaotoka katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, na Hospitali za Rufaa Mbeya na Bugando. Katika mwaka 2016/17, Hospitali ya Kibong'oto itaboresha mifumo ya uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko kwa Kanda ya Kaskazini pamoja na kutoa huduma za mikoba za Kibingwa kwa hospitali zinazotoa huduma za Kifua Kikuu Sugu.

70. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, **Hospitali ya Bugando** imehudumia jumla ya wagonjwa **327,080**. Idadi hiyo ilijumuisha wagonjwa wa nje **291,840** wagonjwa wa ndani **35,240**. Aidha, jumla ya wagonjwa **7,536** walifanyiwa upasuaji na kati yao wagonjwa **88** walifanyiwa

upasuaji wa moyo na kifua, ambapo wagonjwa **12** walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo. Jumla ya wagonjwa **3,392** walipata matibabu ya saratani. Vilevile, Hospitali imefanya upasuaji kwa Wanawake **148** wenye matatizo ya fistula (VVF) na imefanikiwa kununua mashine nyingine ya Varian LINAC ya matibabu ya ugonjwa wa saratani na kufanya mashine za LINAC kuwa **2**. Pia, Hospitali imefunga CCTV Cameras **185** kuimairisha ulinzi na usalama na kununua mashine kubwa ya kufua hewa ya Oksijeni na tayari mabomba yamefungwa kusambaza hewa hiyo kwenye wodi zote **12** zinazohitaji uangalizi wa karibu.

71. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Hospitali ya Bugando itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma ikiwa pamoja na kliniki za wagonjwa wa nje, jengo la saratani, na kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Aidha, Hospitali itafunga mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za hospitali. Vilevile, Hospitali itafunga CT-Scan simulator kwa ajili ya kupanga matibabu na mashine mbili za VARIAN & ELEKTA LINAC kwa ajili ya matibabu ya saratani. Hatua hiyo itasaidia wagonjwa wa saratani wa Kanda ya Ziwa kupata huduma ya matibabu ya mionzi Mwanza badala ya Dar es Salaam.

72. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Hospitali ya Rufaa ya KCMC ilihudumia jumla ya wagonjwa **223,198**. Kati yao wagonjwa wa nje ni **198,799** na wagonjwa wa kulazwa ni **24,399**. Baadhi ya huduma zilizotolewa kwa wagonjwa hao ni pamoja na macho **2,273**, upasuaji kwa njia ya tundu dogo **102**, upasuaji katika mfumo wa mkojo **141** na aina mbalimbali za upasuaji **406**. Aidha, Hospitali ilifanya vipimo vya viashiria vya saratani ya mlango wa kizazi pamoja na matiti kwa wanawake **1,095** ambapo wanawake **29** waligundulika kuwa na saratani ya mlango wa kizazi na walipewa matibabu pamoja na Rufaa kwenda Hospitali ya Ocean Road kwa matibabu zaidi. Vilevile, ujenzi wa jengo la huduma za dharura umekamilika.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Hospitali ya Rufaa KCMC itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za saratani, Kitengo cha moyo na kliniki ya wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Aidha, Hospitali itaendelea kutoa huduma za magonjwa ya ngozi na kufungua wodi mpya za wagonjwa walioungua kwa moto na kemikali. Vilevile, itaanzisha kitengo cha ICU kwa ajili ya watoto na itanunua vifaa vya uchunguzi wa magonjwa vya CT Scan, MRI pamoja na vifaa kwa ajili ya jengo jipya la huduma za dharura.

74. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Hospitali ya Rufaa ya Kanda – Mbeya ilinunua na kufunga mitambo ya upasuaji kwa kutumia tundu dogo na kutoa mafunzo kwa wataalam watakaokuwa

wakitumia mitambo hiyo. Aidha, jumla ya wagonjwa **32** ambao figo zao hazifanyi kazi ipasavyo walihudumiwa kwa damu zao kuchujwa, ambapo zaidi ya mizunguko **1,022** ilifanyika.

75. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Hospitali itaanzisha huduma za upasuaji maalum kwa kutumia tundu dogo. Aidha, Hospitali kwa kushirikiana na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili itaboresha huduma za upasuaji kwa wagonjwa wenye matatizo ya mfumo wa fahamu. Vilevile, Hospitali itaboresha huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wenye matatizo ya figo kwa kuwawekea Arterial Veinosis Fistula wagonjwa wa figo wanaochujwa damu badala ya kutumia njia inayotumika sasa ya Temporal Catheter.

Usimamizi wa utoaji wa Huduma za Tiba Nchini

76. Mheshimiwa Spika, Aidha, katika kuhakikisha Wizara inafanyia kazi kwa wakati na kupunguza malalamiko ya wananchi kuhusu ubora wa huduma, Wizara imetoa maelekezo kwa vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini kuweka utaratibu mwepesi kwa wananchi kufikisha malalamiko yao pindi wanapoona kwamba hawakupatiwa huduma za afya kwa kiwango stahiki. Utaratibu huu unajumuisha uwekaji wa namba za simu za viongozi wa afya wa mkoa, halmashauri pamoja na wasimamizi wa vituo vyote vya kutolea huduma vya umma. Katika mwaka 2016/17 Wizara itaendeleo kuhakikisha vituo vyote vya umma vinaweka namba zao viongozi husika katika eneo la wazi na rahisi kuonekana ili kuwezesha wananchi kutoa malalamiko yao na kupata ufumbuzi mara moja.

77. Mheshimiwa Spika, Vilevile katika mwaka 2016/17 Wizara itaendeleo kupokea malalamiko na kero za wananchi kupitia kituo cha kushughulikia malalamiko kwa huduma za Bima ya afya. Huduma hii ya simu kuanzia sasa itatumika na wananchi wote hata wasio wa wanachama wa Bima ili kutoa kero zao pale ambapo hazikutatuliwa katika ngazi za chini. Simu hiyo ni bure na namba yake ni **08001163**. Aidha, namba hizi zitabandikwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma nchini. Vilevile, Wizara itaimarisha usimamizi wa huduma za tiba Kikanda kwa kuanzisha Madawati maalum ambayo yatasimamiwa na Maafisa Maalum ili kuhakikisha utoaji huduma unasimamiwa kwa karibu na malalamiko yote yanafanywa kazi haraka. Madawati haya yatagawanywa katika Kanda **9** ambazo ni Maalum (Dar Es Salaam), Kusini (Mtwara na Lindi), Mashariki (Pwani na Morogoro), Magharibi (Kigoma na Tabora), Nyanda za Juu Kusini (Iringa, Njombe na Songea), Nyanda za Juu Kusini Magharibi (Mbeya, Songwe, Katavi na Rukwa), Ziwa (Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mara na Mwanza), Kaskazini (Tanga, Manyara, Arusha na Kilimanjaro), Kati (Singida na Dodoma).

78. Mheshimiwa Spika, Katikwa mwaka 2015/16 uongozi wa juu wa Wizara tumekuwa umetembelea vituo vya kutolea huduma za afya kwa lengo kufuatilia utuaji wa huduma kwa wananchi na pia kusikia kero zao. Hadi ya Aprili 2016, hospitali za Rufaa Mikoa yote nchini na baadhi ya hospitali za halmashauri, vituo vya afya na zahanati vimetembeleo. Tumeona mambo mazuri yanayotekelezwa na watoa huduma wetu lakini pia tumeona changamoto kubwa inayoikabili sekta ya afya ikiwemo dawa, upungufu wa watumishi na huduma zisizo kidhi ubora wa huduma.

Huduma za Matibabu kwa Wazee

79. Mheshimiwa Spika; katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu utolewaji wa huduma ya matibabu bure kwa wazee. Katika kutekeleza azma hiyo, vituo vyote vya kutolea huduma za afya katika halmashauri, mikoa na rufaa vimeelekezwa kutenga dirisha maalum kwa ajili ya matibabu ya wazee. Hadi kufikia Machi 2016 jumla ya madirisha ya wazee **24** katika hospitali za mikoa na **133** katika hospitali za halmashauri yametengwa kwa ajili ya matibabu ya wazee. Aidha, mwezi Aprili, 2016, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ilizindua Kampeni ya **Mzee Kwanza**, ili kuhamasisha Jamii kutoa umuhimu na kipaumbele kwa Wazee katika huduma ikiwemo huduma za matibabu. **Kampeni** inasisitiza watoa huduma na wananchi kutoa kipaumbele kwa wazee katika kupata huduma za afya.

80. Mheshimiwa Spika; Wazee ni hazina, hivyo Wizara inaelekeza uongozi wa vituo vya afya vya umma siyo tu kutenga dirisha la wazee bali kuweka sehemu maalum ya kutolea huduma kwa wazee ili kuwapunguzia usumbufu Waganga Wafawidhi wanawajibu wa kuhakikisha kuwa wazee wanapata dawa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuhamasisha halmashauri kuweka utaratibu wa kuwakatia Bima ya Afya ya Jamii (CHF) ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma ya afya kwa kundi hilo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaandaa mkakati wa kuboresha huduma za afya kwa wazee, itaboresha upatikanaji wa takwimu zinazohusu wazee katika ngazi zote za kutolea huduma, itahakikisha kuwa dawa zinazotakiwa kutibu magonjwa yanayowasibu wazee mara kwa mara zinapatikana kwa kutenga fedha maalum kwa ajili ya kununulia dawa hizo na itaboresha sehemu inayoratibu huduma za afya kwa wazee katika ngazi zote

Huduma za uchunguzi

81. Mheshimiwa Spika katika 2015/16, Jumla ya maabara **18** ziliingizwa katika mchakato wa kuinua viwango vya ubora wa huduma za maabara kwa utaratibu wa Shirika la Afya Duniani wa kutoa nyota za ithbati hatua kwa

hatua na kufikia jumla ya maabara **66**. Kati ya hizo, maabara **25**, zimefikia viwango vya ubora wa nyota 1 hadi 3. Aidha, Wizara iliendelea kusimamia utoaji wa ithibati kwa viwango vya kimataifa (ISO 15189) kwa Maabara za ngazi ya Taifa na Kanda. Maabara ya KCMC ilipewa ithibati mwezi Julai, 2015 na kufanya jumla ya maabara za Afya zenye ithibati ya kimataifa kuwa tano (5); ambazo ni Maabara ya Taifa ya Uboora na Mafunzo (NHLQATC), Bugando, Mbeya Rufaa na Muhimbili.

82. Mheshimiwa Spika katika 2016/17, Wizara itaendelea kuboresha na kuimarisha viwango vya ubora wa huduma za maabara ngazi ya mikoa, wilaya na Vituo vya Afya, kwa utaratibu wa Shirika la Afya Duniani, wa kutoa Ithibati hatua kwa hatua, kwa kutoa nyota za viwango vya ubora wa huduma za maabara. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia na kuimarisha huduma za Maabara za Afya za Jamii kwa kuifanya Maabara ya Taifa ya Afya za Jamii kutambuliwa kisheria na kuwa Taasisi inayojitegemea kwa kuanza ujenzi wa maabara hiyo katika eneo la Mabibo, Dar es salaam.

83. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuboresha huduma za uchunguzi kwa kufanyia matengenezo na kununua vifaa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika mwaka 2015/16, mashine mpya za kisasa za radiolojia za CT scan, Digital X-Ray na Ultrasound zimefungwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Aidha, Mafunzo ya matengenezo na matumizi ya vifaa tiba yalitolewa kwa wataalam **30** wa ufundi wa vifaa tiba toka katika hospitali za Halmashauri, Mikoa na Karakana za Kanda ili kuwaandaa kuweza kufanya matengenezo ya vifaa katika maeneo yao.

84. Mheshimiwa Spika katika 2016/17, Wizara itaboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa njia ya mionzi kwa kutekeleza Mradi mpya wa ORIO. Mradi huo utaboresha huduma za radiolojia kwenye jumla ya hospitali **37** ambapo kati ya hizo hospitali **7** ni za Wilaya, **23** za Rufaa za Mikoa na **7** za Kanda na Taifa. Mradi huo utahusisha uboreshaji wa huduma za uchunguzi wa radiolojia kwa wagonjwa, wanawake wajawazito, na watoto chini ya miaka 5 katika hospitali husika. Aidha, Wizara itatoa vifaa tiba, itakarabati majengo na miundo mbinu, itatoa mafunzo maalum kwa watumiaji na wahandisi/mafundi wa vifaa tiba na pia mpango wa matengenezo kinga ambao utatekelezwa kwa miaka 5. Kwa kuwa sehemu kubwa ya tiba ni uchunguzi, Wizara inazielekeza halmashauri kuweka kipaumbele katika kuboresha huduma za uchunguzi kwa kununua vifaa ikiwemo x-ray, ultrasound kwa ajili ya hospitali za wilaya na vituo vya afya.

Huduma za Damu Salama

85. Mheshimiwa Spika katika 2015/16, Wizara iliendelea kusimamia na kuimarisha huduma za Damu Salama. Jumla ya chupa **71,600** kati ya chupa **140,000** zilizokusudiwa kwa mwaka sawa na asilimia **51** zilikusanywa. Aidha, Wizara, imewajengea uwezo watumishi watatu katika kila Halmashauri za mikoa 12 ya Kagera, Simiyu, Mara, Kigoma, Pwani, Mbeya, Dar es Salaam, Manyara, Lindi, Arusha, Katavi na Rukwa ili waweze kukusanya damu. Katika 2016/17, Wizara itakamilisha ujenzi wa vituo vya kukusanya damu salama katika mikoa ya Iringa, Simiyu, Mara, Geita na Mwanza. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha halmashauri zote kusimamia zoezi la ukusanyaji na uhifadhi wa damu. Ninatoa rai kwa wananchi kuchangia damu.

Huduma za kinywa

86. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara ilitengeneza vipeperushi na mabango ya kufundishia elimu ya afya ya kinywa mashuleni na kutoa elimu hiyo katika shule za msingi zilizopo katika majiji ya Mwanza (Nyamagana), Tanga na Mbeya. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza mashine nne (4) za kutibia meno ambazo zimefungwa katika hospitali tatu (3) za rufaa za mikoa ya Mtwara, Dar es salaam (Amana) na Kagera, na pia hospitali ya Mgulani JKT. Vilevile, Wizara ilifanya matengenezo ya vifaa na mashine za kutibia meno katika kliniki za meno zilizopo katika hospitali za rufaa za mikoa ya Dodoma, Mtwara, Dar es salaam (Amana na Temeke), Iringa, hospitali ya Mbagala Rangi Tatu (Dar es salaam) na Chuo cha Tabibu Meno Tanga.

87. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha huduma za tiba ya kinywa na meno, katika mwaka 2016/17, Wizara itanunua jumla ya mashine nne (4) za kutibia meno na kuzisambaza katika hospitali za rufaa za mikoa ya Shinyanga, Mwanza na Tanga, na Hospitali ya Rufaa ya Mbeya. Aidha, Wizara itafanya matengenezo kinga ya vifaa na mashine za kutibia meno katika kliniki za meno za mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Mwanza na Tanga. Vilevile, katika kuboresha huduma za kinga kwa magonjwa ya kinywa na meno, Wizara itaendelea kutekeleza mpango wake wa kuboresha elimu ya afya ya kinywa na meno mashuleni katika majiji ya Mbeya, Mwanza na Tanga. Mpango huo umelenga kuongeza uelewa kwa watoto wa shule juu ya kujikinga na magonjwa ya kinywa na meno.

Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

88. Mheshimiwa Spika, kati a mwaka 2015/16, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Dawa za Asili Muhimbili- MUHAS ilitoa mafunzo kwa waganga wa tiba asili na tiba mbadala **25** kuhusu namna bora ya kutengeneza dawa za asili. Aidha, wanafunzi **59** wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa walipata mafunzo kuhusu Tiba Asili, Tiba Mbadala, Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Taaluma hiyo. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya Tiba Asili na Tiba Mbadala. Aidha, Wizara inasisitiza juu ya wamiliki wa vyombo vya habari kuhakikisha matangazo yote ya Tiba Asili na Tiba Mbadala yanayotolewa katika vyombo vyao yameidhinishwa na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala. Wizara inaangalia uwezekano wa kurekebisha sheria ili kufuta matangazo ya Tiba Asili na Tiba Mbadala.

HUDUMA ZA DAWA

89. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika suala zima la upatikanaji wa dawa kwa kununua, kutunza na kusambaza dawa, vifaa, vifaa ti na vitendanishi kati a vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, kati a kuhakikisha upati anaji wa dawa kati a hospitali za rufaa za kitaifa, kanda na za mikoa unaboreshwa, Serikali imefanya mapiti ya kina ya mfumo wa ununuzi, utunzaji na usambazaji kati a Bohari ya Dawa kwa lengo la kuimarisha upati anaji wa dawa.

90. Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa nyezo ijulikanayo kama *PilferageTool* itakayotumika kufanya ukaguzi wa upotevu wa dawa unaosadikika kutokea kuanzia mzigo unapoingia bandarini mpaka kumfikia mgonjwa au mtumiaji wa mwisho. Nyezo hiyo iko katika hatua za majaribio na itaanza kutumika hivi karibuni. Pia, katika kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinapata dawa kwa wakati, Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi **420** kutoka hospitali **140** kuhusu uagizaji wa dawa kutoka Bohari ya Dawa kwa njia ya kielektroniki. Katika mwaka 2016/17, hospitali **117** zilizobaki zitapatiwa mafunzo hayo. Wizara itatoa mafunzo, kusambaza na kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa ufanisi wa kazi kupitia mfumo wa 5S Kaizen TQM ili kuimarisha usimamizi wa takwimu za dawa.

91. Mheshimiwa Spika, Ili kuepuka kulipa kodi na tozo zilizo juu kutokana na misaada inayoletwa nchini bila ya kuwa na utaratibu maalumu wa kupokea misaada hiyo, Wizara yangu imefanya mapitio ya Mwongozo wa Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi vya msaada *Donation*

Guideline ya mwaka 1995 ili uendane na hali halisi ya sasa. Mwongozo huo upo tayari na umeanza kutumika.

92. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Bohari ya Dawa imewashirikisha washitiri binafsi **13** katika kanda za Dar es Salaam, Mbeya, Iringa, Moshi, Mtwara na Dodoma. Ushirikishwaji wa washitiri binafsi umesaidia kuongezeka kwa upatikanaji wa dawa. Aidha, Bohari ya Dawa imempata mtaalam mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa mikataba mahususi ya kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya uzalishaji wa dawa nchini. Vilevile, Bohari ya Dawa inatumia mfumo wa kufupisha mzunguko wa usambazaji wa dawa kwa kutumia king'atuzi cha *Supply Chain Guru*.

93. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Bohari ya Dawa itaboresha upatikanaji wa dawa kwa vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuzipa uwezo zaidi Bohari za kanda kujiendesha kimkakati. Hatua hiyo, itaenda sambamba na utumiaji wa washitiri wakubwa na ufungaji wa mfumo wa kompyuta wa kusajili dawa kwa kutumia **Bar Code** katika maghala yake yote. Lengo ni kuongeza ufanisi katika utunzaji na usambazaji wa dawa nchi nzima. Aidha, katika kupunguza fedha za uendeshaaji wa Bohari ya Dawa, jumla ya mita za mraba **11,433** ambazo zilikuwa zimekodishwa kwa gharama kubwa zitaachiwa, baada ya **Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli** kuiwezesha MSD kupata kiwanja chenye ukubwa wa **hekari tano** eneo la Luguruni, Dar es Salaam. Mkakati huo wa kutopanga maghala hayo utaokoa takribani shilingi **bilioni nne na nusu** kwa mwaka.

94. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Bohari ya Dawa itaendelea kufungua maduka ya dawa katika hospitali **10** nchini kwa kushirikiana na hospitali husika. Aidha, Bohari itaendelea kuendesha maduka ya dawa katika hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa Mbeya, Sekou Toure, Mount Meru na Wilaya ya Chato ili yawe mfano katika uendeshaaji maduka ya kutolea huduma za dawa katika hospitali zote nchini. Vilevile, Bohari itaanza kununua dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji. Hatua hiyo itawezesha upatikanaji wa dawa nyingi zaidi kwa gharama nafuu.

HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA

95. Mheshimiwa Spika, katika mwaka, 2015/16, Wizara imetayarisha Mpango Mkakati kwa ajili ya huduma za Uuguzi na Ukunga. Lengo la Mpango huo ni kutoa dira ya huduma za Uuguzi na Ukunga nchini. Aidha, Wizara, imetayarisha mwongozo wa usimamizi shirikishi unaojumuisha suala la utoaji mafunzo kazini. Katika mwaka, 2016/17, Wizara

itaandaa mwongozo utakaoelekeza mahitaji halisi ya wauguzi na wakunga kwa kila aina ya Kituo cha kutolea huduma za afya pamoja na aina ya huduma inayotolewa.

UHAKIKI UBORA WA HUDUMA ZA AFYA

96. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia ubora wa huduma za afya zinazotolewa nchini. Katika mwaka 2015/16, Wizara imefanya tathmini ya ubora wa huduma katika vituo vyote vinavyotoa huduma za afya ya msingi katika mikoa **20** ya Geita, Kigoma, Mara, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Dar es Salaam, Pwani, Singida, Tanga, Manyara, Tabora, Rukwa, Mtwara, Lindi, Morogoro, Ruvuma, Dodoma na Katavi. Vituo vilivyofanyiwa tathmini vimepewa hadhi ya nyota kulingana na ubora wa huduma zinazotolewa. Jumla ya vituo **5,235** vimefanyiwa tathmini, kati ya vituo hivyo, vituo **2,016** sawa na asilimia 38.51 vimepata nyota sifuri (0), vituo **2,583** sawa na asilimia 49.34 vimepata nyota moja, vituo **561** sawa na asilimia 10.72 vimepata nyota mbili, vituo **68** sawa na asilimia 1.30 vimepata nyota tatu na vituo **vitano** sawa na asilimia 0.10 vimepata nyota nne. Lengo ni kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya vituo vilivyofanyiwa tathmini vinapata nyota 3 au zaidi ifikapo mwezi Juni, 2018. Aidha, tathmini iliyofanywa imeonesha kuwa vituo vinahitaji maboresho ili kutoa huduma stahiki na mipango ya maboresho hayo kwa kila kituo imeandaliwa na kuanza kutekelezwa kwa kutumia Timu za Uendeshaji Afya za Halmashauri.

97. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya usimamizi shirikishi katika mikoa yote **26** ili kuhakikisha huduma za afya zinazotolewa kwenye vituo zinazingatia viwango na miongozo mbalimbali inayotolewa na Wizara. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mipango ya uimarishaji wa utoaji wa huduma bora katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kwa kufanya usimamizi shirikishi na kufanya tathmini ya marudio. Vilevile, Wizara itafanya ukaguzi maalumu wa huduma za afya kwenye vituo endapo kutakuwa na taarifa za kuwepo na ukiukwaji wa maadili na taratibu za utoaji huduma.

98. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imetoa mafunzo ya kukabiliana na Dharura na Maafa kuhusu huduma za dharura kwa majeruhi wengi kwa wataalamu wa afya katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, Tanga, Mbeya na Iringa. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma za afya katika dharura na majanga yaliyotokea hapa nchini yakiwemo mafuriko na ajali za barabarani.

99. Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kipindupindu umedumu kwa takriban miezi 7 kuanzia mwezi Agosti, 2015, ambapo hadi Aprili, 2016, jumla ya

waathirika **21,059** waliugua ugonjwa huo, na kati yao watu **331** wamepoteza maisha. Hadi sasa ni mikoa miwili tu ya Njombe na Ruvuma ambayo haijaathiriwa na ugonjwa huo. Katika kukabiliana na ugonjwa huo, Wizara imeimarisha uratibu na utoaji dawa, vifaa na wataalamu kwenda katika mikoa iliyoathirika kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya juu ya kukabiliana na ugonjwa huo. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya vyoo, usafi wa mazingira na umuhimu wa kutumia maji safi na salama.

100. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara kwa kupitia mabaraza ya taaluma ilisimamia maadili na kusajili wataalam waliokidhi viwango vya kutoa huduma za afya nchini. Mabaraza hayo ni pamoja na Madaktari na Madaktari wa Meno, Uuguzi na Ukunga, Famasia, Maabara, Upeo wa Macho Kuona na Afya ya Mazingira. Kupitia usajili unaofanywa na mabaraza mbalimbali ya afya, jumla ya wataalam **54,834** wa kada mbalimbali za afya walisajiliwa. Wataalam hao wakiajiriwa watapunguza pengo lililopo la mahitaji ya watumishi nchini. Aidha, ili kuongeza idadi ya wataalam katika sekta ya afya, Wizara imesajili vyuo **8** vya mafunzo ya uuguzi na ukunga na vyuo **viwili** vya Famasia katika ngazi ya cheti (astashahada)

101. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imewasajili waganga wa tiba asili na tiba mbadala **2,935** kutoka mikoa yote nchini na hivyo kufikisha waganga **10,958** waliosajiliwa. Hii ni hatua muhimu katika kutokomeza vitendo vya ukatili na mauaji dhidi ya watu wenye ualbino, wazee na watoto wachanga vinavyochochewa na imani hatarishi za kishirikina/uchawi. Aidha, Baraza lilifanya ufuatiliaji wa huduma za tiba asili katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Geita, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Kagera, Mtwara na Lindi na kutoa elimu kuhusu Sheria, Kanuni, Miongozo mbalimbali kwa waratibu **75** wa mikoa hiyo pamoja na baadhi ya waganga **890** wa tiba asili.

102. Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi nchini, imeendelea kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa kusajili vituo mbalimbali vinavyotoa huduma za afya. Katika mwaka 2015/16, Wizara kupitia Bodi ya Ushauri ya Uongozi wa Hospitali Binafsi ilisajili vituo vya kutolea huduma za afya **36**, Makampuni na Mashirika **14** yasiyo ya Kiserikali yalisajiliwa kutoa huduma za Afya, hivyo kufikia jumla ya vituo **1,927** kati ya vituo **7,285** vya kutolea huduma za afya. Vituo hivyo binafsi ni sawa na asilimia **26.45** ya vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Wizara kupitia Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ilisajili maabara binafsi za afya **60**, hivyo kufikia jumla ya maabara binafsi **647** kati ya maabara **4,852**. Maabara binafsi ni sawa na asilimia **13.33** ya maabara zote za kutolea huduma za afya nchini. Vilevile, Baraza la

Uuguzi na Ukunga limesajili vituo vipya **12** vya huduma binafsi za uuguzi na ukunga na hivyo kufikisha jumla ya vituo kuwa **90**.

103. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Baraza la Famas limesajili Maduka ya Dawa Moto 163 na kufikia jumla ya maduka ya dawa moto 1,104, Maduka ya Dawa Muhimu (ADDO) 770 na kufanya jumla ya ADDO nchini kuwa 9,100. Serikali imezingatia umuhimu wa kusogeza huduma za upatikanaji wa dawa kupitia sekta binafsi karibu na wananchi. Baraza la Optometria limesajili optometri kliniki 12, na vituo vya kutengeneza miwani tiba vinne na duka moja linalouza vifaa vya Optometri. Jumla ya kliniki za Optometri katika hospitali za umma ni 87, hospitali binafsi ni 146 na hivyo kufikia vituo 233 na maduka yanayouza vifaa vya Optometri kuwa **tisa**.

URATIBU, UFUATILIAJI NA UGHARAMIAJI HUDUMA ZA AFYA

Uratibu na Ufuatiliaji Huduma za Afya

104. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha ushirikishwaji wa wananchi na uwajibikaji katika kutekeleza vipaumbele vya sekta ya afya, Wizara imeendelea kutekeleza utaratibu wa kufanya tathmini shirikishi kwa kutumia nyenzo ya kijamii (Community Score Card) kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji ili kuboresha kiwango cha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi. Tathmini hiyo imeendelea kufanyika katika zahanati na vituo vya afya vya Serikali vya Halmashauri za Wilaya **23** za Mikoa ya Shinyanga (4), Mwanza (5) Geita (5), Simiyu (5) na Pwani (4) **(Kiambatisho Na. 4)**

105. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha dhana ya utawala bora inazingatiwa katika sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imefanya usimamizi shirikishi katika Bodi **44** za Halmashauri za Huduma za Afya. Usimamizi huo ulizingatia uwepo wa Hati Rasmi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Bodi na kamati za usimamizi za vituo vya afya.

106. Mheshimiwa Spika, Wizara imeboresha upatikanaji wa takwimu za afya kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, ikiwa ni pamoja na kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kutoa taarifa za vituo vya afya nchini yaani "Health Facility Registry". Mfumo huo unamuwezesha mwananchi kupata taarifa za sifa ya kituo, huduma zinazotolewa, taarifa za kijografia, na aina ya kituo. Taarifa hizo zinapatikana kwa njia ya mtandao kwa anuani ya ehealth.go.tz. Wizara pia, imezindua mtandao wa kutoa taarifa za takwimu za afya kupitia anuani ya hmisportal.moh.go.tz.

107. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kutekeleza mkakati wa ehealth strategy 2013-2018. Katika mwaka 2015/16, Wizara imesambaza mwongozo wa ufungaji wa mfumo wa kielektroniki na miundombinu yake katika Hospitali na Vituo vya Afya. Mwongozo huo unatoa maelekezo kuhusu sifa, ubora na viwango ambavyo mfumo wa kielektroniki unatakiwa kukidhi. Aidha, Wizara ilikamilisha kufunga mfumo wa kielektroniki katika Hospitali Maalumu ya Kibong'oto, Mirembe na hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Amana, Ndanda, Lindi na Mount Meru. Vilevile, Wizara imekamilisha kutengeneza mfumo wa kielektroniki wa kuandaa mipango na matumizi katika halmashauri unaojulikana kama "centralized web based PlanRep" na kukamilisha kufanya tathmini ya tiba mtandao (telemedicine) katika hospitali saba za Bagamoyo, Amana, Mwananyamala, Hydrom, Tumbi, KCMC na Hospitali ya Taifa Muhimbili zilizokuwa katika majaribio ya kutoa huduma hiyo.

108. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya tathmini ya mfumo iliyofungwa ya kielektroniki ya kukusanya mapato na taarifa za hospitali katika hospitali za rufaa za Kanda, Mikoa na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa mfumo hiyo inakidhi viwango, sifa na ubora kwa mujibu wa miongozo ya Wizara yangu na Wakala wa Serikali Mtandao (eGA). Tathmini hiyo itawezesha Wizara kutoa bei elekezi ya kufunga na kuendesha mfumo ya kielektroniki ili kuhakikisha mfumo hiyo haiongezi gharama kwa mgonjwa na kuboresha huduma.

109. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2016/17, Wizara itafunga mfumo wa kielektroniki unaoitwa "*Integrated Health Facility Management Information System*" (iHMIS) katika Taasisi ya Huduma ya Mifupa Muhimbili (MOI), Hospitali ya Benjamin Mkapa (Dodoma), hospitali za rufaa za mikoa ya Tabora (Kitete), Singida, Tanga (Bombo), Mtwara (Ligula), Mwananyamala na Temeke. Aidha, Wizara itakarabati vifaa vya tiba mtandao (telemedicine) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za kanda Bugando, KCMC na Mbeya, hospitali za rufaa za mikoa za Mwananyamala, Temeke, Amana, Tumbi na Hospitali ya Halmashauri ya Bagamoyo. Vilevile, Wizara itaanzisha mfumo wa kielektroniki wa kutumia simu ya kiganjani (mHealth) kwa wananchi ili kutoa taarifa za ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Ugharamiaji wa Huduma za Afya

110. Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa Mkakati wa Ugharamiaji huduma za afya ambao una lengo la kutafuta vyanzo mbalimbali vya uhakika vya kuongeza rasimali fedha katika Sekta. Nia ni kuhakikisha kuwa wananchi wote wanapata huduma za afya bila kuwa na kikwazo cha fedha pindi wahitajipo huduma za afya.

111. Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaelekeza kuwa wananchi wote wapate huduma za afya bila kikwazo cha fedha wala kujali hali yao ya kiuchumi katika jamii. Aidha, Sera imesisitiza uwepo wa vyanzo vya fedha vinavyoaminika pamoja na kuhakikisha sekta ya afya inapata raslimali za kutosha za kugharamia huduma za afya. Katika kutekeleza matakwa ya Sera hiyo, Wizara imekuwa ikibuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa wanufaika wa bima ya afya. Hadi kufikia Desemba 2015, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Jamii (CHF) ulikuwa unahudumia jumla ya **wanufaika 11,729,281** sawa na asilimia **27** ya Watanzania wote kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012. Kati ya hao wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii ni **8,390,526** na wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni **3,338,755** (**Kiambatisho Na. 5**). Mafanikio haya yametokana na juhudi mbalimbali za kuhamasisha jamii kujiunga na huduma za Mfuko hiyo zilizowezesha kuongezeka kwa wanachama walioandikishwa kutoka makundi mbalimbali kama; vikundi vya wajasiriamali na ushirika, wanafunzi, Taasisi za kidini, na mashirika binafsi.

112. Mheshimiwa Spika, huduma za Mfuko kwa wanachama wake zimeendelea kuboreshwa, Hadi tarehe 31 Desemba, 2015 Mfuko umeanzisha kituo cha huduma kwa wateja (**Simu na 0800 110063 bila malipo**). Huduma hiyo itawawezesha wananufaika kutoa kero na maoni yao kwa mfuko kwa haraka na bila kikwazo cha malipo. Aidha, Mfuko umevilipa vituo vilivyotoa huduma kwa wanufaika wa Mfuko kiasi cha **shilingi 101,772,424,344.00** (**Kiambatisho Na. 6**). Vilevile, Mfuko umeanza kutoa kwa mara ya kwanza, huduma za upasuaji wa moyo na uzibuaji wa mishipa ya damu kwa wanachama wa Mfuko katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete. Fao hilo limewezesha kupunguza idadi ya wagonjwa wanaoenda nje ya nchi na kuimarisha matibabu ya ndani. Aidha asilimia 80 ya kazi za uendeshaji wa Mfuko zinafanywa kupitia mifumo habari (TEHAMA) iliyosaidia sana utambuzi wa wanachama kabla ya kupata huduma na kuwalipa watoa huduma kwa wakati kwa mujibu wa Sheria.

113. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango wa Afya ya Jamii Mijini –Tiba kwa Kadi (TIKA), Halmashauri za Manispaa za Tabora, Kigoma Ujiji na Morogoro; Halmashauri za miji midogo za Kibaha, Kasulu, Geita, Mpanda, Njombe, Makambako na Babati zimeanzisha huduma ya Tiba kwa Kadi. Aidha, Halmashauri za Uvinza, Buhigwe, Itigi na Mkalama zimeridhia uanzishwaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na hivyo kufanya jumla ya halmashauri zote zinazotekeleza huduma ya Mfuko wa Afya ya Jamii CHF/TIKA kufikia **151** kati ya **182**. Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na kwa kushirikiana na Wadau, imeendelea kuuboresha Mfuko wa Afya ya Jamii kwa lengo la kuongeza ufanisi wake na huduma zake kwa wananchi kugharamia huduma za matibabu kwa Watoto wenye umri chini

ya miaka 18 bila kuangalia uhusiano uliopo kati ya mtoto na mchangiaji. Hatua hiyo inakusudia kuongeza wigo wa walengwa na kuwawezesha watoto walio katika familia kubwa au wanaolelewa na walezi nje ya wazazi wao ikiwemo wale wanaoishi katika mazingira magumu kupata huduma za Mfuko.

114. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, utafanya Tathmini ya Tano ya Uhai wa Mfuko (*Actuarial Valuation*), ili kuangalia uwezo wa Mfuko kuhimili utoaji wa huduma kwa kipindi kirefu kijacho. Maandalizi ya kazi yamekwisha anza na moja kati ya Hadidu Rejea itakuwa ni kuangalia namna bora ya kuunganisha huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, utaanza kugharamia huduma za matibabu kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 bila kuangalia uhusiano uliopo kati ya mtoto na mchangiaji. Hatua hiyo inakusudia kuongeza wigo wa walengwa na kuwawezesha watoto walio katika familia kubwa au wanaolelewa na walezi nje ya wazazi wao ikiwemo wale wanaoishi katika mazingira magumu kupata huduma za mfuko.

115. Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa Waheshimiwa wabunge wote, kwa nafasi zao na ushawishi mkubwa walionao katika jamii tunayoishi, kuendelea kuwaelimisha wananchi wote umuhimu wa kujiunga na bima ya afya. Aidha, naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inatarajia kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Bima ya Afya. Muswada huo una mapendekezo mbalimbali ikiwemo sharti la ulazima wa wananchi wote kujiunga na Bima ya Afya na wale wote wenye uwezo kuchangia bima hiyo. Ni mategemeo yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtaunga mkono jitihada hizo za Serikali na kupitisha Muswada huo pindi utakapowasilishwa.

116. Mheshimiwa Spika, Wizara imeanzisha mfumo wa kuimarisha sekta ya afya kwa kuvipatia fedha vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kulingana na ubora wa huduma wanazozitoa kwa wananchi. Mpango huo unaitwa malipo kwa ufanisi (Results Based Financing - RBF). Lengo ni kuviwezesha vituo kupata fedha za kuboresha utoaji wa huduma na vilevile kutoa motisha kwa watumishi kutokana na utendaji wao. Utekelezaji wa Mpango huo ulianza katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mwaka 2015 ambapo kuanzia Januari 2016 Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga zimeshaingizwa katika mpango huo na Mkoa wa Mwanza umeanza utekelezaji Aprili 2016. Aidha, Mfumo huo umeanza kuonesha manufaa katika vituo husika kwa kuongezeka kwa utumiaji wa huduma za afya za msingi na ubora wa utoaji wa huduma hizo. Uboa huduma umeongezeka kutoka **asilimia 48** hadi **64** kwa kipindi cha Aprili hadi Desemba 2015 kwa Halmashauri ya Kishapu.

117. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kuingiza mikoa mingine minne katika Mpango wa RBF. Mikoa hiyo ni Pwani, Simiyu, Tabora na Kigoma. Mikoa hiyo imepewa kipaumbele kutokana na mahitaji makubwa yaliyobainishwa na viashiria vya afya katika Mikoa hiyo. Hata hivyo, Mikoa mingine itaendelea kuongezwa katika utaratibu huo kulingana na upatikanaji wa fedha.

UDHIBITI WA KEMIKALI NCHINI

118. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2015/16, Wakala imepata ithibati ya maabara kwa kiwango cha kimataifa cha "ISO 17025:2005" ya Maabara ya Uboru wa Vyakula kwa vigezo vya SADCAS na imekarabati jengo la Kanda ya Mashariki lililopo makao makuu Dar es Salaam, hivyo kuimarisha uwezo wa nchi katika kufanya uchunguzi wa uboru wa vyakula. Katika mwaka 2016/17, Wakala itakamilisha zoezi la kupata hati ya ithibati ya maabara katika kiwango cha kimataifa cha "ISO 17025:2005" kwa maabara ya vinasaba vya binadamu (DNA).

119. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilipokea jumla ya sampuli **4,121** zilizofanyiwa uchunguzi na matokeo kutolewa. Sampuli zilizochunguzwa ni za vyakula, dawa, kemikali, maji na maji taka, bidhaa za viwandani na mazingira, za makosa ya jinai na matatizo ya kijamii. Aidha, Wakala ilitoa elimu kwa wadau **359** kutoka katika taasisi mbalimbali nchini zikiwemo za sekta binafsi juu ya taratibu sahihi za uingizaji, utunzaji, na usafirishaji wa kemikali pamoja na matumizi salama ya kemikali ili kulinda afya na mazingira. Wadau **402** wanaohusika na biashara ya kemikali walisajiliwa na maeneo **650** yalikaguliwa. Vilevile, Wakala ilitoa mafunzo kwa wadau **56** ya kukabiliana na ajali zinazohusika na Kemikali.

120. Mheshimiwa Spika, Aidha, Wakala ilifanya ukaguzi wa mizigo ya kemikali 14,578 iliyopita katika bandari, bandari kavu, na viwanja vya ndege ambapo mizigo iliyokidhi viwango iliruhusiwa kuingia nchini. Katika mwaka 2016/17, Wakala itaendelea kufanya ukaguzi wa mizigo ya kemikali inayoingia nchini.

UDHIBITI WA UBORA WA CHAKULA, DAWA, VIPODOZI NA VIFAA TIBA

121. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Chakula na Dawa imeendelea kudhibiti usalama na uboru wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kukagua maeneo **6,896** yanayohusika na uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hizo ambapo maeneo **4,515** sawa na asilimia **65** yalikidhi vigezo. Maeneo yaliyokaguliwa ni pamoja na ya kusindika chakula na sehemu **3,718** za kuuzia chakula; maduka **954** ya dawa; vituo

vya afya **414**; maduka **1,406** ya vipodozi; maduka **316** ya vifaa tiba; viwanda **70** vya dawa nje ya nchi; viwanda **12** vya dawa vya ndani; na viwanda **6** vya vipodozi. Maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya Sheria, wamiliki walielekezwa kufanya marekebisho husika ndani ya muda maalum.

122. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2015/16 Mamlaka ya Chakula na Dawa ilisajili na kuhusha vibali vya maeneo **3,186** ya kufanyia biashara za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Aidha, Mamlaka ilitathmini maombi **4,207** ya kusajili bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ikiwa ni sawa na **asilimia 85** kati ya maombi **5,083** yaliyopokelewa. Jumla ya maombi **2,747** sawa na asilimia **65** ya maombi yote yaliyofanyiwa tathmini yalisajiliwa. Vilevile, Mamlaka ilitoa vibali **5,705** vya kuingiza bidhaa nchini na **1,179** vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi.

123. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilisimamia uteketezaji wa bidhaa ambazo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Jumla ya tani **226.8** zenye thamani ya **Shilingi 1,983,230,330** ziliteketezwa ambapo vipodozi ni tani **66.8** sawa na asilimia **29.5**; vyakula ikijumuisha pombe bandia aina ya viroba tani **145.37** sawa na asilimia **64.1**; dawa tani **14.48** sawa na asilimia **6.4** na vifaa tiba tani **0.15** sawa na asilimia **0.1**. Aidha, Mamlaka ilichunguza sampuli **2,736** za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo sampuli **2,567** ikiwa ni sawa na asilimia **94** zilikidhi viwango vya ubora na usalama. Bidhaa zote ambazo hazikukidhi viwango aidha zilizuliwa kuingizwa nchini au zile zilizokutwa sokoni ziliondolewa na matumizi yake kusitishwa. Pia, Mamlaka iliendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kupitia radio, luninga, magazeti na mikutano. Jumla ya vipindi **22** vya radio na luninga vilirushwa hewani na mikutano ya wazi **29** ikihusisha makundi mbalimbali ikiwemo wanafunzi wa vyuo na mashuleni ilifanyika.

124. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Mamlaka itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kudhibiti ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba nchini. Aidha, Mamlaka itaimalisha matumizi ya mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kuboresha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na kufuatilia malalamiko ya wateja, kuyapatia ufumbuzi na kutoa mrejesho kwa wakati. Pia, elimu kwa umma itaendelea kutolewa kwa lengo la kujenga uwezo wa wananchi kutambua bidhaa duni na bandia na hivyo kutoa mchango katika udhibiti. Vilevile, Mamlaka inatarajia kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la Ofisi na Maabara ya Kanda ya Ziwa katika jiji la Mwanza lengo likiwa ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

UTAFITI WA MAGONJWA YA BINADAMU

125. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu iliendelea na utafiti unaolenga kubaini kiwango cha maambukizi ya kichocho na minyoo ya tumbo katika Wilaya za Rorya na Butiama mkoani Mara. Matokeo ya awali yanaonesha kwamba ugonjwa wa kichocho cha tumbo ni tatizo kubwa la kiafya katika wilaya zote mbili. Katika mwaka 2016/17, Taasisi itafanya utafiti utakaotathmini kama chanjo moja dhidi ya virusi vinavyosababisha saratani ya shingo ya kizazi (Human Papilloma Virus, (HPV)) itakuwa na uwezo wa kutengeneza kinga mwilini sawa na chanjo mbili au tatu. Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti wa awali wa kuangalia ubora na usalama wa chanjo dhidi ya virusi vya Ebola. Vilevile, Taasisi kwa kushirikiana na Kikundi cha Kudhibiti UKIMWI mkoani Tanga (TAWG), itafanya majaribio juu ya ubora na usalama wa dawa asili aina ya TASHACK ya tiba ya UKIMWI ambayo imeboreshwa na kutengenezwa kiwandani.

B: MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Maendeleo ya Jamii

126. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Wizara yangu iliendelea kuratibu utekelezaji wa majukumu ya maafisa maendeleo ya jamii kwa kutoa elimu na kuchochea ari ya wananchi ya kujitea maendeleo yao wenyewe na ya taifa kwa ujumla. Aidha, Wizara yangu kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii imehamasisha wazazi na walezi haki ya kuwaendeleza watoto kielimu ambapo kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuhusu uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi inaonesha kuwa wananchi wamehamasika na kuwapeleka watoto shule na kufanya lengo la uandikishaji katika shule za msingi kufikia **asilimia 119.5**. Pamoja na jitihada hizo za Maafisa Maendeleo ya Jamii, bado kuna upungufu mkubwa wa wataalam hao katika ngazi ya Kata ambapo kati ya Kata **3,957** zilizopo nchini, ni Kata **1,332** pekee ndizo zenye wataalam hao na Kata **2,625** hazina wataalam hao kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 7**. Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kutoa hamasa kwa jamii kujitea maendeleo jumuishi ikiwa ni pamoja na kuwapeleka watoto shule bila kujali jinsia, hali ya ulemavu au uwezo wa kiuchumi wa wazazi.

127. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia azma ya **Mheshimiwa Rais Dr. John Pombe Joseph Magufulu** ya kujenga ari ya kufanya kazi kwa watanzania, katika mwaka 2015/16 Wizara yangu kupitia vyombo vya habari ilihamasisha jamii kujenga ari ya kufanya kazi kwa bidii na kujitea maendeleo.

Mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia vyombo vya habari na Maafisa Maendeleo ya Jamii wa ngazi ya halmashauri na mkoa itaendelea kutoa hamasa kwa wananchi kupenda kufanya kazi.

Vyuo vya Maendeleo ya Jamii

128. Mheshimiwa Spika, Wataalam wa Maendeleo Jamii ni chachu katika kuwezesha jamii kujitea maendeleo. Katika mwaka 2015/16, Wizara yangu imeendelea kusimamia taaluma hiyo na kuzalisha wataalam hao kupitia vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii (Kiambatisho Na.8) na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (Arumeru). Taaluma hiyo inatolewa katika ngazi za Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya uzamili. Katika mwaka 2015/16, jumla ya wanachuo 2,130 (Ke: 1,270, Me: 860) walidahiliwa katika fani ya maendeleo ya jamii ikilinganishwa na wanachuo 3,594 waliidahiliwa mwaka 2014/15 ikiwa ni pungufu ya asilimia **48**. Upungufu huu umesababishwa na uchakavu wa majengo na miundombinu. Kupungua kwa udahili katika vyuo kutasababisha upungufu wa wataalam wenye ujuzi wa taaluma ya maendeleo ya jamii katika jamii. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuvutia vijana wengi kujiunga na vyuo hivyo. Aidha, Wizara imetenga kiasi cha **shilingi milioni 200** kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi kwa ajili ya kutatua mgogoro wa ardhi katika chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba.

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi

129. Mheshimiwa Spika, Wizara imeweza utoaji wa mafunzo ya Elimu ya Wananchi na Ufundi Stadi kwa wananchi 24,619 (Me:12,563, Ke: 12,056) kupitia vyuo 55 vya maendeleo ya wananchi (Kiambatisho Na. 9). Kati yao, wananchi 4,353 (Me:2,983, Ke: 1,370) walipata mafunzo ya Ufundi Stadi ikilinganishwa na wananchi 4,288 waliopata mafunzo hayo mwaka 2014/15 na wananchi 2,758 (Me:1,847, Ke:911) walipata mafunzo ya Elimu ya Wananchi ikilinganishwa na wananchi 3,818 ambao walipata mafunzo hayo mwaka 2014/15. Aidha, mafunzo ya muda mfupi yalitolewa kwa wananchi **13,570** (Me: 5,906, Ke: 7,664) ikilinganishwa na wananchi **8,875** ambao walipata mafunzo hayo mwaka 2014/15. Kadhalika, mafunzo nje ya vyuo yalitolewa kwa wananchi **2,816** (Me: 1,270, Ke: 1,546) ikilinganishwa na wananchi **1,281** waliopata mafunzo hayo mwaka 2014/15. Katika mwaka 2016/17 Serikali inatarajia kupima maeneo ya vyuo, kufanya ukarabati wa miundombinu na kuzalisha wahitimu **2,400** wa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa viwanda, ajira na maendeleo ya jamii.

130. Mheshimiwa Spika, elimu ya awali imeendelea kutolewa kwa watoto wadogo kupitia vituo vya kulelea watoto wadogo mchana

vilivyopo katika Vyuo **36** vya Maendeleo ya Wananchi. Jumla ya watoto wadogo **1,122** (wavulana 557 na wasichana 565) walipata mafunzo ya malezi na makuzi kwa watoto chini ya miaka mitano, ikilinganishwa na watoto **909** waliopata mafunzo kama hayo mwaka 2014/15. Vilevile, vifaa vya michezo na vifaa vya kujifunzia na kufundishia watoto wenye umri chini ya miaka mitano wanaopata Elimu ya Awali vilitolewa katika vituo **55** vya kulelea watoto wadogo mchana vilivyopo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kutoa elimu ya awali kupitia vyuo hivyo ambapo jumla ya watoto **1,650** wanatarajiwa kudahiliwa.

Maendeleo ya Jinsia

131. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unafikiwa hapa nchini, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2015/16 na mpango wa mwaka 2016/17 umegawanyika katika maeneo yafuatayo:

Uingizaji wa Masuala ya Jinsia Katika Sera na Mipango

132. Mheshimiwa Spika, uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera, mipango, mikakati, programu na bajeti ni muhimu katika kuhakikisha masuala hayo yanazingatiwa ipasavyo ili kuondoa tofauti za kijinsia nchini. Mwaka 2015/16 Wizara kupitia Kikosi Kazi cha Uingizaji wa Masuala ya Jinsia katika Sera za Kitaifa iliwezesha uingizaji wa masuala ya jinsia katika Hadidu za Rejea za kufanya mapitio ya utekelezaji wa MKUKUTA II.

133. Mheshimiwa Spika, Aidha, Wizara yangu iliendelea kuratibu madawati ya jinsia katika Wizara, Idara na Wakala za Serikali. Madawati haya ni muhimu katika kufanya uchambuzi wa kijinsia na kuingiza masuala ya jinsia kwenye sera, mikakati, mipango, programu na bajeti katika sehemu ya kazi. Hata hivyo, utendaji wa madawati haya unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa bajeti na vitendea kazi. Naomba nitoe wito kwa Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Idara, Wakala, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kutenga rasilimali fedha na kuyapatia madawati haya vitendea kazi pamoja na kuyashirikisha katika maandalizi na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuratibu uingizwaji wa masuala ya jinsia katika Sera za Kitaifa hasa katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17- 2020/21). Wizara pia itahuisha uingizaji wa masuala ya jinsia kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo Endelevu (2030) na Agenda ya Afrika Tuitakayo 2063 inayolenga kufikia maendeleo jumuishi katika jamii. Vilevile Wizara itakuwa inatambua mchango wa Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali ili

kuhamasisha na kujenga ari katika uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sera, Mipango na Mikakati yao.

Ukatili wa Kijinsia

134. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kwa jamii dhidi ya ukatili wa kijinsia. Waathirika wa ukatili huo mara nyingi ni wanawake na watoto ambapo huwasababishia madhara ya kimwili, kisaikolojia, kiafya na kiuchumi. Takwimu zinaonesha kuwa ukatili wa kijinsia bado ni tatizo kubwa hapa nchini ambapo kati ya Januari hadi Disemba 2015, matukio **22,876** yameripotiwa. **(Kiambatisho Na. 10)**. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau katika kusimamia sheria na kutoa elimu kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia.

Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi

135. Mheshimiwa Spika, moja ya vipaumbele vya Serikali ya awamu ya tano ni kuwawezesha wanawake kiuchumi. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeendelea kuratibu utendaji wa Benki ya Wanawake Tanzania na Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake ili kuwainua kiuchumi.

136. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Benki ya Wanawake Tanzania imetoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo kwa wananchi **12,874** wakiwemo wanawake **9,693** (1,485 wakiwa ni wanawake wa vijijini) na wanaume **3,181**. Hadi kufikia Machi 2016, jumla ya **shilingi 20,124,874,328** zilikopeshwa ambapo wanawake walipata mikopo yenye thamani ya **shilingi 12,878,977,228** na wanaume mikopo yenye thamani ya **shilingi 7,245,897,100**. Mikopo hiyo, imewawezesha wanawake wajasiriamali wadogo wadogo kujiajiri katika shughuli mbalimbali za biashara, kilimo na ufugaji na hivyo kuinua vipato vyao na vya familia. Katika mwaka 2016/17, Benki ya Wanawake Tanzania inatarajia kufungua dirisha maalum la kutoa mikopo yenye riba nafuu ili kuwafikia wanawake wengi zaidi.

137. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake chini ya Wizara umetoa jumla ya **shilingi milioni 54** kwa Halmashauri **7** za Chato, Kaliua, Busega, Uvinza, Wanging'ombe, Mkalama na Momba. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya mfuko ambayo inaonesha pamoja na mambo mengine kuwa kuna mwitikio mdogo wa halmashauri kuchangia asilimia tano kama zinavyotakiwa **(Kiambatisho Na.11)**. Aidha, kwa kutumia mapendekezo ya tathmini hiyo Wizara iliandaa mkakati wa kuboresha usimamizi, uendeshaji na uratibu wa mfuko. Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea na usimamizi na uratibu wa utoaji wa mafunzo, mikopo, urejeshaji na

kuhakikisha halmashauri zinachangia asilimia tano kutoka katika vyanzo vya mapato ya halmashauri.

138. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan** kwa kuteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa **Mheshimiwa Ban Ki Moon** kuwa mjumbe wa jopo la ngazi ya juu la Umoja wa Mataifa la kuwawezesha wanawake kiuchumi. Uteuzi huu unakuja wakati Wizara yangu inaandaa mikakati ya kuongeza jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi hasa katika kupata huduma za kifedha. Tafiti za matumizi ya huduma za kifedha hapa nchini zinaonesha kuwa wanawake wachache sawa na **asilimia 51.2** wanatumia huduma rasmi za kifedha ikilinganishwa na wanaume sawa na **asilimia 63**. Aidha, tafiti zinabainisha kuwa wanawake wanaomiliki simu za kiganjani ni wachache sawa na **asilimia 53.2** ikilinganishwa na wanaume sawa na **asilimia 70.5**. Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu itashirikiana na Mhe. Makamu wa Rais katika kutimiza dhamira yake ya kuanzisha kampeni ya kitaifa ya kuhamasisha na kuwawezesha wanawake kufungua akaunti za Benki na kutumia benki mtandao. Naaminini kwa kufanya hivyo wanawake wengi wataweza kutumia benki mtandao kupata huduma mbalimbali za kifedha ikiwemo VICOBA na SACCOS. Samamba na hilo Wizara itaendelea kuhamasisha wanawake wengi wanapata fursa za kukopa na kujiwekea akiba na hivyo kuondokana na umaskini.

Maendeleo ya Watoto

139. Mheshimiwa Spika, mwaka 2015/16 Wizara iliandaa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Afrika wa Haki Ustawi wa Mtoto na kuiwasilisha kwa Kamati ya Umoja wa Afrika ya Haki na Ustawi wa Mtoto mwezi Julai, 2015. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitekeleza mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto. Taarifa hiyo pamoja na mambo mengine, ilibainisha kuendelea kuwepo kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni hasa katika mikoa ya Mara, Singida, Dodoma, Shinyanga na Geita. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuinua uelewa na uwezo wa jamii kushiriki kikamilifu katika kutokomeza na kuzuia mimba na ndoa za utotoni katika halmashauri 29 kutoka mikoa yenye kiwango cha juu.

140. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016 Wizara iliwajengea uwezo Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii katika Wilaya

64 kuhusu zana ya mawasilian ya elimu ya malezi ya familia na kusambaza nakala 2000 za kitini cha eleimu ya malezi kwa familia kwa ajili ya kuzuia vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Mafunzo hayo yamesaidia kuongeza uwezo wa jamii kubaini na kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili. Mfano, utoaji wa taarifa kupitia mtandao wa simu wa watoto 116 uliongezeka kutoka **24,675** mwaka 2014/15 hadi kufikia **33,675** mwaka 2015/16. Mwaka 2016/17 Wizara itaendelea kuwajengea uwezo wa matumizi ya kitini hicho Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Halmashauri **27** nchini. Vile vile, Wizara itaendelea kuelimisha wazazi, walezi na jamii kutoa taarifa punde vitendo vya ukatili vinapotokea na kuratibu uhamasishaji wa utoaji elimu ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto kupitia kipindi cha walinde watoto kinachorushwa na radio jamii **19** zilizopo katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

141. Mheshimiwa Spika, ukeketaji ni miongoni mwa vitendo vya ukatili vinavyochochewa na mila na desturi zenye kuleta madhara kwa watoto wa kike. Katika kukabiliana na tatizo hilo mwaka 2015/16 Wizara ilihamasisha jamii kuhusu madhara ya ukeketaji ikiwa ni pamoja na vifo vya watoto wa kike. Aidha, jamii ilihamasishwa kuachana na ukeketaji na kushiriki kikamilifu katika kupinga vitendo hivyo. Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kufuatilia na kuelimisha jamii kuachana na ukeketaji.

142. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha haki ya mtoto ya kuendelezwa hasa kwa mtoto wa kike, mwaka 2015/16, Wizara yangu imeendelea kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuwapatia elimu watoto wa kike sawa na watoto wa kiume. Vilevile, Wizara imehamasisha jamii na wadau mbalimbali kujenga mazingira mazuri ya wasichana kuendelea na masomo. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha jamii na wadau wa maendeleo kuboresha mazingira ya shule kuwa rafiki kwa watoto wa kike. Aidha, itahamasisha uanzishwaji wa klabu za wasichana shuleni zitakazo wasaidia kujijenga kielimu na kimaisha.

143. Mheshimiwa Spika, mabaraza ya watoto ni muhimu katika kuwajengea uwezo wa kujiamini na kushiriki katika maamuzi mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wao. Mwaka 2015/16 mabaraza 5 yalianzishwa na kufanya idadi ya mabaraza hayo kuongezeka kufikia **122** mwezi Machi, 2016 (**Kiambatisho Na. 12**). Napenda kuzihimiza halmashauri ambazo hazina mabaraza ya watoto kuanzisha mabaraza hayo haraka. Kupitia mabaraza haya, watoto wanapata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali na kuwajengea uwezo wa kujiamini. Nitumie fursa hii kumpongeza **mtoto Getrude Clement** mwenye umri wa miaka 16 aliyeweza kushiriki na kuhutubia kwa kujiamini Mkutano wa Baraza la Umoja wa Mataifa Kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Marekani chini ya uenyekiti wa Katibu Mkuu wa Umoja huo Mheshimiwa Ban Ki Moon. Nawahimiza wazazi/walezi kuwaruhusu watoto wao kujunga na mabaraza na klabu mbalimbali za watoto. Katika

mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuimarisha utendaji kazi wa mabaraza hayo pamoja na kuhamasisha halmashauri kuyaanzisha na kutenga rasilimali fedha kwa ajili ya kuyaendesha hasa katika ngazi ya halmashauri na kata.

Maendeleo na Ustawi wa Wazee

144. Mheshimiwa Spika, mauaji ya wazee bado ni tatizo kubwa hapa nchini ambapo mwaka 2015/16 jumla ya wazee **167** wameuwa kwa sababu ya imani potofu. Mwaka 2015/16, Wizara yangu iliendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ulinzi, matunzo na usalama wa wazee kupitia maadhimisho ya kimataifa ya Siku ya Wazee Duniani, makongamano na vyombo vya habari. Katika mwaka 2016/17, Wizara inatarajia kuwasilisha mswada wa Sheria ya Wazee pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu ulinzi, matunzo na usalama wa wazee. Wazee ni hazina tuna wajibu wa kuwalinda, kuwatunza na kuwathamini. Sote ni wazee watarajiwa.

145. Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeendelea kutoa matunzo kwa wazee wasiojiweza katika makazi 17 yanayoendeshwa na Serikali. Matunzo hayo ni pamoja na huduma ya chakula, malazi na matibabu. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya makazi ya wazee na kuboresha upatikanaji wa chakula kwa ajili ya wazee katika makazi.

Ustawi wa Jamii

146. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu, kutoa na kusimamia huduma ya malezi ya kambo na kuasili watoto ambapo jumla ya mashauri **61** yalipokelewa na watoto **35** wapo katika malezi ya kambo, watoto **25** waliasiliwa na maombi 26 bado yanaendelea kufanyiwa kazi ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa polisi, taarifa za kimataifa, uchunguzi wa kijamii, pamoja na kurekebisha taarifa zenye upungufu. Katika Mwaka 2016/17, Wizara itaendelea kuratibu huduma za unasihi, usuluhishi na upatanishi katika mashauri ya ndoa zenye mifarakano na migogoro katika Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

147. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16, Wizara imeendelea kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vyuo vya walezi wa watoto. Jumla ya vituo **28** vya kulelea watoto wadogo mchana na chuo kimoja cha malezi vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo **51** vya kulelea watoto na vyuo **vivili** vya walezi wa watoto vilivyosajiliwa mwaka 2014/15. Jumla ya walezi **1,019** walipatiwa mafunzo ili kuboresha huduma zitozewazo katika vituo hivyo ikilinganishwa na walezi **600** waliopatiwa mafunzo mwaka 2014/15. Mwaka 2016/17 Wizara

itaendelea kuratibu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana na vyuo vya walezi wa watoto.

148. Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na Manispaa ya Temeke Wizara iliandaa mafunzo kwa wamiliki na walezi **50** wa vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, Kanuni za Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana na Watoto Wachanga za mwaka 2012 pamoja na namna ya kuanzisha na kuendesha vituo hivyo kwa kuzingatia viwango vya ubora wa huduma katika manispaa husika. Aidha, nakala 1,000 za kadi za ufuatiliaji wa malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto (miaka 0 – 8) zilichapishwa ili kuhamasisha wazazi na walezi kufanya ufuatiliaji wa karibu wa makuzi na maendeleo ya watoto.

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Wizara iliendelea kusimamia na kutoa huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusu za watoto na shule ya maadilisho. Wizara imehudumia jumla ya watoto **346** wakiwemo **327** wanaume na **19** wasichana waliohifadhiwa katika mahabusu za watoto za Mbeya, Moshi, Tanga, Arusha, Dar es Salaam na Shule ya Maadilisho Irambo ikilinganishwa na watoto **357** kati yao, wavulana walikuwa **304** na wasichana **33** waliohudumiwa mwaka 2014/15. Aidha, watoto waliohudumiwa mahakamani katika mwaka 2015/16 ni **164** wakiwemo **133** wanaume na **31** wasichana. Mwaka 2016/17, wizara itaendelea kuelimisha jamii kuhusu malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto. Wizara pia itaendelea kuhudumia mahabusu ya watoto, shule ya maadilisho na makao ya watoto.

Taasisi ya Ustawi wa Jamii

150. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/16 Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilidahili wanafunzi **1,308** ikilinganishwa na wanafunzi **1,376** waliodahiliwa mwaka 2014/15. Katika mwaka 2016/17, taasisi imepanga kudahili wanafunzi **2,280**. Mikakati itakayotumika kuongeza udahili ni kutangaza chuo, kutembelea shule za sekondari zenye kidato cha tano na sita na kuzungumza na wanafunzi kwa kuwashawishi kujiunga na taasisi watakapomaliza elimu ya sekondari. Aidha, taasisi inataraji kufungua matawi ya chuo Mbeya, Mwanza na Arusha.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

151. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yashiriki kikamilifu na kuchangia katika kuleta maendeleo ya jamii na taifa. Katika mwaka 2015/16, jumla ya Mashirika

Yasiyo ya Kiserikali **428** yalipatiwa usajili chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2005 na kufanya idadi ya mashirika haya kuongezeka kutoka **7,060** mwezi Machi, 2015 hadi kufikia **7,626** mwezi, Machi, 2016 (**Kiambatisho Na. 13**). Aidha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali **108** yalifutiwa usajili wao kutokana na kukosa sifa za kisheria za kuendelea kufanya kazi. Katika mwaka 2016/17, Serikali itaendelea kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yatakatayokidhi matakwa ya kisheria.

152. Mheshimiwa Spika, idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyowasilisha taarifa za mwaka za kazi na fedha imeongezeka kutoka mashirika **187** mwaka 2014/15 hadi kufikia mashirika **375** mwaka 2015/16 ikiwa ni ongezeko la **asilimia 100.5**. Wizara ilichambua taarifa hizo na kutoa mrejesho kwa mashirika husika. Taarifa za mashirika hayo zinaonesha kuwa, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yameendelea kushiriki katika shughuli za maendeleo hususan masuala ya sera, utawala bora, utoaji huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo mbalimbali ikiwemo elimu, afya, kilimo, ardhi, mazingira, mabadiliko ya tabianchi, maendeleo ya jinsia, ajira, ustawi wa jamii na maendeleo ya mtoto.

153. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Serikali itafuatilia utendaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini na kutambua mchango wa mashirika hayo katika maendeleo. Katika kutekeleza hilo, Serikali itapitia taarifa za mwaka za kazi na fedha zinazowasilishwa na mashirika hayo na kukagua miradi ya mashirika husika katika maeneo ya utekelezaji. Aidha, itaainisha na kutambua mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika sekta mbalimbali kwa kuandaa taarifa ya mchango wa mashirika hayo katika maendeleo na kuisambaza kwa wadau kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

154. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Serikali itawezesha kufanyika kwa tathmini ya Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 ili kupima utekelezaji wake, kuainisha mafanikio yaliyofikiwa, changamoto na fursa zilizopo katika kuiboresha sera husika kwa ajili ya kuyawezesha mashirika haya kutoa mchango mkubwa zaidi katika kuwahudumia wananchi kwa kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wengine.

Uratibu wa Sera, Programu na Mipango ya Wizara

155. Mheshimiwa Spika, mwaka 2015/16 Wizara iliratibu mipango na programu mbalimbali za Maendeleo ya Jamii. Katika mwaka 2016/17, Wizara itafanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (Julai 2011-Juni, 2016) na kuandaa Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (2016/17 – 2020/21) utakaoendana na Mpango

wa Pili wa Maendeleo (2016/17-2020/21) na mabadiliko ya Wizara yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano. Aidha, Maafisa Maendeleo ya Jamii wa Mikoa na Halmashauri watajengewa uwezo wa kukusanya, kuchambua, kuandaa na kutoa taarifa za sekta ya maendeleo ya jamii kupitia Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ulioandaliwa.

USHIRIKIANO WA NDANI NA NJE YA NCHI

156. Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kushirikiana na nchi rafiki katika kuimarisha Sekta ya Afya nchini. Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki kwenye mikutano ya jumuiya za kikanda za SADC, EAC, ECSA-HC na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa na katika kutekeleza maamuzi ya pamoja yenye manufaa kwa taifa. Katika mwaka 2016/17, Wizara itaimarisha ushirikiano na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia Wizara yangu. Aidha, itaimarisha ushirikiano na sekta nyingine ambazo zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za afya za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kuhamasisha na kufikisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya siku hizo niza Afya, Malaria Afrika, UKIMWI, Kifua Kikuu, Ukoma, Wazee, Kutotumia Tumbaku, Tiba Asili ya Mwafrika, Wachangia Damu, Utepe Mweupe, Siku ya Wauguzi na Fimbo Nyeupe na Siku ya Mtoto Njiti duniani.

SHUKRANI

157. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark (DANIDA), Uswisi (SDC), na Ireland (Irish Aid), Canada (DFATD) na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNICEF, na UNFPA kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini. Aidha, naishukuru na kuipongeza Korea Kusini kupitia shirika lake la Maendeleo (KOICA) kwa kuamua kujiunga na nchi zinazochangia fedha katika Mfuko wa pamoja kwa ajili ya huduma za afya kuanzia mwaka 2016/17. Pia, napenda kuzishukuru nchi za Canada, China, Cuba, Hispania, India, Italia, Japan, Marekani, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani na Ufaransa na ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa njia mbalimbali.

158. Mheshimiwa Spika, vilevile nayashukuru mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika haya yanajumuisha Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika (BADEA), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), GAVI, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI (UNAIDS), Shirika la Umoja wa

Kimataifa la Maendeleo (UNDP), UNFPA, UN-Women, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Benki ya Dunia (WB). Wengine ni Abbott Fund, BASIC NEED (UK), ACF – Canada, Baylor College of Medicine ya Marekani, Canadian Bar Association, CDC, CORDAID (Netherlands), CUAMM, DANIDA, DFID, Engender Health (USA), EED, Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF), Family Health International (FHI360), FINIDA, GIZ, Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), HelpAge International, ILO, Jane Adams School of Social Work ya Chuo Kikuu cha Illinois Marekani, John Snow Incorporation (JSI), JICA, KOICA, KfW, Global Partnership for Education (GPE), Madaktari Afrika na Madaktari Wasio na Mipaka (Medicins Sans Frontieres – MSF), MSERIOR, ORIO, P4H, SAREC, SDC, SIDA (Sweden), Shirika la Upasuaji la Spain, SIGN la Marekani, na Shirika la Human Resource Capacity Project, Touch Foundation, USAID na Children Investment Foundation Fund (CIFF), World Lung Foundation.

159. Mheshimiwa Spika, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo ambao ni African Programme for Orchorceriasis Control, Africare, Axios International, Aids Relief Consortium, AIHA, ASCP, ASM, APHL, Balm and Gilead Foundation, Bill and Melinda Gates Foundation, Clinton Health Access Initiative, CLSI, CMB, Christoffel Blinden Mission (CBM), Christian Relief Services (CRS), Citi Bank, Department of Defence ya Marekani, Community of Saint Egidio (DREAM), Duke University, ECSA, Futures Group, Glaxo Smith Kline (GSK), Global Fund to fight AIDS, TB and Malaria (GFATM), General Electric (GE – USA), Havard University na University of Maryland, Helen Keller International, Henry Jackson Foundation, IMA, ICAP, International Trachoma Initiative, Intrahealth, International Eye Foundation, I-TECH, Jhpiego, Johns Hopkins University, Labiofarm Industry, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Management Science for Health (MSH), MEDA, Merck & Company, Malaria No More, Military Advancement for Medical Research, NOVARTIS, Pathfinder, PATH, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Pharm Access International, PactWorld, Plan International, Pfizer, Qiagen, Research Triangle Institute (RTI), Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), Saint Thomas Hospital-London, Save the Children, SightSavers International, Supply Chain Management Systems (SCMS) na University of Columbia, URC, USA- Presidential Malaria Initiative (PMI), World Vision, FXB, Walter REED Army Institute of Research (WRAIR) na World Education Inc.

160. Mheshimiwa Spika, niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, Benjamin William Mkapa HIV/AIDS Foundation, CCBRT, CSSC, CCT, Counsenuh, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT,

AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, MEWATA, MUKIKUTE, FAWETA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosiation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya sekta ya afya.

161. Mheshimiwa Spika, navishukuru Vyuho Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Dodoma, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, IMTU, Tumaini, St. Agustino, CUHAS, Sebastian Kolowa, St. John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Arusha pamoja na Vyuho vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za radio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na maendeleo ya jamii.

162. Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki cha utendaji wangu wa kazi nikiwa Waziri, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla (Mb.)**, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha naomba kuwashukuru **Dkt. Mpoki M. Ulisubisya** Katibu Mkuu (Afya) na **Bibi Sihaba Nkinga** Katibu Mkuu (Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) kwa mchango wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Vilevile, nawashukuru **Prof. Muhammad Bakari Kambi**, Mganga Mkuu wa Serikali Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara yangu. Nawashukuru pia, Mkurugenzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, na Wakurugenzi wa Hospitali Maalum na za Rufaa za Kanda na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vyuho vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, ya Kujitolea na Binafsi. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya, maendeleo ya jamii na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaomba waendeleo kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya taifa letu.

163. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, kwa uvumilivu wao na pia kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Kwa wananchi na hasa wanawake wa Mkoa wa Tanga nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuendeleza Mkoa wetu. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Mkoa wetu.

MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2016/17

164. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza kazi zilizopangwa katika mwaka 2016/17, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Makusanyo ya **Shilingi 166,138,358,857** kutoka katika mashirika na Taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu na vyanzo vya makao makuu. Aidha naomba pia Bunge lako Tukufu likubali na kuidinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara pamoja na Taasisi zake yenye jumla ya **Shilingi 845,112,920,056.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 317,752,653,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 527,360,267,056.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mchanganuo kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

Fungu 52 – Afya

Mapato

165. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17 Wizara imekadiriya kukusanya mapato ya **Shilingi 163,755,679,857.00** kati ya fedha hizo **Shilingi 146,968,868,000.00** zitakusanywa katika mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na **Shilingi 16,786,811,875.00** ni kutoka katika vyanzo vya makao makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji wa huduma za afya, tozo na ada mbalimbali, usajili wa vituo binafsi vya kutolea huduma, maabara binafsi na Mabaraza ya Kitaaluma.

Matumizi ya Kawaida

166. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara inakadiriya kutumia kiasi cha **Shilingi 277,604,173,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 58,151,377,000.00** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 219,452,796,000.00** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara **Shilingi 41,198,409,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Wizara, Makao Makuu na **Shilingi 178,254,387,000.00** ni kwa ajili ya watumishi wa Taasisi, Mashirika na Wakala zilizo chini ya Wizara.

Miradi ya Maendeleo

167. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 518,511,683,780.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo fedha za ndani ni **Shilingi 320,134,600,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 198,377,083,780.00**.

Fungu 53 – Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Mapato

168. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Fungu 53 inatarajia kukusanya **shilingi 2,382,679,000** kutokana na ada za wanafunzi kutoka Vyuo 8 vya Maendeleo ya Jamii, ada ya usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mauzo ya vitabu vya zabuni

Matumizi ya Kawaida

169. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 40,148,480,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 21,479,351,200** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 18,669,128,800** zitatumika kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

Miradi ya Maendeleo

170. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/17 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 8,848,583,276** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,365,400,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 3,483,183,276** ni fedha za nje.

171. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto www.moh.go.tz. na www.mcdgc.go.tz.

172. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ahsante! Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jami.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII, KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. PETER J. SERUKAMBA - MWENYEKITI KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2015/2016, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba ripoti yangu yote iingie kwenye *Hansard* kwa sababu sitasoma yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na kufanya uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2016/2017 ambayo ni Fungu 52 - Idara Kuu ya Afya na Fungu 53 - Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa hii ambayo itafafanua mambo makuu manne:-

(i) Hali halisi katika utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya mwaka unaoisha;

(ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya mwaka wa Fedha 2015/2016 na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(iii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2016/2017; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016, Kamati ilifanya mapitio ya maoni na mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha bajeti ya mwaka 2015/2016. Jumla ya mapendekezo kumi na nane yalitolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016; katika kikao cha kufanya maamuzi ya uamuzi na mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2015/2016 kilichofanyika tarehe 12 hadi 13 Aprili 2016 na marekebisho yaliyofanywa na Wizara na kuwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 4 Mei, 2016, Kamati ilijikita katika kufanya uchambuzi wa maduhuli ikifanya ulinganisho wa upatikanaji wa fedha hizo kadri ya malengo ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara katika mwaka huo wa fedha. Njia zilizotumika ni pamoja na kupitia taarifa zilizowasilishwa katika Kamati kwa mwaka ya fedha uliopita wa 2015/2016 na mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ili kuona hali halisi ya makusanyo ya maduhuli pamoja na mahojiano yaliyofanyika wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na taarifa nyingine muhimu zilizowasilishwa mbele ya Kamati wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, Kamati ilifanya uchambuzi wa matumizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 katika fedha zilizoidhinishwa, zilizopatikana pamoja na matumizi yake kwa mwaka huo kadri ya mgawanyiko wa kila fedha katika mafungu yote mawili ya Wizara yaani Fungu 52 na Fungu 53. Ilikuwa ni matarajio ya Kamati kukutana na matokeo kuwa asilimia 75 ya mwaka mzima wa fedha zilizoidhinishwa, kutolewa na kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika uchambuzi huo, Kamati imegundua kwamba, hadi kufikia mwezi Machi 2016 ambayo ni robo tatu ya mwaka wa fedha 2015/2016, hakuna fungu hata moja ambalo limeweza kupewa fedha zilizoidhinishwa angalau kwa asilimia 50 kutoka Hazina. Kamati inasikitishwa na kitendo cha Serikali kutopeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Wizara hii pamoja na umuhimu wake katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa Fungu 52 - Idara Kuu Afya, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, kiasi cha fedha kilichopelekwa na kutumika ni asilimia 31 tu ya bajeti nzima hali kadhalika Fungu 53 kwa Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Kwa mwenendo huu, Kamati inaona juhudi na mpango wa Serikali wa kujali afya za wananchi wa Tanzania itabaki kuwa ndoto na hivyo kuendelea kuwa na Taifa lisilokuwa na wananchi walio na afya bora ambayo ndiyo msingi mkuu wa Maendeleo ya nchi.

Naomba kunukuu msemu mmoja wa mwanazuoni mmoja alisema; *“you are young if you are healthy and rich when you have no debts”* kwa maana isiyo rasmi ni kwamba, unakuwa kijana kama una afya na unakuwa tajiri kama huna madeni. Kamati inaona kwamba kwa kutopeleka fedha hizo kwa asilimia 69 hadi Machi 2016 ambalo ni deni kubwa, Serikali haijawatendea haki wananchi katika kutekeleza azma ya kuwapelekea huduma ya afya bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), katika mwaka wa fedha wa 2015/2016, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Fungu 52, iliidhiniwa kiasi cha shilingi 14,900,000,000 kwa ajili ya mradi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road wa kujenga vyumba maalumu (Bunkers) kwa ajili ya kusimika mashine mpya za kisasa za kutibu saratani na hivyo kuimarisha huduma za tiba ya saratani. Aidha, fedha hizo zililenga kufanya manunuzi ya mashine za kisasa za kutibu saratani *Linear Accelerator (LINAC)*, *CT Simulator* na kubadilisha chanzo cha mionzi. Katika mradi huu kulikuwa na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Shirika la Atomiki Duniani ya kuchangia katika manunuzi ya mashine hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kutekeleza mradi huu ulioanza Machi 2015 na unatarajiwa kukamilika Juni 2016, *specifications* za LINAC zimekwishaandaliwa na kupitishwa na taratibu za ununuzi wa mashine zinaendelea. Aidha, mpaka Kamati inakwenda kufanya ukaguzi wa mradi huo, shughuli za ujenzi wa vyumba maalum kwa ajili ya kuhifadhia mashine hizo ulikuwa umefikia katika hatua nzuri ya kukamilika kwa asilimia 95 ambapo mradi upo katika hatua za umalizikaji wa kufanya ukuta kuwa laini (*scheming*), kuweka sakafu, mifumo ya umeme, mifumo ya maji safi na majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi huu, kuna changamoto ambazo zimeikabili Taasisi ya Ocean Road zikiwemo fedha za mradi kutokutolewa kwa wakati ambapo kati ya fedha zilizotengwa ni asilimia 26 tu ndizo zilizopelekwa na kufanyia shughuli za utekelezaji wa mradi huo kusuasua. Aidha, Shirika la Atomiki Duniani (*International Atomic Energy Agency*) wameweka bayana kwamba kwa sasa hawataweza kuchangia ununuzi wa mashine hiyo kwa sababu ya Serikali kuchelewesha utoaji wa fedha kwa wakati mwaka 2013/2014 kinyume na makubaliano yalivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa na kukosekana kwa fedha hizo kwa sababu ya uzembe wa Serikali yetu kutotimiza makubaliano ya utoaji wa fedha. Pamoja na Wizara kutoa taarifa katika Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango juu ya uamuzi wa kutokutolewa kwa fedha hizo na kusisitiza juu ya umuhimu wa fedha iliyobaki kutolewa kwa sasa, Kamati inaliomba Bunge lako liitake Serikali kukamilisha utoaji wa fedha hizo zilizotengwa kwa asilimia 74 iliyobaki ili kuweza kukamilisha mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya MOI Kamati iliweza pia kufanya ziara ya Ukaguzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pamoja na taasisi zake ikiwemo Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI). Katika ukaguzi wa mradi wa upanuzi wa MOI awamu ya III ambao ni ujenzi wa jengo la ghorofa saba (7) kwa ajili ya kutolea huduma za uchunguzi ikiwemo

CT-Scan, MRI, X-Ray, Ultra Sound, vyombo vya upasuaji, maabara, hifadhi ya damu, huduma za dharura, ICU, vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu, vyumba vya wagonjwa wa kulipia na kuchangia. Kukamilika kwa mradi huu ambao utaigharimu jumla ya shilingi bilioni 27.23 ambazo ni mkopo ambao taasisi hiyo imekopa kutoka katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kudhaminiwa na Serikali. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha Hospitali kuwa na vitanda vya kulaza wagonjwa 340 na kuweza kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la wagonjwa kulala chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha utekelezaji wa mradi ni cha kuridhisha ambao umefika katika kiwango cha asilimia 95 na asilimia 5 zimebaki kukamilishwa kwa kiasi cha fedha shilingi bilioni 9.26 ambazo bado Serikali haijapeleka. Aidha, ununuzi wa vifaa tiba na samani uliotengewa na Serikali kiasi cha shilingi bilioni 12.5 katika bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 bado haujafanyika kwani Serikali bado haijatoa fedha hizo. Hata hivyo Kamati imeshtushwa na ongezeko la gharama za ujenzi huo kwani katika baadhi ya makadirio ya ujenzi huo kuna ongezeko kwa zaidi ya asilimia kumi ya gharama zilizokadiriwa mwanzo. Kamati inaliomba Bunge likubali kuiagiza Serikali kufanya uchunguzi wa ongezeko la gharama hizo ili kuweka bayana gharama halisi za ujenzi wa jengo hilo.

Pili, Kamati inaliomba Bunge likubali kuitaka Serikali kutoa fedha zilizobaki shilingi bilioni 9.26 kabla ya mwaka wa fedha wa 2015/2016 haujaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inampongeza Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuruhusu jengo hilo kuanza kutumika ili katika kuendeleza juhudi za utoaji wa huduma bora ya afya kwa wananchi hasa katika kutatua changamoto ya wagonjwa waliokuwa wanalala chini katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Kamati inaunga mkono maamuzi hayo ya kuwasaidia wagojwa kutoendele kulala chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari ya Dawa (MSD); Kamati ilifanya ukaguzi katika Bohari ya Dawa (MSD) ambapo kuna mradi wa upanuzi wa ofisi za bohari hiyo ulioanza Julai 2013. Mradi ulitengewa kiasi cha shilingi bilioni 7.23 kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ya bohari ya dawa. Mpaka kufikia Machi, 2016 kiasi cha shilingi 5,159,184,372 zilikuwa zimeshatolewa na kutumika na mradi umekamilika kwa asilimia 68 kwa maelezo kuwa asilimia 32 itakamilika ifikapo mwezi Mei, 2016. Kamati inaliomba Serikali kuendelea kuisimamia Bohari ya Dawa kuweza kutoa kiasi kilichobaki katika mwaka wa fedha 2015/2016 ili kuweza kukamilisha mradi huo ili kuweza kutatua tatizo la uhaba wa ofisi kwa watumishi wa Bohari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Uchambuzi wa mpango

wa makadirio ya mapato na matumizi ya kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara inatarajia kutekeleza jumla ya malengo matano kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Malengo hayo ni pamoja na:-

(i) Kutoa huduma bora za afya ya msingi katika ngazi ya jamii na vituo vya kulelea watoto;

(ii) Kutoa huduma zinazofikika na kwa usawa kwa kutoa kipaumbele kwa maeneo yenye mzigo mkubwa wa magonjwa na kwa kuzingatia makundi yenye mahitaji maalum;

(iii) Kushirikiana na jamii kikamilifu kwa lengo la kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma;

(iv) Kutoa njia za kisasa katika usimamizi ikiwa ni pamoja na ubunifu katika utoaji wa huduma; na

(v) Kushirikiana na sekta mbalimbali na kuhamasisha ujumuishwaji wa masuala ya sekta ya afya katika sera na mikakati ya sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya mapato, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii ina mafungu mawili kama nilivyoeleza awali. Katika Fungu 52 - Idara Kuu Afya pamoja na taasisi zake inatarajia kukusanya mapato kiasi cha shilingi 170,011,902,000 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 47.02 ambayo ni sawa na asilimia 27.6 ya kilichokadiriwa kukusanywa mwaka wa fedha wa 2015/2016 ambayo ni shilingi 122,998,941,500.00. Aidha, Fungu 53 - Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 2.382 ikiwa ni pungufu ya makadirio ya mapato ya mwaka 2015/2016 ambayo yalikadiriwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 2.713. Upungufu huo ni kiasi cha shilingi milioni 331 ikiwa sawa na asilimia 12.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Wizara kupitia Fungu 52 inaomba jumla ya makadirio ya matumizi ya fedha kiasi cha shilingi bilioni 796.115, Katika fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 277.604 sawa na asilimia 28 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi bilioni 518.511 sawa na asilimia 72 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara kupitia Fungu 53, imekadiria kufanya matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 48.9 ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 40.148 ambayo ni sawa na asilimia 82 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo mishahara ya watumishi na matumizi mengineyo na kiasi cha shilingi bilioni 4.8 sawa na asilimia 18 ni fedha kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, maoni na mapendekezo ya Kamati; kutokana na uchambuzi wa kina wa makadirio ya mapato na

matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 uliofanyika mnamo tarehe 12 na 13 Aprili 2016, Kamati ina mapendekezo, maoni na ushauri katika maeneo 20 yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa usimamizi wa masuala ya sekta ya afya. Wakati Kamati inafanya uchambuzi wa utekelezaji bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2016/2017, Wajumbe walibaini changamoto ya mfumo wa *Development by Devolution* umesababisha Wizara na Kamati kukosa mamlaka ya kufuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha watendaji walioko chini ya Wizara husika na hivyo kupunguza ufanisi katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na Wizara ya Afya kupewa mamlaka katika usimamizi wa sera pekee sehemu ambayo haimuwezeshi mwananchi kuona mafanikio ya utoaji wa huduma ya afya na kuacha sehemu kubwa kuwa katika Wizara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano watumishi kama Waganga, Wauguzi, Maafisa Maendeleo ya Jamii, wote wako chini ya Ofisi ya Rais - Tawala na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Wizara imepewa madaraka ya kusimamia sera ya sekta ya afya, utekelezaji wake uko katika Wizara ya TAMISEMI. Kamati inashauri kwamba, masuala yote yanayohusu sekta ya afya yarejeshwe Wizara ya Afya ili kuweza kusimamia kuanzia sera, watumishi na miundombinu, badala ya kutenganisha kila Wizara mbili tofauti inayosababisha TAMISEMI kuonekana ni kichaka au ni kimbilio la kutekeleza shughuli za afya wakati Kamati inapohitaji taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake yasiyo ya kisera. Kamati inashauri, kama haitawezekana kuondoa masuala ya afya TAMISEMI ni vema ukaandaliwa mfumo bora wa mawasiliano, ushirikiano, uwajibikaji kati ya Wizara ya Afya na TAMISEMI, kutoa taarifa ya matumizi ya fedha ili ziwasilishwe katika Kamati zote mbili, Huduma ya Maendeleo ya Jamii na TAMISEMI. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya sekta ya afya; bajeti ya mwaka 2016/2017 inaonekana kuongezeka kitakwimu kila mwaka, lakini Kamati inaona kwamba ongezeko hilo la fedha haliendani na hali halisi ya thamani ya fedha. Hivyo, Kamati inashauri kutenga fedha za sekta ya afya, ukizingatia thamani ya fedha ya nchi na dunia kiu jumla kwani fedha hizo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji makubwa ya sekta ya afya. Ikumbukwe kwamba afya ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Naomba kumnukuu mwanazuoni mwingine aliyewahi kusema; *"Health is the core of the human development."* Hivyo basi, tukitaka kusonga mbele kimaendeleo Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha katika sekta ya afya ambayo ndiyo kitovu cha maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari Kuu ya Dawa (MSD); kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi ya kukosa dawa muhimu (*essential medicines*), katika vituo vya kutolea huduma ya afya. Hii pia ilidhihirika wakati Kamati ilipotembelea Bohari Kuu ya Dawa kujionea ghala la dawa muhimu likiwa tupu na maghala ya magonjwa mengine kama dawa ya kupunguza makali ya virusi vya UKIMWI, chanjo. Hali ya ukosefu wa dawa inawaumiza wananchi wenye bima ya afya, fedha taslimu kupata haki yao ya msingi wanaokwenda hospitali kupata matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Bohari Kuu ya Dawa kuweka muda maalum wa upelekaji wa dawa katika vituo vya kutolewa huduma ya afya mara baada ya kupokea fedha kutoka kwa wateja wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutopeleka fedha za mradi kwa wakati. Wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji ya bajeti ya mwaka 2015/2016, Kamati iligundua kwamba, mpaka kufikia mwezi Machi, 2016 ambayo ni robo tatu ya mwaka wa fedha uliopita, Wizara ilikuwa imepata asilimia 31 tu ya bajeti iliyopitishwa. Kamati inaishauri Serikali kupitia Hazina kupeleka fedha hizo kabla ya mwaka wa fedha haujaisha ili Wizara iweze kutimiza malengo yake iliyojiwekea kwa ajili ya kuimarisha afya ya wananchi wetu nchini. Ikumbukwe kwamba Taifa ambalo lina watu ambao hawana uhakika wa afya zao kwa maana ya kwamba hakuna huduma bora ya afya ni Taifa legelege na ni Taifa ambalo haliwezi kufanya kazi ya uzalishaji na kukuza uchumi wake hivyo, Taifa letu kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli ya mwaka 2016/2017. Makadirio ya makusanyo ya mwaka wa fedha 2016/2017 yamekadiriwa kwa kiwango cha chini sana. Ukifanya uangalifu wa mapato ya Wizara hii kwa kuwa Wizara yenyewe imeieleza Kamati kupitia taarifa zao za mwaka 2015/2016 kuwa walifanikiwa kukusanya maduhuli zaidi ya kile kilichokadiriwa na kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato. Hivyo, basi Kamati inashauri Wizara iendelee kuweka mifumo bora na imara kwa ajili ya kukusanya hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za ujenzi wa kiwanda cha dawa, NIMR. NIMR ilitengewa shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza dawa asilia, lakini mpaka Kamati inakutana na Wizara hakuna fedha iliyotolewa. Kutokana na umuhimu wa kiwanda hicho kinachotengeneza dawa asili Kamati imeiagiza Wizara katika bajeti ya mwaka huu wafanye *realocation* kwenye mafungu yake na kuipatia NIMR hata shilingi milioni 800, ili mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifo vya akinamama vinavyotokana na uzazi. Kumekuwa na vifo vingi vya akina mama vinavyotokana na masuala ya uzazi,

ikiwemo wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua, hata ndani ya siku 40 baada ya kujifungua. Tunaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuendelea kupunguza vifo hivi hapa nchini, lakini bado hali hairidhishi. Takwimu zinaonesha kwamba, takribani akinama 15,056 wanapoteza maisha kila mwaka, hii maana yake ni kwamba, akina mama 1,255 wanafariki kila mwezi na kila siku inapoteza akina mama 42 na kila baada ya saa moja akinamama wawili wanaaga dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa gari aina ya coaster lenye uwezo wa kubeba abiria 36 toka Dodoma kuelekea Morogoro likipata ajali na likauwa watu wote ndani ya gari hilo viongozi wenye dhamana watafunga safari kuelekea katika eno hilo la tukio, hata kusababisha Bunge kusimama kwa dakika moja kuwaombea marehemu na kusitisha shughuli za Bunge kwa ajili ya ajali hiyo na vifo hivyo vilivyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mengine kila siku ajali ya coaster iliyobeba akina mama 36 waliokaa na wengine waliosimama sita inatokea na inauwa akina mama wote. Ilitakiwa kulifanya Bunge hili kila siku liwe linasimama kwa ajili ya kuwaombea akina mama 42 wanaofariki kwa sababu ya uzazi na hakuna anayeshtuka kuona kama hii ni hatari kubwa kwa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuwanusuru akina mama hawa 42 wanaopoteza maisha kila siku wakitimiza wajibu wao wa kiasili kuongeza watu duniani ambao ni msingi na hawana hatia kabisa. Akina mama hawa ni mama zetu, ni watoto wetu, ni mawifi zetu, ni dada zetu, ni binamu zetu, ni mama zetu, ni shemeji zetu na ni Watanzania wenzetu kwa ujumla wake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa vituo vya kutolea huduma ya afya nchini. Sera ya Afya inatuelekeza kuwa zahanati kila kijiji, kituo cha afya kila kata, ukiangalia takwimu za idadi ya kata hapa nchini takribani kata 3800, kwa maana hiyo basi mpaka kufikia sasa nchi yetu ilitakiwa iwe na vituo vya afya visivyopungua 3800. Tunakaribia kufikia idadi hiyo, Kamati inasikitika kueleza kwamba vituo vya afya nchini ni 484 vinavyomilikiwa na Serikali, mashirika ya dini 141, vituo vya afya binafsi 79, taasisi 12 na kwa hiyo, jumla ya vituo vya afya ni 716 ambayo ni sawa na asilimia 18.8 ya mahitaji ya vituo vya afya kiseru. Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha inaeleza Sera ya Afya kuwa zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya kama Sera inayotekelezeka. Kwa kufanya hivyo itasaidia kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi ambavyo vingine vinasababishwa na akina mama kujifungua nyumbani kwa kukosa huduma za uzazi katika maeneo ya karibu na wanapoishi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa watoa huduma nchini. Kumekuwa na changamoto ya uhaba wa watoa huduma ya afya katika vituo vingi vya kutolea huduma ya afya katika nchi yetu. Ni kwa sababu Serikali haijaamua

kuwaajiri watoa huduma hao ili waweze kufanya kazi. Takwimu zinaonesha kuna zaidi ya wataalam 30,000 lakini kibali kilichotoka kuajiri wataalam wetu ni 10,000 ambayo ni theluthi moja tu ya wataalam waliopo na hawajapata kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwezi Machi, 2016 Kamati ilitua Wajumbe wanne ambao waliambatana na Taasisi ya Benjamin Mkapa ambayo inaisaidia Serikali katika kuendeleza na kuimarisha huduma za afya, kuongeza rasilimali watu kwa kujenga miundombinu zikiwemo nyumba za upasuaji hata nyumba za watumishi. Wajumbe hao walikwenda Mikoa ya Simiyu, Rukwa na Shinyanga ili kuona mafanikio na changamoto zinazokabili Halmashauri za Wilaya kuhusiana na uhaba wa watumishi wa afya pamoja na motisha zinazotolewa na Halmashauri za Wilaya kwa watumishi wa afya ili Kamati iweze kuishauri Serikali namna ya kutatua changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara hiyo, ilibainika kuwa Wilaya ya Bariadi, Kalambo na Kishapu zina uhaba wa wasaidizi wa maabara kwa asilimia 100. Wilaya ya Bariadi ina uhaba wa Madaktari kwa asilimia 87, ikifuatiwa na Sumbawanga asilimia 86, Kalambo asilimia 75. Aidha, Wilaya ya Kishapu inakabiliwa na uhaba wa wauguzi kwa asilimia 87 ikifuatiwa na Bariadi asilimia 76, Sumbawanga asilimia 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya za mwaka 2014 katika ngazi ya zahanati kulikuwa na uhaba wa Wateknolojia kwa Maabara asilimia 93, Wauguzi wa Cheti kwa asilimia 65, Maafisa Tabibu kwa asilimia 52. Aidha, vituo vya afya vilikuwa na upungufu wa Wauguzi kwa ngazi ya Cheti kwa asilimia 65, Wateknolojia ya Maabara Wilaya asilimia 52, Maafisa Tabibu kwa asilimia 20, wakati katika Hospitali za Wilaya upungufu ni mkubwa zaidi ya asilimia 77.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inasikitisha kwani siyo kwamba watu wenye taaluma hawapo mtaani, wapo, lakini vibali vya ajira havitolewi licha ya upungufu huu mkubwa! Takribani wahitimu wa Kada za Tabibu, Wauguzi wa Teknolojia ya Maabara wako 4491, waliohitimu mafunzo mwaka 2015 bado hawana ajira!

Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa wataalam hawa wa kuajiriwa, ili wakatoe huduma kwa wananchi wetu na kupunguza changamoto za vituo vya afya kukosa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ya uhaba wa Madaktari katika Hospitali katika maeneo mbalimbali hapa nchini, hii ni kutokana na maslahi duni kwa wataalam hao kutoka Serikalini na hata yale yanayopatikana yamekuwa na tofauti hasa katika mishahara. Madaktari wamekuwa wakisita kwenda kutoa huduma katika Hospitali za Mikoa kutokana

na utofauti wao wa malipo. Kwa mfano, Daktari mwenye Shahada ya Kwanza (*First Degree*) waliomaliza masomo pamoja wanaokwenda kufanya kazi Hospitali ya Taifa Muhimbili, KCMC, Bugando, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, mishahara yao inatofautiana na Madaktari wanaokwenda kufanya kazi katika Hospitali za Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la watu nchini. Kwa mujibu wa takwimu hadi kufikia 2010 Tanzania itakuwa ni nchi ya saba duniani katika Bara la Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya watu. Takribani watu milioni moja huongezeka kwa mwaka. Kamati inatoa rai kwa viongozi wote wa nchi wakiwemo wa kisiasa, kidini, hata kimila kulizungumzia suala hili kwa nia njema kabisa kuwa na Taifa imara na bora lenye afya na idadi inayoendana na rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda kumshukuru Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla, kwa ushirikiano wao mkubwa waliutoa katika Kamati ilipokuwa ikijadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Vilevile napenda kuwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake, kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru wadau wote wa sekta ya afya kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kwa Serikali yetu katika kuendeleza huduma za afya hapa nchini. Naomba kuwataja kwa uchache wao pamoja na PEFA, Mfuko wa Dunia (*Global Fund*), mchango wao wa fedha wa maendeleo katika nchi yetu. Pia, Kamati inawapongeza Taasisi ya Benjamin Mkapa kwa jitihada zao za kuendeleza na kupeleka wataalam wa afya wakiwemo Madaktari katika maeneo mbalimbali nchini na hata kujenga vituo na kutoa huduma za afya. Kamati inawaomba sana wadau kuendelea kuwa na ushirikiano huo na Serikali yetu kama inaweza kuboresha huduma katika sekta ya afya. Kamati inaiomba Serikali na Wizara kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa wadau hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Thomas Kashililah - Katibu wa Bunge, ndugu Athuman Hussein - Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, kusaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee namshukuru ndugu Dickson Bisile pamoja na ndugu Pamela Pallangyo, ndugu Agnes Nkwera - Makatibu wa Kamati na Mwimbe John -

Msaidizi wao kwa kuratibu vema kazi za Kamati kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Taasisi zake kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja, Fungu Namba 52 jumla ya shilingi 796,115,856,780 na Fungu 53 shilingi 48,997,063,276.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, umesoma vizuri sana.

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII KUHUSU UTEKELEZAJI WA WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 6(5)(a) na 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati hii ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Bajeti ya Wizara hii. Aidha, Kamati hii inao wajibu pia wa kushughulikia Bajeti ya kila Mwaka ya Wizara hiyo.

Vile vile, Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka sharti la Kamati za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kufanya Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Naomba kutoa Taarifa kuwa Kamati ilifanya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha chini ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na kufanya Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambayo ni Fungu 52- Idara Kuu ya Afya na Fungu 53- Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, naomba kutoa taarifa hii ambayo inafafanua mambo manne (4) yafuatayo:-

(i) Hali halisi katika Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka unaoisha;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA KAMATI

2.1 Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Katika kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ilifanya mapitio ya Maoni na Mapendekezo yaliyotolewa wakati wa kupitisha bajeti ya Mwaka 2015/2016. Jumla ya Mapendekezo kumi na nne yalitolewa.

Mheshimiwa Spika, Katika Maoni, Ushauri na Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati iliyopita, yapo maoni yaliyoweza kutekeleza kikamilifu, yanayoendelea kutekelezwa na ambayo hayajatekelezwa kabisa na Wizara. Katika ushauri ulioteklezwa, Kamati inaipongeza Serikali na Wizara kwa jitihada hizo na yale ambayo yanaendelea kutekelezwa Kamati inaiomba Wizara kuendelea kusimamia ili yatekelezwe kama ilivyoshauriwa. Na yale ambayo hayajatekelezwa kwa sababu ya kutopata Fedha toka Serikalini Kamati inaiagiza Wizara kufuatilia Fedha hizo na kuyatekeleza mara moja kabla ya

Mwaka wa Fedha 2015/2016 haujamalizika. Ikiwemo kupeleka Fedha za ujenzi wa uzio katika kituo cha waathirika wa madawa ya kulevywa, ununuzi wa mashine ya mionzi katika Taasisi ya Ocean Road kwa kupeleka Fedha zote kwani mashine hizo haziwezi kununuliwa kwa sehemu kama Fedha zinavyotolewa. Aidha utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo Rejea **kiambatisho Namba 1.**

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Katika kikao cha kufanya Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kilichofanyika tarehe **12-13 Aprili 2016** na marekebisho yaliyofanywa na Wizara na kuwasilishwa mbele ya Kamati tarehe **4 Mei 2016**, Kamati ilijikita katika kufanya Uchambuzi wa maduhuli ikifanya ulinganisho wa upatikanaji wa Fedha hizo kadiri ya malengo ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara katika Mwaka huo wa Fedha. Njia zilizotumika ni pamoja na kupitia taarifa zilizowasilishwa katika Kamati kwa Mwaka ya Fedha uliopita wa 2015/2016 na Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa mujibu wa kanuni ya 98(2), ili kuona hali halisi ya Makusanyo ya maduhuli pamoja na mahojiano yaliyofanyika wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na taarifa nyingine muhimu zilizowasilishwa mbele ya Kamati wakati wa vikao vya shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa kutumia jedwali ambalo linatoa ufafanuzi wa ulinganisho wa ukusanyaji wa maduhuli kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/2016 ikiainisha kiasi kwa Mwaka, asilimia na kuonesha tofauti au ulinganisho wa taarifa hizo kwa asilimia.

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli

Jedwali Na. 1

Fungu	Mwaka wa Fedha 2015/2016			Mwaka wa Fedha 2016/2017	
	Makadirio	Makusanyo	%	Makadirio	% Tofauti
52	122,998,941,500	77,403,330,455	62.9	Bilioni 170.011	+27
53	Bilioni 2.713	Bilioni 1.35	49.8	Bilioni 2.382	-12

Chanzo: Randama ya Wizara kwa ajili ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ilikadiria kufanya makusanyo ya kiasi cha shilingi **bilioni 122.998** katika **Fungu 52**-Idara kuu Afya, ambapo hadi kufikia Machi 31 ambayo ni robo tatu ya Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 77.403** ambayo ni sawa na asilimia **62.9** ya makusanyo yote kwa Mwaka mzima.

Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Fungu 52 imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 170.011** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 27** ikilinganishwa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2015/2016. Ongezeko hili ni kutokana na Wizara kuhuisha bei za huduma, kuimarishwa kwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ikiwemo mifumo ya kielekroniki kutoka katika Taasisi zilizoko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kwa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Fungu 53 Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 2.713** na hadi kufikia tarehe 31 Machi 2016, Idara iliweza kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 1.35** ambayo ni sawa na asilimia **49.8** ya makusanyo yote yaliyokadiriwa. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 Fungu 53 inakadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 2.382** ikiwa ni pungufu ya makadirio ya Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kwamba, kutokana na Makadirio ya Mapato yaliyofanywa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kuongezeka kwa asilimia 27 yakilinganishwa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ina uwezo wa kufanya makusanyo mengi zaidi na kuvuka lengo la makadirio hayo ikiwa itaimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato katika taasisi zote zilizoko chini yake. Kwa mfano, kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 Fungu 52 hadi kufikia Machi 31, 2016 ilivuka lengo kwa **asilimia 38** ya lengo walilojiwekea nao wamefanya ongezeko la makadirio kwa **asilimia 27** tu kwa maana ya **asilimia 11** kuachwa ikiwa haina maelezo kamili ya wapi itakwenda au kupotea, au kwanini haitafikiwa. Aidha, Kamati imeshangazwa na Wizara hiyo (Fungu 53) kupunguza kiwango cha Makadirio cha ukusanyaji wa mapato yake kwa **asilimia 12** kwa kigezo cha upungufu wa ukusanyaji wa ada za wanafunzi katika vyuo. Aidha, Kamati inaitaka Wizara kuangalia tena vyanzo vya mapato yake hasa katika Idara kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kuongeza mapato ya Fedha na kuweza kukudhi mahitaji yake kutoka katika vyanzo vyake vya ndani.

3.1.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa matumizi ya bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 katika Fedha zilizoidhinishwa, zilizopatikana pamoja na matumizi yake kwa Mwaka huo kadiri ya mgawanyiko wa kila Fedha katika maFungu yote mawili ya Wizara yaani Fungu 52 na Fungu

53. Ilikuwa ni matarajio ya Kamati kukutana na matokeo kwa **asilimia 75** ya Mwaka mzima katika Fedha zilizoidhinishwa, kutolewa na kutumika.

Aidha, Katika uchambuzi huo, Kamati imegundua kwamba, hadi kufikia mwezi Machi 2016 ambayo ni robo tatu ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, hakuna Fungu hata moja ambalo limeweza kupewa Fedha zilizoidhiishwa angalau kwa **asilimia 50** kutoka Hazina.

Kamati inasikitishwa na kitendo cha Serikali kutopeleka Fedha zilizoidhinishwa na Bunge hili Tukufu kwa Wizara hii pamoja na umuhimu wake katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Katika Uchambuzi wa Fungu 52- Idara Kuu Afya, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2016, kiasi cha Fedha kilichopelekwa na kutumika ni **asilimia 31** tu ya Bajeti nzima hali kadhalika Fungu 53 kwa Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Kwa mwenendo huu, Kamati inaona juhudi na mpango wa Serikali wa kujali Afya za wananchi wa Tanzania itabaki kuwa ndoto na hivyo kuendelea kuwa na Taifa lisilokuwa na Wananchi walio na Afya bora ambayo ndiyo msingi mkuu wa Maendeleo ya nchi. **Naomba kunukuu msemu mmoja wa Vikrant Parsai alisema “You are young if you are Healthy and Rich when you have no debts” kwa maana isiyo rasmi ni kwamba, Unakuwa kijana kama una afya na unakuwa tajiri kama huna madeni.** Kamati inaona kwamba kwa kutopeleka Fedha hizo kwa **asilimia 69** hadi Machi 2016 ambalo ni deni kubwa Serikali haijawatendea haki wananchi katika kutekeleza azma ya kuwapelekea huduma ya afya bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba Serikali kutokupeleka Fedha kwa wakati kunakwamisha Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Majukumu hayo ni pamoja na ununuzi wa dawa, vifaa tiba na kuwalipa watumishi katika kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ya kiofisi. Kutokana na tathmini hii, Kamati inaliomba sana Bunge liitake Serikali kutoa Fedha hizo zilizotengwa kwa Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 kabla ya Mwaka huo haujamalizika. Ulazima huu upo zaidi katika Fedha za maendeleo ambazo zimetolewa kwa **asilimia 4** tu katika Fungu 52 na **asilimia 9.3** katika Fungu 53 ambazo nazo ni Fedha za nje kwa maneno mengine hakuna Fedha za ndani zilizotolewa na Serikali. **Rejea Jedwali Na 2.**

Jedwali: Na.2: Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa na kiasi cha Fedha zilizopatikana

BAJETI			ILIYOIDHINISHWA	UPATIKANAJI	WA FEDHA
Na	FUNGU	MGAWANYO	Kiasi kilichoidhinishwa	Kiasi kilichopokelewa na kutumika hadi Machi 2016	Asilimia ya Fedha zilizopokelewa na kutumika
1.	52	OC	103,743,611,000	70,291,657,440	68
		Mishahara	236,354,660,000	150,198,142,039	63
		Maendeleo	440,642,452,000	18,195,700,420	4
		Jumla	780,740,723,000	238,685,499,908	31
2.	53	OC	11,038,075,000	3,870,651,121	51
		Mishahara	7,589,512,000	2,352,748,720	37
		Maendeleo	8,873,420,000	827,087,080	9.3
		Jumla	27,501,007,000	8,576,148,561	31.2

3.2 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii Fungu 52 (kwa iliyokuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii) ilitengewa kiasi cha shilingi **Bilioni 440,642,452,000.00** ambazo kati ya Fedha hizo shilingi **66,024,000,000.00** zikiwa ni Fedha za ndani na shilingi **374,618,452.00** zikiwa ni Fedha za nje.

Hadi kufikia Februari 2016 kiasi cha shilingi **363,114,914,729.00** ambayo ni sawa na asilimia **82.4** ya jumla ya Fedha zilizoidhinishwa zilipokelewa na kutumika. Kati ya Fedha hizo, kiasi cha shilingi **5,200,000,000.00** sawa na **asilimia 8** ambazo ni Fedha za ndani sawa na asilimia **8** na Fedha za nje ni kiasi cha shilingi **357,914,914,729.00** ambayo ni sawa na asilimia **95.5** ya Fedha zilizoidhinishwa.

Aidha, Fungu 53 Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Kwa iliyokuwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto) ilitengewa kiasi cha shilingi **8,873,420,000.00** ambapo shilingi **5,950,000,000.00** ni Fedha za ndani na shilingi **2,923,420,000.00** ni Fedha za ndani. Hadi kufikia Machi 2016 shilingi **827,087,080.00** ikiwa ni Fedha za nje sawa na **asilimia 28** ya Fedha za nje zilizoidhinishwa. Katika ziara za ukaguzi wa miradi, Kamati iliweza kutembelea mradi wa ujenzi wa **Bunkers** na vyumba maalum vya kusimika mashine, mradi wa upanuzi wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) katika ujenzi wa jengo la ghorofa saba na upanuzi wa Ofisi katika Bohari ya Dawa (MSD).

3.3 Matokeo ya Ukaguzi

3.3.1 Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI)

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Fungu 52, iliidhinishiwa kiasi cha shilingi **14,900,000,000** kwa ajili ya mradi katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road wa kujenga vyumba maalumu (Bunkers) kwa ajili ya kusimika mashine mpya za kisasa za kutibu saratani na hivyo kuimarisha huduma za tiba ya saratani. Aidha, Fedha hizo zililenga kufanya manunuzi ya mashine za kisasa za kutibu saratani "Linear Accelerator" LINAC, CT Simulator na kubadilisha chanzo cha mionzi. Katika mradi huu kulikuwa na makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na shirika la atomiki duniani ya kuchangia katika manunuzi ya mashine hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kwa ajili ya kutekeleza mradi huu ulioanza Machi 2015 na unatarajiwa kukamilika Juni 2016, Specifications za LINAC zimekwisha andaliwa na kupitishwa na taratibu za ununuzi wa mashine zinaendelea. Aidha, mpaka Kamati inakwenda kufanya ukaguzi wa mradi huo, shughuli za ujenzi wa vyumba maalumu kwa ajili ya kuhifadha mashine hizo ulikuwa umefikia katika hatua nzuri ya kukamilika kwa asilimia 95 ambapo mradi upo katika hatua za umalizikaji wa kufanya ukuta kuwa laini (scheming), kuweka sakafu, mifumo ya umeme, mifumo ya maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa mradi huu, kuna changamoto ambazo zimeikabili Taasisi ya Ocean Road zikiwemo Fedha za mradi kutokutolewa kwa wakati ambapo kati ya Fedha zilizotengwa ni **asilimia 26** tu ndizo zilizopelekwa na kufanyia shughuli za utekelezaji wa mradi huo kusuasua.

Aidha, Shirika la Atomiki duniani (International Atomic Energy Agency - IEA) wameweka bayana kwamba kwa sasa hawataweza kuchangia ununuzi wa mashine hiyo kwa sababu ya Serikali kuchelewesha utoaji wa Fedha kwa wakati (2013/2014) kinyume na makubaliano yalivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imesikitishwa na kukosekana kwa Fedha hizo kwa sababu ya uzembe wa Serikali yetu kutotimiza makubaliano ya utoaji wa Fedha. Pamoja na Wizara kutoa taarifa katika Ofisi ya Rais Tume ya Mipango juu ya uamuzi wa kutokutolewa kwa Fedha hizo na kusisitiza juu ya umuhimu wa Fedha iliyobaki kutolewa kwa sasa, Kamati inaliomba Bunge liitake Serikali kukamilisha utoaji wa Fedha hizo tengwa kwa asilimia 74 iliyobaki ili kuweza kukamilisha mradi huo.

3.3.2 Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

Mheshimiwa Spika, Kamati iliweza pia kufanya ziara ya Ukaguzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pamoja na Taasisi zake ikiwemo Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Katika ukaguzi wa mradi wa upanuzi wa MOI awamu ya III ambao ni ujenzi wa jengo la ghorofa saba (7) kwa ajili ya kutolea huduma ya uchunguzi ikiwemo CT-Scan, MRI, X-Ray, Ultra Sound, vyumba vya upoasujaji, maabara, hifadhi ya damu, huduma za dharura, ICU, vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu, vyumba vya wagonjwa wanaohitaji uangalizi wa karibu, vyumba vya wagonjwa wa kulipia na kuchangia. Kukamilika kwa mradi huu ambao utagharimu jumla ya shilingi **bilioni 27.23** ambazo ni mkopo ambao Taasisi hiyo imekopa kutoka katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kudhaminiwa na Serikali. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha Hospitali kuwa na vitanda vya kulaza wagonjwa 340 na kuweza kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la wagonjwa kulala chini.

Mheshimiwa Spika, Kiwango cha Utekelezaji wa mradi ni cha kuridhisha ambao umefika katika kiwango cha **asilimia 95**. Na **asilimia 5** zimebaki kukamilishwa kwa kiasi cha Fedha shilingi **bilioni 9.26** ambazo bado Serikali haijapeleka. Aidha, ununuzi wa vifaa tiba na samani uliotengewa na Serikali kiasi cha shilingi **bilioni 12.5** katika bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 bado haujafanyika kwani Serikali bado haijatoa Fedha hizo. Hata hivyo Kamati imeshtushwa na ongezeko la gharama za ujenzi huo kwani katika baadhi ya makadirio ya ujenzi huo kuna ongezeko kwa zaidi ya mara 10 ya gharama zilizokadiriwa mwanzo. Kamati inaliomba Bunge likubali kuiagiza Serikali kufanya uchunguzi wa ongezeko la gharama hizo ili kuweka bayana gharama halisi za ujenzi wa jengo hilo. Pili, Kamati inaliomba Bunge likubali kuitaka Serikali kutoa Fedha zilizobaki shilingi **bilioni 9.26** kabla ya Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 haujaisha tarehe 31 June 2016 ili kukamilisha mradi huo na jengo lianze kutumika kwa makusudio yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Rais Mh Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuruhusu jengo hilo kuanza kutumika ili katika kuendeleza juhudi za utoaji wa huduma bora ya afya kwa wananchi hasa katika kutatua changamoto ya wagonjwa waliokuwa wanalala chini katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Kamati inaunga mkono maamuzi hayo ya kuwasaidia wagojwa kutoendele kulala chini.

3.3.3 Bohari ya Dawa (MSD)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ukaguzi katika Bohari ya Dawa (MSD) ambapo kuna mradi wa upanuzi wa ofisi za Bohari hiyo ulioanza Julai 2013. Mradi ulitengewa kiasi cha shilingi **bilioni 7.39** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ya Bohari ya Dawa. Mpaka kufikia Machi 2016 kiasi cha shilingi **bilioni**

5,159,184,372 zilikuwa zimeshatolewa na kutumika na mradi umekamilika kwa **asilimia 68** kwa maelezo kuwa **asilimia 32** itakamilika ifikapo mwezi Mei 2016. **Kamati inaiomba Serikali kuendelea kuisimamia Bohari ya Dawa kuweza kutoa kiasi kilichobaki katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 ili kuweza kukamilisha mradi huo ili kuweza kutatua tatizo la uhaba wa ofisi kwa watumishi wa Bohari hiyo.**

3.3.1 Matokeo na Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016

Mheshimiwa Spika, Baada ya Kamati kufanya ziara katika miradi iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Kamati ina Maoni yafuatayo;

(i) Kamati inashauri Serikali itoe Fedha za upanuzi wa majengo katika Taasisi ya MOI, Hospitali ya Muhimbili pia itafute namna ya kukopa Fedha kutoka katika Taasisi mbalimbali nchini kama vile NSSF ili iweze kuendelea na upanuzi wa majengo kwani idadi ya wagonjwa inaendelea kuongezeka siku hadi siku na majengo kubaki yale yale hivyo kusababisha msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili;

(ii) Kutokana na makisio ya gharama kuongezeka kwa kiasi kikubwa Kamati ilishangazwa na maelezo kuwa makisio yalikuwa chini wakati mkandarasi anafanya makisio. Mfano gharama za uingizaji wa gesi (medical gas installation) kutoka milioni 120 hadi kufikia bilioni 1. Kamati inaitaka Wizara na Hospitali kuandaa taarifa maalum inayoeleza kwa kina ni kwanini gharama hizo zimepanda kwa kiasi hicho;

(iii) Kamati inashauri Serikali itoe dhamana (Guarantee) ili MOI iweze kupewa Mkopo wa kumaliza ujenzi wa jengo kiasi cha shilingi **bilioni 9.2** kutoka katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ambao ndiyo ulitoa mkopo wa awali. Ikumbukwe kuwa jengo hilo limeanza kutumika kufuatia maelekezo ya Mhe. Rais ili hali likiwa bado halijakamilika kwa kufanya hivyo kutapunguza matukio hatarishi yanayoweza kusababishwa na kutokukamilika kwa jengo hilo;

(iv) Kwa kuwa mkopo huu wa ujenzi haujumuishi ununuzi wa vifaa tiba na samani kwa ajili ya jengo jipya la Taasisi ya MOI, na kwa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Fedha hizi ziliidhinishwa na Bunge lakini hakuna Fedha yoyote iliyotolewa, Kamati inapendekeza Serikali itoe Fedha zilizoombwa na MOI kiasi cha shilingi **bilioni 12.7** kabla ya Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 haujaisha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na samani ili kuleta mantiki na tija ya ujenzi wa jengo hilo;

(v) Serikali iongeze bajeti ya Taasisi ya Ocean Road kwani haiendani kabisa na huduma zinazotolewa. Idadi ya wagonjwa wanaotibiwa inaongezeka kila siku wakati bajeti inaendelea kupungua kila Mwaka na ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa Sera ya Afya ya Taifa, wagonjwa wa Saratani wanatakiwa kupata huduma hii **BILA MALIPO**. Kamati ilipokea malalamiko ya wagonjwa waliokuwa wakisubiri huduma wakielezea changamoto kubwa ni ya upatikanaji wa dawa kwa gharama kubwa za kununua dawa na kusubiri kwa muda mrefu kupata huduma kutokana na uhaba wa miundombinu zikiwemo mashine;

(vi) Katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road wataalam wanaotoa huduma ya tiba ya mionzi wanafanya kazi katika mazingira hatarishi sana. Kamati inashauri watumishi hao walipwe posho maalum ya kufanya kazi katika mazingira hatarishi (**Risk Allowances**) ili kuwapa motisha ya kuendelea kufanya kazi ambayo kwa ufupi ni hatari kwa maisha yao.

(vii) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa huduma za matibabu ya magonjwa ya Moyo katika Taasisi ya Jakaya Kikwete, ambayo imepunguza gharama kubwa za matibabu nje ya nchi. Kutokana na kuwepo kwa Taasisi hii kwa Mwaka 2015 zimeokolewa takribani shilingi **4,000,000,000.00** za serikali kwa kutoa matibabu ya moyo kwa wagonjwa 207 waliotakiwa kwenda kupata matibabu nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuingiza gharama za matibabu hayo katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili gharama hizo zilipwe na Bima zikiwemo gharama za vipandikizi, vifaa tiba pamoja na matibabu kwa makundi maalumu wakiwemo watoto wa chini ya miaka mitano kwa mujibu wa Sera ya Afya, badala ya Taasisi kuingia gharama hizo za kununua vifaa tiba pekee na mgonjwa kulipa gharama za oparesheni (Operational Procedure) ambapo inaisababishia Taasisi kuwa na mzigo mkubwa na hivyo kushindwa kujiendesha na kukua katika utoaji wa huduma za matibabu ya Moyo.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Wizara inatarajia kutekeleza jumla ya malengo matano (5) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Malengo hayo ni pamoja na:

(i) Kutoa huduma bora za afya ya msingi katika ngazi ya jamii na vituo vya kulelea watoto,

(ii) Kutoa huduma zinazofikika na kwa usawa kwa kutoa kipaumbele kwa maeneo yenye mzigo mkubwa wa magonjwa na kwa kuzingatia makundi yenye mahitaji maalumu;

(iii) Kushirikiana na jamii kikamilifu kwa lengo la kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma;

(iv) Kutoa njia za kisasa katika usimamizi ikiwa ni pamoja na ubunifu katika utoaji wa huduma;

(v) Kushirikiana na Sekta mbalimbali na kuhamasisha ujumuishwaji wa masuala ya Sekta ya Afya katika sera na mikakati ya Sekta nyingine;

Mheshimiwa Spika, Kamati iliridhika na malengo hayo ya Wizara kwa kuwa yanashabihiana na malengo ya utoaji wa Huduma bora za Afya nchini ambayo yamejumuishwa katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Pia malengo hayo yameainishwa katika vipaumbele vya Taifa kupitia Mipango na Sera mbalimbali za Taifa ikiwemo Sera ya Taifa ya Afya, Mpango wa Taifa wa awamu ya II, Mpango wa Afya ya Msingi (MMAM 2007-2017) na Mpango Mkakati wa Nne wa Sekta ya Afya (HSSP IV 2016-2020).

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii ina maFungu mawili kama nilivyoeleza awali. Katika Fungu 52 (Idara Kuu Afya) pamoja na Taasisi zake inatarajia kukusanya Mapato kiasi cha shilingi **170,011,902,000.00** ikiwa ni ongezeko la shilingi **47,012,960,500.00** ambayo ni sawa na **asilimia 27.6** ya kilichokadiriwa kukusanywa Mwaka wa Fedha wa 2015/2016 ambayo ni shilingi **122,998,941,500.00**. Aidha, Fungu 53 (Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto) inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi **bilioni 2.382** ikiwa ni pungufu ya makadirio ya Mapato ya Mwaka 2015/2016 ambayo yalikadiriwa kuwa kiasi cha shilingi **bilioni 2.713**. Upungufu huo ni kiasi cha shilingi **milioni 331** ikiwa sawa na **asilimia 12.2**.

Mheshimiwa Spika, Katika makadirio ya makusanyo ya Mapato ya Wizara Fungu 52, makusanyo makubwa yanatarajiwa kutoka katika kifungu **000** Mashirika yaliyo chini ya Wizara, kiasi cha shilingi **146,968,868,000.00** ambayo ni sawa na **asilimia 86.4** ya makadirio ya makusanyo yote, ambapo kifungu hiki kitakusanya Fedha zitokanazo na uchangiaji wa huduma za afya katika Hospitali zilizo chini ya Wizara, ada za usajili, tozo na ada za huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi, Mashirika na Hospitali.

Makadirio ya kiasi kidogo kabisa yanatarajiwa kutoka katika **kifungu 1001** cha kiasi cha shilingi **125,356,000** kutokana na mauzo ya nyaraka za tenda na marejesho ya masurufu kutoka kwa watumishi waliosafiri kutokana na sababu

mbalimbali ambazo zitarudishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa utaratibu maalum.

Aidha, Fungu 53, mapato yake makubwa yanatarajiwa kutokana na ada za wanafunzi katika vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii ambapo kiasi cha shilingi **bilioni 2.08** ambayo ni sawa na **asilimia 87.5** ya makadirio yote yanayotarajiwa kukusanywa na kiasi kidogo cha makusanyo kitatokana na mauzo ya vitabu vya Zabuni ambacho ni shilingi **3,000,000.00**.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona Makadirio hayo ya Fedha yapo chini kwani Wizara ikiweka mifumo bora na imara ya ukusanyaji wa Mapato, Wizara itakusanya Fedha nyingi zaidi ya makadirio ambayo Wizara imejiwekea. Kamati imeliona hilo kwa sababu, Katika makadirio ambayo Wizara ilijiwekea kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 iliweza kuvuka malengo yake hadi kufikia **asilimia 152** katika **kifungu 2001** cha Tiba na Mwaka wa Fedha 2016/2017 wameweza kujikadiriya hadi kufikia **asilimia 406** ambayo kutoka kiasi cha shilingi **bilioni 2.888** hadi shilingi **bilioni 14.619**. Hivyo basi ni imani ya Kamati kwamba Wizara inaweza kuongeza makusanyo ya mapato hayo hata katika vyanzo vingine vya mapato ndani ya Wizara.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Wizara kupitia Fungu 52 (Idara Kuu ya Afya) inaomba jumla ya makadirio ya matumizi ya Fedha kiasi cha shilingi **bilioni 796.115** Katika Fedha hizo kiasi cha shilingi **bilioni 277.604** sawa na **asilimia 28** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kiasi cha shilingi **bilioni 518.511** sawa na **asilimia 72.0** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara kupitia Fungu 53, imekadiriya kufanya matumizi ya jumla ya **shilingi bilioni 48.997** ambapo kati ya Fedha hizo shilingi bilioni **40.148** ambayo ni sawa na **asilimia 82** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwemo Mishahara ya Watumishi na matumizi mengineyo na kiasi cha shilingi **bilioni 8.848** sawa na **asilimia 18** ni Fedha kwa ajili ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Katika makadirio haya kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 yameongezeka kwa kiasi cha shilingi **bilioni 15.375** (Fungu 52) na kiasi cha shilingi Bilioni **21.496** (Fungu 53). Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii kwani inaleta imani kubwa na kuendelea kuonesha nia ya Serikali kuleta huduma nzuri na bora za Afya kwa wananchi wake ili kuweza kujenga taifa lenye watu wenye afya bora kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla. Kuna msembo kwa tafsiri isiyo rasmi unasema Taifa tajiri linaanza na watu wenye afya (***A Wealthy Nation begins with Healthy People***). Malengo na matakwa ya muda mrefu ya wananchi hayawezi kufikiwa bila kuwa na watu wenye afya na maisha yenye furaha. Ongezeko hili la Fedha inaonesha muendelezo wa kulifikia lengo la Abuja 2002 pamoja na ukomo wake kuwa

umepita tangu Mwaka 2015 lakini halituzuii kuendelea kuongeza bajeti ya Afya katika nchi yetu kulingana na ukuaji wa uchumi wa chi yetu.

SEHEMU YA TATU

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZOI YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, Kutokana na Uchambuzi wa kina wa makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 uliofanyika mnamo tarehe 12-13 Aprili 2016, Kamati ina Mapendekezo, Maoni na Ushauri katika maeneo kumi na mbili (12) yafuatayo:

5.1 Mfumo wa Usimamizi wa Masuala ya Sekta ya Afya

Mheshimiwa Spika, Wakati Kamati inafanya Uchambuzi wa Utekelezaji Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2016/2017, Wajumbe walibaini changamoto ya mfumo wa **Developmet by Devolution** umesababisha Wizara na Kamati kukosa mamlaka ya kufuatilia kwa karibu ikiwa ni pamoja na kuwawajibisha watendaji walioko chini ya Wizara husika na hivyo kupunguza ufanisi katika Sekta hii.

Hii ni kutokana na Wizara ya Afya kupewa mamlaka katika usimamizi wa **SERA** pekee mbayo ni sehemu ambayo haimuwezeshi mwananchi kuona mafanikio ya utoaji wa huduma ya afya na kuacha sehemu kubwa kuwa katika Wizara nyingine. Kwa mfano Watumishi kama Waganga, Wauguzi na Maafisa maendeleo ya Jamii wote wako chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Wizara imepewa madaraka ya kusimamia Sera za Sekta ya Afya na Utekelezaji wake upo katika Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kwamba, Masuala yote yanayohusu Sekta ya Afya yarejeshwe Katika Wizara ya Afya ili iweze kusimamia kuanzia Sera, Watumishi na Miundombinu badala ya kutenganisha katika Wizara mbili tofauti hali inayosababisha TAMISEMI kuonekana ni kichaka au kimbilio la kutotekeleza shughuli za Afya wakati Kamati inapohitaji Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu yake yasiyo ya Kisera. Kamati inashauri, kama haitawezekana kuondoa masuala Afya TAMISEMI, ni vyema ukaandaliwa mfumo bora wa mawasiliano, Ushirikiano na Uwajibikaji kati ya Wizara ya Afya na (TAMISEMI) katika kutoa Taarifa za Matumizi ya Fedha ili ziliwasilishwe katika Kamati zote mbili ya Huduma na Maendeleo ya Jamii na TAMISEMI.

5.2 Bajeti ya Sekta ya Afya kwa ujumla

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 inaonekana kuongezeka kitakwimu kila Mwaka, lakini Kamati inaona kwamba ongezeko hilo la Fedha haliendani na hali halisi ya thamani ya Fedha, hivyo Kamati inashauri

kutenga Fedha za Sekta ya Afya ikizingatia thamani ya Fedha ya nchi na dunia kiujumla kwani Fedha hizo ni ndogo ukilinganisha na mahitaji makubwa ya Sekta ya Afya. Ikumbukwe kwamba Afya ndiyo msingi wa maendeleo ya nchi yeyote duniani, naomba kunukuu **Mr. Gro Harlem Brundtland** aliwahi kusema”**(Health is the Core of Human Development)**”.Hivyo basi tukitaka kusonga mbele kimaendeleo Serikali ihakikishe inatenga Fedha za kutosha katika Sekta ya Afya ambapo ndiko kitovu cha maendeleo ya nchi kipo.

5.3 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi ya kukosa dawa muhimu (*Essential Medicines*) katika vituo vya kutolea huduma ya Afya. Na hii pia ilidhihirika wakati Kamati ilipotembelea Boharii Kuu ya Dawa (MSD) na kujionea ghala ya dawa muhimu likiwa tupu na ghala za magonjwa mengine kama Dawa za kupunguza makali ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), Chanjo n.k. Hali ya ukosefu wa dawa inawaumiza wananchi wenye Bima za Afya, fedha taslimu kupata haki yao ya msingi wanapokwenda hospitali kupata matibabu. Kamati inaitaka Bohari Kuu ya Dawa kuweka muda maalumu wa upelekaji wa dawa katika Vituo vya kutolea huduma ya afya mara baada ya kupokea fedha toka kwa wateja wao.

5.4 Serikali kutopeleka Fedha za Miradi kwa Wakati

Mheshimiwa Spika, Wakati wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2015/2016, Kamati iligundua kwamba mpaka kufikia mwezi Machi 2016 ambayo ni robo tatu ya Mwaka wa Fedha unaoisha, Wizara ilikuwa imepata **asilimia 31** tu ya bajeti iliyopitishwa, Kamati inaishauri Serikali kupitia Hazina kupeleka Fedha hizo kabla ya Mwaka wa Fedha haujaisha, ili Wizara iweze kutimiza malengo yale yaliyojiwekea kwa ajili ya kuimarisha Afya za wananchi wetu. Ikumbukwe kwamba taifa ambalo lina watu ambao hawana uhakika na afya zao kwa maana ya kwamba hakuna huduma bora za Afya ni Taifa legelege na ni taifa ambalo haliwezi kufanya kazi za uzalishaji ili kukukuza uchumi wake hivyo Taifa hilo kuwa **MASIKINI**.

5.5 Makadirio ya chini ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 yamekadiriwa kwa kiwango cha chini sana ukifanya ulinganifu wa Mapato ya Wizara hii na kwakuwa Wizara yenyewe imeieleza Kamati kupitia Taarifa zao za Mwaka wa Fedha 2015/2016 kuwa walifanikiwa kukusanya Maduhuli zaidi ya kile walichokikadiria kwa kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa Mapato. Hivyo basi, Kamati inashauri Wizara kuendelea kuweka mifumo bora na imara kwa ajili ya kuhahakisha Fedha zote halali zinakusanywa kwa ajili ya

kuimarisha huduma bora za afya kwa wananchi, makusanyo yatokanayo na Wizara hii ni vyema yakakusanywa kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya.

5.6 Fedha za Ujenzi wa Kiwanda cha Dawa za Asili (NIMR)

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 NIMR ilitengewa jumla shilingi milioni 800 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Kiwanda cha kutengeneza dawa asili lakini mpaka Kamati inakutana na Wizara hakuna fedha iliyotolewa. Kutokana na umuhimu wa Kiwanda hicho katika kutengeneza dawa asili Kamati imeiagiza Wizara katika Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017 kufanya *Re-allocation* kwenye mafungu yake na kuipatia NIMR kiasi hicho cha fedha shilingi milioni 800 ili mradi huu uweze kukamilika. Kamati inaendelea kusisitiza fedha hizi zitolewe zote na kwa wakati.

5.7 Vifo vya Akina mama vinavyotokana na Uzazi

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na vifo vingi vya akina mama vinavyotokana na masuala ya uzazi, ikiwemo wakati wa ujauzito, wakati wa kujifungua na hata ndani ya siku arobaini (40) baada ya kujifungua. Tunaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuendelea kupunguza vifo hivi hapa nchini lakini bado hali hairidhishi. Takwimu zinaonesha kwamba takribani akina mama **15,056** wanapoteza maisha kila mwaka na hii maana yake ni kwamba ni akina mama **1,255** wanafariki kila mwezi na kila siku Tanzania inapoteza akina mama **42** na kila baada ya saa moja akina mama wawili (**2**) wanaaga dunia.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano gari aina ya *Coaster* yenye uwezo wa kubeba abiria **36** toka Dodoma kuelekea Morogoro ikapata ajali na ikaua watu wote ndani ya gari hiyo, Rais au Waziri mwenye dhamana atafunga safari kuelekea katika eneo la tukio na hata kusababisha Bunge kusimama kwa dakika moja kuwaombea marehemu na hata kuahirisha shughuli za Bunge kwa ajili ya ajali hiyo na vifo hivyo vilivyotokea. Kwa maneno mengine kila siku ajali ya *Coaster* iliyobeba akina mama **36** waliokaa kwenye viti na wengine **6** waliosimama inatokea na inaua akina mama wote kulitakiwa kulifanya Bunge hili kila siku liwe linasimama kwa ajili ya kuwaombea akina mama hao **42** wanaofariki kwasababu ya Uzazi na hakuna anayeshituka kuona kama hii ni hatari kubwa kwa taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali, kuwanusuru akina mama hawa **42** wanaopoteza maisha kila siku wakati wakitimiza wajibu wao wa kiasili wa kuongeza watu duniani ambao kimsingi hawana hatia kabisa. Akina mama hawa ni wake zetu, watoto wetu, mawifi zetu, dada zetu, binamu zetu, mama zetu, shemeji zetu na ni watanzania wenzetu kwa ujumla.

5.8 Uhaba wa vituo vya kutolea Huduma ya Afya nchini

Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya inatuelekeza kuwa na Zahanati kila kijiji, Kituo cha Afya kila Kata. Ukiangalia takwimu za idadi ya Kata hapa nchini ni takribani 3800, kwa maana hiyo basi mpaka kufikia sasa nchi yetu ilitakiwa iwe na Vituo vya Afya visivyopungua **3800** au tunakaribia kufikia idadi hiyo. Kamati inasikitishwa kuelezwa na Wizara kwamba vituo vya Afya nchini vya Serikali ni **484**, vinavyomilikiwa na Mashirika ya Kidini **141**, vituo vya afya binafsi ni **79** na vituo vya taasisi ni **12** ambavyo jumla yake ni vituo vya afya **716** tu ambayo ni sawa na asilimia **18.8** ya mahitaji ya vituo vya afya kisera. Kamati inaiomba Serikali kuhakikisha inaitekeleza Sera ya Afya ya kuwa na Zahanati, Vituo vya afya na hata Hospitali za Wilaya kama Sera inavyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, Kwa kufanya hivyo, kutasaidia kupunguza vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi ambavyo vingine vinasababishwa na akina mama kujifungulia nyumbani kwa kukosa huduma ya uzazi katika maeneo ya karibu na wanapoishi.

5.9 Uhaba wa Watoa huduma ya Afya nchini

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na changamoto ya uhaba wa watoa huduma ya afya katika vituo vingi vya kutolea huduma ya afya katika nchi yetu. Na hii ni kwasababu Serikali haijaamua kuajiri watoa huduma hao ya afya ili wakafanye kazi. Takwimu zinaonesha kuna zaidi ya wataalamu elfu thelethini (30,000) lakini kibali kilichotoka cha kuajiri ni wataalamu elfu kumi tu (10,000) ambayo ni theluthi moja tu ya wataalamu waliopo ambao hawajaajiriwa, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo wa wataalamu hao kuajiriwa ili wakatoe huduma kwa wananchi wetu na kupunguza changamoto ya vituo vya kutolea huduma ya afya kukosa wataalamu.

5.10 Tofauti za kiwango cha Mishahara kwa Madaktari

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na changamoto ya uhaba wa Madaktari katika Hospitali katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Na hii ni kutokana na maslahi duni kwa wataalamu hao toka Serikalini na hata yale yanayopatikana yamekuwa na utofauti hasa katika mishahara. Madaktari wamekuwa wakisita kwenda kutoa huduma katika Hospitali za Mikoani kutokana na utofauti huo wa malipo. Kwa mfano, Madaktari wenye Shahada ya kwanza (*1st Degree*) waliomaliza masomo pamoja, wale watakaokwenda kufanya kazi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, KCMC, Bugando au Hospitali ya Rufaa Mbeya mishahara yao itatofautiana na Madaktari watakao kwenda kufanya kazi katika Hospitali ya Mkoa wa Rukwa, Katavi, Ruvuma, Mara na maeneo

mengine. Hali hii inapelekea Madaktari wengi kukataa kwenda kufanya kazi katika Hospitali za Mikoani kwa sababu ya utofauti wa mishahara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inshauri Serikali kufanya marejeo ya mishahara na maslahi mengine kwa ajili ya wataalamu wetu ili kuleta usawa bila kujali wapi anakwenda kufanya kazi kwakuwa wote wana taaluma inayofanana na ikiwezekana kuwapa motisha zaidi wale wanaokubali kwenda kufanya kazi maeneo ya pembezoni ikiwemo motisha ya kufanya kazi katika mazingira magumu (**Hardship Allowances**) ili kuwawezesha Madaktari kwenda katika maeneo mbalimbali hapa nchini ili kutoa huduma ya Afya kwa Watanzania popote walipo.

5.11 Mafunzo ya Shahada ya Juu kwa Madaktari walioko Kazini

Mheshimiwa Spika, Katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilibaini kwamba Bajeti ya Mafunzo ya Shahada ya Juu kwa Wataalamu wa Udaktari (Postgraduate Degree) imeondolewa katika Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Na kwa Mujibu wa majibu kutoka Wizara ya Afya ni kwamba jukumu hilo limepelekwa katika Wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kamati inatia mashaka kwamba kama kweli TAMISEMI imetenga fedha hiyo kwa ajili ya kuwapeleka Madaktari hao katika masomo ya Elimu ya juu na kama wataipa uzito unaostahili kwa kuwa TAMISEMI ina kada nyingi inazosisimamia katika kuwapeleka watumishi wake masomoni. Aidha, Kamati inashauri fedha hizo zitengwe na zirudishwe katika Wizara ya Afya ili wao waweze kusimamia kwa ukamilifu kwa kuangalia mahitaji ya Madaktari Bingwa kwa nchi nzima na kuwapeleka masomoni. Kwa kufanya hivyo basi nchi itakuwa na uhakika wa kupata Madaktari Bingwa kulingana na uhitaji na kuwawezesha Wananchi wote wanapata matibabu hapa nchini bila ya Serikali kuingia gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi.

5.12 Ongezeko la Watu kwa kasi kubwa nchini

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa takwimu, hadi kufikia Mwaka 2100 Tanzania itakuwa ni nchi ya saba duniani na ya pili katika Bara la Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya watu. Takribani ya watu milioni moja (1,000,000) huongezeka kila Mwaka kwa wastani wa uzazi wa watoto watano (5) kwa kila mwaamke aliye katika umri wa kuzaa maana yake ni ongezeko kubwa na la kasi. Kamati inaishauri Serikali na Wizara yake kuendelea kutenga bajeti ya kutoa elimu kwa wananchi wetu kuhusu matumizi ya Uzazi wa Mpango na kuimarisha huduma katika Sekta nyingine ikiwemo Elimu, Uchumi ili kuweza kusaidia Taifa hili kuweza kudhibiti ongezeko la watu nchini. Ikumbukwe kwamba ongezeko hilo la watu haliendani na ongezeko la rasimali nyingine ikiwemo ardhi. Kamati inatoa rai kwa viongozi wote wa nchi wakiwemo wa

kisiasa, kidini na hata kimila kulizungumzia suala hili kwa nia njema kabisa ili kuwa na taifa imara na bora na lenye afya kwa idadi inayoendana na rasilimali zilizopo.

5.13 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kukopesha kwa faida (NHIF)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekuwa ikikopa Fedha kutoka katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kutekeleza shughuli za maendeleo ya Sekta ya Afya na Fedha hizo kutorejeshwa kwa wakati na bila riba, Kamati inashauri Serikali kuuruhusu Mfuko huo kuweza kukopesha kwa faida ili kuendelea kuukua Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya badala ya kukaa na Fedha ambazo hazizalishi. Pia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iombe kupewa dhamana (**Guarantee**) kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kununua Vifaa Tiba kwa ajili ya Hospitali zote za Rufaa za mikoa nchini ili kuweza kuboresha huduma ya afya na kuwapa fursa wananchi kupata huduma hizo katika Hospitali hizo na kwa kufanya hivyo, kutapunguza sana msongamano mkubwa unaoikumba Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Waziri wa Afya kwa kuwachukulia hatua kali (kwa kutumbua majipu) watendaji wabadhilifu wa Mfuko wa NHIF kwa kufanya ubadhilifu katika Ofisi za Mkoa wa Mara. Pia Kamati inamshauri Waziri kufanya uchunguzi wa kina katika Mikoa mingine na kuona kama hakuna ubadhilifu mwingine kama huo. Aidha, Kamati inamshauri Waziri kuendelea kuimarisha mifumo ya uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

5.14 Bima ya Afya kwa Wajawazito, Watoto na Wazee

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sera ya Afya ya nchi yetu, zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wakiwemo watoto chini ya miaka mitano (5), Wajawazito na Wazee wenye umri kuanzia wa miaka sitini (60) na kuendelea wanatakiwa kupata matibabu bila malipo, hivyo basi Kamati inashauri Serikali kuhakikisha makundi hayo tajwa yanapewa Bima ya Afya ili kuwawezesha kupata huduma ya afya yenye uhakika lakini pia kuweza kuwapunguzia mzigo wa malipo hayo Hospitali husika wanapokwenda kupata matibabu bila malipo kama Sera ya afya inavyoelekeza.

5.15 Marekebisho ya Viwango vya Malipo ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Mheshimiwa Spika, Katika utoaji wa huduma ya afya kwa wananchi katika Hospitali za Serikali na Binafsi, kumekuwa na upendeleo wa kutoa huduma hiyo kwa kuangalia aina ya Bima ya mteja au mgonjwa hasa katika Hospitali zinazomilikiwa na watu au mashirika Binafsi kwa kigezo cha ucheleweshwaji wa malipo kutoka katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na viwango vya malipo kuwa chini vilivyopangwa na Mfuko huo na matokeo yake

kuwapendelea wale wagonjwa wanaolipa Fedha taslimu. Suala hili linapelekea kuleta ukakasi katika upatikanaji wa huduma ya afya kwa wananchi hasa wanapotumia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Kamati inaiomba na kuishauri Serikali, kuangalia tena viwango hivyo vya malipo vinavyoendana na hali halisi ya gharama za matibabu na kuweka mifumo bora ya kuharakisha malipo hayo ili wananchi waendeleo kufaidika na huduma bora za afya kwa kutumia Bima zao za afya.

5.16 Maendeleo na Ustawi wa Jamii

Mheshimiwa Spika, Maendeleo na Ustawi wa jamii wa nchi hii huanzia katika ngazi ya familia, Mtaa, Kijiji na Kata. Katika kutafuta maendeleo hayo wananchi wanahitaji wataalamu wa kuwashauri namna gani ya kufikia maendeleo hayo kwa Ustawi bora wa jamii husika. Changamoto imekuwa kubwa katika kupatikana kwa wataalamu wa Ustawi na Maendeleo ya jamii. Hadi mwezi Machi 2016 kuna upungufu wa wataalamu hao kwa **asilimia 66.3** ya mahitaji ya nchi nzima. Hata hivyo kwa wale ambao wapo hakuna uwiano wa mgawanyo wa Wataalamu hao. Kuna maeneo ambayo yamepewa Maafisa Maendeleo ya Jamii kuzidi mahitaji yake ikiwemo Manispaa ya Temeke, Ilala, Kinondoni, Monduli lakini pia kuna maeneo ambayo hayana kabisa wataalamu hao zikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Bahi, Nyag'wale, Kyerwa, Mlele, Lindi, Mji wa Bunda, Chalinze, Sikonge, Nzega na maeneo mengine mengi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba kila Kata katika nchi hii inapatiwa wataalamu wa Maendeleo ya jamii na Ustawi wa Jamii ili kushirikiana na wananchi katika kujiletea maendeleo katika maeneo yao ifikapo mwisho wa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inapeleka Fedha zote zitakazoidhinishwa na Bunge katika masuala ya Maendeleo ya jamii, kwani imekuwa ni kawaida kuifanya Idara hii kuwa haina msingi na umuhimu ili hali ni sehemu nyeti na ya muhimu sana katika kulifanya Taifa hili linastawi na kuendelea katika misingi yote na Sekta zote ikiwemo Elimu, Kilimo, Afya na Kiuchumi.

5.17 Uhamasishaji wa kuzuia Magonjwa yasiyo ambukiza (Non-Communicable Diseases)

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Wizara imejikita sana katika kutenga Fedha kwenye masuala ya **TIBA** ya magonjwa mbalimbali yanayoambukiza na yasiyo ambukiza. Kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa yasiyo ambukiza kama kisukari, kansa, magonjwa ya moyo yatokanayo na mabadiliko ya kimaendeleo, teknolojia, miundo mbinu n.k . Kamati inaishauri Wizara pamoja na Serikali, kuanzisha programu ambazo zitaweza kuwahamasisha wananchi kuzuia magonjwa hayo kwa kufanya mazoezi, umuhimu wa Lishe bora. Pia, Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) wafanye utafiti wa kina na takwimu zake zitumike katika kupanga vipaumbele vya

kutekeleza shughuli za kuzuia magonjwa hayo kutokea, kama tunavyofahamu Kinga ni bora kuliko Tiba (**Prevention is Better than Cure**). Aidha, kuna magonjwa mengiikiwemo udumavu wa akili na mwili ambayo yanaweza kuzuilika kuanzia mtoto akiwa tumboni mpaka siku elfu moja (siku 1000) kwa mjamzito kupata Lishe bora. Kamati inaishauri Wizara kuipatia Taasisi ya Chakula na Lishe jukumu la kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa lishe bora kwa watanzania pia kuhamasisha jamii katika kufanya jitihada za kuzuia magonjwa yasiyoambukiza.

5.18 Bei kubwa ya Maziwa ya Watoto ya S26

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kumekuwepo na mtu moja ambaye anahodhi (Monopolize) uzalishaji wa **Maziwa ya Watoto S26** hali inayopelekea Maziwa hayo kuuzwa kwa bei ya juu ikilinganishwa na gharama halisi. Maziwa hayo ambayo yanazalishwa nchini Afrika ya Kusini bei yake halisi ni kati ya shilingi 8,000/= hadi 10,000/= za kitanzania, lakini kwa kuwa amekuwepo mtu mmoja tu ambaye ameelekezwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kuingiza Maziwa ambayo yanakuja yakiwa yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili maziwa hayo yanauzwa kati ya shilingi 30,000/= hadi 35,000/=kwa kopo moja bei ambayo ni kubwa ambayo inapelekea wazazi wengi kushindwa kumudu. Kamati ina amini kazi ya TFDA ni kuangalia ubora wa bidhaa na siyo kupanga bei. Hivyo basi Kamati inashauri kuwepo na soko huru lenye kuruhusu maziwa yote ya **S26** yaliyoandikwa kwa Kiswahili na Kiingereza kuingizwa nchini hali itakayopelekea bei ya Maziwa hayo kushuka.

5.19 Utunzaji wa Wazee

Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na msemo ya mtoto wa leo ni Taifa la kesho na kusahau kuwa kijana wa leo ni mzee wa kesho. Serikali imejisahau katika utunzaji wa wazee wa nchi hii ambao walitumikia nchi kwa nguvu na kwa moyo wao wote kwa kutokujali makazi yao na hata kuwasahau katika kuwahudumia chakula na malazi bora. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara kuhakikisha wazee hao wana boreshewa huduma zao zikiwemo masuala ya malazi bora, chakula na matibabu ili kuliepusha Taifa hili kuingia katika laana isiyo ya msingi kutoka kwa wazee hao walioko katika makazi maalumu ya kuwatunza wazee wetu na inayoweza kuzuilika kwa kuwathamini na kwa kuwapa huduma bora. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya sensa ya wazee na kuunda sheria ya kuwapa jukumu watoto na ndugu wa karibu kuwatunza wazee wao bila kusahau mila na desturi za nchi yetu kwamba watoto wana jukumu la kuwatunza wazazi wao wanapofikia umri wa uzee.

5.20 Benki ya Wanawake Tanzania

Mheshimiwa Spika, Kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake ililenga kuwafikia wanawake wote nchi Tanzania ili kuwawezesha kiuchumi kwa kuwapa mikopo yeye riba na masharti nafuu. Lakini utekelezaji wake umekuwa wa kusua sua na katika maeneo machache sana na kuacha wanawake wengi

kutofikiwa katika maeneo mengi nchini. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Benki hiyo kimtaji ili iweze kufungua matawi mengi nchini ili azma hiyo ya kuwasaidia wanawake wa nchi hii iweze kufikiwa. Pia Kamati inaishauri Benki ya Wanawake kuanzisha Dirisha la akina mama litakalowawezesha Wanawake nchini kupewa mikopo kwa Riba nafuu ambayo siyo ya Soko ili kuleta unafuu kwa Wanawake katika kupata mtaji na kuweza kujikomboa na umasikini. Aidha katika jitihada za kukuza mtaji wa Benki hii, Kamati inaishauri Wizara na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufungua akaunti zao katika Benki ya Wanawake ili kuiinua kwa kupata Fedha za uendeshaji (*Operational Fees*) badala ya fedha hizo kuzipeleka katika Benki nyingine.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto Mheshimiwa Ummy A. Mwalimu (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Hamis Kigwangala (Mb) kwa ushirikiano wao mkubwa waliutoa wakati Kamati ilipokuwa ikijadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vilevile napenda kuwashukuru Katibu Mkuu wa Wizara Idara kuu Afya na Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Maafisa Waandamizi na Wizara na Taasisi zake zote kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati hii ya kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wadau wetu wote wa Sekta ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa ushirikiano wao mkubwa wanautoa kwa Serikali yetu katika kuendelea kutoa huduma bora ya Afya kwa wananchi wetu. Naomba kuwataja kwa uchache Wadau hao ni pamoja na PEPFAR, Mfuko wa Fedha wa Dunia (Global Fund) kwa mchango wao wa kifedha za maendeleo katika nchi yetu. Pia Kamati inawapongeza Taasisi ya Benjamin Mkapa kwa jitihada zao za kuendelea kupeleka Wataalamu wa afya wakiwemo Madaktari, Wauguzi katika maeneo mbalimbali nchini na hata kujenga vituo vya kutolea huduma ya afya. Kamati inawaomba sana Wadau hao kuendelea kuwa na ushirikiano huo na Serikali yetu katika kuendelea kuboresha huduma katika Sekta ya Afya. Aidha, Kamati inaiomba Serikali na Wizara kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa Wadau hawa ili kupata mafanikio makubwa katika Sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Kwa nafasi ya pekee kabisa naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Uzoefu na utaalamu wao katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta ya Afya umesaidia kufanikisha kazi hii kwa

ufanisi mkubwa. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina Waheshimiwa wafuatao:

1. Mhe. Peter J. Serukamba, Mb, - Mwenyekiti
2. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hussein Mohamed Bashe, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Dkt. Charles J. Tizeba, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Peter A. P. Lijualikali, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Joseph O. Mbilinyi, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Faustine E. Ndugulile, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Kasuku S. Bilago, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Dkt. Elly M. Macha, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Lucia Ursula M. Mlowe, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Dkt. Jasmine T. Bunga, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Susan Anselm Lyimo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Juma S. Nkamia, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Seleman S. Bungara, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Zitto Z. R. Kabwe, - Mjumbe
16. Mhe. Boniphace M. Getere, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Bernadetha K. Mushashu, - Mjumbe
18. Mhe. Neema William Mgaya Mb -Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, Ndugu Athman Brambath Hussein Mkurugenzi Idara ya Kamati za Bunge kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kipekee, nawashukuru Ndugu. Dickson Bisile, Bi. Pamela Pallangyo na Bi. Agnes Nkwera (Makatibu Kamati) na Mwimbe John msaidizi wao kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja Fungu 52 jumla ya shilingi **796,115,856,780.00** na Fungu 53 jumla ya shilingi **48,997, 063,276.00**.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Mh. Peter Joseph Serukamba (Mb),

MWENYEKITI

KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII

11 MEI, 2016

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, juu ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa ruhusa ya kusoma Hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima wa afya njema kuweza kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Ninachukua nafasi hii kumshukuru Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe, kwa kunianimi na kuiteua kusimamia jukumu hilo zito kwa kuwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, katika Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimshukuru, nimpungeze Spika, Naibu Spika pamoja na wewe kwa kuteuliwa jana kwa kuonesha kwamba umeungwa mkono na pande zote. Ninategemea uweze kuliunganisha Bunge hili liweze kuwa kitu kimoja, siyo tu katika mambo kama ya dole, lakini mambo mazito yanayolihusu Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niwashukuru wananchi wa Wilaya ya Siha kwa kuniadini na kunichagua kuwa Mbunge wao, bila kumsahau mke wangu Elivesta Godwin Mollel. Hakika naahidi kufanya kazi hii ya kuwakilisha kwa moyo mkunjufu na kamwe sitawaangusha, naahidi uwakilishi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inadai kuwa imedhamiria kuwa ya uchumi wa kati na viwanda. Azma hii inaonekana kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2020. Hii itawezekana tu kama Taifa lenye afya na lenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa ajili ya huduma za jamii kama afya bila kutegemea wadau wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati bajeti ya Taifa imepanda kwa zaidi ya takribani shilingi trilioni 6.5 kutoka shilingi trilioni 22 ya mwaka 2016 hadi shilingi trilioni 29 ya mwaka 2016/2017 bajeti ya Wizara ya Afya imepungua kwa shilingi bilioni 18 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hii inamaanisha kuwa Wizara ya Afya haijapata kipaumbele. Maana yake ni kwamba huduma za afya zitakuwa mbaya na hafifu kuliko katika mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Afya sambamba na ongezeko la Bajeti ya Taifa ili angalau sekta ya afya ibakiwe kuwa na asilimia 11.4 ya Bajeti ya Taifa kama ilivyo katika mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kupungua kwa fedha za wadau na maendeleo ilianza kuonekana tangu kwenye kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne, toka mwaka wa fedha wa 2015/2016 mpaka 2016/2017 kwenye sekta ya afya wadau wa maendeleo wamepunguza pesa za kibajeti kutoka shilingi bilioni 374.6 mpaka bilioni 198.4 ikiwa ni punguzo la shilingi bilioni 179 sawa na asilimia 47. Hii ina maana kuwa bila Serikali kutenga fedha zake yenyewe huduma za afya zitadorora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye juhudi za maksudi kutenga fedha zake yenyewe, ili wadau wa maendeleo wakiondoka Taifa liendeleo kuwa na afya kwa kuwa, afya ya wananchi ni jukumu la msingi la Serikali. Kitendo cha Serikali kushindwa kutimiza jukumu lake la msingi kumepelekea kukubali masharti yanayotolewa na ambayo yanakiuka maadili na mila na tamaduni za Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*). Mpango huu ulilenga kuwahudumia wananchi nchi nzima ulionesha kusuasua sana hususan maeneo ya vijijini. Hata hivyo, unakumbwa na changamoto lukuki ikiwemo kukosa usawa (*uniformity*) katika uchangiaji. Baadhi ya wanachama kushindwa kuendelea kuchangia, hakuna mfumo unaoleweka wa kufanya rufaa. Uhamasishaji duni na kampeni hafifu katika kutangaza mpango huu. Kutokuwa na mfumo imara wa ukusanyaji taarifa za wanachama, hususan maeneo ya vijijini na kukosekana kwa mawasiliano kama ilivyoainishwa katika Mpango wa *CHF* iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko huu kwa muda mrefu haujaweza kuleta tija iliyotegemewa hasa kwenye kufikia watu wengi. Taasisi nyingi za tiba zimekwepa kutokana na kuwa hela hizi zinakwenda Wilayani na mara nyingi haziwarudii wahusika. Kumekuwa na mifuko mbalimbali ya bima ya afya ya jamii kama *CHF*, *TIKA* na kadhalika na kumekuwa na ushauri wa kuiunganisha mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri tofauti kidogo, tunashauri kuweko na bima moja ya Taifa (*National Health Insurance – NHIF*) kwa kila Mtanzania mwenye kitambulisho cha uraia. Hii itafanya Taifa liwe na afya na kurahisisha uendeshaji wa shughuli za afya kwa urahisi na uendeshaji wa kila hospitali kuwa rahisi. Najua swali linakuwa ni nani atalipia bima hiyo kwa raia wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jibu ni rahisi sana, ni kuangalia bila kuathiri mambo mengine wala kusababisha athari kwa thamani ya hela zetu kwa kila kodi kuwepo kodi maalum ya bima ya afya na uadilifu wa kutosha uwepo kupeleka gawio hilo bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya hospitali zilizotembelewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ni hospitali binafsi zinazoendeshwa kwa kutoa huduma kwa sifa inayolingana na Hospitali zetu za Wilaya na za Rufaa. Baadhi ya hospitali hizo kwa taarifa hazipati kabisa ruzuku kutoka Serikalini, lakini ubora wa huduma zake kuanzia upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa tiba na huduma ni nzuri kuliko za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama mapato ya hospitali hizo kwa kiasi kikubwa yanatokana na bima. Hivyo basi, ukiwapa Watanzania wote bima kwa kiasi kikubwa, hospitali zetu zitapata uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa madawa, vitendanishi na baadhi ya vifaa tiba. Vilevile watu wetu watapata nafasi kubwa ya kupata huduma pale wanapoona huduma ni bora na kuongeza ushindani wenye tija kwa manufaa ya wagonjwa na Taifa. Lakini vilevile Serikali kujitoa kwenye uendeshaji wa siku hadi siku wa hospitali za Serikali ikajikita kwenye miradi mizito zaidi ya kuboresha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari ya Dawa (MSD). Upungufu wa madawa unaweza kuongezeka kwani Serikali imetenga shilingi bilioni 65.1 kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Kiasi hiki kinatosha mahitaji ya nchi kwa mwezi mmoja na nusu tu. Kwa kukadiria kuwa Tanzania ina watu takribani milioni 49.8 wanaohitaji matibabu, kiasi kilichotengwa kinatosha kutibu watu milioni 5.6 kwa mwaka. Je, watu wengine milioni 48 watakaobaki watatibiwa na nini na ni wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali iongeze bajeti ya dawa kutoka asilimia 11 yaani shilingi bilioni 6.1 mpaka angalau asilimia 50 ya mahitaji yaani shilingi bilioni 295.9. Ili dawa na vifaa tiba visambazwe MSD inahitaji kupewa fedha iliyoomba. Mpaka Machi, 2016 MSD walikuwa wakiidai Serikali shilingi bilioni 131. Serikali imetenga shilingi bilioni 108 kulipa deni la nyuma hivyo kubakiza deni la shilingi bilioni 23. MSD waliomba kutengewa shilingi bilioni 114 kwa ajili ya ukomboaji wa mizigo bandarini na kusambaza dawa na vifaa tiba, wametengewa shilingi bilioni 35 tu, kiasi hiki kikipungua kwa shilingi bilioni 79.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hiki kilichotengwa kinakidhi mahitaji ya MSD kwa miezi minne tu. Je, Serikali inataka dawa na vifaa tiba viozee bandarini kwa miezi mingine? Ikiwa MSD itakopa ili kujiendesha kwa mwaka basi inahitaji kukopa shilingi bilioni 79 hivyo deni lake mpaka Juni 2017 itakuwa ni shilingi bilioni 102, tutakuwa tumetengeneza deni jipya la kulipa mwakani. Utaona tunaenda kutengeneza deni lingine la shilingi bilioni mbili kwenye eneo moja tu, bandari

na usafirishaji. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iongeze bajeti ya MSD angalau kulipia deni lote ambalo baki yake ni shilingi bilioni 23 na hela za usafiri na bandari shilingi bilioni 79.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI walioko kwenye dawa mpaka mwaka 2015 inakisiwa kuwa watu 670,000 waliokuwa kwenye matibabu ya ARV. Kiasi hicho kinakadiriwa kuongezeka na kufikia watu 988,000 mpaka Julai, 2017. Kiasi kilichoombwa ni shilingi bilioni 451 lakini kiasi kilichotengwa ni takribani shilingi bilioni 48 sawa na asilimia 11. Kama wastani wa kila mtu anahitaji dola 120 kwa mwaka basi fedha iliyotengwa inatosha kutibu watu takribani 200,000 tu. Hii ina maana kuwa hata wale waliokuwa kwenye matibabu watakosa dawa, zaidi ya watu 400,000 watakosa dawa za ARV hivyo itakuwa ni janga lingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze pesa kwa ajili ya UKIMWI kutoka asilimia 11 yaani shilingi bilioni 48 mpaka angalau asilimia 50, shilingi bilioni 218. Timu ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilitembelea nchi ya Kenya kujua hali ya dawa kwenye hospitali zao na kujifunza uwekezaji katika viwanda vya dawa. Katika ziara hiyo Kenya pamoja na Tanzania tumejifunza kuwa viwanda vyetu vinatengeneza dawa katika *stage* ya umalizaji (*finishing industry*), tunaagiza dawa nje tunakuja kumaliza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali ianze kujiwekeza katika hali ya kuhakikisha tunaweza kutengeneza baadhi ya dawa na kutafuta vitu vya kutengeneza dawa katika nchi yetu. Kwa mfano Lushoto, kuna miti ya mikwinini na vilevile katika nchi za kitropiko kuna miti ya *artemisia* ambayo tunaweza kutumia majani yake kutengeneza dawa maarufu aina ya ALU. Inamaanisha kwamba tukiwekeza katika eneo hili, tutaweza kupunguza kwanza gharama za uagizaji wa dawa, tutaiingizia nchi pato, lakini vilevile upatikanaji wa dawa utakuwa wa uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, afya ya mama na motto. Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 46(1)(g) inaelezea wazi haki za wanawake kupata huduma ya afya. Pamoja na haki zao kutambuliwa katika Katiba na sera mbalimbali bado wanawake wamekuwa wakiteseka sana na wengi kupoteza maisha kwa sababu ya huduma duni za afya. Waathirika wakubwa zaidi katika sekta hii ya afya ni wanawake wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya vifo vinavyotokana na uzazi katika nchi yetu ni ya kutisha. Katika ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka huu 2016 (*World Bank 2016 Maternal Mortality Ratio*) takwimu zinaonesha vifo vinavyotokana na uzazi kwa mwaka 2011 ni 483, kwa mwaka 2012 ni 464, kwa mwaka 2013 ni 438, kwa mwaka 2014 ni 418, kwa mwaka 2015 ni 398 kwa kila wanawake 100,000. Hali hii inaonesha bado juhudi zinahitajika kufanywa na Serikali kuhakikisha

inapunguza kabisa vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi. Kiwango hiki ni sawa na akina mama 1,255 kwa mwezi na akina mama 42 kila siku sawa na akina mama wawili kwa saa. Kama ukiwakusanya hawa akina mama wanaokufa ni zaidi ya basi la abiria aina ya coaster wanakufa kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii zetu tunatambua mchango mkubwa anaoutoa mama katika malezi na makuzi ya familia ikiwemo kuchangia katika kipato cha familia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, wanawake wanatoa mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi japo wengi hufanya kazi katika mfumo usio rasmi, tena kwa kipato kidogo na mazingira magumu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango mkubwa alionao mwanamke ndani ya familia na Taifa kwa ujumla, ni vyema Serikali ikauthamini sana. Mama anapofariki mara nyingi waliobaki katika familia husika wanapata taabu sana, familia nyingi husambaratika kabisa. Watoto wengi wameishia kuwa ombaomba, kujihusisha na biashara za ngono, dawa za kulevya na hata kukosa kabisa mwelekeo wa maisha. Kwa umuhimu wa kipekee, Serikali haina budi kuja na mkakati wenye tija kupunguza vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuhakikisha inakuja na mpango madhubuti ulio rahisi katika kumaliza tatizo hili la vifo vya akina mama. Ni lazima Serikali itekeleze wajibu wake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mtoto na mama wanaishi kama agenda ya Kitaifa inavyotaka. Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya tathmini ya uhakiki kuhakikisha inajua idadi kamili ya vifo vya akina mama vinavyotokana na uzazi kwani bado akina mama wengi wanazalia nyumbani hasa maeneo ya vijijini ili kuweza kubaini athari za kiuchumi zinazotokana na vifo vya akina mama pamoja na kupata mkakati wa kutatua tatizo hili na kuhakikisha inapunguza vifo vinavyotokana na uzazi na akina mama ambapo bado takwimu siyo za kutosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe mwaka 2010/2011 jumla bajaji 400 zilinunuliwa kwa fedha za walipa kodi zitumike kama *ambulance* za kusafirishia wajawazito kwenda hospitalini. Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa za uhakika za kushindwa kufanya kazi kwa bajaji hizo na nyingi kutelekezwa kutokana na changamoto za kijiografia za maeneo mbalimbali na ubovu wa miundombinu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi lakini ni dhihaka kwa akina mama wajawazito. Kambi Rasmi ya Upinzani

Bungeni inahoji Serikali ni kigezo gani walitumia kufikia maamuzi ya kununua pikipiki hizo ambazo ziligharimu shilingi milioni 26 kwa kila moja huku ikionekana kabisa pikipiki hizo mama akikamatwa na uchungu akiwa juu ya pikipiki hiyo uwezekano wa kuipindua pikipiki hiyo ni mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki jinsia na afya ya mwanamke. Kuna uhusiano mkubwa sana katika kuongeza rasilimali katika elimu ya mtoto wa kike na kuboresha afya ya mama, mtoto na jamii kwa ujumla. Vilevile kuna uhusiano wa kupata jamii fumbuzi yaani *innovative society*. Zifanyike jitihada za makusudi kuondoa kabisa mila na desturi zinazopuuza uwezo wa akili ya mwanamke na nafasi ya mwanamke kwenye jamii. Kuthamini akili ya mwanamke, kuheshimu mwili wa mwanamke na kumpa mwanamke elimu bora sio tu itaboresha maisha ya mwanamke bali italiboresha Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la utapiamlo kwa watoto nchini. Tatizo la ukosefu wa chakula nchini na lishe duni bado linaathiri familia nyingi hasa watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kutokana na lishe duni, watoto wamekuwa wakiugua utapiamlo na kudumaa. Kutokana na madhara haya watoto wengi wanaathirika ubongo na kupunguza uwezo wa akili na hata wakifika umri wa utu uzima huathirika uwezo wao wa kuzalisha na kuchochea umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na *Ifakara Health Institute*, takwimu zinaonesha zaidi ya watoto milioni 2.5 katika Taifa hili wamedumaa na vifo vinavyotokana na utapiamlo ni takribani vifo 43,000 kwa mwaka. Pamoja na hayo, watoto wenye utapiamlo uliokithiri ni takribani watoto laki nne kila mwaka na miongoni mwao walio katika hatari ya kufa endapo hatua za haraka hazitachukuliwa ni takribani watoto 100,000. Kwa idadi hii, vifo vinavyotokana na utapiamlo takwimu zinaonesha mtoto mmoja hufariki kila baada ya dakika 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ripoti mbalimbali za afya zinaonesha Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye tatizo kubwa la utapiamlo Barani Afrika na duniani. Kwa ujumla tumefikia kufananishwa na Congo DRC iliyoko katika vita. Katika ripoti hizo ikiwemo Shirika la Utafiti la TWaweza inaonesha Tanzania ni ya kumi duniani kwa ukubwa wa tatizo hili ukilinganisha na nchi kama Ethiopia ikiwa ya saba, Sudani ya Kusini ikiwa 15 ambazo nchi hizi zimekuwa zikikumbwa mara kwa mara na balaa la njaa, hii ni aibu kwa ustawi wa jamii yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko ina mkakati gani wa kuhakikisha inatumia mfumo wa kuongeza virutubisho katika kila lishe inayokwenda sokoni ili kuhakikisha wananchi wanakula mlo wenye virutubisho, vilevile kusaidia jamii kutofautisha kati ya lishe na shibe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rasilimali watu katika sekta ya afya. Kwa takwimu za Wizara ya Afya za mwaka 2014, kuna watumishi wa afya 15 kwa kila watu 10,000 ilhali Shirika la Afya Duniani linapendekeza kuwepo watumishi 41 kwa kila watu 10,000 ili kuweza kutoa huduma bora za afya kwa kila mwananchi. Pamoja na Tanzania kuwa ni nchi yenye uhaba mkubwa wa wataalam wa tiba, wale wachache waliopo wamekuwa wakipata tabu kubwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Mazingira wanayofanyia kazi ni hatarishi, kuanzia hali ya shughuli zao hata uduni wa huduma za afya kutokana na ukosefu wa dawa na vifaa tiba na kupelekea lawama nyingi kuelekezwa kwa Madaktari, Wauguzi hadi kufikia kupigwa na wananchi wanaokosa huduma hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya afya ni sekta ya utoaji huduma, hivyo utendaji katika sekta hii kama zilivyo sekta nyingine za utoaji wa huduma zinategemea kwa kiasi kikubwa watendaji wake wana morali ya kazi kwa kiasi gani na akili zao ziko katika hali ya utulivu kwa kiasi gani. Utoaji wa huduma unategemea kwa kiasi kikubwa aina ya vifaa vilivyopo, morali ya kazi inayotokana na jinsi gani watendaji wanapata mahitaji yao ya kimsingi ili nao wasiwe katika hali ya kukata tamaa ya maisha na kutokuweka vizuri akili ili watoe huduma kwa upendo wenye ari kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kujitafakari upya kuhusu maslahi ya watoa huduma katika sekta nzima ya afya ili matarajio yao yaweze kufikiwa. Ukweli ni kwamba unaweza ukawa na dawa, vifaa tiba na vitendanishi bila watendaji walio na moyo wa kazi, hakuna huduma bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira za wataalamu wa afya. Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kupatiwa sababu za kwa nini wanafunzi waliohitimu mafunzo kwenye sekta ya afya na maendeleo ya jamii hawajapatiwa ajira ilhali kuna upungufu mkubwa wa utumishi hao hususani katika vituo vilivyojengwa chini ya mpango wa MMAM na kwa nguvu za wananchi. Inakadiriwa kuwa wataalam hao wa afya ambao hawajaajiriwa kwa mwaka 2015 ni takribani 1,025 hadi sasa. Tunaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni hatua zipi za haraka zitachukuliwa kwa ajili ya kuwaajiri wahitimu hawa na kuziba pengo lililopo baina ya mahitaji halisi ya watoa huduma na wahitaji wa huduma za afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali za Wilaya na Hospitali Teule za Wilaya. Uendeshaji wa hospitali za Wilaya umeendelea kuwa wa kusuasua na mgumu kutokana na Serikali kutotenga fedha za kutosha kwa maendeleo, vifaa tiba, dawa na vitendanishi. Pamoja na baadhi ya Hospitali za Wilaya kuendelea kuandikia na kutoa taarifa kwa Wizara juu ya upungufu huo, hali imeendelea kujirudia kila mwaka inayosababisha ukwamaji wa shughuli mbalimbali kama utoaji wa huduma za afya kwa wananchi ambao wengi wana kipato cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali Teule za Wilaya ni moja ya wahanga wa tatizo hili. Fungu la dawa ni dogo, fungu la pamoja limepunguzwa na fungu la matumizi mengineyo halipelekwi kabisa ilhali shughuli za msingi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha pamoja na idadi ya wagonjwa zinaongezeka kila siku.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kutoka fedha za ndani ili kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi katika utendaji wa Hospitali Teule. Nitolee mfano Hospitali ya Selian, pamoja na kutoa huduma za mama na mtoto bure, wazee bure, watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI bure, saratani bure, huduma za watoto bure, yatima zaidi ya 600 na upasuaji wa fistula bure na kuwatembelea wagonjwa majumbani, baadhi ya huduma hizi hospitali za Serikali hazitoi, ikizingatiwa kuwa bei ya tiba ni sawa bado huduma za hospitali za dini ni bora kuliko za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kufikiri kirahisi kuwa hospitali za dini kuwa zinapata msaada toka nje lakini tujiulize Serikali na dini nani mwenye jukwaa bora zaidi la kusema na wahisani? Bila shaka ni Serikali. Hospitali hizo Teule pamoja na kutopata ruzuku kama ilivyo kwenye mikataba, bado wanatoa huduma bure zilizopo kwenye sera ya umma cha kushangaza huduma zao ni nzuri kuliko hospitali za Serikali. Kwa mfano, hospitali hiyo inalipa watu mishahara kwa mwezi shilingi milioni 178 ambapo milioni 80 zinatoka Serikalini na shilingi milioni 98 wanakusanya kwenye makusanyo ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kujiuliza ni kwamba hospitali za Serikali hawalipi mishahara kutoka mapato ya ndani, mishahara inatoka Serikalini, lakini huduma zake bado ziko chini ukilinganisha na hizi Teule pamoja na kuwa majukumu na tozo zao zinafanana. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia kwa makini tatizo liko wapi na kutafuta tiba ya kudumu ili kuondoa tatizo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali za Mikoa zina hali isiyoridhisha na huduma hazikidhi mahitaji yanayotakiwa kutolewa kama zilivyoitwa Hospitali za Rufaa na za Mikoa. Hali hii inatokana na bajeti ndogo toka Serikalini pamoja na mitazamo mibovu ya uendeshaji.

Kambi Rasmi ya Upinzani ilitembelea hospitali zaidi ya tano za Mikoa, katika hospitali mojawapo ya Mkoa tuliwakuta wakiandaa bajeti kulingana na kiwango cha fedha walichoagizwa yaani ukomo wa bajeti. Tulikuja kugundua katika Hospitali hiyo moja ya Mkoa, waliomba kwa muda wa miezi minne vitendanishi vya maabara. Baada ya miezi minne ndiyo walipata majibu kutoka MSD lakini cha ajabu tulikuta hapo waliwekewa kwa mwezi mmoja matumizi ya

vitendanishi vya maabara ni shilingi milioni 12 lakini katika bajeti yao waliotengewa mwaka ujao wa fedha ni shilingi milioni 13, hii inamaanisha kwa miezi 11 wataenda kuendesha hospitali bila vitendanishi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kuuliza kama maabara itaendeshwa bila kuwa na vitendanishi, je, hospitali hiyo itakuwa ni hospitali au itakuwa ni kituo cha kupiga ramli? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduka kwenye hospitali za Serikali. Maduka ya MSD yalipelekwa karibu na hospitali za Serikali sio tu kwamba yanapingana na dhana ya *cost sharing* (uchangiaji wa afya) lakini vilevile imeenda kuthibitisha kwamba dhana iliyokuwa imeaminika kwamba ni Madaktari wanaiba dawa siyo kweli ila ni MSD haina dawa. Niseme tu vilevile ni dhana iliyoeleweka vibaya kwamba baadhi ya hospitali kuanzisha maduka nje ya hospitali kwani lengo lilikuwa ni kuweka dawa zile ambazo haziko ndani ya *catalogue* ya MSD na hazipatikani MSD na kuweza kufanya ndani ya hospitali wagonjwa waweze kupata dawa zote kwenye mzunguko mmoja wa hospitali. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali iende ikajifunze kutoka kwenye hospitali hizo ili kuweza kuhakikisha mgonjwa anapoingia ndani ya hospitali basi dawa ziweze kupatikana katika eneo la hospitali kama ilivyokuwa lengo na siyo kama sasa ilivyoeleweka vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kusema shujaa ni mtu yule anayemjali mtoto wa kike. Mimi ni shujaa, je, wewe ni shujaa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naomba kuwasilisha. (Makofi)

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIWA DR GODWIN OLOYCE MOLLEL (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2016)

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema ya kuweza kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Nachukua nafasi hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mhe. Freeman A. Mbowe kwa kuniamini na kuniteua kusimamia jukumu hili zito kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, niwashukuru wananchi wa wilaya ya Siha kwa kuniamini na kunichagua kuwa mbunge wao, bila kumsahau mke wangu Elivester Godwin Mollel, hakika naahidi kufanya kazi hii ya uwakilishi kwa moyo mkunjufu na kamwe sitawaangusha, bali naahidi uwakilishi uliotukuka.

Mheshima Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inadai kuwa imedhamiria kuwa ya uchumi wa kati na viwanda. Azima hii inaonekana kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016-2020). Hii itawezekana tu kwa taifa lenye afya, na lenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwaajili ya huduma za jamii kama afya bila kutegemea Wadau wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wakati bajeti ya Taifa imepanda kwa zaidi ya takribani Trilioni 6.5 (kutoka trilioni 22.4 ya mwaka 2015/16 hadi trilioni 29 ya mwaka 2016/17), bajeti ya Wizara ya Afya imepungua kwa bilioni 18 kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hii inamanisha kuwa Wizara ya Afya haijapata kipaumbele, maana yake ni kwamba huduma za afya zitakuwa mbaya na hafifu kuliko katika mwaka wa fedha unaoisha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Afya sambamba na ongezeko la bajeti ya Taifa ili angalau sekta ya afya ibakie kuwa 11.4% ya bajeti ya Taifa kama ilivyo katika mwaka unaoisha.

Mheshimiwa Spika, Hali ya kupungua kwa fedha za Wadau wa Maendeleo ilianza kuonekana tangu kwenye kipindi cha serikali ya awamu ya nne, na toka mwaka wa fedha wa 2015/16 mpaka 2016/17 kwenye sekta ya afya, Wadau wa Maendeleo wamepunguza pesa za kibajeti kutoka shilingi bilioni 374.6 mpaka bilioni 198.4 ikiwa ni punguzo la shilingi bilioni 179 sawa na asilimia 47%. Hii ina maana kuwa bila ya serikali kutenga fedha zake yenyewe, huduma za afya zitadorora zaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye juhudi za makusudi kutenga fedha zake yenyewe ili Wadau wa Maendeleo wakiondoka taifa letu liendelee kuwa na afya kwa kuwa afya ya wananchi ni jukumu la msingi la Serikali. Kitendo cha Serikali kushindwa kutimiza jukumu lake la msingi kumepelekea kukubali masharti yanayotolewa na ambayo inakiuka maadili, mila na tamaduni za kitanzania.

2.0 MFUKO WA BIMA YA AFYA YA JAMII (CHF)

Mheshimiwa Spika, Mpango huu uliolenga kuwahudumia wananchi nchi nzima umeonyesha kusuasua sana hususani maeneo ya vijijini. Hata hivyo unakumbwa na changamoto luluki ikiwemo kukosa usawa yaani (**uniformity**) katika uchangiaji, baadhi ya wanachama kushindwa kuendelea kuchagua, hakuna mfumo unaoeleweka wa kufanya rufaa, uhamasishaji duni na kampeni hafifu katika kutangaza mpango huu, kutokuwa na mfumo imara wa ukusanyaji taarifa za wanachama hususani maeneo ya vijijini na kukosekana kwa mawasiliano (unreliable network) kama ilivyodainishwa katika mpango wa CHF Ulioboreshwa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu kwa muda mrefu haujaweza kuleta tija iliotegemewa hasa kwenye kufikia watu wengi, taasisi zingine za tiba zimekwepa kutokana na kuwa hela hizo kwenda wilayani na mara nyingi haziwarudii wahusika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mifuko mbalimbali ya bima ya afya ya jamii kama CHF, TIKI etc na kumekuwa na ushauri wa kuunganisha mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri tofauti kidogo, tunashauri kuwe na bima moja ya taifa yaani NHIF kwa kila mtanzania mwenye kitambulisho cha uraia, hii itafanya taifa liwe na afya na kurahisisha uendeshaji wa shughuli za afya kuwa rahisi na uwendeshaji wa kila hospitali kuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika najua swali litakuwa ni nani atalipia bima hiyo kwa raia wote, jibu ni rahisi sana ni kuangalia bila kuadhiri mambo mengine wala kusababisha athari kwa thamani ya hela zetu, kwa kila kodi kuwepo kodi maalumu ya bima ya afya na uadilifu wa kutosha uwepo kupeleka gawio hilo bima

Mheshimiwa Spika, moja wapo ya hospitali zilizotembelewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ni hospitali za binafsi zinazoendeshwa kwa kutoa huduma kwa sifa inayo lingana na hospitali zetu za wilaya na za rufaa, baadhi ya hospitali hizi kwa taarifa hazipati kabisa ruzuku kutoka serikalini lakini ubora wa huduma zake kuanzia upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa tiba na huduma, ni nzuri kuliko za serikali.

Mheshimiwa Spika, ukitizama mapato ya hospitali hizo kwa kiasi kikubwa yanatokana na bima. Hivyo basi ukiwapa watanzania wote bima kwa kiasi kikubwa hospitali zetu zitapata uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa madawa na vitendanishi na baadhi ya vifaa tiba, vivile watu wetu watapata nafasi kubwa ya kupata huduma pale wanakoona huduma ni bora na kuongeza ushindani wenye manufaa kwa mgonjwa na taifa, lakini vivile serikali kujitoa kwenye uendeshaji wa siku hadi siku wa hospitali serikali ikajikita kwenye miradi mizito zaidi ya kuboresha afya.

3.0 BOHARI YA DAWA (MSD)

Mheshimiwa Spika, Upungufu wa madawa unaweza kuongezeka kwani Serikali imetenga shilingi bilioni 65.1 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, kiasi hiki kinatosha mahitaji ya nchi kwa mwezi mmoja na nusu tu. Kwa kukadiria kuwa

Tanzania ina watu takribani milioni 49.8¹ wanaohitaji matibabu, kiasi kilichotengwa kinatosha kutibu watu milioni 5.6 kwa mwaka. Je, watu wengine milioni 44 wanaobaki watatibiwa na nini na wapi?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali iongeze bajeti ya madawa kutoka 11% (shilingi bilioni 65.1) mpaka angalau 50% ya mahitaji (shilingi bilioni 295.9).

Mheshimiwa Spika, Ili dawa na vifaa tiba visambazwe, MSD inahitaji kupewa fedha illiyoomba. Mpaka Machi 2016, MSD walikuwa wanaidai serikali shilingi bilioni 131. Serikali imetenga shilingi bilioni 108 kulipa deni la nyuma, hivyo kubakiza deni la shilingi bilioni 23. MSD waliomba kutengewa shilingi bilioni 114 kwa ajili ya ugomboaji wa mizigo bandarini (Clearance & Forwarding) na kusambaza madawa na vifaa tiba. Wametengewa shilingi bilioni 35 tu, kiasi hiki kikipungua kwa shilingi bilioni 79.

Mheshimiwa Spika, Kiasi hiki kilichotengwa kinakidhi mahitaji ya MSD kwa miezi minne tu. Je, serikali inataka dawa na vifaa tiba viozee kwenye bohari na bandarini kwa miezi mingine? Ikiwa MSD itakopa ili kujiendesha kwa mwaka mzima, basi itahitaji kukopa shilingi bilioni 79 hivyo deni lake mpaka Juni 2017 litakuwa shilingi bilioni 102. Tutakuwa tumetengeneza deni jipya tena la kilipa mwakani .

Mheshimiwa Spika, Utaona tunaenda kutengeneza deni lingine la billion 102 kwenye eneo moja tu ,bandari na usafirishaji ,Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iongeze bajeti ya MSD angalau kulipia deni lote ambalo baki yake ni shilingi bilioni 23 na hela za usafiri na bandari bilioni 79.

Mheshimiwa Spika, Watu wanaoishi na virusi vya ukimwi walioko kwenye dawa mpaka Machi 2015, watu 670,000 walikuwa kwenye matibabu (ARV), kiasi hicho kinakadiriwa kuongezeka na kufikia watu 988,000 mpaka Julai 2017. Kiasi kilichoombwa ni shilingi bilioni 451 lakini kiasi kilichotengwa ni takribani shilingi bilioni 48 sawa na 11%. Kama kwa wasitani kila mtu anahitaji dola 120 kwa mwaka, basi fedha iliyotengwa inatosha kutibu watu takribani 200,000 tu. Hii ina maana kuwa hata wale waliokuwa kwenye matibabu watakosa dawa; zaidi ya watu 400,000 watakosa dawa za ARV. Hili litakuwa ni janga jingine.

Mheshimiwa Spika, Serikali iongeze fedha kwa ajili ya UKIMWI kutoka 11 % (shilingi bilioni 48) mpaka angalau 50% (shilingi bilioni 218).

¹ NBS (2015) inakadiri kuwa mpaka 2014 Tanzania Bara ilikuwa na watu milioni 47.4 ongezeko la watu milioni 1.2 kwa mwaka, hivyo mpaka 2016 inakadiriwa kuwa idadi ya Watanzania ni watu milioni 49.8.

Mheshimiwa Spika, timu ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilitembelea nchi ya Kenya kujua hali ya dawa kwenye hospitali zao na kujifunza uwekezaji wa viwanda vya dawa, katika ziara hiyo nchini Kenya, pamoja na Tanzania tumejifunza kuwa viwanda vyetu ni viwanda vya umaliziaji (finishing industry) yaani tunaagiza dawa nje tunakuja kumalizia hapa.

Mheshimiwa Spika, kwasababu tunaelekea kwenye uwekezaji hili ni eneo pia muhimu kuwekeza mfano Lushoto kuna miti ya miquinini (sinchona tree), magome yake yamebeba ndani yake alkaloid quinine ambayo hutengeneza dawa ya quinine ya kutibu malaria na dawa hii ni silaha ya mwisho kutibu malaria vilevile tunaweza kuotesha mimea ya kuzalisha ambayo majani yake hutumika kwaajili ya dawa mseto marufu ALU (Artemisia) na mengine mengi ambazo zinastawi katika nchi za tropikali.

Mheshimiwa Spika ninataja haya hapa juu kwani kwenye viwanda vyetu katika nchi mbili hizi tunaagiza malighafi inayoweza kuzalishwa hapa ili kupunguza gharama za tiba, kurahisisha upatikanaji wa dawa na kuchangia pato la taifa

4.0 AFYA YA MAMA NA MTOTO

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 46 (1) (g) kinaeleza wazi haki za wanawake kupata huduma za afya (women with the right to health care). Pamoja na haki zao kutambuliwa katika katiba na sera mbalimbali bado wanawake wamekuwa wakiteseka sana na wengi kupoteza maisha kwa sababu za huduma duni za afya. Waathirika mkubwa zaidi katika sekta hii ya afya ni wanawake wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Spika, Hali ya vifo vinavyotokana na uzazi katika nchi yetu ni ya kutisha. Katika ripoti ya Bank ya Dunia mwaka huu wa 2016 (World Bank 2016 Maternal mortality ratio) takwimu zinaonyesha vifo vilivyotokana na uzazi (maternal mortality rate) kwa mwaka 2011 (483) 2012 (464) 2013 (438) 2014 (418) na 2015 (398) kwa kila wanawake 100,000. Hali hii inaonyesha bado juhudi zaidi zinaitajika kufanywa serikali kuhakikisha inapunguza kabisa vifo vya kina mama vinatokana na uzazi.

Mheshimiwa Spika, Kiwango hiki ni sawa na akina Mama 1,255 kwa mwezi na akina Mama 42 kila siku sawa na akina Mama wawili kwa saa. Kama ukiwakusanya hawa akina Mama wanaofariki, ni zaidi ya basi la abiria aina ya Costa wanakufa kila siku.

Mheshimiwa Spika, katika jamii zetu tunatambua mchango mkubwa anaotoa mama katika malezi na makuzi ya familia ikiwemo kuchangia katika kipato cha familia (women contribute substantially to household income). Pamoja na hayo wanawake wanatoa mchango mkubwa sana katika kukuza

uchumi wa nchi hii japo wengi hufanya kazi katika mfumo usio rasmi tena kwa kipato kidogo na mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, Mchango mkubwa alionao mwanamke ndani ya familia na taifa kwa ujumla ni vema serikali ikauthamini sana. Mama anapofariki mara nyingi wale waliobaki katika familia huishi kwa tabu sana familia nyingine husambaratika kabisa. Watoto wengi wameishia kuwa omba omba, kujihusisha na biashara za ngono na madawa ya kulevya na hata kukosa kabisa mwelekeo wa kimaisha. Kwa umuhimu wa kipekee serikali haina budi kuja na mkakati wenye tija wa kupunguza vifo vya kina mama husussani vinavyotokana na uzazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha inakuja na mpango madhubuti ulio rahisi katika utekelezaji zinaonyesha viko juu sana. Ni lazima serikali itekeleze wajibu wake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mtoto na mama wanaishi kama agenda ya kitaifa (Make Child and mother survival a core national health concern). Vilevile, **Kambi Rasmi ya Upinzani** inaitaka serikali kufanya tathimini ya uhakika kuhakikisha inajua idadi kamili ya vifo vya mama vinavyotokana na uzazi kwa kuwa bado kina mama wengi wanazalia majumbani haswa maeneo ya vijijini ili kuweza kubaini athari za kiuchumi zinazotokana na vifo vya kina mama pamoja na kupata mkakati wa kutatua tatizo. (evidence based strategies) kuhakikisha inapunguza vifo vinavyotokana na uzazi kwa kina mama ambavyo bado takwimu siyo za kutosheleza.

Mheshimiwa Spika, Ikumbukwe kuwa mwaka 2010/2011 bajaj 400 zilinunuliwa kwa fedha za walipa kodi ili zitumike kama 'ambulance' za kusafirisha wajawazito kwenda hospitalini. Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa za uhakika za kushindwa kufanya kazi kwa bajaj hizo na nyingi kutelekezwa kutokana na changamoto za jiografia ya maeneo mbalimbali na ubovu wa miundombinu. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi lakini ni dhihaka kwa wajawazito nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaihoji Serikali ni kigezo gani walitumia kufikia maamuzi ya kununua pikipiki hizo ambazo ziligharimu milioni 26 kwa moja, huku ikionekana kabisa pikipiki hizo mama akikamatwa na uchungu akiwa juu ya pikipiki hiyo uwezekano wa kuipindua pikipiki hiyo ni mkubwa sana.

4.1 Haki jinsia na afya ya Mwanamke.

Mheshimiwa Spika, kuna uhusiana mkubwa sana katika kuongeza rasimali katika elimu ya mtoto wa kike na kuboresha afya ya mama , mtoto na jamii kwa ujumla ,vilevile uhusiano na kupata jamii vumbuzi (**innovative society**).

Mheshimiwa Spika, zifanyike jitihada za makusudi kuondoa kabisa mila na desturi zinazo puuza uwezo wa akili ya mwanamke na nafasi ya mwanamke kwenye jamii.

Mheshimiwa Spika, kuthamini akili ya mwanamke, kuheshimu mwili wa mwanamke na kumpa mwanamke elimu bora siyo tu itaboresha maisha ya mwanamke bali italiboresha TAIFA

5.0 TATIZO LA UTAPIAMLO KWA WATOTO NCHINI

Mheshimiwa Spika, Tatizo la ukosefu wa chakula nchini na lishe duni bado linaathiri familia nyingi hasa watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kutokana na lishe duni watoto wamekuwa wakiugua utapiamlo na kudumaa (malnutrition and stunt). Kutokana na madhara haya watoto wengi wanaathirika ubongo na kupunguza uwezo wa akili (blunts intellect), na hata wakifikia umri wa utu uzima huathiri uwezo wao wa kuzalisha na hivyo kuchochea umaskini .

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Ifakara Health Institute takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya watoto milioni 2.5 katika taifa hili wamedumaa, na vifo vinavyotokana na utapiamlo ni takribani vifo 43, 000 kwa mwaka. Pamoja na hayo watoto wenye utapiamlo uliokithiri ni takribani 430,000 kila mwaka na miongoni mwao walio katika hatari za kufariki endapo hatua za haraka hazijachukuliwa ni takribani watoto 100,000. Kwa idadi hii ya vifo vinavyotokana na utapiamlo takwimu zinaonyesha mtoto 1 hufariki kila baada ya dakika 12.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hayo, ripoti mbalimbali za afya zimeonyesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye tatizo kubwa la utapiamlo barani Afrika na duniani kwa ujumla tumefikia kufananishwa na Kongo DRC ilioko katika vita.

Mheshimiwa Spika, Katika ripoti hizo ikiwemo ya Shirika la utafiti la Twaweza zinaonyesha Tanzania ni nchi ya kumi (10) duniani kwa ukubwa wa tatizo hili ukilinganisha na nchi kama Ethiopia ikiwa ni ya saba (7) na Sudan Kusini ikiwa ni ya kumi na tano (15) ambapo nchi hizi zimekuwa zikikumbwa na mabaa ya njaa mara kwa mara.Hii ni aibu kubwa kwa ustawi wajamii yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka serikali kutoa tamko ina mkakati gani wa kuhakikisha inatumia mfumo wa kuongeza virutubisho katika kila lishe inayokwenda sokoni ili kuhakikisha wananchi wanakula mlo wenye virutubisho na vilevile kusaidia jamii kutofautisha kati ya **lishe** na **shibe**

6.0 RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

Mheshimiwa Spika, Kwa takwimu za Wizara ya Afya za mwaka 2014 kuna watumishi wa Afya 15 kwa kila watu 10,000 ilihali Shirika la Kazi Duniani linapendekeza uwepo wa watumishi 41 kwa kila watu 10,000 ili kuweza kutoa huduma bora za Afya kwa kila mwananchi.

Pamoja na Tanzania kuwa ni nchi yenye uhaba mkubwa wa wataalamu wa tiba, wale wachache waliopo wamekuwa wakipata tabu kubwa katika utekelezaji wa majukumu yao, mazingira wanayofanyia kazi ni hatarishi, kuanzia hali ya shughuli zao na hata uduni wa huduma za afya kutokana na ukosefu wa dawa na vifaa tiba na kupelekea lawama nyingi kuelekezwa kwa madaktari na wauguzi hadi kufikia kupigwa na wananchi wanaokosa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya afya ni sekta ya utoaji wa huduma, hivyo utendaji katika sekta hii kama zilivyo sekta nyingine za utoaji wa huduma zinategemea kwa kiasi kikubwa watendaji wake wana morali ya kazi kwa kiasi gani, na akili ziko katika utulivu kwa kiasi gani. Utoaji wa huduma hutegemea kwa asilimia kubwa aina ya vifaa vilivyopo; morali ya kazi kutokana na jinsi gani watendaji mahitaji yao ya kimsingi yanatatuliwa, ili nao wasiwe katika hali ya kukata tamaa ya maisha na kuwaweka vizuri kiakili ili watoe huduma kwa upendo wenye ari kuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujitafakari upya kuhusu maslahi ya watoa huduma katika sekta nzima ya afya hasa madaktari kwenye **“call allowance, postmortem allowance na motisha zingine”** ili matarajio yao yaweze kufikiwa, ukweli ni kuwa unaweza kuwa na madawa, vifaa tiba na vitendanishi bila watendaji walio na moyo wa kazi hakuna huduma bora.

6.1 Ajira za wataalamu wa Afya

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kupatiwa sababu za kwa nini wanafunzi waliohitimu mafunzo kwenye sekta ya afya na maendeleo ya jamii hawajapatiwa ajira ilihali kuna upungufu mkubwa wa watumishi hao, hususan katika vituo vipya vilivyojengwa chini ya Mpango wa MMAM na kwa nguvu za wananchi? Inakadiriwa kuwa wataalamu hao wa afya ambao hawajaajiriwa kwa mwaka 2015 ni takribani 1,025 hadi sasa. Tunaitaka serikali kulieleza bunge hili ni hatua zipi za haraka zinachukuliwa kuwaajiri wahitimu hawa na kuziba pengo lililopo baina ya hitaji halisi la watoa huduma na wahitaji wa huduma za afya nchini.

7.0 HOSPITALI ZA WILAYA NA HOSPITALI TEULE ZA WILAYA

Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa hospitali za wilaya umeendelea kuwa wa kusuasua na mgumu kutokana na Serikali kutotenga fedha za kutosha za maendeleo, vifaa tiba madawa na vitendanishi. Pamoja na baadhi ya hospitali

za wilaya kuendelea kuandikia na kutoa taarifa kwa wizara juu ya upungufu huo, hali hii imeendelea kujirudia kila mwaka hali inayosababisha ukwamaji wa shughuli mbalimbali muhimu katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi ambao wengi wana kipato duni.

Mheshimiwa Spika, hospitali teule za wilaya ni moja ya wahanga wa tatizo hili, fungu la dawa ni dogo, fungu la pamoja (basket fund) limepunguzwa na fungu la matumizi mengineyo (**OC**) hawapati kabisa, shughuli za msingi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha pamoja na idadi ya wagonjwa inayoongezeka kila siku. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kutoka fedha za ndani ili kuongeza ufanisi.

7.1 Ufanisi katika utendaji wa Hospitali teule

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano hospitali ya Selian pamoja na kutoa uduma ya mama na mtoto bure, wazee bure, watu wanoishi na virusi vya ukimwi na saratani bure (cancer) na huduma kwa watoto yatima zaidi ya 600, upasuaji wa vistulla bure na kuwatembelea nyumbani wagonjwa (home based care). Baadhi ya huduma hizi hospitali za serikalini hazitoi, ikizingatiwa kuwa bei ya tiba ni sawa, bado huduma hospitali za Dini ni bora kuliko za serikali

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukafikiri kirahisi kuwa hospitali za dini kuwa zinapata msaada toka nje, lakini tujiulize je kati ya serikali na dini nani mwenye jukwaa bora zaidi la kusema na wahisani? bila shaka ni serikali, hospitali hizo teule pamoja na kutopata ruzuku kama ilivyo kwenye mikataba bado wanatoa huduma bure zilizoko kwenye sera ya umma, cha kushangaza huduma zao ni nzuri kuliko hospitali za serikali, na kulipa watu mishahara mfano hospitali ya Selianin Arusha mishara mil 178 kila mwezi, na milioni 80 ikiwa ruzuku ya serikali, milioni 98 wamekusanya kwenye mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, jambo la kujiuliza ni kwamba hospitali za serikali hawalipi mishahara kutokana na mapato ya ndani mishahara inatoka Serikali, lakini huduma zake bado ziko chini wakati ukilinganisha na hizi teule pamoja majukumu na tozo zina fanana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia kwa makini tatizo liko wapi na kutafuta tiba ya kudumu ili kuondoa tatizo husika.

7.2 Hospitali za Mikoa

Mheshimiwa Spika, Hospitali za mikoa zina hali isiyoridhisha na huduma zake hazikidhi mahitaji yanayotakiwa kutolewa kama zilivyoitwa hospitali za rufaa za mikoa hali hii inatokana na bajeti ndogo toka serikalini pamoja na mtizamo mbovu wa namna ya uendeshaji,

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya upinzani ilitembelea hospitali zaidi ya tano za mikoa kupata hali ilivyo ,katika hospitali moja wapo ya mkoa tuliwakuta wakiandaa bajeti yao kulingana kiwango cha fedha walicho agizwa (ukomo wa bajeti) kuwa ndio wanachoweza kupata , kiwango ambacho kilikuwa ni kidogo sana na haitoshi hata kuendesha hospitali kwa kipindi cha miezi sita

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano eneo moja la vitendanishi vya maabara; tulipofanya ziara tulibaini kuwa zipo hospitali walizoomba vitendanishi kwa zaidi ya miezi minne kutoka MSD bila mafanikio, kwa bahati nzuri siku hiyo ndio siku waliyofanikiwa kupata majibu yao toka MSD, baada ya kusubiri kwa miezi minne iliyopita. Katika majibu hayo, walipewa bei ya vitendanishi vya maabara vya matumizi kwa mwezi mmoja tu. Na hii ikiwa ni sehemu tu vitendanishi vyote.Vitendanishi hivi vilikuwa vinagharimu milioni 12.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote ni kwamba hospitali hiyo imepewa gawio la milioni 13 kwa mwaka ujao kwa ajili ya vitendanishi, kwa bei hizo za MSD. Hii inamaanisha kuwa hospitali hiyo kwa mwaka ujao itakaa miezi 11 bila vitendanishi vya maabara

Mheshimiwa Spika, swali, Je, kama maabara haifanyi kazi wananchi watapataje huduma bora ya afya? vipi kuhusu upunguzaji wa vifo vya mama na mtoto? Je, bila maabara hospitali itakuwa hospitali au ni kituo cha kupiga ramli?

7.3 Maduka ya dawa kwenye Hospitali za Serikali

Mheshimiwa Spika, Maduka ya MSD yalipelekwa karibu na hospitali. Hii siyo tu inapingana na zana nzima ya uchangiaji huduma (cost shairing),lakini jambo kubwa ni kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani iliojionea kwenye maduka haya ni kwamba inawapelekea uhibitisho kwa wananchi kuwa imani iliyokuwa imejengeka kuwa madaktari walikuwa wakiiba dawa kwa kiasi kikubwa sio kweli bali serikali ilikuwa haileti dawa. Wananchi sasa wanapata fursa ya kujionea kwa macho yao kuwa MSD hakuna dawa.

Mheshimiwa Spika, katika Hospitali mojawapo ambayo ni binafsi iliyotembelewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa na duka la dawa nje ya hospitali. Dhana nzima ya kuweka duka hili ilikuwa tofauti na vile ilivyoeleweka na MSD. Nia ya MSD ilikuwa ni kuweka dawa, vitendanishi na vifaa tiba ambavyo havipatikani MSD. Lakini duka hilo nilikuwa likifanya biashara ya vitendanishi na vifaa tiba hivyo kama chanzo cha kuongeza mapato ya ndani katika kuendesha hospitali hiyo. Kambi rasmi ya Upinzani, inaishauri serikali ijifunze kutoka sekta binafsi jinsi ya kuweza kuendesha maduka ya dawa ambayo wameyaanzisha kwenye hospitali zetu.

8.0 MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA- TFDA

Mheshimiwa Spika, Serikali ina Mamlaka ya chakula na dawa nchini (TFDA) ambayo ina jukumu la kukagua vyakula, madawa na vipodozi vinavyoingia nchini, Pamoja na mamlaka hizi kuna mamlaka lukuki zinazohusika na ukaguzi wa bidhaa hizi, kuanzia zinapoingia nchini mpaka zinapomfikia mlaji

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya madawa na vipodozi yamekuwa mzigo mkubwa kwa vijana hususani vijana wa kike. Katika ripoti iliyoandika na YWCA “Beauty at any cost” Ulibaini kuwa wanawake wanatumia fedha nyingi katika kubadilisha muonekano wa maumbile yao.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hayo athari za madawa na vipodozi haramu kiafya ni kubwa kwani imechangia ongezeko la magonjwa ya saratani ya ngozi, via vya uzazi, na hata madhara makubwa kwenye viungo vingine vya mwili.

Mheshimiwa Spika, Bila shaka madawa na vipodozi hivi haramu nchini vinapita katika viwanja vya ndege, bahari na hata mipakani kwa njia ya barabara Lakini Pengine rushwa na uzembe vinaweza kuwa chanzo cha ukiukwaji wa taratibu za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, hapo juu umeona gharama kubwa inayotumika kuagiza na kusafirisha madawa, vitendanishi na vifaa tiba toka nje ya nchi kupitia bandarini, Kambi Rasmi ya Upinzani wakati wa ziara yake Ilibaini kuna baadhi ya madawa na vifaa tiba ambayo havipatikani nchini lakini vinapatikana katika nchi za Afrika Mashariki ,lakini hizo dawa hazija sajiliwa nchini na TFDA kutokana na urasimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali ijiridhishe kwanini tuagize kutoka India wakati vitu hivi vinapatikana Afrika Mashariki? Pili, serikali ijiulize kama tunaagiza madawa yanayopatikana Afrika Mashariki kutoka nchini India Je, tunazingatia vigezo gani ?

9.0 HUDUMA ZA AFYA KWA WATOTO WAISHIO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI

Mheshimiwa Spika, Suala la Afya ni suala muhimu kwa kila binadamu, afya haichagui rangi, kabila, dini, umri, jinsia wala mazingira anayotoka mtu. ***(Health is vitally important for any human being, whatever our differences maybe, health is our most important commodity.***

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni moja ya nchi iliyoridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto “Convention on the Right of a Child” (CRC). Mkataba huo umeelezea bayana katika kifungu cha 24 kuwa nchi washiriki

watahakikisha hakuna mtoto atakae kosa haki yake ya kupata huduma ya afya
“They shall strive to ensure that no child is deprived of his or her right of access to such health care services”

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Haki ya Mtoto ya mwaka 2009 (Law of the Child Act), inatambua haki ya kila mtoto kupata huduma bora ya afya bila ubaguzi. Lakini haki hii imekuwa ikikiukwa au kuporwa hasa kwa watoto waishio maeneo hatarishi. Katika takwimu mbalimbali zilizotolewa na mashirika yanayotoa huduma kwa watoto waishio mitaani imeonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watoto waishio mitaani. Hii ni kutokana na changamoto mbalimbali za kimaendeleo, mifumo wa kiuchumi, mabadiliko ya malezi na makuzi, n.k. Ni vyema serikali ikatambua wapo watoto waliozaliwa na kukulia mitaani kinyume na mapenzi yao. Watoto hawa hawafahamu ndugu wala jamaa zao zaidi ya wale wanaoishi nao huko mitaani. Watoto hawa hawapati huduma yoyote ya msingi ikiwemo huduma za afya. Hata pale anapougua akiwa mtaani imekuwa ni vigumu sana kwenda zahanati kupata huduma ya afya. Hii ni kwa sababu watoa huduma hizi hawatengenezi mazingira rafiki ya kuwahudumia watoto hao, changamoto ya kukosa fedha kwa ajili ya matibabu na dawa, na zaidi ni kukosa uelewa kuhusu maswala ya afya.

Mheshimiwa Spika, pengine serikali haijaona moja kwa moja madhara haya makubwa kwa watoto na vijana waishio mitaani kukosa elimu ya afya na huduma za afya. Endapo hali hii ya kuwanyima watoto wa mitaani haki ya kupata huduma ya afya na elimu juu ya masuala ya afya ni dhahiri watoto hawa watakuwa katika hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa na hata kuambukiza wengine na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Watoto hawa waishio mitaani wengi husumbuliwa na magonjwa mbalimbali, yakiwepo magonjwa ya zinaa (sexually transmitted diseases) ikiwemo UKIMWI. Vilevile, kwa kukosa elimu ya afya wengi hawatambui madhara ya matumizi ya dawa za kulevya, dalili za magonjwa na namna ya kujikinga na magonjwa. Kutokana na mazingira watoto hawa wanapoishi wako katika hatari kubwa ya kupata magonjwa ya milipuko kama kuhara na kipindupindu na hivyo kuiweka jamii nzima katika hatari ya maambukizi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa katika makundi maaalum ya wanaofaidika na huduma ya afya bila malipo nchini katika hospitali za serikali ikiwemo wazee, watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na kina mama wajawazito basi watoto wainaoishi mitaani wawe kati ya kundi litakalopata huduma ya afya bila malipo (exemption). Kuonyesha upendo kwa watoto hawa ni njia kuweza kufungua milango ya mazungumzo ili kutafuta mbinu ya kuwaondoa mitaani au kupunguza ongezeko.

10.0 MAENDELEO YA JAMII

Mheshimiwa Spika, ni ukweli tupo hapa tulipo kwa ajili ya kutokujali au kutokutilia mkazo kazi zinazofanywa na wataalam wa maendeleo ya Jamii. Taaluma hii ndiyo inayohusika kwa kiasi kikubwa kuelimisha jamii juu ya maadili, na sasa hivi kama taifa tunatatizo kubwa sana la maadili. Tasnia hii ikitumika na kupewa umuhimu unaostahili tutaboresha **“maadili kwa Taifa”**.

10.1 Maendeleo ya Wazee Nchini

Mheshimiwa Spika, wazee ni hazina ya taifa. Na kwa mujibu wa sensa ya makazi na watu ya mwaka 2012, idadi ya wazee nchini ni milioni 4.15 sawa na asilimia 9.5 ya idadi ya watu wa Tanzania bara pekee ambapo kati yao, wanawake ni milioni 2.18 na wanaume ni milioni 1.97. Wazee wa taifa hili wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo umaskini uliokithiri, mauaji dhidi ya vikongwe, ubakaji, ukosefu wa huduma za afya, upungufu wa chakula, kukosekana kwa makazi ya wazee na kadhalika. Hali halisi ni kwamba wazee wengi wamejiajiri katika sekta isiyo rasmi na wengi wanajishughulisha hasa na kilimo duni na wengine wana majukumu ya kulea familia zao duni.

Mheshimiwa Spika kuna tatizo kubwa katika utoaji wa huduma za afya kwa kundi hili la wazee ambapo pamoja na Serikali kutoa maamuzi ya kutoa huduma za afya bila malipo kwa wazee mwaka 2007, agizo kwa halmashauri kutenga dirisha maalum kwa ajili ya huduma kwa wazee bado kuna ombwe kubwa katika utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwao. Leo hii, wazee wengi wanapata matibabu duni kwenye hospitali hizo ambapo mzee anamuona daktari tu bure lakini hapati dawa wala huduma nyengine hazipatikani kwa bure kama inavyotakiwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inataka kujua, pamoja na halmashauri kuagizwa kutenga dirisha maalum la kuhudumia wazee, je ni halmashauri ngapi mpaka sasa zimetenga madirisha hayo na halmashauri ngapi zimechukuliwa hatua kwa kushindwa kutekeleza agizo hilo? Ni lini Serikali itagharamia matibabu kwa wazee kwa kupitia mfumo wa bima ya afya?

10.2 VYUO VYA MAENDELEO YA JAMII NA WANANCHI

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na changamoto za kiutendaji ikiwemo miundombinu mibovu, mazingira duni na uchakavu wa majengo hali inayopelekea kuwa na mazingira magumu ya kujifunzia na kufundisha. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 vyuo vya maendeleo ya jamii vilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 2 fedha za ndani lakini mpaka Machi, hakuna fedha zilizotolewa.

Aidha, Taasisi ya maendeleo ya jamii ya Tengeru ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa maktaba nayo pia haikupata hata shilingi moja ya fedha zilizotengwa. Pamoja na Serikali kueleza kuwa udahili wa

wanafunzi katika vyuo hivyi umeongezeka, kuna hatari kubwa ya vyuo hivyi kufungwa kutokana na uchakavu mkubwa wa majengo na uwezo duni wa kuweza kutoa elimu kwa wadahiwa na hata kuzalisha wahitimu hewa wasio na elimu bora kutokana na uhaba wa vifaa vya kufundisha.

10.3 Uhitaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii Nchini.

Mheshimiwa Spika, kuendelea kuporomoka kwa maadili nchini kwa kiwango kikubwa kunachangiwa na uhitaji mkubwa wa maafisa maendeleo ya jamii. Hata hivyo, katika halmashauri 180 nchini (Tanzania Bara) kuna uhaba wa takribani asilimia 66.3 wa maafisa maendeleo ya jamii kwani katika kata 3957, kuna upungufu wa maafisa maendeleo ya jamii 2625 . Je kwa hali hii mmomonyoko wa maadili unaweza kuepukika?

11.0 BENKI YA WANAWAKE TANZANIA

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonesha kuwa wanawake nchini Tanzania ni asilimia 51 ya watanzania wote. Kwa mwaka 2015/16 inaonesha kuwa jumla ya shilingi 20,124,874,328 zilikopeshwa ambapo wanawake walipata mikopo nyenye thamani ya shilingi 12,878,977,228

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha kuwa bado serikali haijaonyesha nia ya dhati ya kuwasaidia wanawake kupitia benki hii. Mpaka sasa kati ya mikoa 30 ni mikoa 7 tu ndio wanaonufaika na mikopo kupitia benki hii ya wanawake. Kati ya mikoa hiyo ni mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Njombe na hakuna mkoa wowote kutoka Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hayo bado riba inayotozwa na benki hii ni kubwa sana. Tofauti na benki nyingine nchini zenye riba nafuu, benki hii ya wanawake inatoza riba ya asilimia 19. Huku ni kuongeza umaskini kwa mwanamke wa Tanzania na sio kumkomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni lini serikali itahakikisha kuwa Benki hii inapunguza riba ili kuwanufaisha wanawake wajasiriamali? Vilevile serikali ituambie mkakati wake wa kuhakikisha inapanua wigo wa kutoa huduma nchini ili kuhakikisha wanawake nchi nzima wananufaika?

11.1 Kuzuia Ukatili wa Kijinsia

Mheshimiwa Spika, Bado tatizo la ukatili wa kijinsia nchini ni kubwa sana. Matukio yanayotokana na ubakaji, ulawiti, vipigo kwa wanawake, tohara kwa wanawake na watoto wa kike, ndoa na mimba za utoto bado vinaripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari japo matukio mengi pia yanashindwa kuripotiwa kutokana na changamoto mbalimbali za kimawasiliano.

Mheshimiwa Spika, vitendo hivi vinadhalilisha utu wa mwanamke na ni kinyume cha Azimio la Beijing la mwaka 1995 ambapo nchi yetu ni miongoni mwa nchi zilizoridhia azimio hilo. Kuendelea kushamiri kwa vitendo hivi hususani maeneo ya vijijini kunaonyesha uhitaji mkubwa wa kuanzisha Dawati la Jinsia mpaka ngazi ya vijiji kwa vitendo na sio kinadharia kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, Je, serikali imetenga kiasi gani cha fedha katika bajeti yake ili kuhakikisha kuwa kila kijiji kinakuwa na Dawati la Jinsia hii ikiwa ni pamoja na kuwaajiri watumishi wa dawati la Jinsia?

11.2 Huduma za Sheria

Mheshimiwa Spika, *“injustice anywhere is a threat to justice everywhere”* **Udhalimu mahali popote ni tishio la haki kila mahali**” Bado kuna manyanyaso, ukatili na hakuna haki kwa watoto wengi walioko magerezani au wale wenye kesi. Watoto hawa wananyimwa haki kuanzia kwenye usikilizwaji wa kesi zao mpaka kwenye mazingira wanayoishi ndani ya magereza. Katika Randama ya taarifa ya Utekelezaji ya mwaka 2015/2016 taarifa ya hali za magereza nchini ilikiri kuwa haki za watoto katika mahakama zetu zinakiukwa sana. Watoto wadogo wanachanganywa na watu wazima, wenye tabia tofauti, wenye kesi zinazohatarisha hata usalama wa watoto hao ndani ya magereza. Wapo wenye kesi za kulawiti na kubaka, majambazi sugu n.k wote hawa wanachanganywa na watoto hao. Hii yote ni ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto na udhalilishaji wa utu wa watoto hao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, huduma za msaada wa kisheria kwa watoto hawa imekuwa ni changamoto kubwa kwa kuwa mawakili wanaojitokeza kuwasaidia ni wachache au mashirika yanayotoa huduma ya msaada wa kisheria yamezidiwa na wingi wa kesi. Pia watoto hawa wanatoka katika familia duni, na kesi zao zinachukua muda mrefu. Katika Randama ya taarifa ya utekelezaji ni watoto 25 tu waliopata msaada wa kisheria na watoto 16 tu ndio waliopata uwakilishi mahakamani. Serikali haitendi haki kwa watoto hawa hata kidogo nani ukiukwaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto (Convention on the Right of the Child).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa watoto ho wanaochanganywa na watu wazima wanatengwa mara moja ili kulinda haki na utu wao kama watoto. Serikali ituambie ina mpango gani wa kuanza kutumia paralegals ili kuweza kuwasaidia watoto hao kupata haki zao kama ilivyofanikisha kutumia para social workers katika maeneo mbalimbali nchini?

Mheshimiwa Spika, SHUJAA NI MTU YULE ANAEMJALI MTOTO WA KIKE MIMI NI SHUJAA, JE WEWE?

Naomba kuwasilisha.

DR GODWIN OLOYCE MOLLEL (MB)

Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi-Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia wazee na Watoto.

11.05.2016

MWENYEKITI: Ahsante kwa kusoma vizuri na kuchunga muda.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye hatua ya michango na naanza na Mheshimiwa Shabiby.

MHE. AHMED M. SHABIBY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kwanza ya kuchangia. Kwanza nimpongeze dada yetu, Waziri wa Afya pamoja na msaidizi wake, Ndugu yetu Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla kwa kuwakilisha hotuba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita katika sehemu chache tu na za muhimu sana kwa watu wetu wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na huu Mfuko wa Afya ya Vijijini (CHF). CHF ukiiangalia sana muundo wake na jinsi ilivyoanzishwa iko ki-theory sana. Ukiiangalia utajua labda huu mfuko ni ukombozi wa wananchi wanaoishi vijijini. Lengo lake kwa wanachama wake ni kuchangia ili kupata huduma za dawa pamoja na vifaa vinavyohusiana na tiba.

Ukiangalia kiundani katika *practical* hakuna kitu kama hicho. Utakuta vituo vya afya au zahanati zinachangia Mfuko huu wa CHF, zile pesa zinakwenda CHF makao makuu, badala ya watu kuletewa dawa hawaletewi dawa, utakuta wanaletewa *condom* au vitu vingine tu havina hata msingi, hata chanjo za watoto vijijini zinashindikana. Mimi sioni huu mfuko wa CHF maana yake nini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiangalia katika muundo wake kwa kweli una maana kubwa sana. Mwanachama wa CHF akienda kwenye kituo cha afya au kwenye zahanati kitu atakachoambulia kupata pale ni kipimo tu kama akiambiwa ana malaria hicho kipimo kidogo basi ameshamaliza, zaidi ya hapo dawa nenda kanunue, hakuna dawa. Sielewi mpango huu wa CHF una faida gani!

Mimi nitoe ushauri kama huu mpango wa CHF umeshindikana kwa nini msiunganishe hii mifuko ili mfuko wa bima uwe mmoja? Nina maana kwamba CHF na NHIF uwe mfuko mmoja, kuna faida gani ya kuwa na mifuko mingi ambayo haina faida yoyote? Hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu madaktari, kwa mwaka wanahitimu zaidi ya madaktari 1,000 lakini wanaojiriwa hawazidi 300. Halafu tunakwenda vijijini na kwenye vituo vya afya tunawaambia watu wachangie kujenga vituo vya afya na zahanati. Kwa mfano, pale Gairo kuna zahanati zaidi ya sita zimeshajengwa, vituo vya afya viwili mpaka leo havina Muuguzi wala Daktari sasa maana yake nini? Tukija hapa tuna kazi ya kuambiwa tu tuwashawishi wananchi. Mimi kama Mbunge kwa kweli sasa hivi nimechoka simshawishi mtu hata mmoja ajiunge CHF, namwambia kwanza achana nayo nenda na hela yako cash, haina maana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba dada yangu aliangalie sana hili kwa sababu ni Waziri mgeni uwe makini sana na suala hili. Tunapozungumzia habari za afya za watu basi Madaktari muwape ajira na mhakikishe kwamba wanafika Wilayani. Kwa mfano, Wilaya ya Gairo mpaka sasa hivi haina Madaktari kabisa na Wauguzi. Mwaka huu mmetupangia Wauguzi wanne Wilaya nzima na hao Matabibu watano Wilaya nzima kwa kweli haina maana ya aina yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu nataka kufahamu, hii Wizara ya Afya iko tu kazi yake kutengeneza sera au iko kwenye majukumu? Maana mimi naona iko kwenye kutengeneza sera kwa sababu yenyewe inapohudumia inahudumia mwisho Hospitali za Rufaa tu, lakini ukija huku kwenye Hospitali za Wilaya utakuta ziko chini ya Halmashauri. Ukiuliza *ambulance*, utaambiwa *ambulance* kwani ninyi hamna mapato? Sasa hizi Halmashauri zinatakusanya wapi mapato ya kutosha wakati *ambulance* moja ni zaidi ya shilingi milioni 150 au 200! Hizi Halmashauri zitawezaje kupata vitu vyote hivi, zihudumie elimu, maji, majengo yao na *ambulance*? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kufahamu maana inaonekana hii Wizara ingekuwa Bodi tu ingekuwa hamna tena Wizara ya Afya iwekwe Bodi fulani tu basi kwa sababu ukiangalia huduma zake zote ziko chini ya TAMISEMI. TAMISEMI ndiyo imebebebwashwa kila aina ya mzigo. Ukiangalia TAMISEMI siyo imebebebwashwa mizigo tu imebebebwashwa hata majitu mabomu mabomu yale yote yasiyojua kazi yote yako TAMISEMI, sasa kuna huduma gani hapo itakayofanyika ya ukweli? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nazungumza kile kitu cha ukweli, ndiyo ukweli huo. Huduma za afya ni mbovu na utakuta Halmashauri za Wilaya kama kituo cha afya kiko mjini manesi pamoja na upungufu kama wako watano au

sita, utakuta wanne wako kwenye kituo cha mjini, kule kijijini utakuta wakati mwingine kama kuna Daktari mmoja ndiyo huyo mpaka anazalisha akina mama, tunawadhalilisha akina mama. Sasa mimi sielewi, kama iko kiseru, mimi nataka kujua kiseru tu kwa sababu ukija kwenye TAMISEMI ndiyo ina mambo yote ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia pale Gairo, namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii alizungumza kwamba unaweza ukatoka hapa unaenda Morogoro ukapata *accident*, sasa ukiangalia katikati ya Tumbi ya Morogoro hapa ni Gairo, kilomita 131 kutoka Dodoma na kilomita 131 kwenda Morogoro, kila siku tunapiga kelele pawepo na madaktari na *ambulance* lakini mpaka leo hakuna. Mimi nashangaa hapa mkitoa mifano mnatolea Kanda ya Ziwa tu sijui wapi hakuna madaktari mbona hamtolei mfano Gairo, Gairo Madaktari hawapo na ndiyo barabara kuu hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee MSD. Naomba pesa zao wanazodai walipwe zaidi ya shilingi bilioni 130, wapewe hela zao ili watoe huduma safi. Ule mpango wa MSD kuweka maduka ya dawa kwenye Hospitali ya Rufaa isiwe hivyo, waweke maduka yao mpaka Hospitali za Wilaya. Kinachotakiwa kufanyika pale wao wapewe nafasi tu lakini waweke maduka yao. Wanaopenda huduma za afya siyo kwamba wako mijini tu, wako vijijini na Wilayani basi angalau wapewe nafasi kwenye Hospitali ya Wilaya ili nao waweke maduka ili wananchi nao wa sehemu za vijijini na kwenye Halmashauri wapate huduma za MSD. Naona kila atakayezungumza au kwenye vyombo vya habari utasikia MSD imeweka duka Muhimbili sasa hivi ina mpango wa kuweka Morogoro, ina mpango wa kuweka wapi, huku Wilayani vipi au MSD haiko Kitaifa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kugongewa kengele ya pili nafikiri kwa haya machache nimeelewewa, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma na Mheshimiwa Godluck Mlinga wajiandae.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii muhimu sana ya sekta ya afya, kwa kweli bila afya hatuwezi kuwa hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nipongeze sana hotuba ya Kambi ya Upinzani na ile ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii na Maendeleo kwa sababu ndiyo ukweli wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kuzungumzia *statistics* za Wizara na uhalisia wa mambo yanavyokwenda kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati hii.

Kabla ya kuanza kwa sababu Wizara hii pia inahusika na masuala ya maendeleo ya jinsia, nitoe masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye anasema kwamba yeye ni balozi wa wanawake ameweza kukemea mambo yaliyotokea nje, lakini yaliyotokea humu ndani ameshindwa kukemea. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Naibu Waziri kama kweli wewe ni balozi ungekuwa muwazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la upungufu wa wataalam. Ni jambo la kusikitisha na nichukue fursa hii kuipongeza sana Taasisi ya Benjamin Mkapa kwa jinsi ambavyo inafanya kazi kubwa ya kuboresha afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha na nashangaa Serikali inakuwa wapi. Tumeambiwa na *Benjamin Mkapa Foundation* wametengeneza *theatres* tisa, wameshazikabidhi kwa Halmashauri, tena zile za mipakani Rukwa, Kishapu na nashangaa Mbunge wa Kishapu anayesema shapu lakini kwake upungufu wa wauguzi ni 86%. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Siyo raia.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, *theatre* hizi tisa zimekabidhiwa kwa Serikali ni tatu tu zinafanya kazi, sita zipo tu na kuna watumishi lakini hazifanyi kazi, sasa tunajiuliza hii Serikali ya namna gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni vibali, tuna wataalam wa afya 4,491 wame-graduate toka mwaka 2014 mpaka leo hawajapata ajira. Madaktari Wauguzi na wataalam wa maabara wako mitaani, lakini hapo hapo tunasema tuna ukosefu mkubwa wa watumishi, sasa tunajiuliza kuna tatizo gani? Vibali hivi vinaenda kumaliza muda wake tarehe 30 Juni, watu wako nje. Kwa hiyo, naomba tutembeke kwenye maneno yetu, tufanye kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuje kwenye suala la dawa, hapa tunapoongea dawa muhimu yaani *essential medicine* tuna upungufu wa asilimia zaidi ya 87. MSD ambao wanaohitaji shilingi bilioni 21 kwa mwezi kununua dawa wanapewa shilingi bilioni mbili tu za dawa muhimu. Ina maana kwamba kwa mwaka wanatumia fedha za mwezi mmoja tu. Hii ina maana gani? Ina maana Watanzania zaidi ya asilimia 80 hawapati dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye suala la ukosefu wa watumishi na hapa nizungumzie *lab technician*. Tumetoka kwenye suala zima za *symptom* yaani mtu haangalii tu dalili zako kwa macho, inatakiwa upimwe majibu yatoke

laboratory lakini tuna upungufu wa asilimia 100 kwenye maeneo mengi nchini hapa. Tunaambiwa mikoa ya pembezoni zahanati hazina wataalam hata mmoja. Kwa hiyo, muuguzi au daktari anaenda kwa kukuangalia tu unaeleza historia yako anakupa dawa, ina maana Watanzania wengi wanapata dawa ambazo labda siyo za magonjwa yanayowasumbua. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ambacho kinasikitisha zaidi ni *data* tulizopewa za wanawake wanaokufa kila siku. Haiwezekani *whether* ni za Serikali kwamba ni wanawake 24 au hizo ambazo zinatoka kwenye *National Bureau of Statistics* kwamba leo wanawake 42 wanakufa kwa siku maana yake ni wanawake 1,300 kwa mwezi, kwa mwaka ni wanawake 15,000 sawa na wapiga kura wa Jimbo moja kule Pemba au Zanzibar. Hatuwezi kama akina mama kukubali hali hii iendele. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu nchi hii ina uwezo, kama tuliweza kununua magari ya washawasha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia, kama tuliweza kununua magari ya washawasha 777 na ni 50 tu yalitumika kwenye uchaguzi na gari moja nime-google kwa Alibaba ambao ndiyo wanaleta magari lina gharama ya shilingi milioni 150 mpaka 400 lakini tuchukue wastani wa dola 300,000 kwa moja ina maana kwa magari 700 ni dola 210 milioni. Ukizipeleka kwenye hela za Kitanzania ni bilioni 420...

WABUNGE FULANI: Uuuuh! (Makofi)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Shilingi bilioni 420 kwa kata 3,990 tulizonazo Tanzania nzima zingeweza kupata *ambulance*. Nime-google *ambulance* moja ambayo tena ni *advance* inaenda kwa shilingi milioni 105, ukigawanya ina maana kila kata hapa Tanzania ingepata *ambulance*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunajiuliza *priorities* za nchi hii ni zipi, ni afya ya Mtanzania au ni kitu gani? Kwa sababu nimesema magari 77 ya washawasha yangeweza kubaki, tunazungumzia yale 700 yaliyobaki yaani yangetosha kununua *ambulance* kila kata hapa nchini. Kibaya zaidi hayo magari ya washawasha yametumika 50 *according to data*. Sasa tunajiuliza hivi huu utaratibu ukoje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mbwembwe sana, tukaambiwa kwamba CT-Scan imenunuliwa, hela zilizokuwa zifanye sherehe ya Wabunge zimenunua vitanda. Tumeenda Muhimbili ile CT-Scan ilitoka UDOM. Sasa watueleze hivi Wagogo na watu wengine wanaoishi Dodoma hawahitaji kutibiwa? Vilevile tunaambiwa hata vitanda vilitoka sehemu nyingine

havikununuliwa. Sasa tunataka kujua zile hela za sherehe ya Wabunge zilienda wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la Benki ya Wanawake. Kumekuwa na mazungumzo mengi hapa Bungeni kwa nini hatufungui matawi mikoani. Serikali hii hii ambayo iliahidi kutoa shilingi bilioni mbili kila mwaka kwa ajili ya hii benki hawajatoa. Mwaka huu ukiangalia kwenye kitabu cha maendeleo wametoa shilingi milioni 900. Tuliwashauri Wizara, Wizara hii ina taasisi kubwa nyingi, ni kwa nini taasisi kama ya Bima ya Afya, MSD, NIMR na nyingine wasipitishie fedha zao kwenye benki hiyo ili benki hiyo iweze kukua na kwenda mikoani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisikitika sana Mheshimiwa Waziri alivyomgombeza sana Mkurugenzi wa Benki hii lakini kwa kweli ukiangalia haiwezi kutoa riba nafuu kwa sababu haina fedha. Kwa hiyo, naomba kutoa pendekezo kwa Mheshimiwa Waziri kwamba ni lazima ifike mahali kama Serikali haina fedha iweze sasa kuchukua hayo mashirika niliyoyazungumza waweze kuwekeza fedha zao kwenye benki hii. Vilevile na Wabunge wanawake tunaweza kufungua akaunti kwenye benki hiyo ili iweze kwenda mikoani kusaidia akina mama ambao wanateseka sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie sasa na suala la wazee. Naomba ni-*declare interest* mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Wazee wa CHADEMA Taifa. Wazee nchi hii wanajulikana kwa idadi lakini kibaya zaidi Sera ya Wazee imetungwa toka mwaka 2003 mpaka leo tunavyoongea miaka 14 baadaye hakuna sheria, hakuna kanuni, hakuna mwongozo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wazee wameteseka sana katika nchi hii, wameuwawa kwa sababu ya macho mekundu lakini hakuna sheria. Leo Waziri anasema mwezi wa tisa wataleta Muswada, tunakushukuru lakini tuseme tu kwamba umechelewa. Tunashukuru kwa hatua hiyo lakini ni kweli umechelewa. Tunaamini sasa huo Muswada na Sheria ikipitishwa, kanuni nazo zitatungwa mara moja ili wazee hawa waweze kuona kwamba wanaishi katika nchi yao kwa amani lakini wajue mchango wao katika nchi hii unathaminika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kiteto Zawadi Koshuma, ajiandae Mheshimiwa Goodluck Mlinga halafu tunaingia Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar.

MHE. KITETO Z. KOSHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na namshukuru Mungu kwa kuendelea kunipa uwezo wa kushiriki katika Bunge hili Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu, mama ambaye ameufahamu wajibu wake kwa nafasi aliyopewa kwa kuwaangalia wanawake wa Tanzania kwamba wana upungufu wa damu na hivyo kuweza kuhamasisha katika Mkoa wa Dodoma na watu wamekwenda kujitolea damu. Tunaamini kwamba mama yetu Mama Samia Suluhu ataendelea kutambua na mikoa mingine kwamba wanawake wengi wanakufa kila siku kwa ajili ya upungufu wa damu pale wanapokwenda kujifungua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pongezi hizo, sasa naomba nijikite katika kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Afya. Natokea Mkoa wa Mwanza ambapo tuna Wilaya ya Ilemela ambayo bado ni changa ilianzishwa mwaka 2012. Kwa masikitiko makubwa sana Wilaya ya Ilemela hakuna Hospitali ya Wilaya. Kwa bahati mbaya sana Halmashauri ya Ilemela wakati imekatwa kutoka kwenye Halmashauri ya Jiji la Nyamagana iliomba shilingi milioni 300. Baada ya kupatiwa fedha hizo Halmashauri hii imeweza kutumia shilingi milioni 193 kuanzisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nyamagana kwa kuanza na jengo la *emergence*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilipokuwa nikitazama kwenye vitabu mbalimbali vya bajeti ya Wizara ya Afya sijaona ni wapi ambapo Serikali imetenga pesa kwa ajili ya kuweza kutusaidia Wilaya ya Ilemela kujenga majengo yetu ya Hospitali ya Wilaya ya Ilemela. Hivyo basi, namuomba Waziri wa Afya, dada yangu pale, aweze kutusaidia kiasi ambacho kimeombwa na Halmashauri ya Ilemela shilingi bilioni mbili na milioni mia tatu kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ilemela. Nitamuomba Waziri wetu wa Afya anaporudi kujibu hoja basi atusaidie kutueleza ametenga kiasi gani au Serikali imetenga kiasi gani kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongelea suala la upungufu wa dawa. Tumeona katika Mkoa wa Mwanza limefunguliwa duka la MSD, lakini kwa masikitiko makubwa sana dawa katika lile duka hakuna. Namuomba Waziri aweze kufanya uchunguzi kwamba katika hilo duka ni dawa gani zimepelekwa au hizi dawa zimeishia wapi. Yawezekana dawa zimepelekwa lakini zimebaki zina-*hang somewhere* na hazijaweza kufika katika hili duka la MSD ambalo limefunguliwa pale katika Hospitali ya Rufaa ya Sekou-Toure. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana, Mkoa wa Mwanza hakuna mashine za CT-Scan. Watu wengi wamekuwa wakifa kutokana na matatizo ya ubongo. Tunafahamu kabisa CT-Scan ina uwezo wa kutambua mgonjwa ana matatizo gani kwenye kichwa ili kuweza kuepuka mgonjwa kupata *stroke*. Tumeweza kuwa na wagonjwa wengi sana ambao wanapata *stroke*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba Waziri atakapokuja aje na majibu sahihi tena ya uhakika kwamba katika Mkoa wa Mwanza hususani Hospitali ya Bugando ambayo imesemekana kwamba kuna CT-Scan lakini ninao uhakika wa asilimia mia moja, hata sasa hivi Waziri akisema tupande ndege twende Mwanza au twende kwa basi au kwa gari gani lakini twende Mwanza sasa hivi tukakague Hospitali ya Bugando CT-Scan hakuna. Naomba sana Wizara yetu iweze kuwa makini katika kuangalia vifaa ambavyo vinakuwa vinapelekwa je vimefika au havijafika? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukazia kuomba CT-Scan katika Hospitali yetu ya Rufaa ya Sekou-Toure. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy aliahidi na kusema kwamba CT-Scan itapelekwa mara moja iwezekanavyo. Hivyo basi, nakuomba Waziri wakati ukiangalia bajeti yako utusaidie pale Mwanza utupelekee CT-Scan katika Hospitali yetu ya Rufaa pale Mwanza ya Sekou- Toure. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ilemela Mkoani Mwanza inazo kata 19. Mheshimiwa Rais alitoa ari kwamba kuwepo na vituo vya afya katika kila kata, lakini pawepo na zahanati katika kila kijiji. Kwa masikitiko makubwa sana Wilaya ya Ilemela tunazo kata kumi na tisa lakini tuna vituo vya afya vitatu kikiwepo Kituo cha Sangabuye, Bugogwa pamoja na Karume. Kwa bahati mbaya hivi vituo vyote vitatu havina hadhi ya kuitwa vituo vya afya. Ukiangalia katika Kituo cha Karume hakina huduma nzuri, vitanda hakuna, kuna vitanda viwili tu, hakuna kitanda cha akina mama kujifungulia, huduma ya kufanyiwa upasuaji akina mama pia hakuna. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Ummy kwa kuwa na wewe ni mwanamama na unafahamu kabisa kina mama tunapopata matatizo wakati wa kujifungua, utusaidie. Kwa kuwa umesema akina mama wengi wanapoteza maisha wakati wakipata haki yao ya msingi ya kutuletea watoto hapa duniani, naomba utusaidie basi kutuboreshea vituo vya afya hivi vichache tu ambavyo vipo katika Wilaya ya Ilemela. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namuomba pia Waziri aweze kuisaidia Halmashauri ya Ilemela kwani ni change, kila inapotenga pesa kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma bora za afya haiwezi kufanikiwa kwa sababu inakuwa ina majukumu mengi na hivyo kuelemea halmashauri. Hivyo, namuomba Waziri aweze kutusaidia basi Wilaya ya Ilemela tuondokane na hivi vituo vitatu basi walau atuongeze vituo viwili ili tuweze kusogeza huduma karibu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia leo nilikuwa sina mengi sana lakini naongelea pia kuhusiana na suala zima la Benki ya Wanawake. Naomba Serikali iweze kuingalia hii Benki ya Wanawake. Mheshimiwa Mbunge ambaye amechangia katika hili suala la huduma ya Benki ya Wanawake amesema

kwamba Serikali imetenga shilingi milioni 900, ninasita mimi katika kusoma bajeti ya Serikali, nimeona Serikali imetenga shilingi milioni 500 tu na siyo shilingi milioni 900. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri Ummy aliwahi kusema kwamba atatoa shilingi bilioni mbili kila mwaka. Kwa mwaka huu wa fedha kama Serikali imetenga shilingi milioni 500 tu sioni kama tutafikia malengo ya kuweza kuiendeleza Benki hii ya Wanawake hapa Tanzania. Ukiangalia benki hii sasa hivi ina mtaji wa shilingi bilioni 20 tu peke yake. Kwa hiyo, kama katika mwaka huu watafanikiwa kuongeza hizo shilingi milioni 500 ambazo zimetengwa bado benki hii haiwezi kuwasaidia wanawake. Hakuna matawi mengi hapa nchini, kuna matawi machache sana ambayo yako kwenye mikoa michache nadhani ni mitano au nane...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Goodluck Mlinga ajiandae Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba Waheshimiwa Wabunge wanipongeze kwani katika Bunge hili la 2015-2020, mimi ni Mbunge wa kwanza kupeleka *ambulance* ya kisasa Jimboni kwa kutumia gharama zangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kufika hapa mpaka leo hii maana huko nje magazeti yote Mlinga, Mlinga, kamtu kenye hata kwenye mkono hakaenei. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yangu ya Wilaya Mheshimiwa Waziri ina shida sana. Japokuwa mimi Mbunge nimejitahidi nimepeleka *ambulance* lakini kuna upungufu mkubwa wa vifaa tiba, hata mashine ya kufulia hakuna, watumishi hakuna, wapo wachache mno. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba katika bajeti yako unikumbuke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Idara ya Maendeleo ya Jamii hakuna watumishi wa kutosha, hakuna vitendea kazi, wako maofisa hata pikipiki hawana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba unikumbuke katika bajeti yako hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa suala la NHIF. Waheshimiwa Wabunge ni-declare interest mimi nilikuwa Compliance Officer - NHIF. Nafahamu shida zilizopo katika shirika hili lakini hata hivyo nashukuru viongozi

waliopo wamejitahidi. Kuna suala la mashirika ya umma kukataa kwenda kujiunga na *NHIF* na kusababisha huu mfuko ufe. Kama sisi Wabunge tumejiunga na *NHIF*, haya mashirika yana nini mpaka washindwe kwenda kujiunga na *NHIF*? Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge niwape siri moja, hii mifuko binafsi ya *insurance* ina mikono ya wakubwa.

MBUNGE FULANI: Wataje.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: *TCRA* hawataki kujiunga na *NHIF* kwa nini? *EWURA* hawataki kujiunga na *NHIF* kwa nini? Kama sisi Wabunge tumeweza kujiunga kwa nini wao wasijiunge? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiwa *Compliance Officer* nilishawahi kwenda *TRA* kuonana na Mkurugenzi Mkuu ili wafanyakazi wa *TRA* wajiunge na *NHIF*. Jibu alilonipa, haki ya Mungu ni kwa sababu ilikuwa ofisini kwake lakini angekuwa ofisini kwangu asingetoka. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na bahati nzuri ameshatumbuliwa jipu, aliniambia sisi pesa sio tatizo maana nilimwambia *NHIF* mnachangia kidogo mnapata matibabu mengu, wigo wa matibabu ni mpana. Halafu pia sheria inataka mashirika ya umma yajiunge na *NHIF*. Akaniambia sisi hela kwetu sio shida, nikamuangalia kimoyomoyo nikasema hizi fedha za kwako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hilo, mashirika mengi ya umma hawataki kujiunga na *NHIF* kwa sababu wanapewa *ten percent* wanapokwenda kujiunga na mashirika binafsi ya *insurance*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kinanisikitisha sana nacho ni ubakaji wa wazee, sijui Wizara hii mnaliangaliaje suala hili. Kuna mikoa ubakaji wa wazee umeshamiri. Huwa najiuliza shida ni nini au wanawake wa maeneo ya huko wagumu kuelewa somo mpaka hawa watu wanaenda kubaka wazee? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba mfanye utafiti mgundue ni nini kinachosababisha tatizo hili. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utulivu Waheshimiwa Wabunge, nimepata tuhuma nyingi sana jamani. Nimeitwa teja, jamani Waheshimiwa Wabunge hebu mnitazame, teja anaweza akawa anashinda amevaa suti zimenyooka namna hii? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba ukiniita mbilikimo nitachukia kwa sababu ukweli mimi ni mbilikimo na kila nitakapokuona nitakuchukia lakini ukiniita teja siwezi kuchukia kwa sababu sio ukweli na ukweli huwa unauma, kwa hiyo siwezi kuchukia. Nimepata vitisho

vingi, lakini naamini Serikali yangu ipo. Kama wanajeshi walienda kuwakomboa wananchi wa Kongo wakaisambaratisha M23 watashindwa kunilinda mimi tena Mbunge? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Waheshimiwa Wabunge wamefurahi lakini naomba mnisaidie kumwambia Waziri wa Ujenzi, naomba Daraja la Kilombero liishe mwaka huu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi, naomba kumaliza kwa kusema naomba uje ukitembelee Kituo changu cha Afya cha Lupilo. Sitaki kuongelea hapa lakini naomba uje ukitembelee kituo changu cha afya uone jinsi kilivyo, hakifanani kufanya matibabu ya binadamu, sisemi lakini naomba tuondoke wote uende ukajionee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi, ndio hayo tu. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, hayupo?

MBUNGE FULANI: Yupu.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili bila kuwasahau wananchi wangu wa Newala ambao wamenifanya niwe katika jengo hili, nawashukuru. Niwaambie kwamba waendele na maandalizi ya msimu wa korosho wa 2016/2017 ambapo wamebakiza miezi miwili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutoa mchango wangu kwa Wizara hii, nianze kumpa pongezi Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchapa kazi nzuri. Pia nimpe pongezi Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Vilevile niwapongeze Mawaziri wangu na niwaambie kwamba nawapongeza sana lakini waendele kuchapa kazi pamoja na ugumu wanaoupata katika bajeti hii, wao waendele tu hivyo hivyo na sisi tutaendelea hivyo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukakosa kila kitu maisha yakaendelea, lakini huwezi kukosa afya maisha yakaendelea maana huo utakuwa ndio mwisho wa uhai wako. Hii inaonesha umuhimu wa Wizara hii ya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua nia nzuri ya Serikali yangu kwamba sera ya Chama cha Mapinduzi ni kujenga vituo vya afya kwa kila kata na kujenga zahanati katika kila kijiji. Pia kutoa maisha bora kwa watumishi wote ambao watakuwa katika hivyo vituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikumsikia Mheshimiwa Waziri ambaye ndiye mwenye dhamana akizungumzia kuhusu mpango wa kujenga vituo vya afya. Maana nilitarajia Mheshimiwa Waziri angekuja na mpango mkakati wa kuonesha kwamba je, hiyo sera yetu ya Chama cha Mapinduzi ya kujenga vituo vya afya kila kata utakuwaje na kwa maeneo yapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matibabu ya wazee na tumeanza kutoa michango ya matibabu ya wazee tangu tukiwa Madiwani karibu miaka mitano au sita huko nyuma, kila siku tumekuwa tukizungumzia kwamba sera ya wazee inatayarishwa na ipo mezani. Sisi ambao tulikuwa tunapita kunadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tulikuwa tunawaambia kwamba Mheshimiwa Magufuli akishapita basi tunatarajia kwamba matibabu kwa wazee yatakuwa bure. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hakuja na mpango mkakati wa kuonesha wale wazee ambao hawana uwezo watatibiwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sasa hivi wakati umefika kuwa na mkakati kuhakikisha wale wazee ambao wapo katika vijiji maana yeye amezungumzia wale wazee waliopo katika vituo kwamba wanatoa vyakula na kutoa huduma za kimsingi lakini Serikali ina mpango gani kuhusu wale wazee ambao hawapo katika vituo vya kulelea wazee? Vijijini ndiko ambako kuna wazee wengi ambao kwa kweli wengine hawana uwezo, hawana hata pesa ya kuweza kununua dawa. Kwa hiyo, ni wakati umefika Serikali kuona hawa wazee ambao hawana uwezo ni nani ambaye anaweza akawalipia hizi bima za matibabu ili na wao waendeleo na maisha kwani sote hapa ni wazee watarajiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata kule ambako kuna vituo vya afya vichache hakuna watumishi katika vituo hivyo. Mimi natokea katika Wilaya ya Newala, nina vituo vya afya viwili lakini nina kata 22 ambako kuna vijiji zaidi ya 146 lakini hatuna watumishi katika vituo hivyo vya afya. Vituo hivyo vya afya vilijengwa *early 1970's* wakati Waziri wa Afya akiwa Mheshimiwa Nangwanda Sijaona lakini vilijengwa jengo tu lakini hakuna zile huduma za mama na mtoto, ina maana sehemu ya akina mama kujifungulia hakuna. Kwa hiyo, sisi tunapata matatizo kwani akina mama hawa wanajifungulia kwenye chumba kidogo hivyo kukosa uhuru na kushindwa kujifungua kwa nafasi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hao watumishi wachache waliopo hawana sehemu ya kuishi. Mheshimiwa Waziri hakuja na mkakati wa kuonesha

kwamba hawa watumishi wachache waliopo katika hivi vituo vya afya watajengewa nyumba ama wataboreshewa vipi makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemuomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atueleze vile Vituo vya afya vya Kitangali na Chihango ambavyo vilijengwa miaka ya 70 ambavyo vilishindwa kumaliziwa na Serikali za awamu mbili au tatu ambazo zimepita, Serikali hii ina mpango gani wa kuweza kuzimalizia ili ziwe na sifa ya kusema kweli kwamba hivi ni vituo vya afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu dawa au tiba tunazozipata hospitalini maana tunapokwenda tunakosa dawa lakini unapokwenda kununua katika maduka ya dawa unakuta dawa ambazo zimeruhusiwa kuingia hapa nchini ni dawa kutoka India tu. Ina maana kwamba wanaotengeza dawa ni watu kutoka India pake yake katika dunia hii na watu wote wananunua dawa kutoka India? Huko India kuna kitu gani, ina maana Wazungu wao wananunua dawa huko? Inasemekana kwamba magonjwa mengi ya ini na figo yanatokana na matumizi ya dawa ambazo hazikidhi viwango. Ina maana sisi tunakula dawa nyingi ambazo zinakosa viwango na ambazo zipo chini viwango. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inavyosemekana baadhi ya dawa kutoka India zinakosa vile viwango na ndiyo maana watu wengi wanatumia zile dawa kwa muda mrefu bila kupata unafuu.

Kwa hiyo, naomba kama kuna dawa zinapatikana katika nchi zingine ambazo zina viwango vya juu basi Serikali ifanye mkakati wa kuingia katika hilo soko ambalo nchi zingine au nchi za Ulaya au soko la Ulaya wanaenda kununua hizo dawa siyo kufanya masihara au mchezo na maisha ya Watanzania. Maana nchi bila afya njema haiwezi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza awali kwamba unaweza ukakosa kila kitu, ukakosa barabara, ukakosa huduma ya maji lakini ukikosa afya njema hilo Taifa haliwezi kuwa na nguvu. Naomba Wizara hii ijikite katika kuhakikisha kwamba dawa ambazo tunanunua ni zile ambazo zipo katika soko la awali au dunia ya kwanza ndizo wanazokula na sisi tule hizo ili tuwe na afya bora. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine tumeambiwa hapa kwamba bajeti ambayo ilikuwa imetengwa mwaka jana ni asilimia 100 lakini iliyofika kule ni asilimia 39, tatizo ni nini? Kama Wizara zingine zimekwenda kule asilimia mpaka 70, afya tumeifanyia masihara. Jamani tuache kufanya masihara na afya zetu, afya ni jambo la muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuhakikishe kwamba hao vijana ambao hawajaajiriwa waajiriwe ili wawepo katika hivi vituo vya afya. Mbona Wizara ya Elimu imeweza japokuwa kunakuwa na upungufu lakini ule upungufu wa Wizara ya Elimu hauwezi kufananishwa na Wizara ya Afya. Wizara ya Afya ni kweli kabisa hasa katika wilaya au mikoa iliyoko pembezoni kule hakuna kabisa watumishi. Unamkuta mtumishi au nesi, yeye ndiye anayekupokea, anaandika cheti, ndiye anayekupa dawa. Hivi inawezekana vipi ukapiga kona wewe mwenyewe na ukaenda ukafunga wewe mwenyewe, inawezekana hiyo? *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Haiwezekani!

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri afanye tathmini hasa kwa hii mikoa iliyopo pembezoni mwa nchi hii. Kwa mfano, sisi Wilaya ya Newala ina Hospitali ya Wilaya pale lakini wale watu wanaokuja kutibiwa wengine wanatoka Msumbiji. Pamoja na kuwa na hiyo Hospitali ya Wilaya lakini nina vijiji karibu 146 na hiyo *Town Council* yenyewe ina vijiji karibu 80, je, vinatosha?

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. AJALI R. AKBAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Mgeni Jadi dakika tano na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea dakika tano kwa pamoja.

MHE. MGENI JADI KADIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, mwenye kunipa nguvu na afya njema nikaweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Maalim Seif Shariff Hamad kwa hekima yake na busara zake kuweza kuwatuliza Wazanzibari kwa matokeo ya Uchaguzi Mkuu. Kama si hekima zake basi sasa hivi tungekuwa tayari wengi wamekufa na wengi wamepata vilema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, sasa nakuja kwenye hoja. Mimi naanzia kuchangia hoja kwenye suala la UKIMWI. UKIMWI ni janga la Taifa na unapoteza nguvu kazi za vijana wetu katika Taifa hili. Pamoja na utafiti wa Serikali kusema kuwa UKIMWI umeshuka kuanzia asilimia 8.8 mpaka kufikia asilimia 5.1 lakini bado UKIMWI unaongoza. Utafiti unaonyesha mikoa mitano ya Tanzania ndiyo inaongoza kwa UKIMWI ambayo ni Mbeya, Iringa, Shinyanga, Dar es Salaam pamoja na Njombe. Mimi nataka kuzungumzia Mkoa wa Shinyanga kwa sababu ndiyo tulioutembelea na tukaona hali halisi ya wagojwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu wanasema, kuanzia Januari mpaka kufikia Disemba wagonjwa waliofika kwenye kituo cha afya na kupimwa wakaonekana ni waathirika katika Mkoa wa Shinyanga walikuwa ni wagonjwa 34,826, maambukizi mapya yalikuwa 953, hii ni asilimia kubwa. Nakuja kwa wajawazito, wajawazito waliofika kupimwa kati ya mwezi wa Januari mpaka Disemba walikuwa 81,509 na waliogundulika wameathirika ni wanawake 2,737, ni asilimia 3.4. Hii inaonyesha ni maambukizi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri alizungumzia kuwa ataongeza vituo na dawa lakini hakuzungumzia chakula. Wagonjwa hawa wa UKIMWI wanapokula dawa za ARV basi ni lazima wapatiwe chakula kwa sababu dawa zina nguvu na wanazidi kuathirika. Kwa hiyo, naomba Serikali itenge fungu maalum la kuwasaidia hawa waathirika walio katika mikoa hii iliyoambukizwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nakuja kwa wakunga jadi. Wakunga wa jadi ni watu ambao wanatoa msaada mkubwa katika kuwasaidia akina mama wajawazito vijijini. Naiomba Serikali wawape mafunzo hawa waliokuwa hawajapata na waliopata mafunzo waajiriwe, Halmashauri ziwatazame, ziwape angalau posho za kupata sabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya afya na zahanati ziboreshwe kwa sababu miundombinu yake ni mibovu. Hakuna maji, umeme na vitendea kazi na isitoshe vituo vya afya vinajengwa mbali na wananchi. Kwa hiyo, ni shida, mzazi akipakiwa kwenye baiskeli mpaka akifika kwenye kituo cha afya basi huyo hali yake ni taabani, hana nguvu za kusukuma mtoto inampelekea kufariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali ifanye juhudi za makusudi ili kuwapatia wanawake hawa gari angalau kila kata au kila kituo kipatiwe *ambulance*. Wenzangu wengi wamesema na mimi naomba hilo ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia watoto wa mitaani. Watoto wa mitaani ni wetu lakini inakuwa ni kero. Watoto hawa ni kweli maisha ni magumu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi lakini pia nikupongeze kwa niaba ya Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa nimpongeza sana Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni ukweli na itakuwa busara sana Wizara ya Afya ikaichukuwa na kuyatumia yale yote ambayo yameainishwa mle. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano kupitia Rais, Mheshimiwa John Pombe Magufuli ameahidi kutupatia vituo vya afya kwenye kila kata. Kwa hiyo, hili ni deni ambalo Serikali ya Awamu ya Tano tunaidai. Tulikuwa tunategemea katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa ita-reflect moja kwa moja kwenye ahadi ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ama amezitaja au hakuzitaja lakini nataka Wizara ijue kwamba sisi kama Watanzania tunategemea kuona vituo vya afya kwenye kila kata. Mimi nikuambie tu Temeke ambako nina kata 13 tuna kituo cha afya kimoja na Hospitali ya Temeke kwa hiyo nakudai vituo vya afya 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati wako nitakufuata uniambie tunavipataje ndani ya miaka hii mitano. Kama ni kupata viwili kila baada ya mwaka, kupata vitatu kila baada ya mwaka itakuwa ni jambo zuri. Kimsingi tunahitaji ahadi mlizozitoa zitekelezwe kwa sababu wananchi wanazisubiria. Laa kama mnaona yale mlioyaahidi hayawezi kutekelezeka basi isemwe ili tujue kwamba tunatafuta source zingine kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kwa sababu sisi kama Wabunge bado tuna nia thabiti ya kuwasaidia wananchi kuhakikisha kwamba huduma ya afya inapatikana katika maeneo yao ya karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilitaka kuishauri Wizara ya Afya, wakati inafanya *allocation* au namna ya kuzisaidia hizi hospitali izingatie sana mazingira ya kijiografia. Sisi katika Hospitali ya Temeke tunapata taabu sana

pale kwa sababu muda wote hospitali inazidiwa na wagonjwa kwa sababu tu ya mazingira ya kijiografia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Temeke inapakana na Mikoa ya Kusini mwa Tanzania kwa maana ukitoka Temeke sasa ndiyo unaelekea Kusini. Kwa jiografia tu mbaya ya Mkoa wa Pwani, nasema jiografia mbaya kwa maana Mkoa wa Pwani umekakwa kati na Mkoa wa Dar es Salaam. Sasa mtu hawezi kutoka na mgonjwa labda Utete akampeleka Tumbi - Kibaha yaani avuke Temeke, haiwezekani maana yake atamshusha Temeke. Mtu hawezi kutoka na mgonjwa Kibiti akaipita Temeke aende Tumbi - Kibaha atamshusha Temeke halikadhalika na Mkuranga. Kwa hiyo, kumbe Hospitali ya Temeke haihudumii tu watu wa Temeke, inahudumia na watu wa mikoa ya jirani. Sasa tunapofanya zile *allocation* tuangalie mazingira haya ya kijiografia kwa sababu sisi tunakuwa tumezidiwa si kwa maana ya wakazi wa Temeke lakini kwa maana ya jirani zetu na unafahamu suala la huduma ya afya huwezi kumwambia mtu kwamba wewe hutokei Temeke nenda huko, kwa hiyo lazima wote tuwasaidie pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Wizara mlizipandisha daraja hizi hospitali za Temeke, Ilala na Mwananyamala, cha ajabu bado mmeuacha mzigo kwa halmashauri. Serikali irudi na itekeleze majukumu yake kwenye hizi hospitali kwa ni mzigo mkubwa sana kwa Halmashauri. Unaita Hospitali ya Mkoa halafu inahudumiwa na Halmashauri, vyanzo vyetu havitoshelezi kuzihudumia hizi hospitali. Ni lazima Serikali itekeleze wajibu wake kuhakikisha kwamba hizi hospitali zinakuwa na wafanyakazi, wataalam na vifaa tiba. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana mpaka leo mwana mama anapokwenda kujifungua abebe na vifaa vidogo vodogo vya kwenda kumsaidia kujifungua hospitalini. Huu ni udhalilishaji mkubwa wa mama zetu. Kwa nini Serikali ishindwe hata kuweka vifaa vidogo vidogo kama *groves*, sindano, uzi, beseni, kweli? Miaka zaidi ya 50 kweli tunashindwa kupata sindano za mama kujifungulia?

Kwa hiyo, wako kina mama wengine wanadhalilika, wanajifungulia kwenye daladala kwa sababu tu hakwenda hospitali mapema alikuwa hajatimiza hivyo vifaa vya kwenda kujifungulia. Hebu tujaribu kuyatengeneza haya mazingira ya kujifugulia akina mama yawe mazuri na yenye staha kwa ajili ya kulinda heshima ya mwanamke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Ngeleja.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza na mimi naungana na wenzangu kukupongeza sana kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuipongeza Wizara kwa hotuba yao nzuri. Katika kuwapongeza pia nitawakumbusha baadhi ya mambo yanayohusu Jimbo langu la Sengerema lakini pia nitaomba maombi katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nina ombi langu la muda mrefu, naikumbusha Wizara, naamini watendaji wa Wizara pia wako hapa wanasikiliza. Wilaya ya Sengerema tuna Hospitali Teule ambayo kimsingi inamilikiwa na watu binafsi, ni Shirika la Kidini la *Roman Catholic* lakini ndiyo hiyo hiyo hospitali ambayo imekuwa ikisaidia wananchi wa Sengerema na maeneo mengine yanayozunguka eneo letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nimekuwa nikipumbusha na leo nakumbusha tena kwa mara nyingine na naamini nitapata majibu sahihi leo kwamba *formula* inayotumika pale kutoa ruzuku ya Serikali ambao ni utataribu wa kawaida ina-base kwenye vitanda 150 lakini leo hii hospitali ile ina uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa kwa kuzingatia uwezo wa sasa wa vitanda zaidi ya 375. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu liko Wizarani, naamini Katibu Mkuu yupo anaelewa, ambacho namuomba Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati wanatoa majumuisho ya ufafanuzi wa hoja zao kesho basi hoja hiyo ya ombi letu la Sengerema ambalo ni ombi la muda mrefu walitolee majibu. Hospitali ya Sengerema kwa kweli inasaidia Wilaya nyingi zilizoko upande wa Magharibi mwa Mkoa wa Mwanza, kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi kuhusu ongezeko la ruzuku kwenye Hospitali Teule ya Sengerema. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu walioshauri kwamba Bohari ya Dawa ifungue maduka yake katika kila Hospitali za Wilaya. Tunafahamu juhudi zinazofanywa katika Hospitali za Rufaa pamoja na Mikoa, lakini haitoshi. Inawezekana kabisa kwamba changamoto yake ni kwenye bajeti lakini kama nilivyoshauri wakati nachangia Ofisi ya Rais na kama Wabunge wengine walivyoshauri, mafungu haya bado hatujaridhia, eneo hili la huduma ya afya ni muhimu sana, usambazaji wa dawa ni mojawapo ya jambo muhimu sana katika uendelezaji wa Taifa letu. Tungependa kuona huduma hii inawasogelea zaidi wananchi hasa katika hospitali za Wilaya. Tuangalie namna ambavyo tunaweza kurekebisha bajeti zetu tukawezesha hii Bohari ya Dawa kupitia Wizara ya Afya tuwasogezee

wananchi huduma katika kufungua maduka ya dawa katika hospitali zetu za Wilaya. Hilo ni jambo la pili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nilikuwa nasoma hotuba ya Wizara, uko ukurasa umeelezea Hospitali za Kikanda hasa za rufaa, nadhani ukurasa wa 52, wameelezea mambo mengi. Nina ombi hapa, Taifa kwa muda wote limekuwa linajitahidi sana kujenga hospitali za rufaa kikanda kurahisisha huduma kwa kusaidiana na sekta binafsi na hasa masharika ya dini. Nafahamu zipo hospitali kubwa ambazo zina hadhi ya rufaa ambazo zinamilikiwa na makampuni ama mashirika binafsi. Hata hivyo, bado Serikali pia haijawahi kusimamia juhudi zake za kufungua hospitali kubwa za rufaa zinazomilikiwa na Serikali. Ombi langu kwa Wizara ya Afya izingatie na itafakari upya mwelekeo wa ufunguaji wa hospitali za rufaa. Ombi langu naloliweka mbele ya Bunge lako Tukufu ni ujenzi wa hospitali inayomilikiwa na Serikali yenye hadhi ya rufaa katika Kanda ya Ziwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 52 hapa utaona zipo kanda ambazo zimeainishwa zingine zina mikoa miwili, sitaki kusema hizi zenye mikoa miwili zidharauliwe, hapana! Ninachotaka kulisitiza pamoja na kwamba Kanda ya Ziwa tuna hospitali inayoitwa Hospitali ya Bugando kwa kweli imezidiwa. Sisi tunaotoka kule tunafahamu huduma zilizoko pale sasa hivi, sitaki kuwabeza juhudi wanazozifanya wauguzi na madaktari waliopo pale, lakini kimsingi wamezidiwa. Hii ndiyo Kanda ambayo ina mikoa mingi zaidi lakini ina hospitali moja tu ya rufaa ambayo kwa kweli kwa mazingira tuliyo nayo sasa hivi haimudu na haikidhi! Huko nyuma tulishatoa ombi hili na tukaahidiwa kwamba Serikali ilikuwa inatafakari kujenga Hospitali ya Rufaa katika Kanda ya Ziwa. Tunaomba sana Serikali kupitia Wizara hii itafakari na baadaye mtupe maelekeo na matumaini tunakoelekea ni wapi. Uwezekano wa kujenga Hospitali ya Rufaa kwa Kanda ya Ziwa upo au haupo? Hilo ni jambo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kushauri na kwa kweli ni kwa kuzingatia hali halisi tu ilivyo ni kuhusu hizi huduma za wazee. Tunaona juhudi za Serikali zinafanyika, madawati ya wazee yamefunguliwa kwa kila Hospitali ya Wilaya lakini jambo hili linahitaji ufuatiliaji wa makini. Nashukuru mmesema sasa hivi kutakuwa na madawati ya kutoa taarifa lakini sisi tulioko *site* tunafahamu, kama alivyosema Mheshimiwa Shabiby na Waheshimiwa wengine, kwa kweli madawati yale yamekuwa kama vile ya kutoa huduma za vipimo na kuandikiwa tu ambacho wewe kinakusibu maana wazee wakifika pale mara nyingi hawapati dawa. Naomba jambo hili tuliangalie kwa umakini na kwa macho mawili ili kuimarisha huduma za afya kwa wazee. Kama alivyosema Mheshimiwa Waziri sisi wote tuliopo hapa hata kama siyo wazee ni wazee watarajiwa tu, ndiyo *nature* ilivyo tutafika hatua hiyo, kwa hiyo, naomba sana wazee wetu tuwazingatie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, naishukuru sana Wizara, Mheshimiwa Naibu Waziri lakini pia Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Ummu ameniahidi kwamba baada ya bajeti hii atafika Wilaya ya Sengerema, tunamkaribisha sana. Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, miezi miwili iliyopita alikuwa Sengerema tunamshukuru sana kwa juhudi zake alizofanya. Tunaomba tena msichoke kuwazungukia wananchi kwa sababu kadri mnavyofika ndivyo mnavyoimarisha utoaji wa huduma zinazotakiwa katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mwongozo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) kuhusiana na jambo lililojitokeza mapema wakati Mheshimiwa Susan Lyimo alipokuwa anachangia. Pia sambamba na Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inazungumzia kuhusiana na kutoa taarifa ambazo si sahihi. Vilevile pamoja na Kanuni ya 63(4) mpaka (5) ambayo inanitaka mimi nithibitishe sasa kuhusiana na hizo taarifa ambazo amezitoa Mheshimiwa Mbunge kwamba si sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan wakati anachangia alisema kwamba kuna magari 777 ya washawasha ya Polisi yameingizwa nchini. Mimi nikiwa kama Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, taarifa za uhakika ambazo ninazo ni magari 32. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia akasema kwamba magari hayo ya washawasha, hayo aliyosema yeye 777 hayana umuhimu wowote, lakini mimi nafahamu magari haya yamesaidia sana kuimarisha amani wakati wa uchaguzi. (Makofi)

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hivi tunavyozungumza, kuna mazungumzo yanaendelea kati ya Jeshi la Zimamoto na Jeshi la Polisi ili magari haya ya washawasha yaweze pia kutumika kwa ajili ya shughuli za kuzima moto.

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia nalithibitisha ni kuhusiana na gharama. Amezungumzia kwamba gharama za magari haya ni shilingi bilioni 420 kitu ambacho siyo kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ikiwa Mbunge huyu ambaye ametoa taarifa hizi ambazo si sahihi kwa maeneo haya matatu ambayo nimeyachambua ni hatua gani anapaswa kuchukuliwa? *(Makofi)*

(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, order. Jamani hizi Kanuni zipo na tumezitunga wenyewe mwaka huu katika Bunge hili, wote tumeshiriki. Kanuni hizi zinampa fursa kila Mbunge kupata haki ndani ya Bunge hili kwa upande wowote wa vyama vyote.

Mheshimiwa Waziri ameomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 64(a) lakini ameongeza vilevile Kanuni ya 63(1). Kwa bahati mbaya mhusika Mheshimiwa Susan Lyimo hayumo humu ndani, jioni atakaporudi mwongozo wangu kwa Mheshimiwa Susan Lyimo aweze kufuta maneno yake au kama hataweza kufuta maneno yake alete uthibitisho ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Katibu wa Jumuiya St. Thomas More anakumbushia tena kuwa leo baada Bunge kuahirishwa saa saba mchana kutakuwa na ibada ya misa takatifu katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wote wanaohusika wanaombwa kuhudhuria.

Waheshimiwa Wabunge, jioni wachangiaji wetu wa kwanza watakuwa Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Susan Kiwanga na Mheshimiwa Yahaya Massare.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

(Saa 7.03 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Ahsante. Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA - KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali, kwamba Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante, wachangiaji wetu wa kwanza mchana huu ni hawa watatu, Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Susan Kiwanga na Mheshimiwa Yahaya Massare. Tunaanza na Mheshimiwa Bobali.

MHE. HAMIDU H. BOBALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nianze kwa kusema kwamba binafsi sina mashaka na uwezo, dhamira na nia ya Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii. Ukimtazama usoni unaona kabisa huruma aliyonayo kwa Watanzania, kwa hiyo, sina mashaka kwamba anaweza kuitendea haki huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo mtunzi mmoja wa vitabu maarufu sana, anaitwa Mudhihir Mohamed Mudhihir, aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo ninaloliongoza mimi sasa, ametunga kitabu kinaitwa Mwele Bin Taaban. Dibaji ya kitabu hiki imeandikwa na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Maudhui yaliyopo ndani ya kitabu hiki ya Mwele Bin Taaban naona kama yanafanana na uhalisia uliopo katika nchi yetu hususan namna bajeti ya Wizara ya Afya mwaka huu ilivyopangiwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 9 ya Katiba yetu (i), kinasema kwamba utajiri na rasilimali za nchi hii zitawekezwa kwenye kuhakikisha kwamba zinaondoa matatizo ya umaskini, maradhi na ujinga. Maradhi yanagusa Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa takwimu zinaonyesha kila mwaka Watanzania tunaongezeka kwa idadi ya watu 1,000,000, Wizara ya Afya badala ya kuongezewa pesa yenyewe ndiyo inapunguziwa. Mwaka huu imepunguziwa shilingi bilioni 18 kutoka kwenye bajeti ya mwaka jana wakati wale watu 1,000,000 wameendelea kuongezeka, matatizo ya afya yameendelea kuongezeka, uwezo wa kuyatatua kwa fedha hizi naamini hakuna. Dada yangu hapa ameongea vizuri na nilikuwa namtazama usoni nikiona kabisa dhamira

yake, lakini fedha huna dada! Kwa bajeti hii inaashiria kabisa kwamba *you are going to fail, business* itakuwa vilevile, *business as usual*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano Hospitali ya Rufaa ya Mtwara ya Ligula, mwaka jana mlitenga shilingi bilioni mbili, mwaka huu tena mmetenga shilingi bilioni mbili, nikuulize shilingi bilioni mbili za mwaka jana umepeleka shilingi ngapi, aibu! Mwaka huu tena mmetenga shilingi bilioni 2, najua ni ku-copy na ku-paste tu, pesa hizi haziendi. Kama mwaka jana mlitenga na hamkupeleka, mwaka huu hiyohiyo tu, hamtapeleka fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Mkoa ya Sokoine - Lindi, aibu! Hospitali ile haina chumba wala sehemu ya watu waliowasindikiza wagonjwa kuweza kupumzika. Kwa hiyo, kuna mtu anapeleka mgonjwa wake akifika pale akikaa yeye mwenyewe kesho anageuka kuwa mgonjwa kwa sababu ataugua malaria, atang'atwa na mbu usiku kwa hiyo badala ya kusindikiza mgonjwa na mwenyewe anakuwa mgonjwa, *otherwise* asimame usiku mzima. Hakuna sehemu ya kupumzika watu wanaopeleka wagonjwa Hospitali ya Mkoa ya Sokoine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la Kituo cha Afya Kitomanga kilichopo kwenye Jimbo la Mchinga. Ndiyo maana nasema *this government is it serious?* Pale Kitomanga kuna kituo cha afya, kwenye Jimbo langu la Mchinga, mmepeleka vifaa tiba kama X-ray, mashine za CT-Scan, mmepeleka vifaa vingi na kile kituo cha afya lengo lake ilikuwa mkifanye Hospitali ya Wilaya, huu ni mwaka wa nne, vifaa vile vinaharibika, vinaliwa na panya, ni aibu! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa tatu mwaka huu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya alitembelea pale badala ya kutoa majibu kwamba ni lini kituo hiki kitapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya amekwenda kufanya *issue* kuwa *too much complicated* watu wamekata tamaa. Ameongea na wananchi pale anawaambia kwa namna taratibu na sheria zilivyo, kituo hiki kuja kuwa hospitali itatuchukua muda mrefu, vifaa vile mlipeleka ili iweje? Pia katika maeneo yale watu hawana hospitali ya karibu kwa hiyo wanaendelea kuteseka. Namuomba Mheshimiwa Waziri wakati anakuja kuhitimisha hoja yake hapa aje anipe majibu ni lini mtakipandisha Kituo cha Afya Kitomanga kuwa Hospitali ya Wilaya? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la wazee. Nimemsikia Mheshimiwa Waziri anasema kwamba Serikali ina mpango wa kuleta *Bill of Right* hapa ili Sheria ya Wazee iweze kupitishwa. Sera ya Wazee imepitishwa mwaka 2003 mpaka leo haina sheria. Kinachokuja kutokea Maafisa wa Maendeleo wa Jamii kwenye Wilaya huko kazi wanayojua wao ni ku-deal na wanawake na vijana tu kundi la wazee limesahaulika, hii ndiyo *reality*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata haya mambo yanayozungumzwa kwamba kutakuwa na fedha shilingi milioni 50 za Magufuli za kila kijiji, Maafisa wa Maendeleo ya Jamii wanahamasisha vijana, wanahamasisha wanawake waanzishe vikundi vya ujasiriamali wawapatie fedha, wazee wanaachwa. Ni kwa sababu hawana sheria, kungekuwa na sheria haya yasingetokea. Ukiangalia sera ya wazee ni sera nzuri, yenye lengo zuri la kuwatetea wazee, *unfortunately* kwa sababu hakuna sheria basi ndiyo hivyo mambo yanakwenda tu, *business as usual*, wazee wetu wanataabika. Lililo baya sisi wote ni wazee watarajiwa ikiwa tutafika, kwa hiyo, lazima tuhakikishe tunatengeneza mazingira na sisi miaka 20 mbele ikija tukiwa wazee mambo haya yawe vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo suala la Mfuko wa CHF (Mfuko wa Afya ya Jamii). Mimi jimboni kwangu ndani ya Halmashauri yetu na Mheshimiwa Nape tuko Halmashauri moja, sisi tumekubaliana kwamba tutahamasisha wananchi wetu wote wajiunge na mkakati ilikuwa wakati huu wa msimu wa ufuta wananchi wote wakate kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii. *Unfortunately* tumesitisha na nimewaambia wananchi wangu wasijiunge kwa sababu wanaibiwa bure tu. Mtu anakata kadi kwenye zahanati ya Kilolambwani akienda Mvuleni, kilometa tatu tu anaambiwa hutambuliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia dawa, Halmashauri wanatumia fedha za Mfuko wa Afya ya Jamii kwenye matumizi yao. Kwa hiyo, mtu amekata kadi anakwenda hospitali hana dawa. Wanasema Mheshimiwa sasa hii haja ya kukata kadi inatokea wapi, bora twende tulipe shilingi 5,000. Kwa hiyo, kama kuna hoja ambayo Mheshimiwa Waziri anatakiwa ai-address ni hii issue ya Mfuko wa Afya ya Jamii. Wananchi wameitikia sana, mimi nimewasimamisha jimboni kwangu nimewaambia *never*, mpaka mimi niseme, msijiunge kwa sababu mnaibiwa na mnaibiwa kwa sababu mtu anakata hapa, kilometa tatu anaambiwa hutambuliki lakini pia dawa hakuna, kwa hiyo, anafanana na mtu ambaye hana kadi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie suala moja kwa haraka haraka sana linalohusu pia mambo ya wazee. Sera ya Wazee inasema wazi kwamba wazee na watoto watatibiwa bure, lakini kwa masikitiko makubwa sana, mwezi wa 12 nilipoteza wazee zaidi ya watatu kutoka Jimboni kwangu pale Sokoine. Wazee wale walifariki kwa sababu tu ya kukosa matibabu ya operesheni ya mshipa ngiri eti hawana fedha. Iliniuma sana na inaendelea kuniuma, kama sera inaweka wazi kwamba wazee wanatibiwa bure kwa nini mzee anakwenda hospitali hapati matibabu kwa kigezo tu kwamba hana fedha? Tuwe na huruma na wazee wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kututunzia muda. Tunaendelea Mheshimiwa Susan Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Massare.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hotuba hii ya Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kabisa na kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 75 - 76, naomba kunukuu, nitakwenda pale mwishoni kidogo; "Naomba kutoa taarifa kwamba Serikali inatarajia kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu Muswada wa Mabadiliko ya Sheria ya Bima ya Afya. Muswada huo una mapendekezo mbalimbali ikiwemo sharti la ulazima wa wananchi wote kujiunga na Bima ya Afya na wale wote wenye uwezo kuchangia bima hiyo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kipengele kimenitetemesha mwili mzima nikaikumbuka Mlimba, wananchi watakaolazimishwa kuchangia ikishakuwa sheria ya nchi hii. Mlimba yenye kata 16, yenye kituo kimoja cha afya yaani sitaki hata kusema, ndiyo maana nilikuomba Mheshimiwa Waziri ufike uone mwenyewe. Kama alivyosema Mbunge aliyetangulia kwamba unaonekana una haiba na kweli ndivyo ulivyo, lakini mzigo huu wa Wizara uliyopewa ni mkubwa sana, lakini bila pesa utaishia kulia jinsi kina mama, wazee na watoto wanavyoteseka katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana Mheshimiwa Waziri nimekukaribisha uje Mlimba, mnakwenda tu kwenye yale maeneo ambayo mmeyazoea, naomba mje Mlimba, Jimbo lenye kata 16, vijiji 61, vitongoji mia mbili na zaidi. Mimi nitakupeleka kwenye kitongoji, kutoka kwenye kitongoji mpaka kijiji ni kilometa 20 yaani kutoka kitongojinini mpaka katika kijiji kilometa 20 halafu hapo kwenye kijiji hakuna zahanati, unatakiwa uende tena kilometa 30, ukiongeza na 20 zinakuwa 50, mtoto anaumwa umembeba, wakati wa mvua barabara hazipitiki, maji mpaka kiunoni unaweza kuogelea, jamani kama kuna watu wanakufa nchi hii basi ni Jimbo la Mlimba, hali ni mbaya kuliko maelezo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuuliza ni lini katika bajeti hii itatambua kwamba Mlimba kuna wananchi? Bahati mbaya sana Mlimba tulikuwa wachache, lakini leo tumewapokea watu wa aina mbalimbali, kila kabila unaloliona humu ndani liko Mlimba, ndugu zenu wako kule. Kwa sababu gani, Mlimba ni eneo la rutuba, ukipanda ndizi twende, mpunga twende, kokoa twende, ufuta twende, miti usiseme, mahindi twende, kwa nini wasikimbilie kule, kila kitu kinakubali. Gesi ndiyo iko kule, umeme wa Kihansi upo, kuna shida tena Mlimba? Kwa hiyo, watu wameingia wengi lakini huduma sifuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nimesimama hapa kuchangia hii hotuba, siwezi nikachangia maeneo makubwa sana ya Kitaifa kwa sababu nina wajibu ndani ya Jimbo la Mlimba. Naomba chonde chonde, mje mtembelee Mlimba, mlinganishe na haya ninayoyasema halafu mtaona wenyewe kama hamkulia huku mimi nawaambia. Mimi wakati wa kampeni nilikuwa nalia, hata nilivyokuwa nasikia ooh, waganga wa kienyeji wanafungiwa, fungieni huku huku, kule watu wanatibiwa na waganga wa kienyeji. Hakuna hospitali, hakuna zahanati, hakuna chochote, kwa nini mtu asiende kwa mganga wa kienyeji. Hiyo huduma mnayosema ya wazee labda mjini huku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini dada yangu hapa Mheshimiwa Mollel anasema alikuwa huko Muhimbili, ameshuhudia kwa macho yake mzee amekuja Muhimbili aliambiwa aende akapimwe lakini amekwenda kule *laboratory* akaambiwa baba shilingi 40,000 ni mzee anatembelea mkongojo. Mheshimiwa Mama Mollel akaingilia kati kwa uchungu, kwa nini mnaacha kumtibu huyu baba, wanasema bila shilingi 40,000 hakuna bure, ikabidi atoe amalipie yule mzee apate matibabu. Sasa hii huduma ya wazee iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Dar es Salaam namna hii Mlimba kuna kitu tena kule? Giza totoro, haki ya Mungu kama hatujapata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba chonde chonde, mfike Mlimba. Kwa sababu kama kuna kata 16 kituo cha afya kimoja na chenyewe kinademadema, hawana wodi ya wazazi yaani ni aibu kwa Jimbo la Mlimba. Kutoka Mlimba mpaka Ifakara ambapo kuna Hospitali ya Wilaya ama *St. Francis* ni kilometa 150 barabara zote kama zina makaburi ya watoto kutokana na hayo mashimo, tumewakosea nini? Kule ni hatari jamani, naomba mje muone. Halafu unamwambia ananitania tu, jamani pelekeni vitu kule Jimboni vya Bunge, aah sasa hivi hatuwezi kwenda mvua, kwani tunaoishi kule wanyama? Twendeni hata wakati wa mvua mkaone hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa TAMISEMI kama mpo hapa mchukue, haiwezekani vijiji 61 kuna zahanati 18, haiwezekani! Wananchi kule wanapata wapi matibabu! Hali ni mbaya kuliko maelezo! Kina mama wanakufa kule, kina baba wazee wanateseka kule, watoto wanakufa kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ukurasa wa 75 mlivyoandika kwamba mnakwenda kuleta bima ya afya lazimishi, Mlimba muite katika hayo mambo, hiyo sheria iseme kabisa Mlimba aah aah, tutalazimisha maeneo mengine tu. Kwa sababu haiwezekani, kwanza dawa zenyewe hawapati sasa unalazimishaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, muandae kwanza mazingira ya kuandaa vituo vya afya venye Madaktari, Manesi na dawa za kutosha, mkilazimisha hiyo ni sawa. Msilete sheria kabla hamjaandaa mazingira sahihi ya watu kupata huduma, nendeni mkakague mjiridhishe. Kwa hiyo, mimi naomba hii sheria mmeiandika tu hapa lakini ichelewe kabisa, bado tuko miaka 20 nyuma. Ni nzuri sana kwa sababu nchi za wenzetu wanatekeleza sheria hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichukua takwimu kutoka kwenye halmashauri yangu, nina takwimu hapa na nitakuletea lukuki, kama za TAMISEMI ziende TAMISEMI, kwenye Wizara yako, maana hapa tunapiga, uchungu mwingine, mateso mengine wanatuletea TAMISEMI, ninyi TAMISEMI ninyi, ni matatizo makubwa! Haiwezekani sera inasema zahanati kila kijiji lakini vijiji vyote havina zahanati. Wananchi maeneo mengine wamechangia, wamejenga zahanati, haijamaliziwa, hakuna choo, hakuna mtumishi, hakuna chochote. Kwa nini mnawafanyia hivyo Watanzania? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina maneno mengi, nasema mje Mlimba mjionee wenyewe kama haya maneno ninayosema ni ya uongo ili watu wapate huduma yao kwa mujibu wa kodi wanazolipa, mtushirikishe. Kambi ya Upinzani wamesema vizuri, lakini sasa Serikali hii hata mkishauri mpango mzuri hapa, basi kwa mpango huu CHF na dawa, ili Wizara ya Afya ipate hela ingizeni hata shilingi 50,000 kwenye mafuta ya magari, uongo, kweli? Tukikubaliana hapa kama REA hela sijui mmeipeleka wapi, ninyi vipi? Yaani hapa hata tukipitisha mpango mzuri wa kukusanya shilingi shilingi kwa Watanzania mnapeleka hela sehemu nyingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niishie hapo. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Yahaya Massare, atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Shonza na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ajiande.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uteuzi mzuri wa Baraza la Mawaziri, wameteuliwa majembe ambayo kwa hakika tunaamini yatatufikisha katika safari yetu hii ambayo tunayo. Niwashukuru tena kwa mara nyingine wananchi wangu wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwa kuniamini na kunileta humu na mimi ninaamini kwamba sitawaangusha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Waziri, Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara

hii kwa kuimarisha hospitali yetu kubwa ya Taifa, Hospitali ya Muhimbili lakini Hospitali ya Saratani ya Ocean Road. Kuna changamoto kadhaa ambazo tunatakiwa tuzione na Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha wagonjwa wote hawaendi katika hospitali hizi kubwa na ili wagonjwa wasiende katika hospitali hizi kubwa lazima tuimarishe hospitali za kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 2011/2012 hivi, Serikali ya Awamu ya Nne kuna hospitali ilizipandisha hadhi kuwa Hospitali za Rufaa ikiwemo Hospitali ya Mtakatifu Gaspar ya Itigi ambayo inatoa huduma kwa wananchi wa Itigi lakini kwa Kanda nzima ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ile ina gharama kubwa sana kutokana na Serikali kuachia wananchi kuhudumiwa kwa gharama za Wamisionari wale ambao kwa wakati fulani kule nyuma walikuwa wakipata dawa kutoka kwa wahisani wao lakini baadaye Serikali iliwazuia wakawa wanatakiwa wachukue dawa kutoka MSD, ruzuku wanayopata ni kidogo, matokeo yake hospitali ile imekuwa na gharama kubwa sana sasa na itapelekea hospitali hizi kubwa za Muhimbili, KCMC na nyingine kupata mzigo mkubwa kwa sababu hizi Hospitali za Kanda na za Rufaa hazifanyi kazi vizuri. Gharama zile ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni katika uchaguzi uliokwisha. Wananchi wale ni waaminifu walikipa chetu Chama cha Mapinduzi kura nyingi sana na Mheshimiwa Rais walimpa kura nyingi lakini moja ya ahadi yake ilikuwa kwamba atatoa ruzuku ya Serikali kwa Hospitali ile ya Mission ili iwasaidie wananchi wa maeneo yale ikiwemo wananchi wa Jimbo langu la Manyoni Magharibi hususani wananchi wa Mji wa Itigi na vijiji ambavyo vinaizunguka takribani kata 13 ikiwemo Wilaya nzima ya Manyoni watu wanakimbilia pale wanaposhindwa katika Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi ya Mheshimiwa Rais ilikuwa ni kupeleka Madaktari Bingwa pale lakini kuongeza ruzuku na kutoa mgao kutoka MSD. Tukilifanya hili tutakuwa tumewasaidia wananchi wa Jimbo langu na watakuwa wameendelea kumuamini Mheshimiwa Rais wetu na ahadi zake zitakuwa endelevu kwa sababu aliyasema haya katika mkutano wa hadhara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wagonjwa wafike katika hospitali hizi kubwa wanatokea katika vituo vya afya. Katika Jimbo langu la Manyoni Magharibi kuna kata 13 lakini tuna vituo vya afya viwili na kimoja ndiyo tuko katika kuhangaika kujenga na mafungu yenyewe ndiyo haya ya taabu. Kwa hiyo, niombe sasa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kupitia Mawaziri hawa, madaktari na maprofesa watusaidie sasa wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi kwa kuhakikisha tunajenga kituo cha afya kwa kila kata lakini na hospitali kila kijiji na sisi tutasaidia pale ambapo tutapaswa kuwajibika katika maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna janga kidogo hapa katika vituo vidogo hivi vya zahanati za vijiji hazina matabibu wale kwa maana ya *Clinical Officers* hawapo kabisa. Baadhi ya zahanati kama Gurungu, Njirii, Ipande, Kitopeni, Ukimbu na hata Kintanula. Kuna nesi mmoja huyo huyo ndiye anaenda kukuandikia dawa, anakupatia tiba na baadaye anakutolea dawa. Sasa ni wakati muafaka wa kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuyafanya haya yawe mepesi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya ahadi zetu katika chaguzi ilikuwa ni pamoja na kusogeza huduma hizi lakini kusaidia wazee na kwamba watapata matibabu haya bila usumbufu, lakini bure. Hii imekuwa changamoto kubwa, matibabu ya bure yamekuwa na udhia sana kwa wazee hasa wanapofika hospitali. Kama nilivyokwishatangulia kusema mimi katika Jimbo langu watu wangu wanatibiwa katika Hospitali ya Wamisionari. Jambo hili wamekuwa hawalitambui sana, sasa si vibaya Serikali ikaingilia kati iwasaidie wananchi wale ili wazee nao wanufaike na mpango huo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ni bima ya afya, kuna huu Mfuko wa CHF umekuwa na changamoto nyingi. Wakati mwingine watu wanachangia zile fedha lakini anapofika katika kituo cha afya au zahanati anakuta dawa hazipo. Niombe sasa juhudi za makusudi kwa Serikali hii kushirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Afya wayafanye haya yawe mepesi ili wananchi wetu kule vijijini waendeleo kuwa na imani hii ambayo wanayo sasa ya kutuchagua sisi viongozi tunaotokana na Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo nimetaka kulizungumzia kidogo, tumeweka nguvu sana kwenye matibabu ya moyo katika hospitali hizi kubwa. Niipongeze Serikali kwa juhudi hizi ilizochukua kuhakikisha sasa magonjwa haya makubwa yatatibiwa katika Hospitali yetu ya Taifa. Hata hivyo, kuna janga lingine la magonjwa haya yasiyoambukiza ukiwemo ugonjwa wa kisukari, tumekuwa hatuchukui hatua za kutosha na sasa watu wengi wakiwemo Waheshimiwa Wabunge ni wagonjwa wa ugonjwa huu wa kisukari. Ni vyema sasa Serikali nayo ikatafuta matabibu wazuri, Madaktari Bingwa aidha watu wetu wakaenda kusoma kwa nchi ambazo tayari zinaonyesha kwamba zina maendeleo mazuri juu ya tafiti na kugundua tiba nzuri ya magonjwa ya kisukari. Watu wetu wamekuwa wakifa kwa kupewa dawa ambazo pengine si sahihi au utaalamu ambao hautoshi. Niombe Serikali yangu Mawaziri hawa ambao mimi nawaamini kwa asilimia mia moja kutokana na ushirikiano wanaotupa sisi Wabunge basi na hili jambo walichukue, walifanyie kazi ili baadaye ugonjwa huu usiwe tatizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaki kupigiwa kengele, naomba kumalizia hapa na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Juliana Shonza atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuweza kukushukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Afya. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kasi kubwa anayoenda nayo ya kuhakikisha kwamba anatumbua majipu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme kwamba inashangaza kuona waliokuwa wakipiga kelele kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni dhaifu sasa wamegeuka wanasema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni ya kibabe, wamegeuka wanasema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina utawala wa kiimla. Nashindwa kuelewa ni kipi ambacho hawa wenzetu wanataka tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakumbuka kwamba siku zote wamekuwa wakipiga kelele na bahati nzuri *Hansard* za Bunge hili zipo wamekuwa wakisema kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kabisa kukusanya mapato. Tumeshuhudia baada ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kasi yake ya kuendelea kutumbua majipu, TRA kwa mwezi Aprili wameweza kukusanya mapato ya shilingi trilion 1.035. Hii yote ni matokeo ya kasi kubwa na uwezo mkubwa wa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli lakini wenzetu hawa wamegeuka wanasema kwamba Serikali hii ni ya kibabe inatumbu majipu hovy, hali hii inasikitisha. Kwa sisi kama wanasiasa vijana tunashindwa kujua nini hasa ambacho tutajifunza kutoka kwa hawa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijielekeze kuzungumzia Wizara ya Afya. Kwa kuzingatia kwamba mwaka 2015 ilikuwa ni ukomo wa kuweza kufikia Malengo ya Milenia ambapo Lengo Kuu la Tano ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunapunguza vifo vya akina mama kufikia asilimia 75. Mpaka sasa hivi takwimu zinaonyesha kwamba vifo vya akina mama kila mwaka ni zaidi ya 15,000. Hali hii inatisha sana, inatisha kwa sababu akina mama wetu kule vijijini wanapata shida sana inapofika suala la huduma za kiafya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kwa kina mama ukija kwenye vifo vya watoto, takwimu zinaonyesha kwamba ni zaidi ya watoto 40,000 kila mwaka wanafariki ndani ya saa 24. Takwimu hizi sisi kama Taifa hatupaswi kabisa kuweza kuzifumbia macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile takwimu zinaonyesha kwamba akina mama 250,000 kila mwaka wanapata vilema vya uzazi, hali hii inasikitisha sana.

Mimi niombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ambayo ni sikivu iweze kuwahurumia kina mama hawa mfano mama zangu wa kule Songwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niishukuru sana Serikali kwa sababu imeweza kutupatia mkoa. Mkoa wetu wa Songwe, ni mpya lakini kama unavyojua changamoto ni kubwa kwa hii mikoa mipya. Mkoa wa Songwe hatuna kabisa Hospitali ya Mkoa, hiki ni kilio chetu, mimi nikiwa kama mwakilishi wa akina mama wote wa Mkoa Songwe naomba utusaidie katika jambo hili. Nashukuru kwa sababu Waziri wa Wizara hii ni mwanamke mwenzetu, Wanawake wa Mkoa wa Songwe wanapata shida sana, tunaomba na sisi muweze kutufukiria muweze kutujengea Hospitali ya Mkoa ili basi akina mama wale waweze kupata tiba kiurahisi. (Makofi)

Mheshimiwa mwenyekiti, vilevile katika Wilaya ya Momba ambayo ni Wilaya mpya, cha kushangaza mpaka leo hii hatuna kabisa Hospitali ya Wilaya. Unaweza ukaona akina mama wa Wilaya ya Momba wanapata shida kiasi gani? Wilaya ile hakuna Hospitali ya Wilaya na sera katika Wizara ya Afya inasema kwamba ni kuhakikisha kwamba kila Halmashauri kunakuwa na Hospitali ya Wilaya. Halmashauri ile ya Momba mpaka leo hii hakuna kabisa Hospitali ya Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kituo cha Afya pale Tunduma lakini ni kidogo, hakiwezi kutosheleza kuweza kuhudumia Wilaya nzima. Ni kituo ambacho kwa sasa hivi kinatumika kama Hospitali ya Wilaya ya Momba lakini kina changamoto nyingi. Naomba Waziri aweze kukiangalia Kituo kile cha Afya cha pale Tunduma. Kituo kile hakina madaktari wa kutosha, hakina x-ray za kutosha, ukiangalia hata sehemu ambako mama zetu wanaenda kujifungulia kwa kweli hali pale inasikitisha. Inafika mahali mama mjamzito anayeenda kujifungua katika kituo kile lakini hakuna sehemu ambayo mama huyo anaweza akaendelea kujisubirishia wakati anasubiri kwenda *theater*. Naomba sana Serikali iweze kukiangalia kile kituo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi navyoongea kuna vitanda vinne tu vya akina mama kujifungulia. Hicho ni kituo cha afya ambacho kinatumika kama hospitali ya wilaya lakini chagamoto zake ni kubwa mno. Mpaka sasa hivi kuna vitanda vitano tu ambavyo vinatumika kwa akina mama kupumzika baada ya kuwa wameshamaliza kujifungua. Kama unavyojua mama akishamaliza kujifungua inatakiwa akae chini ya uangalizi wa daktari si chini ya saa 24 lakini kwa sababu ya uhaba wa vitanda wanawake wale wanalazimika kutolewa ndani ya saa mbili, tatu kurudi nyumbani. Naomba sana suala hili liangaliwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kuweza kukumbusha ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni. Alipita pale Momba na kwa bahati nzuri pale Momba tuna majengo yako pale Chipaka. Majengo yale yalikuwa ni ya wakandarasi yameachwa pale, ni makubwa mno yanafaa kabisa kuweza kutumika kama hospitali ya Wilaya. Jambo zuri ni kwamba Mheshimiwa Rais alituhidi kwamba majengo yale ataweza kuyakabidhi kwa Serikali ili yaweze kutumika kama Hospitali ya Wilaya. Nimesimama mahali hapa kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Songwe kuweza kumkumbusha Mheshimiwa Rais akumbuke ahadi yake aweze kuwapatia akina mama wale majengo yale ili basi Wilaya ya Momba tuweze kuwa na Hospitali ya Wilaya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nizungumzie kidogo Idara ya Maendeleo ya Jamii. Idara hii ni muhimu sana kwa Taifa letu na ni mtambuka. Huwezi kwenda vijijini kwenda kutoa elimu ya ujasiriamali kwa akina mama kama hujatumia idara hii. Nionyeshe masikitiko yangu makubwa kwamba idara ile imesahaulika sana, wale Maafisa Maendeleo wamekaa pale kwenye Halmashauri hawana kazi, hawapelekewi pesa za OC ambazo zitawasaidia kushuka kule kijijini kuhakikisha kwamba wanatoa elimu ya ujasiriamali kwa akina mama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawaomba Mawaziri wetu na nashukuru sana kwa sababu tuna Mawaziri ambao ni sikivu, dada yangu Ummy naomba sana wakati mwingine utakapokuwa ukitembelea hospitali unavyoenda unakutana na ma-DMO uchukue nafasi uweze kuonana pia na Maafisa Maendeleo ili waweze kukupa changamoto zao. Wamekaa pale Halmashauri hawana kazi, wanalila sana, kilio chao wanaomba ukisikie na mimi nina imani kabisa kwamba Serikali hii ni sikivu, itaweza kwenda kuwasikiliza na siku moja changamoto hizi zitafika mwisho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni huduma ya afya katika Wilaya ya Mbozi. Wilaya ya Mbozi ndiyo makao makuu ya Mkoa wetu wa Songwe. Ukifika pale ile wodi ya kujifungulia kwanza ni ndogo mno, wanalala kitanda kimoja akina mama wawili, watatu, inafika mahali mpaka wengine wanajifungulia chini. Naomba Serikali na naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutuangalia katika wodi ile ya akina mama pale Mbozi kwa kuiongeza ukubwa ili basi wa akina mama wale waweze kujifungua mahali ambako ni salama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naamini kwamba maombi haya yamezingatiwa na kilio cha akina mama wa Mkoa wa Songwe kitafika mwisho, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Juliana Shonza kwa mchango wako.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ameunga mkono hoja, ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuandaa hotuba nzuri sana yenye kuleta matumaini. Nawashukuruni sana na nawapa pongezi sana kwa kazi nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa niaba ya Mkoa wangu wa Simiyu na Wilaya yangu ya Maswa napenda niwapongeze Naibu Waziri pamoja na Waziri kwa kutembelea katika Hospitali ya Wilaya ya Maswa. Kulikuwa kuna majengo mapya ya *OPD* na *theater*, nawashukuru jengo la *OPD* limeanza kufanya kazi baada ya kukamilika kwa muda mrefu, lakini lilikuwa halijaanza kufanya kazi. Kwa sasa wananchi wa Maswa wanapata huduma kupitia *OPD* mpya, nawashukuruni sana kwa hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda tu kuendelea kusema kwamba changamoto imebaki kwenye *theater*. *Theater* zimejengwa kubwa na nzuri, lakini hazina vifaa, madaktari ni wachache, tunaomba muendeleo kuweka juhudi zenu basi *theater* ya pale Maswa ambayo ni *theater* kubwa na ya kisasa ianze kufanya kazi hasa tukizingatia kwamba Hospitali ya Wilaya ya Maswa ni tegemeo katika Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu lingine katika Wilaya yangu hiyo ya Maswa ni kwamba hospitali hiyo basi ikiwezekana muipandishe hadhi kwa sababu ni hospitali ambayo ina vifaa vingi vya kutosha lakini haijapandishwa hadhi. Ki-*capacity* ni kubwa, tunaomba basi muangalie uwezekano wa kutuletea madaktari na vifaa vya kutosha ili iweze kutoa huduma zaidi katika Mkoa wetu wa Simiyu. Wagonjwa wengi wanaondoka katika Wilaya yetu ya Maswa na Mkoa wa Simiyu wanapokuwa *referred* katika Hospitali ya Rufaa wanakwenda Bugando. Ni mwendo mrefu, ni kilometa zaidi ya 120 wanakwenda kupata huduma kule. Basi naomba muweze kutusaidia hospitali hiyo muipandishe hadhi ili wananchi wangu wa Maswa waweze kupata huduma nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile nijadili bajeti. Bajeti ya Wizara ya Afya kwa kweli mimi bado inanisikitisha kwani ni ndogo. Kuna upungufu kweli wa shilingi bilioni 18 ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana lakini kinachonipa

moyo ni kwamba utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana ulikuwa ni asilimia isiyofika 40 lakini nina hakika chini ya utawala wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli zimewekwa *ceiling* mpya, hizo *ceiling* mpya za kila Wizara nina hakika utekelezaji unaweza kwenda asilimia zaidi ya 80, hapo ndipo ninapopata matumaini makubwa. Tunaomba tushirikiane na Serikali hii tuweze kuhakikisha kwamba pesa zinakusanywa na utekelezaji wa kupeleka pesa katika Wizara ya Afya uwe wa kutosha na mambo yaweze kwenda vizuri kama ilivyopangwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wizara hii ya Afya kuna matatizo ya wazabuni. Kwa mfano, Chuo cha Uganga Wilaya ya Maswa, toka mwaka 2010 wazabuni wame-*supply* pale vyakula na bidhaa mbalimbali lakini hawajalipwa pesa zao. Kuna deni la shilingi milioni 270 na wazabuni wako 15, wengine wametaifishiwa mali zao na benki kwa sababu hawajalipwa pesa zao na benki zinawadai, kwa kweli wamebaki hohehahe kisa wamefanya biashara na Wizara ya Afya. Mimi nafikiri kufanya biashara na Wizara ya Afya siyo dhambi, ni vizuri mkawajali hawa watu mkawalipa madeni hayo. Pia sehemu zingine zote nchini wazabuni walipwe ili waweze kurudi kwenye kufanya biashara zao. Tunashirikiana na watu binafsi basi tusiwa-*discourage* kwa kutowalipa madeni hayo. Naomba mfanye juhudi ya kutosha muweze kuwalipa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika Wizara hii ni MSD. Nakubaliana kabisa na pande zote mbili ya Upinzani pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Jamii, MSD wapelekewe pesa zao *on time* ili waweze kununua dawa na ku-*supply*. Kwa sababu tutaendelea kuwalaumu wakati kumbe Serikali na yenyewe inahusika kutokupeleka pesa zao kwa muda unaostahili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niongelee kuhusu malipo ya madaktari. Madaktari wetu wanafanya kazi nzuri sana, wanapata shida kwa sababu wanafanya kazi, wanakwenda kwenye *call* zao lakini pesa haziji *on time*. Madaktari wengine wanadai pesa nyingi hawajalipwa mpaka leo.

Naomba Wizara iangalie uwezekano kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 muwalipe madaktari hawa. Madaktari hawa kwa kweli wanafanya kazi kubwa lakini malipo ni madogo, tushirikiane, tushikamane Mheshimiwa Waziri muwalipe madaktari pesa zao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuwa *frustrated* nchi hii soma udaktari. Unasoma sana, unafanya kazi sana lakini malipo ni kidogo. Watu waliosoma mambo mengine unawakuta wanafanya vizuri tu na mambo yao ni mazuri, ukisoma udaktari inakuwa kama vile ni dhambi. Na-*declare interest* na mimi nilipitia huko huko, kwa kweli naomba muilee hii fani kwa sababu ni muhimu, ni fani ambayo huduma yake tunahitaji watu wote, kila mmoja hapa ni mgonjwa

mtarajiwa na anakabiliwa na maradhi. Tunaomba mboreshe huduma za afya na muanzie kwa madaktari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia suala kuhusu mafunzo ya wafanyakazi, muongeze idadi za vyuo na kozi mbalimbali ambazo zinaweza ku-produce wafanyakazi wengi wa Wizara ya Afya. Mmepunguza tatizo kutoka asilimia 58 la upungufu wa wafanyakazi wa afya mpaka asilimia 51, bado haitoshi. Tunataka twende kwenye asilimia ndogo ya upungufu wa madaktari na wafanyakazi wa Wizara ya Afya. Tunaomba huduma iweze kuboreshwa na huwezi kuboresha huduma bila kuwa na wafanyakazi wengi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na ushauri wa Kamati kwamba Wizara hii ikiwezekana itenganishwe na TAMISEMI kwa sababu kunakuwa sasa na mlolongo ambao hauendi sawa. Unakuta madaktari walioajiriwa na Serikali Kuu na madaktari walioajiriwa na TAMISEMI wanagongana katika maslahi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfano mmoja japo siyo mzuri madaktari waligoma walikuwa wanataka mafao yao yalipwe na walikuwa wanataka walipwe stahili zao za kutosha, waligoma kutoa huduma ili kuisukuma Serikali ilete huduma. Hata hivyo, unapogoma wakati wafanyakazi au madaktari walioajiriwa na TAMISEMI wanaendelea na kazi ile *impact* ya kugoma inakuwa haipo, Serikali haiwasikilizi, mwisho wa siku Serikali inawagonganisha, inaonekana kama madaktari wanayumba au wanapishana. Wanayumba na kupishana kwa sababu wameajiriwa na waajiri wawili tofauti, huyu kaajiriwa na Serikali Kuu mwingine kaajiriwa na TAMISEMI. Wanapoungana pamoja kudai maslahi yao ya kutosha inashindikana kwa sababu wanakuwa na waajiri wawili tofauti.

Kwa hiyo, naomba hii Wizara ya Afya ishughulikie masuala yote ya afya pamoja na wafanyakazi wote wa afya kuanzia juu hadi ngazi ya chini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kuongelea suala la huduma za afya. Mheshimiwa Waziri kwa kweli huduma za afya ni duni nchini kwetu. Ukitaka kujua nchi imeendelea ni pale unapopiga simu ya *emergency* uone muda wa waganga au gari la *paramedical* linavyokuja kutoa huduma. Ukienda nchi zilizoendelea ukipiga simu kuna dharura ni dakika tano tu hata haziishi unakuta huduma tayari imeshafika mlangoni. Nchini kwetu ni saa hata 24 unaweza ukapiga huduma haijafika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano mmoja wa ajali zinazotokea barabarani. Ikitokea ajali sasa hivi wanaokufa pale pale *on the spot* ni wachache sana wengi wa wanaokufa ni wale wanaokosa huduma ya

afya. Mtu anapata *bleeding* kwa muda mrefu, anakata roho kwa sababu hakupata huduma ya afya ya haraka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri umefika wakati sasa Wizara iangalie uwezekano wa kuwa na *unit* inayoshughulikia *emergency case*. Tunapoteza wananchi wengi kwa sababu ya kukosa huduma ya haraka ya afya yaani huduma ya kwanza. Unapopata ajali labda upasuke kichwa au kifua hapo ndiyo unakufa *on the spot* lakini wengi wa wanaokufa ni kwa sababu wanakosa huduma ya mwanzo. Tunaomba hili suala Mheshimiwa ulitizame kwa kina ili uweze kulitafutia ufumbuzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hoja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Anafuata Mheshimiwa Anna Lupembe; Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Suzana Mgonokulima wajiandae.

MHE. ANNA L. LUPEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetulinda, ametuleta tena mara nyingine hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja, naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. Wizara yao ni kubwa sana lakini wanajitahidi sana, wana majukumu mazito, naomba mpambane Mungu atawasaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi sasa hivi una miaka kama minne inaelekea mitano, hatuna Hospitali ya Mkoa. Tumeambiwa tumetengewa pesa tujengewe Hospitali ya Mkoa wa Katavi lakini mpaka leo hatuoni jitihada ya aina yoyote. Sasa hivi Mkoa wa Katavi una watu wengi, ukishasema mkoa ina maana umepanua wigo mkubwa kwa hiyo, shughuli mbalimbali zinafanywa ndani ya Mkoa wa Katavi lakini hatuna Hospitali ya Mkoa, tumebaki na Hospitali ya Wilaya ya Mpanda ambayo ndiyo imebeba majukumu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mpanda ni ndogo na wafanyakazi ni wachache, nashukuru na wao wenyewe wamejionea. Wameainisha hapa kwenye hotuba ndani ya Mkoa wetu wa Katavi ukiangalia Wilaya ya Mpanda Vijijini, Mpanda Mjini na Wilaya mpya ya Mlele kuna sehemu wamesema asilimia 100 hakuna wahudumu. Sasa sijui wananchi wa Mkoa wetu wa Katavi wanaoumwa wanafanyaje. Naomba Mheshimiwa Waziri uliangalie kwa makini sana suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamekukaribisha uende kwenye Mikoa yao, naomba Mheshimiwa Waziri uje Katavi ujionee mwenyewe hali halisi ya Mkoa wetu na jinsi wananchi wanavyopata shida ya matibabu. Hospitali ile ya Wilaya, manesi pamoja na madaktari saa nyingine wanachoka, wakichoka sasa lugha zinakuwa tofauti. Wagonjwa wakienda pale kauli zinakuwa tofauti, zinakuwa mbaya kwa sababu si wao, wamechoka. Naomba Mheshimiwa Waziri muangalie kutupatia Hospitali ya Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mlele ina hospitali ambayo imejengwa na Serikali. Naomba niipongeze Serikali imejenga hospitali nzuri sana Inyonga lakini mpaka leo ni kituo cha afya. Mmeweka vifaa vingi na vizuri lakini kasoro yake ni ndogo sana, ni choo tu hakuna ndiyo imefanya hamtaki kuipandisha iwe Hospitali ya Wilaya ina maana Wilaya ya Mlele hakuna Hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Waziri tunaomba tupandishie hii hospitali na tuletee wafanyakazi. Vile vifaa mlivyoleta vimekaa sasa vimeanza kuharibika kwa sababu hakuna wataalam wa kuvitumia. Sasa inakuwa tunachezea hela za Serikali kututangulizia vitu wakati wahudumu na wataalam hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hospitali ambayo iko Inyonga imejengwa vizuri sana lakini tatizo lake ni choo tu. Mmejenga majengo makubwa, mazuri, lakini sijui ilikuwaje huyo mkandarasi aliyewekwa hakuweka choo mpaka leo hii tunashangaa ilikuwaje. Kila mtu anashangaa kwa sababu tunaomba muipandishe hadhi inashindikana, ukiuliza tatizo unaambiwa hamna choo. Sasa sijui katika utaalam ilikuwaje, mmejenga majengo mazuri, mmeleta vifaa vikubwa na vizuri halafu choo hakipo halafu hamtaki kutoa kibali ili iwe Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa naomba mtusaidie kwani wananchi kule wanapata shida, jiografia yetu ya Mkoa wa Katavi jamani ni ngumu, naomba chonde chonde mtusaidie. Ukienda kule Mheshimiwa Waziri utasikitika wananchi wanavyohangaika huduma hamna. Naomba Mheshimiwa Waziri ile hospitali hata kama haina vyoo tupandishieni iwe na hadhi ya Hospitali ya Wilaya ili wananchi wa Wilaya ya Mlele wapate huduma safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa Chuo chetu cha Msaginya. Tuna chuo pale kinaitwa Msaginya, Chuo cha Maendeleo lakini hakifanyi kazi yoyote. Chuo kile ni kizuri, mnakitolea pesa kila mwaka, lakini kwa nini hamna mipango mizuri mkapeleka watu wakajifunza pale? Kuna vijana wengi ambao wamekaa bure hawana kitu chochote cha kufanya wangeenda huko. Vyuo mmevijenga vizuri, wataalam mmewaweka kwa nini vijana wasiende pale wakajifunza useremala na akina mama wakaenda pale wakajifunza ujasiriamali? Vile vyuo majengo yanaharibika na mnapoteza hela nyingi.

Naomba hivi Vyuo vya Maendelo ya Jamii viwekewe mikakati mikali ili vijana wengi wajifunze ujasiriamali kupitia Vyuo hivi vya Maendeleo ya Jamii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa Benki ya Wanawake. Kwanza, naomba nimpongeze Mkurugenzi wa Benki ya Wanawake, Mama Chacha, amefanya kazi nzuri lakini bado hajatufikia sisi akina mama kwenye Mikoa, Wilaya na Vijiji vyetu, ameishia Dar es Salaam na asilimia kubwa ya akina mama wako vijijini. Najua watu wengi wamesema hii benki haiwezekani lakini wanawake wote wana haki ya kupata benki hii kila mkoa kwa sababu hela iliyochukuliwa kuianzisha ni Serikali. Kwa hiyo, kila mkoa tunahitaji Benki ya Wanawake ili wanawake wa Tanzania hii wajivunie benki yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kuzungumzia Bima ya Afya, hii mimi naisemea kila siku. Bima ya Afya dawa hakuna! Tunaomba sasa Bohari Kuu waende moja kwa moja viwandani kuchukua dawa. Kama dawa ziko huko Ujerumani, India waende moja kwa moja wakachukue dawa huko ili waje kuwahudumia Watanzania. Hizi dawa wanazochukua kwa wafanyabiashara hazikidhi mahitaji.

Tunaomba sasa Serikali iwape fungu kubwa Bohari Kuu ya Dawa ili sasa wananchi wote waweze kupata huduma safi na salama wajivunie Serikali yao kupitia Bima ya Afya. Sisi tuko tayari kufanya hamasa, wananchi wote waingie kwenye Mfuko wa Bima ya Afya lakini tunaomba mtuwekee dawa ili wananchi wapate huduma safi na salama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Grace Tendega badala ya Mheshimiwa Suzana Mgonokulima.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya mimi kuchangia Wizara hii muhimu sana ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na data za Wilaya yangu ya Uyui kwamba kuna kata 30, vijiji 156, vitongoji 688. Data za afya ni Hospitali ya Wilaya inatakiwa iwepo moja hakuna, vituo vya afya vinatakiwa 30 kipo kimoja na zahanati mbovu mbovu zipo 45. Eneo hili lina ukubwa wa kilometa za mraba 11,804 na wakazi 404,900. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti kabla ya yote, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya amenisaidia sana kunipitishia zahanati moja kuwa kituo cha afya, kwa hiyo, *theoretically* nina viwili. Pia nitoe pongezi kwa kijiji kimoja kinaitwa Chambola ambacho kimepigana na kuondoa kabisa vifo vya

akina mama, kwa muda wa miaka kumi sasa hakuna mama hata mmoja aliyekufa akijifungua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kituo cha Afya cha Upuge, kituo hiki kimejengwa kwa mkopo wa hela za ADB. Kituo hiki kina mitambo yote ya kisasa, kuna mitambo ya kutengeneza oxygen inaweza kujaza hospitali zote za Kanda ya Magharibi, kuna seti ya kisasa kabisa ya vitanda viwili wanaweza kufanyiwa operesheni akina mama wawili. Mitambo hii ina miaka miwili tangu ilipokamilika na kufungwa lakini haijafanya kazi hata siku moja. Mheshimiwa Waziri naomba aje na jibu zuri la suala hilo kwa sababu wananchi wote na hata ADB waliotupa hizo hela wakija leo watatushangaa sana. Tulienda kuomba mkopo kwamba ni jambo muhimu sana lakini mpaka sasa mitambo mwaka wa pili haijafanya kazi. Namuomba sana Mheshimiwa Waziri aje na mambo mazuri kuhusu suala hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati nyingine, kule kwetu Unyamwezini, kule Uyui hakuna dawa. Zahanati kilometa 50, 100 mtu anakwenda hakuna dawa. Matokeo yake waganga wa kienyeji kina Maji Marefu wangekuja kule wangetengeneza hospitali. Hakuna hospitali kule, kuna majengo mabovu mabovu ya zahanati hakuna dawa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata taabu sana ninaposikia hapa kuna bajeti imeandaliwa ya Wizara ya Afya, nimepitia hii bajeti sioni utashi wa Serikali kunijenge vituo hivi ninavyovidai. Kama Uyui nzima ina kituo kimoja cha afya vinatakiwa 30 ningeona kwenye bajeti hapa Uyui tumeongeza vituo hata viwili, bora kuanza kuliko kukaa pale pale. Mimi ningeshekuru sana kama Mheshimiwa Waziri atakuja na majibu kwamba katika Wilaya ya Uyui hii mpya inakusudiwa kujengewa kituo. Bahati nzuri Naibu Waziri wa Afya anatoka vilevile Tabora na anajua hii hali. Kwa hiyo, ningetegemea kwamba nitapata upendeleo maalum lakini mambo haya yananipa taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maradhi kuondolewa ilikuwa ni ajenda ya kwanza tulivyopata uhuru kwa maana ya maadui wale watatu ilikuwa maradhi, umaskini na ujinga. Kule kwetu Jimbo la Uyui Kaskazini na Wilaya nzima ya Uyui sioni kama kweli ipo kisiasa nia ya kuondoa umaskini pale au nia ya kuondoa maradhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ndugu yangu Waziri, kwanza ni mtani wangu namshukuru sana ananisaidia lakini aje na dawa ya H5 yaani aje aseme natibu, hakuna maji H ya kwanza, H ya pili hakuna umeme kwenye kituo changu cha Upuge hicho, H ya tatu hakuna wataalam, atibu na H ya nne hakuna gari la wagonjwa, atibu na H ya tano hakuna vifaa vya tiba katika zahanati nyingine zote. Mimi nitamshukuru sana Mheshimiwa Waziri akija na mambo hayo ambayo nimeyataja hapo juu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ajaribu kutatua tatizo la dawa. Kila siku nasikia *Medical Store* au *MSD* tunavyoiita wanachoma tani 30, 40 za dawa ambazo zimepitwa na wakati, zime-expire. Dawa hizi wakiona kama bado miaka miwili zigawanywe bure badala ya kuzichoma zitumike kwa sababu kuna watu wanataka dawa leo hawangoji za mwaka kesho. Kama *Medical Store* wanachoma tani tatu au 10 za dawa, inagharimu kuchoma dawa lakini dawa zimenunuliwa na mahitaji ya dawa katika nchi hayajapungua hata siku moja. Uwepo mpango mzuri Mheshimiwa Waziri wa kuzuia kuchoma dawa badala yake zigaiwe bure maana kama mnazichoma wapeni watu bure hizo dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la *Community Health Fund*. Huu mfuko ulikuwa kimbilio yaani kule kwetu waliposikia kuna huu mfuko wamepatikia kweli kweli lakini badala yake mzee mwenye nyumba anafariki amekamata kadi, ameenda hospitali hakuna dawa au kafiwa mama na kadi yake mkononi ya *CHF* hakuna dawa. Kadi zile watu walifikiri labda watapata dawa, lakini kadi zile hazitumiki na zikitumika hakuna dawa Mheshimiwa Waziri. Hii ni *reality* tuje tuangalie, unajua leo naongelea *serious issues* hapa hakuna kipepeo wala kupeperushana nasema ukweli kwamba *CHF* imekuwa kama mchezo fulani. Nakushukuru sana kwenye hotuba yako hii Mheshimiwa Waziri umesema utaileta iwe sheria na mimi naahidi nitawanunulia kadi kaya 2,000 ili mradi kuwepo na dawa, watu wapate kadi ambazo watapatia dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kata moja inaitwa Igulungu ilijengwa zahanati kwa mchango maalum ikafikia mpaka linta, ikaambiwa zahanati hiyo imejengwa karibu na hifadhi ikatelekezwa, huu mwaka wa 15 jengo lipo vilevile. Mimi wakati napiga kampeni nikasema nitalimalizia wakasema huwezi. Mimi nina uwezo wa kulimalizia jengo hilo lakini kuna *stop order* kwamba lipo karibu na Hifadhi ya Wanyama sasa nini bora wanyama au watu? Naomba Serikali itoe mwongozo kuhusu zahanati hii iliyojengwa karibu na wanyama. Watu hawatakwenda kwenye wanyama, kwanza wagonjwa watakimbizaje wanyama, hawawezi kukimbiza wanyama, watakuja kununua dawa au kutibiwa pale kwenye zahanati. Serikali iingilie kati ili tumalizie hiyo hospitali kwani hatutakwenda kukamata wanyama au kuingia kukata misitu, watu wagonjwa hata shoka hawana wanasogeleaje misitu! Hawa watu wana hatari gani, hawana hatari yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda sana kuwa mkweli, naipenda Serikali yangu, nampenda Waziri na Waziri mdogo ni ndugu yangu, mwanangu lakini katika suala hili wamenituma wananchi nje nida hospitali na zahanati zijengwe. Tumepiga kura kumpa Mheshimiwa Rais kwa ahadi hiyo kwenye Ilani na mimi nimetangaza na mtu mzima kama mimi kuonekana muongo kwa wapiga kura hairuhusiwi. Nimewaambia tutaleta zahanati na kutakuwa na

dawa sasa naonekana mimi muongo. Mimi sipendi naomba Mheshimiwa Waziri aje na dawa yangu ile ya H5. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana niachie wengine, naunga mkono hoja hii, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Maige. Tunaendelea na Mheshimiwa Grace Tendega atafuatiwa na Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia katika Bunge hili. Kwa sababu ni mara ya kwanza na mimi kuchangia katika bajeti napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kuweza kuja humu kuwakilisha akina mama wa Mkoa wa Iringa. Napenda pia kushukuru chama changu ambacho pia kimeniwezesha kuwa Mbunge. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie kwa kuanza na kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 89, ukatili wa kijinsia. Kumekuwa na matatizo mengi, kumekuwa na ukatili wa kijinsia ambao unafanyika katika nchi yetu na hasa waathirika wa tatizo hilo ni wanawake na watoto. Tumeona wanawake wengi wanafanyiwa ukatili wa kinyama, tumeona watoto wetu wanafanyiwa ukatili wa kinyama, tumeona watoto wanachomwa moto, tumeona watoto wanamwagiwa maji ya moto, tumeona madhara mengi kwa watoto wetu wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameeleza katika hotuba yake kwamba wataendelea kusimamia sheria, sheria zipo Mheshimiwa. Kama zipo na matukio yanaendelea kuna tatizo kubwa katika nchi hii la usimamizi wa sheria. Nikuombe Waziri unapokuja kuhitimisha hoja zako uweze kutueleza usimamizi huo utakuwaje tofauti na mazoea ya siku za nyuma ambayo yalikuwa yakiendelea ambapo akina mama wengi wananyanyasika, watoto wengi wananyanyasika, watoto wamekosa kabisa wa kuwasemea, tumeona watoto wanafichwa kabisa ndani kwa miaka kadhaa. Inatia uchungu kwa sisi wazazi ukiona matukio yale yanaendelea katika nchi hii ambayo tunasema ina amani na utulivu. Mheshimiwa Waziri tunaomba uweze kulisimamia na kwa sababu ni mwanamke mwenzetu basi uchungu huu najua unao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika masuala ya afya kwa ujumla. Tukiangalia bajeti ambayo imetengwa kwa Wizara hii, asilimia ambazo waliomba 100 wao wamepewa asilimia 11, hivi tutatekeleza kweli haya yote? Ndiyo maana wenzangu waliotangulia wanasema wanamuonea huruma Waziri kwa sababu matatizo ni mengi, mahitaji ya afya ni mengi huko kwenye Wilaya na majimbo yetu kuna matatizo lukuki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikizungumzia katika Wilaya ya Iringa, Jimbo la Kalenga, tumekuwa na shida kubwa ya huduma za afya. Zahanati wananchi wamejenga, ukienda Wasa wamejenga zahanati lakini hakuna madaktari na manesi wananchi wanatoka kule kuja hospitali huku Ipamba ambapo ni mbali. Watu wanatoka Kata ya Magulilwa na kata mbalimbali kwa sababu hakuna hospitali za kuwahudumia na wakifika pale wanapata shida kwa sababu dawa lazima wanunue na dawa ni gharama na wakati mwingine hazipo. Kwa hiyo, kumekuwa na changamoto kubwa sana katika hospitali zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri aweze kutupa majibu hizi changamoto zitatatuliwa lini, huu upungufu wa madaktari na wataalam katika maeneo yetu utakwisha lini? Hawa wananchi wameweza kujitolea kujenga majengo lakini mengine yamekaa kama magofu hakuna madaktari wala dawa. Serikali hii mnasema ni sikivu lakini watu wanapotea na tunasema afya ndiyo mtaji wa kwanza kwa jamii yetu. Sasa kama Serikali hii ambayo mnasema ni ya viwanda kwa sasa hivi, je, hivyo viwanda vitaendeshwa na watu wasio na afya bora. Tunahitaji kuwekeza kwenye afya ili tupate Watanzania wenye fikra bunifu za kuweza kuwekeza huko kwenye viwanda. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri uweze kuja na majibu ya masuala hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwa upande wa wazee, huko ndiyo kabisa. Tunashuhudia wazee wetu wakipata shida hospitalini. Hii Sera ya Wazee kupata huduma ya afya bure haitekelezeki, hawapati dawa. Wazee wanakwenda hospitalini wale wahudumu wetu madaktari na manesi wanatoa maneno ya kashfa kwa wazee wetu, inatia uchungu. Wazee hawa wameifanyia kazi kubwa nchi hii, wameweza kufanya mambo mengi kwa nchi hii lakini sisi hatuwalipi hata fadhila ya kupata dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta ni rahisi kwa nchi yetu na Serikali hii ya CCM kuitisha mkutano wa wazee Dar es Salaam, lakini mara nyingi haiwezi ikawatimizia ahadi zao. Ni rahisi sana wakawa wamewekwa sehemu wazee wasikilize lakini kutimiza ahadi zao inakuwa ni ngumu. Tukuombe Mheshimiwa Waziri uweze kutuambia hawa wazee matibabu bure yatapatikana lini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa huduma za afya kwa watu wenye ulemavu. Mara nyingi tupo nao, tukiwa kwenye foleni hospitalini mnawaona hawa watu hawapewi kipaumbele kama inavyotakiwa. Hawa watu wanahitaji kuhudumiwa kwa ukaribu. Mimi nikuombe tu Mheshimiwa Waziri kwenye hitimisho lako hawa watu ikiwezekana wapewe bima ya afya ili waweze kutibiwa kwa bima ya afya. Kwa sababu wanapata shida sana, wengine hata hawajiwezi, hawajui wapate wapi pesa ya matibabu, hawajui wataendaje

hospitalini lakini hawahudumiwi! Tunaomba wapate bima ya afya kwani itawaokoa wao kuweza kutibiwa na kuweza kuwa kama watu wengine kwa sababu na sisi ni walemavu wa kesho, hakuna ambaye sio mlemavu, ikitokea itakuwa ni bahati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa katika Mfuko wa Bima ya Afya. Mfuko wa Bima ya Afya huko ndio kabisa, ukimgusa mwananchi huko kijijini ukamuelimisha anakuelewa lakini anakuja na swali tukienda hospitalini watu wenye kadi za bima ya afya wanatengwa, hawapati huduma haraka, wananyanyapaliwa sana, hii adha itaisha lini? Unakuta mtu ana bima ya afya lakini akienda pale wanasema tunahudumia kwanza wanaolipa cash wengine mtasubiri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na WAVIU wale Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Rhoda Kunchela atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Ngonyani, ajiandae Mheshimiwa Stella Ikupa Alex.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabla ya kuanza kuchangia napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai ambao amenipatia. Napenda niunge mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa asilimia mia moja. Kwa nini naunga mkono asilimia mia moja, kwa sababu hotuba ya Upinzani imeeleza uhalisia wa maisha ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma katika *document* zilizopita kila siku Wizara hii inapunguziwa bajeti. *Abuja Declaration* ambayo mlisaini mwaka 2001 lengo lake hasa ili kuwa ni ku-improve afya ya Watanzania. Ukisoma kwenye vitabu vyenu kuanzia TAMISEMI mpaka hii hotuba yenu ambayo mmei-present leo inaonyesha dhahiri kabisa kwamba hamjajipanga kwa sababu pesa mlizotenga ni ndogo.

Pia ukiangalia kwenye hii bajeti ya TAMISEMI inasema kwamba mlitenga shilingi bilioni 277 lakini kuna shilingi bilioni 518, jumla inakuwa ni shilingi bilioni 796. Sasa ukipiga kwa asilimia 100 ya shilingi trilioni 22 ambazo zimetengwa unapata ni asilimia 4.5. Shirika la Afya Duniani linasema kwamba mnatakiwa mfikishe asilimia 15. Sasa hii inaonyesha ni kiasi gani mme-fail kutekeleza hii *Abuja Declaration*, ingekuwa haina maana msingesaini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nataka nichangie kidogo kuhusiana na Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi. Siwezi kuunga mkono hoja kwa sababu ni aibu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuendelea kupunguza bajeti, lakini wananchi wetu wanaendelea kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hospitali hii Mheshimiwa Waziri hakuna vitendea kazi lakini aibu nyingine inayoikumba Serikali ya Chama cha Mpinduzi ni kwamba hospitali nzima hakuna *BP machine* wala *thermometer* na *oxygen machine* ipo moja na inatumika kwa wodi sita, sasa hii ni aibu! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie kuhusiana na masuala ya wazee. Wazee ni watu ambao wanateseka kwenye nchi hii lakini ukisoma kwenye hii hotuba ya Waziri haijaonyesha *specifically* mmetenga kiasi gani kwa ajili ya kutunza hawa wazee, mme-generalize tu yaani inaonekana kama hampo *serious* na hawa wazee. Naendelea kuwashangaa wazee kwa nini wanaendelea kukipa kura Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali kwa sababu Halmashauri zetu zimeshindwa kukusanya mapato haya basi sasa zingeachiwa Manispaa kukusanya mapato. Inaonekana kabisa kwamba Wizara ya Afya mmeshindwa kuchukua jukumu lenu la kuwahudumia wazee ingawa mnasema kwamba Sera ya Wazee ni kuwahudumia bure kitu ambacho mnawadanganya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Sera ya Afya. Ukisoma hotuba ya Waziri katika kata 3,990 kwa Tanzania nzima kata 484 ndizo ambazo zina vituo vya afya. Huu ni utani mnaoufanya kwa Watanzania wetu kwa sababu haiwezekani kuna *difference* ya kata 3,506 hazina vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye sera hii ya afya inasema vijiji kuwa na zahanati katika vijiji. Tuna vijiji zaidi ya 12,245, ukisoma kitabu cha Waziri wanasema tuna zahanati kwenye vijiji 4,502 tuna *difference* ya vijiji 8,043 hatuna zahanati na moja ikiwa ni Wilaya ya Mpanda pamoja na vijiji na kata zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la afya ni kwamba tukidumisha afya za wananchi wataweza kufanya kazi, watajenga uchumi wao lakini siyo kuendelea kutupa porojo hizi ambazo mnatupa kila siku. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Katavi imekuwa ni wimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisoma kitabu cha bajeti hapa mmesema kwamba mmetenga shilingi bilioni 1.8 lakini ni *second time*, mara ya kwanza Serikali ilitenga pesa wajanja wakapiga ile pesa wakaila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni Serikali gani ambayo haipo *serious* zinatengwa pesa kwa ajili ya wananchi kujengewa hospitali yao lakini watu wachache wanachukua pesa wanakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui kama hizi pesa zipo *theoretically* au mnaingia sasa kwenye utekelezaji kwa ajili ya kuwajengea Hospitali ya Mkoa wananchi wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe masikitiko yangu na hii inawezekana tukaendelea kupiga kelele kumbe Serikali ya Chama cha Mapinduzi sasa imelemewa na mzigo. Ni Serikali gani ambayo kila kitu ninyi mna-set kwamba ni *priorities* kwenu? Afya, elimu, katiba, viwanda yaani kila kitu, lakini hatuoni utekelezaji. Mna *documents* nyingi sana mmeandika, ni *theoretically*! Sasa ingewezekana basi ingekuwa vizuri mka-set kitu kimoja baada ya kingine, kwamba tunaweka afya na mipango yetu ni moja, mbili, tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ajitahidi basi akatembelee hata Zimbabwe; kuna hospitali inaitwa Palalanyatu, ni hospitali iko Harare pale, ni kama Muhimbili. Huwezi kukuta hata takataka, huwezi kukuta inzi, lakini leo wanapoka magazeti, media, wanasema Muhimbili ina vitanda, huduma zimeboreshwa. Ni uongo na unafiki mtupu! Wakatembelee waangalie Zimbabwe wanafanya nini? Wakaangalie wenzao wanafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, labda niseme, kutokana na upungufu wa vitendea kazi kwenye hospitali zetu hasa Mkoa wa Katavi, maana imefikia kipindi sasa hata wauguzi wetu ni wachache katika zahanati zetu katika hospitali. Nitoe masikitiko yangu kwamba wiki moja iliyopita nilipigiwa simu na ma-nurse kwamba vifaa baadhi ya hospitali vipo lakini wauguzi wetu hawana ule ujuzi wa kuweza kutumia vile vifaa. Sasa unashangaa vifaa vipo lakini mama mjamzito anapelekwa wadini ma-nurse wanashindwa kutumia vifaa vile. Wanakwambia tumtangelize mama wadini wakati tunamsubiri Daktari ili kuja kumtibu huyo mgonjwa. Sasa ni vitu ambavyo vinatia hasira. Kama mko *serious*... (Makofi)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Tunaendelea, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex na Mheshimiwa Hawa Ghasia ajiandae.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa neno la ahsante na vilevile sitafanya vizuri kama sitawashukuru Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunichagua kuwa Mjumbe wa NEC. Nataka niwaambie, siendi kufuata riziki, naenda kuwatetea ninyi wana-

CCM wenzangu, hakuna kukatwa Mbunge wa aina yeyote. Niko tayari kutoa chozi la mwisho kwa ajili ya ninyi Wabunge kuwatetea kule. Tulikuwa tunafanywa kama wanyonge lakini nataka niwaahidi, siendi kwa ajili ya biashara, naenda kwa ajili ya kuwatetea ninyi ndugu zangu Wabunge, Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nianze kuwashukuru wapiga kura wangu kwa kuniamini. Pamoja na kwamba nilikuwa nafanya kazi katika mazingira magumu, nilikuwa naumwa lakini waliniamini na leo hii nimekuwa mwakilishi wao tena, naomba Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kwa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Naibu Waziri wake pamoja na Naibu Waziri wa TAMISEMI. Nawashukuru sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. Usiposhukuru kwa kidogo, hata kikubwa ukipewa hutashukuru. Nawashukuru kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na Wizara yake wameweza kuja kwenye Jimbo la Mkoa wa Tanga mara chungu nzima na kujua kero za wananchi na wakaamua kuzifanyia ufumbuzi wake. Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niwashukuru sana viongozi wa Wizara ya Afya; bila ninyi Wizara ya Afya, leo hii hapa ndani ya Bunge hili asingekuwepo Stephen Ngonyani, mlinitetea sana, mkanipeleka India na leo nimerudi. Pamoja na kwamba naumwa, lakini Wizara ya Afya ni Wizara mama sana, inatakiwa tuiangalie kwa macho yote. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo vinatakiwa viangaliwe kwa macho yote ni Wizara ya Afya. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu Wizara ya Afya, hata kama utakuwa unafanya kazi ya aina yoyote, bila kuwa na afya njema hakuna chochote cha maana ambacho utaweza kufanikiwa nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza Serikali, zile hospitali za Mtwara, Tarime na Dar es Salaam ambazo hazijakwisha, kwanza itengwe pesa ili Serikali ihakikishe zile zahanati au vituo vya afya au hospitali zinakwisha, kwa sababu tutaendelea kujenga hospitali nyingi lakini ziko ambazo wananchi wenyewe waliamua kuzianzisha, lakini hospitali hizo zimefika ukingoni, hazipati msaada wa aina yoyote, hasa kule kwa ndugu yangu Mheshimiwa Matiko, naomba ziangaliwe sana ni vitu muhimu sana hivyo. *(Makofi)*

Ndugu zangu, kumekuwa kuna mchezo hapa, ambapo mtu akishaanza kuchangia anataka kujifananisha na Waganga wa Kienyeji. *Why! (Makofi)*

MBUNGE FULANI: Waambie! *(Makofi)*

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za nyuma hapa nataka niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, hakukuwa na hospitali hata moja; mlikuwa mnatumia tiba asili, tiba mbadala. Leo hii kila atakayefanya makosa; jana Askari Polisi, hapa Askari wa Magereza na Askari wa Jeshi mmewafananisha kwamba wakikosa kazi watakuwa Waganga wa Kienyeji. Hii ni biashara kweli mnafanya hapa? Ndicho kilichowaleta kuchangia! jaribuni kubadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganga wa Kienyeji ni fani kama fani nyingine. Msiwaweke Waganga kama ni watu dhaifu sana. Niliyeko hapa nina hospitali Nairobi. Hulazimishwi kumtibu mtu. Mtu anakuja kwa kupenda kwake. Ninyi mnakuja kututolea mifano hapa! Wakati wa uchaguzi mpo milangoni kwetu! Inakuaje? Wakati wa uchaguzi mko milangoni kwetu, leo hapa mnakuwa ndio watu wa kuwatolea mifano Waganga wa Kienyeji, kwa nini! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msiwadharau watu ambao usiku mko majumbani kwao. Nashangaa! Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Tiba Asili, Tiba Mbadala Tanzania. Hatuwezi kukaa hata siku moja tukaja kusema ni namna gani tunaweza kutatua tatizo la tiba asili, tiba mbadala! Badala ya kutaja kwamba hospitali zenu zinakosa dawa, ninyi mnaona fani kutaja Waganga wa Kienyeji. Inawasaidia? Hivi ninyi hakuna aliyekwenda kutibiwa hapa! Msiseme haya mambo ya kininii hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuanzia leo, msitufananishe. Mkichangia, changieni hoja zenu. Msiwafananishe watu ambao usiku mko majumbani kwao mnakwenda kutibiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yamepita jamani, yamepita. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina hospitali nyingi sana ambazo zinahitaji zipatiwe upembuzi na tiba. Leo hii kuna matatizo ambayo yanakwenda katika mahospitali. Kuna hospitali nyingi Madaktari wenyewe wanafanya kazi katika mazingira magumu, lakini kuna watu ambao sio Madaktari, wakifika pale wanaharibu kabisa taaluma ya Madaktari wetu.

MWENYEKITI: Kwa uzoefu unaonyesha eeh!

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa atuambie kuhusu wale watu ambao wanavaa nguo za manjano ambao sio Madaktari, lakini wanajifanya ni Madaktari, wanachukua pesa za wapiga kura, pesa za walalahoi halafu dawa hawapati, matokeo yake fani yote ya Madaktari wanapewa majina mabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwepo Muhimbili, nilitibiwa vizuri na Madaktari mabingwa wa pale, lakini kuna watu wamevaa vinguo vya manjano eti wasaidizi wa Madaktari ukifika pale wanakupokea wao, hao watu waandikeni namba kwenye mashati yao ili tuwajue. Mkifanya namna hii mtafanikiwa sana na hamtakuwa mnapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ndugu zangu tusiendeleo tu kuangalia, mwangalie dawa. Dawa ni kitu muhimu sana kwa Watanzania. Leo hii hospitali nyingi hazina dawa na tatizo ni kwamba siyo ninyi, huko nyuma watu walikuwa wanapeana uongozi. Huo uongozi walivyokuwa wanapeana, imefika mahali mtu anakwenda kuchukua dawa feki ilimradi hela zinaingia mfukoni mwake halafu tunakuwa hatupati chochote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja aangalie kabisa; anapasua majipu, amepasua majipu vizuri sana, lakini aangalie watu wengine, wanunuzi wa madawa hawa; wanunua dawa zinakwenda wapi? Dawa zinaonekana zimetoka MSD zimekwenda mikoani, mikoani hazijafika, ziko kwa akina nani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona niyaseme hayo, lakini naomba kitu kingine. Hospitali yangu ya Korogwe ni hospitali kubwa sana, ina mikoa karibuni mitatu, Mkoa wa Pwani, Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Kilimanjaro. Kila ajali inayopatikana barabara kubwa wagonjwa wote wanaingia pale Magunga Hospitali, lakini inatengwa sana hii hospitali. Ni kwa sababu gani? Kama Tumbi imekuwa hospitali teule, kwa nini Korogwe isiwe hospitali teule na kila kigezo kiko tayari? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mtu angalie na sisi watu wa Tanga; Mheshimiwa Waziri anatoka Tanga. Yeye anafanya mambo makubwa sana kwenye mikoa mingine, hata Mkoa wake! Amekuja kwangu mara tatu na amefanya kazi kubwa, ametoa madawa, ametoa mashuka hebu apandishe hadhi. Mheshimiwa Simbachawene yupo. Nilikuwa niombe hilo na kwa sababu ana Makamu wake makini na anafanya kazi kwa kujitolea sana, hebu fanyeni kazi mhakikishe kwamba Tanzania hii kwanza mwongezewe pesa, mlizotengewa hapa ni ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufatana na mazingira ya sasa, miaka ya nyuma watu walikuwa milioni 12 wakaja kuwa milioni 25 sasa hivi ni milioni 48, milioni 48 kwa mabilioni haya mnayoyatenga, watu watatosheka kiasi gani? Hebu tubadilike! Kama kweli tunataka kuisaidia hii Wizara ya Afya, bajeti hiyo ni ndogo, iongezwe ili dawa ziende na mashuka yaende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta hospitali nzuri haina vitanda, haina shuka, haina Madaktari. Madaktari pia ni watu wa kutakiwa waonekane sana.

Wengine mnafika mnawatukana Madaktari. Mnawatukana kwa lipi, wakati mgonjwa umekuja pale, umemkuta Daktari ana mgonjwa mwingine; unataka atolewe mgonjwa mwingine aingizwe babu yako eti kwa sababu ni ndugu yake na Maji Marefu. Naomba hili tatizo Mheshimiwa Waziri aliangalie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Fedha yupo hapa, hebu bwana mipango rafiki yangu, ongezeni pesa pale. Mnasema kilimo, maji, umeme, lakini hakutakuwa na umeme bila kuwa na afya; hakutakuwa na elimu nzuri bila kuwa na afya; hebu tuyamalize haya. Tukiyamaliza haya, mambo mengine yote yatakuja. Tufanye vitu vichache ambavyo vitasaidia, watu wataviona kwamba, vimekamilika kuliko... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Lete hayo majina ya wanaokutembelea usiku, nitayatunza. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel ajiandae.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naomba nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kuendesha zoezi zima la uchangiaji wa damu. Katika ukurasa wa 57 wa kitabu cha hotuba ya Waziri imeonesha ni kwa jinsi gani Tanzania inahitaji damu salama kwa ajili ya wanawake wanaojifungua, lakini siyo tu wanawake wanaojifungua, pia na watu wote wanaokuwa na uhitaji wa damu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya hii Wizara, Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara kwa hotuba nzuri ambayo wameiandaa na kuiwasilisha hapa, lakini pia kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la bajeti la Wizara hii. Kutokana na maelezo ya hotuba hii inaonesha kwamba, mpaka kufikia Machi mwaka huu ni asilimia 31 ambayo tayari Wizara hii ilikuwa imeshapelekewa. Pia kwa upande wa mishahara, inaonesha kwamba ni 4.1 billion ambayo ilikuwa imeshapelekwa kufikia mwezi Machi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja atoe ufafanuzi kwamba hii mishahara kama imetolewa asilimia ndogo hivi, amesema kwamba ni asilimia 37, hawa wafanyakazi ni kwamba wanakopwa ama hawapo labda walipunguzwa ama labda bajeti ya fungu la mishahara lilikuwa kubwa ukilinganisha na wafanyakazi waliopo? Kwa hiyo, naomba ufafanuzi katika eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie suala la huduma ya saratani. Naipongeza Wizara kwa mipango yake mizuri kwa mwaka ujao wa fedha. Naomba niishauri Serikali kwamba huduma hii ni muhimu sana, lakini katika hii hotuba tunaona kwamba, kipaumbele kimepewa kwa Hospitali moja ya Ocean Road.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhalisia wa nchi yetu ya Tanzania ni kwamba, watu wengi ambao wanatoka pembezoni, hawana uwezo. Kwa hiyo, utakuta mtu anafariki kwa kukosa tu ile nauli ya kumtoa huko mahali alipo na kumpeleka Dar es Salaam kupata hii huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anapokuwa mgonjwa anahitaji mtu wa kumsaidia, kwa hiyo, hapo inabidi mtu atafute nauli yake yeye mwenyewe mgonjwa na nauli ya mtu ya kwenda kumsaidia kule Dar es Salaam anapokwenda kupatiwa huduma hii. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwamba hii huduma iboreshwe katika maeneo yote ya Tanzania ili watu wasiwe wanakufa kwa kukosa hata nauli ya kuwafikisha hospitali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niishukuru Serikali kwa ajili ya lotion kwa ajili ya watu wenye *albinism*. Huduma hii inapatikana KCMC. Naiomba Serikali ifanye mikakati ya kuwezesha upatikanaji wa lotion hizi kwa sababu imekuwa ikipatikana kikanda. Kuna baadhi ya maeneo lotion hizi hazifiki. Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali kuhakikisha kwamba huduma hii inapatikana *all over the country*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie pia huduma ya Mifuko ya Bima ya Afya. Sijui nitumie lugha gani rahisi, lakini niseme tu kwamba, Mifuko hii inabagua baadhi ya huduma, yaani baadhi ya gharama. Utakuta mtu ndiyo ameshamwona Daktari vizuri, anapokwenda kuchukua dawa, anaambiwa kwamba hii dawa haigharamiwi na Mfuko huu; ama kuna hili suala zima la vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu. Mifuko hii haigharamii vifaa saidizi kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi nikailaumu mifuko hii, nadhani ni zile sera na sheria ambazo zipo. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie ni jinsi gani ya kubadilisha hizi sera na sheria ambazo zinatekelezwa na Mifuko hii ambayo inasababisha baadhi ya huduma kushindwa kutolewa na Mifuko hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niongelee suala zima la wazee. Kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, imeongelea huduma bure kwa wazee. Tunaishukuru Serikali kwa huu mpango na huduma hii ambayo inaendelea, lakini naiomba Serikali iboreshe sana huduma hii, kwa sababu kuna kilio kikubwa cha wazee kwamba wanapofika pale hospitali, kuna baadhi ya huduma ambazo ni nyingi ikiwemo dawa, baadhi ya vipimo kwamba havipatikani kwa sababu tu kwamba, huduma ile inakuwa haipatikani mahali pale. Kwa hiyo, naiomba Serikali iboreshe na iangalie kwa jicho la pekee huduma bure kwa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba niongelee suala zima la ukatili wa kijinsia. Katika ukurasa wa 89 wa hii hotuba inaelezea takwimu zilizopo, kwa kweli zinasikitisha. Naomba nitumie Bunge lako Tukufu kulaani vitendo vya ukatili kwa watoto pamoja na wanawake. Matukio ni mengi ambayo yameendelea kuripotiwa ya watoto kubakwa, kulawitiwa, lakini pia vipigo ambavyo vinawasababishia watoto hawa na wanawake ulemavu wa maisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema namalizia, lakini bado *points* mbili. Pia naomba Serikali iangalie suala zima la Bima ya Afya kwa watu wenye ulemavu. Kuna msemaji ambaye ametoka kuongea hapa, alikuwa ameshanifilisi lakini naomba nami nitilie mkazo. Kundi hili kiukweli linahitaji Bima ya Afya. Ukiangalia ni kwamba hata mlo wa siku moja inakuwa ni tatizo. Kwa sababu katika kitabu hiki inaonesha kwamba Serikali itahamasisha watu wenye uwezo wa kuchangia Mifuko hii waweze kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia mtu mwenye ulemavu, anakuwa hana uwezo hata kupata mlo mmoja kwa siku. Kwa hiyo, naiomba Serikali huduma hii ipatikane bure kwa kundi hili la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Hawa Ghasia, atafuatiwa Mheshimiwa Amina Saleh Mollel na Mheshimiwa Deo Sanga ajiandae.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia. Kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya na uzima wa kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuweza kuichangia hotuba ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Ndani ya

muda mfupi wameweza kutembelea mikoa mbalimbali na kuweza kutoa maelekezo mbalimbali, hali ambayo pia inawatia moyo hata watendaji wanaofanya kazi katika Sekta hii ya Afya. Hongereni sana na mwendelee kuchapa kazi hivyo hivyo na msimwangu she Mheshimiwa Rais. Nyie ni vijana na tunawategemea, mna nguvu pia mnao uwezo mkubwa sana, endeleeni kuchapa kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika maeneo makuu matatu. Kwanza, namwomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, maeneo makuu matatu ambayo ni changamoto sana katika Sekta ya Afya; kwanza ni upatikanaji wa madawa na vifaa tiba; pili, ni suala la miundombinu ya kutolea huduma; na tatu, ni uchache wa watumishi katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upatikanaji wa madawa na vifaa tiba ni imani yangu kwamba Wizara ikidhamiria, ikiweka fedha za kutosha, ni suala ambalo linaweza likatatuliwa hata ndani ya miezi sita. Ni suala la dhamira tu, Serikali ikiamua inaweza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija katika suala la miundombinu, sasa hivi pamoja na juhudi zote zinazofanyika, lakini katika baadhi ya maeneo, miundombinu iliyopo kwa kweli imechoka na pia imeelemewa kutokana na idadi ya watu inayoongezeka kila siku, mfano mzuri ni Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa wanaoiamini hospitali ile kuliko hospitali nyingine zote katika nchi yetu. Ukienda pale, idadi ya wagonjwa ukilinganisha na idadi ya wodi pamoja na vitanda kwa kweli inatia huruma. Unawahurumia hata Wauguzi na Madaktari. Wagonjwa wanalala chini kwa sababu wodi ni chache, hata ukiongeza vitanda hakuna eneo ambalo unaweza ukaweka. Ifike wakati sasa suala la ujenzi wa hospitali ya Mlonganzila kwa kweli lipewe kipaumbele kikubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tunazo hospitali zetu za Kanda zipewe uwezo kwa maana ya Watendaji na vifaa ili ziweze kusaidia Muhimbili kupunguza mlundikano. Kwa upande wa kusini, Mikoa ya Mtwara na Lindi, tunayo Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini ambayo inajengwa pale Mikindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika Bajeti yako Mheshimiwa Waziri, sijaona eneo lolote. Nimeangalia kwenye bajeti ya maendeleo, nimeona Hospitali ya Rufaa Mtwara shilingi bilioni mbili. Sasa sijui zile shilingi bilioni zinakwenda Ligula au zinakwenda Mikindani! Kwa sababu kama ni Mikindani, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini, shilingi bilioni mbili kwa kweli hazitoshi, kwa sababu mpaka sasa hivi kilichojengwa pale ni majengo ya wagonjwa wa nje. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka kweli tuisaidie Muhimbili ni lazima tuhakikishe zile Hospitali za Rufaa za Kanda zinajengwa na zinawezeshwa. Sasa hivi mgonjwa yeyote pale Ligula akishindikana, inabidi asafirishwe kwenda Muhimbili. Wakati mwingine Mheshimiwa unalazimika kama Mbunge kununua viti sita kwenye ndege ili mgonjwa mmoja tu aweze kusafirishwa. Afadhali ikiwa ATC, shilingi milioni unaweza ukasafirisha mgonjwa, lakini ukija kwenye *Precision*, mpaka shilingi milioni 15 kusafirisha mgonjwa mmoja. Kwa kweli kwa wale ambao hawana uwezo hawawezi; na wakati mwingine hata Mbunge huwezi kutoa shilingi milioni 15 kusafirisha mgonjwa mmoja. Tunaomba hospitali ile ijengwe na iweze kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwa upande wa watumishi, tuna vituo vya kutolea huduma zaidi ya 7,249 ukichanganya na sekta binafsi, lakini na mahitaji ya watumishi kwa upande wa Wauguzi ni zaidi ya 46,000 na waliopo ni kama 24,000. Tuna upungufu wa zaidi ya asilimia 49 ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika udahili wa watumishi wetu; nilikuwa naangalia, unakuta Madaktari kwa mwaka wanadahiliwa 1,670 wakati tuna upungufu wa Madaktari zaidi ya 4,000. Kwa upande wa Wauguzi, tuna upungufu wa Wauguzi zaidi ya 22,000, lakini wanaodahiliwa kwa mwaka ni kama 3,499. Hivi kweli tunaweza tukaondoa tatizo hili? Tulikuwa na tatizo la Wahasibu na tatizo la Walimu, Wizara mama zilikuwa zinatenga kiasi cha kutosha ili kuweza kuondoa matatizo haya. Sasa hivi tatizo la Walimu na Wahasibu ni kama limekwisha lakini kwa upande wa Sekta ya Afya, nawaomba wadogo zangu, Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Kigwangalla ni lazima tuje na mpango mahsusi, tupanue vyuo vyetu vya Wauguzi, Madaktari na kada zote za Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima tuwalipie. Serikali itenge pesa kama ambavyo Wizara ya Fedha ilikuwa inatenga pesa kwa ajili ya Wahasibu; kama ambavyo Wizara ya Elimu na Wizara ya Kilimo zilikuwa zinatenga pesa kwa ajili ya kusomesha watumishi wao. Ni lazima Wizara ya Afya tufanye kama *operation*. Tunasema anayekwenda kuchukua *degree* ya Uuguzi atachukua mkopo, lakini wanaokwenda kuchukua Cheti, Diploma tunasema ajitegemee mwenyewe. Karo yenyewe ni zaidi ya shilingi milioni moja. Chakula kinazidi hata hiyo shilingi milioni moja. Kwa kweli kama tunataka kuondokana na upungufu huo, nimwombe Mheshimiwa Waziri, ni lazima tuwe na mpango mahsusi na tuwekee kipaumbele, tutenge pesa za kutosha kuhakikisha tunadahili vijana wa kutosha hasa wale ambao tunawahitaji kule vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani kwa sisi tunaoishi vijijini, unakuta zahanati moja ina mtumishi mmoja, kule Muuguzi anafanya kazi masaa 24, hana Jumamosi, hana Jumapili; kukiwa na mgonjwa saa 5.00 za usiku anakwenda kuamshwa na sidhani kama kuna chochote wanachokipata. Ndiyo maana

unakuta Wauguzi wetu wakati mwingine wanakuwa na lugha zisizostahili. Siyo kwamba wanapenda, ni uchovu wa kazi. Mzigo ni mkubwa wanaoufanya. Kwa hiyo, mtu mmoja halali, usiku kucha anaitwa kazini, asubuhi yuko kazini, Jumamosi yuko kazini, hivi unategemea awe na lugha nzuri? Wakati mwingine ni *stress* tu kutokana na uzito wa kazi ndiyo unaowafikisha wanakuwa na lugha wengine zisizostahili.

Kwa hiyo, kwa kweli lazima tuongeze udahili, hizi tunazosema kila kijiji kiwe na zahanati, kila kata iwe na kituo cha afya; bila kwenda sambamba na udahili, hizo zahanati na vituo vya afya zitakuwa ni nyumba tu za popo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka nichangie, nirudi katika Mkoa wangu. Tunacho Kituo cha Afya cha Nanguruwe ambacho tulikiombea kuwa Hospitali ya Wilaya. Tumekamilisha karibu mahitaji yote yanayotakiwa. Tunayo majengo ya upasuaji, tunavyo vitanda vya kutosha, wodi za kutosha pamoja na Kituo cha Afya cha Nanyumbu; lakini mpaka sasa hivi bado tunasubiri kibali kutoka Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ummy alikwenda kutembelea Kituo cha Afya cha Nanguruwe, nina imani kabisa kwamba yeye mwenyewe amejiridhisha kwamba vipo vifaa vya kutosha na majengo ya kutosha. Tunaomba watoe kibali ili ianze kufanya kazi kama Hospitali ya Wilaya, tupunguzie mzigo hospitali ya Mkoa ya Ligula. Hii ikienda sambamba na hospitali au Kituo cha Afya cha Nanyumbu ambacho nacho kwa muda mrefu kimeshafikia mahitaji ambayo yanatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mtwara Vijijini tunavyo vituo vya afya vya Mahurunga na Kitere. Tumeshajenga vyumba vya upasuaji; vifaa vyote vipo kwa zaidi ya miaka miwili, lakini hakuna huduma inayotolewa pale, tatizo ni lile lile la uchache wa Madaktari. Nakuomba Mheshimiwa Waziri utuletee Madaktari wa kutosha ili vituo vile vianze kutoa huduma ya upasuaji na tuweze kupunguza vifo vya akinamama na watoto hasa wakati wa kujifungua. Pia Mheshimiwa Waziri, wakati unaoandaa hao Madaktari, tunao Madaktari pale Hospitali ya Mkoa ya Ligula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo tatizo katika Wilaya yetu na hata kwa mkoa wetu suala la Mabusha. Kwa vile katika vituo vile huduma zote zipo, vifaa vyote vipo, kwa nini hao Madaktari wasiwe wanapanga siku angalau kwa wiki au kwa mwezi wanakwenda katika Vituo vya Afya vile ambavyo vina huduma za upasuaji, wakawa wanatoa huduma ile kwa wale ambao wanahitaji kufanyiwa *operation* za mabusha? Kwa sababu sasa hivi wanalazimika kuja katika Hospitali ya Mkoa, tunawagharamia, anafika pale anakaa zaidi ya wiki mbili anasubiri zamu. Mara leo sijui tunafanyia wawili, kesho tunawafanyia

watatu; kwa nini wale Madaktari walioko katika mkoa wasiwe wanazunguka na wanakwenda katika maeneo hayo kutoa huduma? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake ni suala la uzazi wa mpango. Nimeangalia katika kitabu cha hotuba haraka haraka, sikuona eneo lolote lililozungumzia suala la uzazi wa mpango. Suala la idadi ya watu na uchumi wa nchi yetu ni muhimu sana. Maeneo mengine kama Wabunge tukienda kule wanatuambia bwana hizi huduma hatuzipati na wanazihitaji. Unakuta kule akinamama wengine tayari ana watoto 10 na uzazi wake ni wa matatizo, ni lazima ajifungulie katika hospitali ya Mkoa. Kwanini wasishauriwe uzazi wa mpango sahihi kwa ajili ya kuwawezesha na wenyewe kuboresha afya zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wanapoteza maisha kwasababu tu kila baada ya mwaka mmoja ana mtoto au unakuta mtu tayari ameshajifungua kwa zaidi ya mara nane hali ambayo ni kihatarishi cha maisha yake kwa sababu kwa kweli baada ya kuzaa kwa zaidi ya mara nane, nadhani Mheshimiwa Kigwangalla, Naibu Waziri wa Afya ananielewa, ni kwamba kila kizazi kinachoongezeka pale ni hatari kwa maisha ya mama yule anayejifungua na hata mtoto anayejifungua. Ukiangalia vifo vingi vinavyotokana na uzazi ni aidha ni vya wale waliojifungua katika umri mdogo au kwenye umri uliopitiliza umri ule ambao kwa kweli mtu anaweza akajifungua salama. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusesitiza suala la Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini. Mheshimiwa Waziri akapokuja tungependa kusikia bajeti yake imetengwa wapi. Kama tunataka kupunguza vifo vya akinamama na watoto, tuangalie suala zima la magari ya wagonjwa. Siku za nyuma tulikuwa na magari ya wagonjwa, yana *radio call* ndani yake, kukiwa na tatizo wanaweza kuwasiliana kwa *radio call* na gari lolote lililoko karibu na eneo ambalo mgonjwa yupo linaweza likienda kumchukua kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwa Mheshimiwa Waziri kwamba sasa hivi tuwe na magari ya wagonjwa ambayo pia ni *surgical*. Mgonjwa anapofuatwa, basi afuatwe na Daktari na akifika siyo kwenda kumchukua na kumkimbiza zaidi ya kilometa mia moja Makao Makuu ya Wilaya au ya Mkoa kwa ajili ya upasuaji. Gari ikifika, aweze kufanyiwa upasuaji kule kule inakomkuta badala ya kuanza kukimbizana naye. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kujua hilo, kama tunao mpango wa kuwa na magari ya wagonjwa ambapo huduma za upasuaji zinaweza kupatikana humo humo ndani ya magari kama ambavyo nchi nyingine zinafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana, tunaendelea. Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Kiula Allan ajiandae

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii kwa hotuba yake. Nampongeza sana kama mwanamke kwa kazi nzuri anayoifanya na nazidi kumtia moyo kwamba wanawake wote wa Tanzania wanamtegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia suala la afya, tunafahamu kwamba afya ni kila kitu katika maisha ya mwanadamu. Tunapozungumzia afya, tunafahamu kwamba bila ya kuwa na afya huwezi kufanya jambo lolote la kuleta maendeleo. Tunakumbuka kabisa kwamba mojawapo ya mambo yaliyokuwa yakipigiwa kelele ni suala la maradhi na maradhi haya ndiyo maana tunasisitiza sana suala la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Afya na hasa Serikali kwa kuleta Mfuko wa Bima ya Afya. Pamoja na hayo, naomba nizungumzie machache hasa changamoto zilizopo katika Mfuko wa Bima ya Afya ambayo kwa namna moja au nyingine, umekuwa ni kikwazo kwa baadhi ya wanachama wanaokwenda kupata huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na vizingiti kwa maana kwamba katika baadhi ya *card* hizi za Bima wanapokwenda kupata huduma ya afya na hasa kama tunavyosisitiza siku zote, ni vyema kwa mwananchi kujua afya yake. Atakapojua afya yake, anajua kabisa kwamba yeye ana matatizo gani ili aweze kukabiliana nayo mapema ili aweze kupata matibabu mapema. Wanachama wengi wa Mfuko wa Bima ya Afya wanalalamika kwa sababu wanapokwenda kwa ajili ya kufanya *check-up* ya miili yao, wanakataliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakataliwa pamoja na kwamba wao ni wanachama wazuri na wamekuwa wakichangia. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa, atuambie ni kwa nini Mfuko wa Bima ya Afya umekuwa ukiwakatalia wanachama kuangalia afya zao ili waweze kujua na pengine kuchukua hatua mapema kutokana na matatizo wanayoyapata? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la dawa pia; kama Mfuko wa Bima ya Afya wamekubali kubeba dhamana ya Watanzania, kwa nini wazuie baadhi ya dawa wasizitoe wakati wanachama wote wanaotibiwa wanachangia Mfuko

huo? Namwomba Mheshimiwa Waziri na naishauri Serikali na Waziri, atakapokuja kuhitimisha, atueleze ni kwa nini Mfuko huu wa Bima ya Afya umekuwa na hivyo vikwazo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwa Madaktari. Madaktari pesa waliyopangiwa na huo mfuko wa afya kama *consultant fees* wanalipwa sh. 2,000/=. Hivi kwa wakati huu tuliopo na Madaktari hawa ambao ni wataalam wetu, tunawategemea, mabingwa, hivi kweli unakwenda kumlipa sh. 2,000/=! Ni aibu kwa Mfuko wa Bima ya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia Mfuko wa Bima ya Afya, naomba moja kwa moja niende katika masuala ya watu wenye ulemavu. Nawapongeza Wabunge wote ambao wamezungumzia suala la watu wenye ulemavu na hasa katika Mfuko wa Bima ya Afya na kuona umuhimu wa wao Serikali kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu kupata card za Bima ya afya ili waweze kutibiwa. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nawaomba pia Wabunge wengine katika Majimbo yao waone umuhimu wa kuwachangia hawa watu wenye ulemavu ili basi wanapokwenda hospitali wasipate tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la vifaa saidizi. Tunafahamu kabisa ulemavu siyo kulemaa; na katika ulemavu unapomsaidia mtu mwenye ulemavu vifaa saidizi kwa wale wanaovitumia, tayari umepunguza vikwazo. Isipokuwa katika Bima ya Afya wanapokwenda, bado halipo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri alione hili kwamba ni muhimu na aone ni kwa jinsi gani atawasaidia watu wenye ulemavu ili waweze kupata vifaa saidizi na kuweza kutimiza majukumu yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba nizungumzie katika hospitali zetu na hasa wanawake wenye ulemavu wanapokwenda kujifungua. Vitanda siyo rafiki; na wakati mwingine hata Madaktari wenyewe au Manesi kwa namna moja au nyingine kauli zao siyo nzuri. Wanapowaona watu wenye ulemavu na hasa mwanamke amekwenda ni mjamzito, maneno ya dhihaka yanakuwepo mengi. Hivi katika suala la mama kumleta mtoto, hata kama mtu ni mlemavu hana ule uhitaji? Kwani wana kasoro gani? Si wanayo maumbile kama wengine? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba, nasimama mbele yao kama mwanamke mwenye ulemavu na naomba kuwatetea hawa, kuwasilisha kilio chao kwa sababu sio wote ambao wanaweza kufika huku na kuwasilisha kilio chao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia masuala ya watu wenye ulemavu, wana changamoto nyingi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hili pia, aangalie ni kwa namna gani basi tutafanya, kama ni kutoa elimu ili kwa namna moja au nyingine lugha hizi waziangalie, wasiwadhihaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuone umuhimu na hasa nimwombe Mheshimiwa Waziri kuona umuhimu wa kuweka Wakalimani katika hospitali zetu. Wanapokwenda watu wenye ulemavu hasa viziwi, inakuwa ni vigumu kwa wao kuweza kuwasiliana. Lugha inakuwa ni gongana! Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Waziri, wakati mwingine tunapojiri basi tuone umuhimu wa kuajiri hawa watu ambao ni wakalimani wa lugha za alama ili waweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Zahanati ya Nduruma. Zahanati hii ya Nduruma tayari imepandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya. Zahanati hii inahudumia Vijiji vya Marurani, Manyire, Mlangarini na maeneo mengi katika Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Arumeru; lakini mpaka hivi sasa hakuna wataalam na hakuna gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inakuwa ni tatizo kwa hata akinamama wanapokuwa wajawazito kwenda hospitali ya *Mount Meru* inakuwa ni shida, wanajifungulia njiani. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aone umuhimu na hasa Waziri mwenye dhamana kutuletea gari la wagonjwa katika Zahanati ya Nduruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la watoto wa kike kwa sababu mimi ni mdau na vile vile niungane na ndugu yangu Mollel aliyesema kwamba shujaa ni yule anayejali mtoto wa kike. Katika shule zetu nyingi, watoto wa kike kwa mwezi hawaendi shule kati ya siku nne mpaka siku kumi. Naomba tu Mheshimiwa Waziri na nimwombe pia kwa sababu Waziri wa Fedha yuko hapa, aone basi umuhimu wa kupunguza...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naunga hoja mkono. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Allan Kiula.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na wachangiaji wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe

Magufuli, Rais wetu; Waziri Mkuu; Makamu wa Rais; Mawaziri na Waziri mwenye dhamana hii ya afya, pamoja na Naibu na Watendaji wake wote, kwa namna ambavyo wameonesha vizuri mwelekeo wa bajeti hii kwa mwaka wa 2016/2017. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe wakweli. Unajua wakati fulani vijembe hivi! Hivi kweli pale Muhimbili hakuna mabadiliko! Muhimbili ukienda sasa hivi pana mabadiliko makubwa kabisa. Duka la MSD Mheshimiwa Rais alisema litakuwa pale, Waziri mwenye dhamana amesimamia liko pale. Vitu vingine, kuna mabadiliko makubwa! Kwa kweli tuwatie moyo kwa kazi nzuri mnayoifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuna mchangiaji mmoja alizungumzia lugha fulani iliyokuwa inagusa akinamama. Akinamama wametuzaa; kalipuka! Ni mama zetu hawa, wametuzaa, lakini mmoja vile vile siku ya nyuma yake pia naye alidhalilisha akinamama hawa hawa! Alitamka kwamba alipokwenda huko wakapigwa, wakakatiwa shanga zao. Hivi ndiyo vya kuzungumza hapa vitu nyeti kama hivyo? Eeh! Sasa niseme, kama Mwenyekiti wa CCM mwenzangu kwa yule kijana ambaye Mbunge alizungumzia lugha ambayo CCM hatukumtuma, mimi namwomba radhi kama Mwenyekiti. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tuliopo hapa, kila mmoja ana akili; na wakati fulani tuliopo hapa wote ni vichaa, lakini vichaa vinatofautiana. Ukienda upande wa elimu na ndiyo maana sekondari, shule za msingi na kadhalika huwa kunakuwa na shule za watu wenye vipaji maalum. Maana yake hawa wana akili kuwazidi wenzao. Sasa baadhi ya Wabunge hapa walizungumzia habari ya viti kumi ambavyo Mheshimiwa Rais anawateua kwa kazi maalum, kwa vipaji maalum. Ndiyo maana alimteua Mheshimiwa Tulia, Naibu Spika kwa kazi maalum. Kwa hiyo, tusimwingilie Mheshimiwa Rais, kazi ambazo anawateua watu, zile nafasi kumi amemteua Waziri wa Fedha, ameteua na wengine, tusimwingilie nafasi zile kumi. Hata Mheshimiwa Mbatia amewahi kuteuliwa kupitia Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie habari ya Jimbo la Makambako. Nilimwandikia Mheshimiwa Waziri ile ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ndugu zangu, naishukuru Serikali, miaka miwili, mitatu iliyopita mmepandisha hadhi Kituo cha Makambako kuwa hospitali na mmetuletea Madaktari wa kutosha, tunao. Tatizo kubwa nimekuwa nikisema hapa na niliseme tena kwa Mheshimiwa Waziri, tuna jengo la upasuaji, tulichokikosa ni vifaa vya upasuaji. Gari letu la wagonjwa limekuwa likipeleka watu Njombe kila siku, mara saba, mara tano mpaka mara nane. Ni gharama kubwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha na nilimltea, akaniambia Daktari anipe orodha ni vitu gani vidogo vidogo ambavyo vimekosekana. Nilimpa! Atakapohitimisha aniambie wamejipangaje kuona sasa tunapeleka vifaa vya upasuaji pale Makambako ili kuwaokoa akinamama na watoto, gari lisiwe linakimbia kwenda Njombe na I lembula. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo hospitali yetu ya Makambako tuna wodi ya akinamama na watoto. Wodi nzuri iliyojengwa zaidi ya miaka miwili, vimebakia vitu fulani fulani havijakwisha; miaka miwili tume-invest pale hela ya Serikali. Nawaomba Wizara waone uwezekano wa kuona tunamalizia jengo hili ili liweze kufanya kazi iliyokusudiwa. Chonde chonde, ili kuokoa hela ya Serikali ambayo imeendelea kukaa kwenye majengo hayo mawili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kufungua maduka ya MSD katika hospitali zetu za mikoa na wilaya, naomba sana, Mkoa wetu wa Njombe ni mpya. Mkoa huu ndiyo Mkoa ambao sasa una kitega uchumi kikubwa ambacho kitaanzishwa, Liganga na Mchuchuma. Kwa hiyo, naomba sana tuhakikishe tunapeleka Duka la MSD la Madawa pale Mkoani Njombe ili kuwasaidia wananchi wetu wa Wilaya na Mkoa wa Njombe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mji wa Makambako tumejenga zahanati tisa katika vijiji tisa; na karibu zahanati saba tumeshazipaua. Naomba Serikali ione upo umuhimu sasa wa kutenga bajeti ya kumalizia kuwaongezea nguvu wananchi hawa wa Mji wa Makambako. Hili linawezekana na ni kwa nchi nzima. Yako majengo ambayo yamejengwa hayajamalizika, tunaomba Serikali itenge fedha kwa ajili ya kumalizia haya majengo ambayo yalishajengwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuna Kituo cha Afya ambacho kilijengwa katika Kata ya Lyamkena. Kituo hiki cha Afya kina zaidi ya miaka miwili. Kilishapauliwa na kadhalika, bado hakijamaliziwa, kimeendelea kukaa pale. Jengo hili la kituo cha afya, inawezekana kabisa na majimbo mengine vituo vya afya kama cha Makambako, vipo! Tutenge fedha kwa ajili ya kumalizia vituo vya afya ili kazi iliyokusudiwa iweze kwenda vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa kasi anayokwenda nayo ambapo yuko nyuma ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, imani yangu na imani ya Wabunge hawa, atatufikisha salama. Nampongeza sana kwa dhati pamoja na Watendaji wake. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasema, atakapokuwa anahitimisha, basi ni vizuri atueleze kwa ujumla wake ili tuweze kuwa kitu kimoja na CCM ahadi ambazo iliahidi, tunamtegemea yeye kupitia Wizara hii ya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya, nisiwachukulie muda wenzangu, niseme tu naunga mkono hoja ya Waziri wa Afya kwa asilimia mia moja. Nawashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea. Naanza utaratibu mpya; Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa Kuchauka Zuberi.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kukupa shukrani kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu jioni ya leo. Nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake kwa *reforms* ambazo zinaendelea katika Sekta ya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza Mbunge aliyepita hapa kwamba ukienda Muhimbili unaona mabadiliko na ziko sehemu nyingi ambapo ukienda unaona mabadiliko; nami nafananisha utendaji kazi wa Rais wetu na Mawaziri hawa kama ile *theory* ya Japan, "*Gemba Kaizen Theory*," ambayo inasema lazima uende kwenye gemba. Lazima uende mahali shughuli zinapofanyika ili uweze kutoa majibu sahihi kwa changamoto sahihi ambazo zinakuwepo...

MBUNGE FULANI: Hatusikii! Hatusikii!

MHE. ALLAN J. KIULA: Ni sababu ya urefu jamani, samahani! Nitakuwa napiga magoti. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba, utendaji kazi wa Waziri na Mawaziri umechukua ile *theory* ya Japan, inaitwa *Gemba Kaizen Theory* ambayo inasema uende kwenye eneo la tukio ili uweze kutatua matatizo. Unaona changamoto, unatatua matatizo hayo. Pia nawapongeza Madaktari na Wauguzi ambao wameendelea kufanya kazi bila kuchoka kwa weledi mkubwa kuokoa maisha ya Watanzania tukitambua kwamba *population* yetu sasa hivi ni zaidi ya milioni 48, hivyo tunahitaji kupata huduma hiyo muhimu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nizungumzie suala la haki ya kupata tiba. Suala la haki ya kupata tiba ni sawa sawa na haki ya kuishi, kwa sababu ukipata tiba ina maana unaendelea na maisha. Sasa nikiwahamisha Bunge hili nilipeleke katika Jimbo langu la Mkalama, tunao wakazi 188,000. Wakazi hao hawana Hospitali ya Wilaya, tunatumia Hospitali ya Mission. Vituo vya Afya vilivyopo ni vitatu, Zahanati zilizopo ni 24. *Facilities* hizo ndizo zinatoa huduma kwa idadi hiyo ya wakaazi. Wakaazi hao wako kwenye *remote area*, yaani maeneo ya pembezoni. Tunaposema maeneo ya pembezoni, maana yake unaondoka kwenye njia kuu za lami unaingia porini, ukiingia porini ndiyo unawakuta hawa wananchi wa Mkalama ambapo wako ndani katika vijiji vinavyofikia 70. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza vifo vya akinamama, watoto na wazee takwimu tunazozisoma humu kwenye vitabu hivi tunavyoandikiwa zinajumuisha vile vifo vinavyorekodiwa kutoka kwenye Hospitali, Zahanati na Vituo vya Afya. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba vipo vifo vingi ambavyo havitolewi taarifa kwa sababu watu wanafariki majumbani. Akinamama wanafariki njiani wakienda kujifungua. Ukiangalia sisi huduma tunategemea Hospitali ya Hydrom kupata matibabu. Ukitoka hapo unaenda Nkhungi, lakini unaenda Singida; na Jimbo lilivyo kubwa huduma hiyo haipatikani kwa urahisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kabisa Wizara iangalie Wilaya hizi mpya na iangalie maeneo ya pembezoni yapate uangalizi wa karibu. Pia kwa kutambua wingi wa watu na Kata; tuna Kata 17; naomba kupitia Wizara hii Zahanati zifuatazo zipandishwe ziwe Vituo vya Afya. Ihuguno, Msiu, Nduguti na Ilunda. Tukipandisha hivyo, tutakuwa na Vituo vya Afya saba. Pia tunalo gari la wagonjwa moja ambapo gari hilo ni chakavu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wasiotambua ni kwamba sisi tumegawanyika kutoka Iramba Magharibi, ndiyo tukapata Iramba Mashariki. Kwa hiyo, tuligawiwa gari moja. Hatuna gari la wagonjwa. Tunalo gari chakavu ambalo halina uwezo tena wa kufanya kazi. Kwa hiyo, namwomba kabisa Waziri anayehusika na Wizara hii na Naibu wake waangalie uwezekano wa kutupatia gari la wagonjwa na gari hilo liwe jipya kwa sababu ya mazingira ya kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia suala la watumishi; tunao Madaktari wawili, watu 188,000 ukigawanya kwa Daktari wawili unapata 94,000; ukigawanya unakuta kwamba kila Daktari anahudumia watu 257 kwa siku katika siku za mwaka ukigawanya. Madaktari hawa watafanyaje kazi kwa utaratibu huo? Nasi kule tunaposema Madaktari, maana yake hata ma- *clinical officer* ni Madaktari. Maana yake hapo wenzetu wanapozungumza Madaktari wanazungumzia Madaktari Bingwa, lakini tunaoishi nao kule ni akina nani? Tuna upungufu wa Madaktari 21, Wauguzi 113 na Maabara 23. Tunaomba ufanyike mpango mahsusi tuweze japo kupunguziwa pengo hilo la wafanyakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali yetu ya Nkhungi ambayo ni ya *Mission* na yenyewe iweze kupelekewa Madaktari Bingwa waweze kuendelea kutoa huduma wakati ambapo tunasubiri mabadiliko zaidi ambayo tunatarajia tutayapata ndani ya miaka mitano hii. Pia ukiangalia sasa hivi kuna magonjwa yasiyoambukiza (*non communicable disease*), sasa kule vijijini watu wanapokuja huku mijini kupata huduma wanakuwa wameshachelewa. *Cancer, fibroid, sukari, BP, Cardiovascular Disease*, magonjwa ya figo, hayo yote ni matatizo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kabisa, uwe unafanyika utaratibu maalum kuwa na *mobile health services* au *Kit Program* za Madaktari; wanapelekwa, wanatembelea wilaya hizo na kuwapima watu na kuwasaidia, hasa akinamama ambao ndiyo waathirika wakubwa. Program hizo zikiwa zinafanyika katika kipindi cha miezi mitatu mitatu, zinaweza kutusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala ambalo limezungumzwa na kila Mbunge hapa linaloitwa CHF. CHF ni tatizo kubwa! Tunasema ni tatizo kubwa kwa sababu tunawahamasisha wananchi wanachanga, wakimaliza kuchanga hawapati matibabu na mwaka ukiisha wanatakiwa wachange tena. Sasa hivi tunatakiwa tuwaambie wananchi wachange na dawa hawakunywa; hiyo ni changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iweze kuangalia jambo hili na kuweka utaratibu mzuri kuhakikisha wananchi wakitoa hizo fedha wapate dawa. Dawa ziwepo wapate na vipimo vinavyohusika, tumeambiwa kwamba dawa zikiwa hazipatikani MSD, kutakuwa na mzabuni kila mkoa. Jambo hilo Mkoa wa Singida halijafanyika na lenyewe liangaliwe ili dawa ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maslahi ya wafanyakazi wa Wizara hii yaangaliwe kwa karibu kwa kuzingatia mazingira magumu. Sisi ambao tuko pembezoni, Madaktari wetu wanafanya kazi masaa 24 kwa siku saba, wanapata kitu gani cha ziada? Siyo hivyo tu, mgawanyo wa Madaktari hao; Madaktari wanaishia mijini. Wakifika Singida, wanageuka, wanarudi walikotoka au wanakwenda kwenye hospitali binafsi. Jambo hilo linatakiwa liangaliwe na Madaktari wafike kule kwa kuweka *incentives* mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matibabu bure kwa wazee na lenyewe liangaliwe. Mheshimiwa Waziri ametoa *circular*, ipo, lakini haijasimamiwa kikamilifu. Bado malalamiko yako kila upande, wazee wetu wanapata tabu, wananyanyaswa. Wilaya ya Mkalama ni wilaya changa, mapato yake ni kidogo sana. Tunapofikia mahali tunasema wilaya ijenge hospitali, hiyo ni changamoto. Tunaomba Wizara itutafutie mfadhili au ichukue hatua za makusudi kuhakikisha kwamba tunapata Hospitali ya Wilaya ili iweze kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, alizungumza Mbunge mmoja suala la mafunzo, naomba Sekta ya Afya, Wizara iangalie namna kwenye Vyuo, wanafunzi hao waweze kupata mikopo, waweze kusoma, kwa ngazi ya cheti, ngazi ya *Diploma* na kwenda mpaka juu. Kwa sababu wakisoma na tukiweka mkakati wa miaka mitano, mpaka itakapokwisha, pengo hili litakuwa limemalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na naomba mambo ambayo tumeyatoa yazingatiwe na hasa sisi ambao tunatoka katika maeneo ya porini. Mimi naita kule ni porini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Nakushuru sana. Kabla hatujaendelea, ngoja ni-break tradition. Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge wote wa kutoka Zanzibar, ni wanafunzi 120, wanasoma Chuo Kikuu chetu cha Dodoma. Wako wapi toka Zanzibar? (Makofi)

Karibuni, sana. Hii ndiyo faida ya Muungano. Someni sana kwa faida ya nchi yetu. Tunaendelea. Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Upendo Peneza na Mheshimiwa Kunti ajiandae.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii jioni ya leo nami nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii ya Afya. Awali ya yote, nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama hapa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kutoa shukrani za dhati kwa wapiga kura wangu, Wanaliwale kwa kunikabidhi jukumu hili la kuwawakilisha na sasa hivi ndiyo hiyo kazi naifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naanza kuwaasa ndugu zangu wa Kambi yetu ya Upinzani. Kambi ya Upinzani ndiyo tuliopewa jukumu la kuishauri Serikali. Serikali hii wanasikia na wanatuelewa. Wenzetu waliobaki kule nyuma, wamepewa kazi ya kushangilia na kupitisha. Sisi ndiyo tunatakiwa tuishauri hii Serikali. Hii Serikali siyo kwamba hawasikii, tatizo la Serikali yetu ni kwamba wako nyuma sana na wakati. Mliwashauri hapa mwaka 2010 kwamba safari za Mheshimiwa Rais hazina tija; Mwaka 2015 wametekeleza; mkawashauri mwaka 2010 kuhusu ufisadi, mwaka 2015 wametekeleza; tatizo ni muda gani wanautumia kuyatekeleza haya tunayowaambia? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzuri wa kusema ni kutazamana, ndiyo maana sisi tumetazamana na Mawaziri, wale wako nyuma, kwa sababu wanajua nini tunaongea. Nataka niwape faida moja; tunapochangia Upinzani na Mawaziri wako busy kuandika, kwa sababu wanajua sasa ndiyo wanashauriwa, kule wanasubiri kushangilia na kupitisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa narudi kwa mabosi wangu, Wanaliwale, naomba niwawakilishe. Wilaya ya Liwale ni Wilaya iliyoasisiwa mwaka 1975 na mwasisi wa Wilaya ile ni Waziri Mkuu wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mzee Rashid Mfaume Kawawa. Nakuja kwenye upande wa hospitali;

sasa bahati mbaya ya wilaya ile, ina vijiji 76, tuna zahanati 30 tu. Wilaya ya Liwale ina kata 20, tuna kituo cha afya kimoja, mfu. Nasema kituo mfu kwa sababu ni mwaka wa tatu huu, vifaa vimekwenda pale vya upasuaji, viko kwenye maboksi mpaka leo. Havijafunguliwa, mchwa wanakula yale maboksi. Nimeyaona haya kwa macho yangu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ya Wilaya ya Liwale ina magari mawili ya wagonjwa; gari moja ndilo ambalo anatumia DMO kama gari la kufanyia kazi na gari moja ndiyo linalotumika kama la kusaidia wagonjwa. Bahati mbaya nyingine ya Wilaya ya Liwale, Mji ule upo; sijui nani anamjua pweza! Barabara zetu ziko mkia wa pweza, kwamba hatuunganishi kutoka kata moja kwenda nyingine, ni mpaka uende urudi, uende urudi. Nakupa mfano wa vijiji vichache vifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka Nahoro kwenda Liwale ni kilomita 135, Napata - Liwale Kilomita 120, Liwale - Lilombe Kilomita 65, Kikulyungu - Liwale Kilomita 120. Hawa wanatembea hizo kilomita 120, kufuata huduma Liwale Mjini. Wakifika Liwale Mjini, hospitali yenyewe ndiyo kama hiyo, takwimu hizo nilizokupa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Liwale kwenye zahanati zetu 30 zinahudumiwa na wale mnaita *one year course*...

MBUNGE FULANI: *Medical attendant.*

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: *Medical attendant* wa *one year course* ndio wanaohudumu kwenye hizi zahanati. Kichekesho, nimekwenda na DMO kwenye baadhi ya zahanati, tumekuta dawa zimeharibika. DMO anasema hizi dawa zimeharibika kwa sababu hawa wahudumu hawazijui. Wanataka *panadol* zilizoandikwa *panadol*. Ukibadilisha boksi siyo *panadol* hiyo. Hili ni tatizo!

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Kuchauka keti kidogo.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mimi naomba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kuchauka!

MBUNGE FULANI: Nimesimama kwa Kanuni ya 68(8) napenda kumpa taarifa mzungumzaji anayeendelea kuchangia, kwamba Waziri Mkuu wa

Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na wala siyo Rashid Kawawa. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zuberi unaikubali taarifa au unaikataa?

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Taarifa yake naikataa, kwa sababu zifuatazo: Waziri Mkuu wa kwanza Tanganyika huru ni Mwalimu Nyerere, lakini Waziri wa Kwanza wa Tanzania ni Mzee Kawawa. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Kawawa ni Waziri Mkuu wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, uwezo wake wa kuifahamu historia haiwezi. (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Endelea!

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Hiyo ni historia fupi tu ameshindwa kuelewa. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Endelea Mheshimiwa na kiti kinakulinda, uko sahihi! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Afya na Naibu Waziri wa Afya, watu wengi wamewasifia na wanaendelea kuwasifia, nami naendelea kuwasifia, lakini nawapa pole. Nawapa pole kwa sababu jukumu mlilondalo ni kubwa, mazingira ya kazi ni magumu, kwa bajeti hii kwa kweli dhamira yenu ni nzuri, nami nataka niwaambie kwamba ili muweze kuonekana angalau mmetekeleza kidogo, mnahitaji kufanya kazi ya ziada. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama takwimu zinavyosema, bajeti ya Serikali imeongezeka kwa triloni sita *point something*, lakini bajeti ya Afya imepungua kwa asilimia 11. Sasa mwone hiyo kazi mliyonayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narejea kule kule Liwale. Liwale sisi tunayo matatizo, sisi tuna upungufu wa *Clinical Officer* 40. Mheshimiwa Waziri atakapokuja naomba anieleweshe, hivi DMO anaruhusiwa kutibia? Anaruhusiwa kuingia ofisini kutibu watu? Maana DMO wangu yeye ni mtawala, hajawahi kuingia ofisini kutibia. Sasa sijaelewa, mimi kwa sababu siyo mtaalam sijaelewa. Hapo mtakapokuja, mtanielewesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, jiografia ya Wilaya ya Liwale kiutendaji kuwa na gari moja la wagonjwa ni tatizo. Gari lile likiondoka, watu

wengine huku nyuma hawana usafiri tena na ni kilomita kama hizo nilizokupa. Liwale hospitali ile, mimi nimeingia haina X-Ray mwaka mmoja uliopita.

Namshukuru Naibu Waziri, nilikwenda ofisini kwake akanisaidia, akanipa njia ya kupata mtaalam, nikampata mtaalam nikapeleka X-Ray ile ikatengenezwa. Kama Waswahili wanavyosema, "Siku ya Kufa Nyani, Miti yote Huteleza." Ile X-Ray sasa hivi ni nzima lakini haina mhudumu. Mpiga picha hatuna, kwa hiyo, tumerudi pale pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Liwale haina *ultrasound*. Mwezi Januari kuna dada mmoja alikwenda pale kwa lengo la kujifungua, wale akinamama wakaenda kumpima, wakampapasa wakamwambia njoo wiki ijayo. Wiki ijayo yule mama hakufika, tumbo likawa la njano wamemrudisha pale yule mama kafa. Hospitali ya Wilaya ya Liwale!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wanamwambia Mheshimiwa Waziri, njoo kwetu, njoo kwetu, mimi sisemi aje Liwale; naomba atusaidie Liwale. Akiona namna ya kuweza kuja, karibu Liwale, aje ajionee haya ninayoyasema. Ile Wilaya imesahauliwa, ni ya siku nyingi, lakini ukienda ukiiangalia utafikiri ni Wilaya ambayo imezinduliwa juzi. Hayo ndiyo matatizo tuliyonayo Wilaya ya Liwale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati napita kuomba kura niliwaambia, sitakubali kuona akinamama wakienda kujifungua wanakwenda kama wameachika; anakwenda na beseni, ndoo, *carpet*; maana hizi *mackintosh* wao hawana, kule wanatumia hizi *carpet* za kawaida. Anakwenda na *carpet*, ndoo, beseni, wembe, kanga, *gloves* na sindano. Nikasema sitalikubali hilo. Kwa kuonesha mfano huo, nimepeleka, *mackintosh* 5,000 mwezi uliopita. Nimeona nianzie hapo, lakini hali yetu ni mbaya, tunaomba msaada wenu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye upande wa MSD. MSD ni tatizo jamani. Nakumbuka siku moja tulikwenda MSD nikiwa kwenye Kamati ya UKIMWI; yule Mkurugenzi alituambia kwamba tatizo la Halmashauri wanatupa *order* haraka. Wanatupa *order* leo, kesho wanataka hela, lakini hii siyo kweli. Sisi Liwale tumepeleka pesa Desemba, shilingi milioni 35. Dawa tulizopata mpaka leo ni za shilingi milioni 20, inaonekana dawa tulizopewa siyo zile tunazozihitaji. Tumepewa dawa zile ambazo MSD wanazo. Mkurugenzi alisema kwamba mkileta pesa, baada ya wiki mbili au wiki tatu mtakuwa mmepata, lakini hii siyo kweli. Huo ndiyo ukweli halisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye CHF. Tarehe 8 Januari, Mkoa wa Lindi ulizindua CHF Kitaifa na mimi mwenyewe nimechangia watu 100 kwenye Jimbo langu, lakini CHF imenitia kitanzi, kwa sababu nimehamasisha Wanaliwale, kabla ya uzinduzi tulikuwa asilimia 10 ya wanajamii wa Liwale, lakini

mpaka namaliza tarehe 30 Aprili, tulikuwa tayari tumefika asilimia 46.4 na nikawaahidi Wanaliwale, kufikia Agosti tukiua ufuta tunataka tusahau masuala ya CHF. Tunataka tuchangie asilimia mia moja. Sasa hiyo imenitia kitanzi. Imenitia kitanzi mimi na Madiwani wangu kwa sababu tuliwaambia, mkienda dirishani mkikosa dawa, njooni kwetu. Sasa vyeti vyote vya dawa vinakuja kwetu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti vyeti vyote vya dawa vinaenda kwa Diwani, vinaenda kwa Mbunge kwa sababu tuliwaahidi mtoe pesa mtapata dawa; dawa hazipo! Tunawaomba Mheshimiwa Waziri, CHF inatutia kitanzi. Nashukuru mwenzangu Mheshimiwa Bobali aliona mbali, akawaambia wasichange kabisa. Sasa mimi nimeji-commit kwamba tunachanga na kweli wananchi kwa sababu wananikubali, nikiwaambia wanatekeleza. Mwezi Agosti Mheshimiwa Waziri alituhidi tutakuwa tumefika asilimia mia moja. Naomba Mheshimiwa Waziri, mnitoe kwenye hiki kitanzi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye hivi mnasema Vituo vya Saratani ya Mlango wa Kizazi. Lindi kuna vituo vinne, Liwale hatuna. Hivi Liwale kuna nini? Jamani, tuoneeni huruma, hata Mzee Kawawa hamumwenzi, simba wa vita! Jamani nawaombeni mtukumbuke na sisi tumo. Kwenye mchango wetu, pato la Taifa tumo! Tunalima korosho kwa wingi, tunalima ufuta kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kwenye masuala ya UKIMWI sasa, nakuja kwenye masuala ya UKIMWI. Takwimu zinaonesha wanaotumia dawa za ARV mpaka mwaka 2015 ni watu 700,000 na inakadiriwa mpaka mwisho wa 2016, wanafika watu 900,000, lakini pesa iliyotengwa ni ya watu 200,000. Maana yake mpaka sasa hivi tunasema watu 500,000 hawana dawa. Hiyo ni takwimu sahihi kabisa zinazohusiana na mambo ya UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Mheshimiwa Waziri hili suala la UKIMWI tulipe kipaumbele. Kama kweli dhamira yetu ni kuwasaidia watu wetu, hili suala la UKIMWI tulipe kipaumbele. Vile vile narudi tena kwenye upande wa MSD. MSD hata hizo dawa chache wanazozileta, kwa jiografia ya Liwale na Mkoa wa Lindi ha... *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Basi.

MHE.ZUBERI M. KUCHAUKA: Nashukuru kwa kunisikiliza.

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea, Mheshimiwa Upendo Peneza, halafu Mheshimiwa Kunti Yusuph na Mheshimiwa George Malima Lubeleje wajiandae.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba tu niseme kwamba, kama Taifa na kama Wabunge, tunahitaji, vita ambayo tunakuwa tumeipigana na ambao wengine wameipigana kabla wengine hatujaingia Bungeni, inapaswa iendele; lile suala la misamaha ya kodi na watu wanaosamehewa kodi kuweza kulipa. Kwa sababu tumechambua hata katika Sekta ya Afya, pesa nyingi haijapelekwa katika Sekta ya Afya, kwa hiyo, tunahitaji kuangalia kila pesa iliko ili tuweze kuhudumia watu wetu wasiweze kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta hii ya Afya tuna Madaktari ambao wanatibu katika maeneo yetu, ambao wengi wamepata elimu kwa ngazi ya Diploma na hawa Madaktari wamekuwa wakisambazwa katika Vituo vya Afya lakini pia vile vile hata katika Hospitali za Wilaya katika maeneo mengi na wamekuwa wakifanya kazi na watu wasio na elimu ya Udaktari kama mimi, siyo rahisi sana kutambua kama ana *degree* ya Udaktari au hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja kwamba hawa watu pamoja na kutuhudumia vizuri na elimu ambayo wameipata kwa miaka mitatu, wakihitajika kwenda kusoma na kupata *degree*, inawalazimu tena kwenda kusoma kwa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iliangelie hili. Mimi sio mtaalamu wa Udaktari, lakini waweze kuangalia ni namna gani wanaweza wakafupisha hii miaka ili angalau, kwa sababu kuna masomo wameshasoma katika kipindi cha Diploma basi wanavyosoma *degree* miaka iweze kupungua. Mfano ni katika elimu ya *engineering* hapa hapa Tanzania, wanafunzi waliomaliza *Diploma* katika vyuo vya *Technical Schools* kama *Arusha Technical*, wanapokwenda kusoma *degree* za *engineering* wanaanzia mwaka wa pili. Kwa hiyo, naiomba Wizara iweze kuliangalia hilo kama angalau tunaweza kuwasaidia hao Madaktari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile hawa wanaosoma *Diploma* kwa jinsia ya kike, inawalazimu wanapomaliza elimu ya *Diploma* kwenda kufanya kazi kwa miaka mitatu ndipo waruhusiwe kwenda kusoma *Degree* kwa miaka mitano. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya alisema ndani ya Bunge hili Tukufu kwamba *menopause* inaanzia miaka 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukipiga mahesabu, kama binti atamaliza *Diploma* kwa miaka mitatu, akafanya kazi kwa muda wa miaka mitatu ndipo akasome hiyo *degree* ya miaka mitano, kwanza ndani ya hiyo miaka mitatu ya kufanya kazi kuna changamoto. Anaweza akaolewa na mambo mengine

hapo katikati yakabadilika. Vile vile anaweza kufikia *menopause* hata hiyo elimu yenyewe ya Udaktari kwa maana ya MD hajaweza kuifikia. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iliangalie hilo na iweze kurekebisha ili watoto wetu wa kike angalau wapunguziwe muda wa kufanya kazi hapo katikati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile natambua juhudi za kuhakikisha kwamba tunaweka usawa wa kijinsia ndani ya Taifa letu. Kumekuwa na juhudi mbalimbali na harakati za wanawake mbalimbali na leo katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri Ummy aliweza kusema na kumshukuru mume wake kipenzi kwa maneno yake, kwa kumsaidia katika utekelezaji wa kazi. Pia nimemsikia Mheshimiwa Mama Mary Nagu, naye anamshukuru anasema mimi Nagu kanisaidia sana! Pia wanawake hapa ndani ya CHADEMA Mheshimiwa Mama Grace Tendega na mama zangu akina Mheshimiwa Susan Lyimo na wenyewe wanawashukuru waume zao kwa kuwasaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba sasa Wizara iangalie umuhimu wa kuwashirikisha wanaume kuweza kuelewa uwezo wa wanawake katika kuwasaidia kuleta usawa wa kijinsia. Hatuwezi tukaifanya hii vita peke yetu, lakini tunahitaji kuwashirikisha wanaume. Kwa hiyo, naiomba Wizara iweze kutoa kama *trainings* kutoka kwa mashirika mbalimbali ili wanaume pia wapatiwe hii elimu wapate kuona nafasi ya mtoto wa kike. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, naomba pia nimshukuru baba yangu mzazi ambaye kwa kupitia kwake, kwa kuona umuhimu wangu kwake, ana watoto watano, wa kiume mmoja na wa kike wanne na aliapa kwamba lazima atengeneze wanawake wanaoweza kujitegemea katika maisha yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kubwa zinazowakabili watoto wetu wa kike. Mheshimiwa Ummy katika Hotuba yake ameweza kutaja kwamba kuna vifo vya wanawake, bado vipo na hii hali inatisha, lakini tunaweza tukatambua kwamba baadhi ya watoto au watu wanaokufa kutokana na hivi vifo ni watu wanaobeba mimba kabla ya kufikia umri halisi wa kuweza kupata mimba. Kuna changamoto za kielimu pia ambazo zinawakabili watoto wetu, ndiyo maana wanashindwa kwenda shule. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, binti anaingia katika kipindi cha hedhi ambapo kama hana vifaa vya kujisitiri (*Sanitary towels*) anashindwa kwenda darasani sawasawa na mtoto wa kiume. Katika *adult level* msichana anaweza kwenda katika kipindi cha hedhi kwa siku nne, *at maximum* siku saba. Sasa binti akikosa darasani siku nne, somo kama ndiyo limeanza leo, baada ya siku nne maana yake hilo somo limekwisha. Kama ni siku saba, hivyo hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue kwamba Serikali imeweka msamaha wa kodi kwenye *sanitary towels*, lakini bado *sanitary towels*

zinapatikana kwa bei ya juu. *Sanitary towels* kwa bei ya chini kabisa Dar es Salaam ni sh. 1,500/=, lakini nyingine ni sh. 2,500/= mpaka bei ya juu zaidi. Sasa hapa suala linalokuja ni kwamba, Serikali itengeneze chombo maalum ambacho. Humu ndani tunapitisha misamaha ya kodi ili iwanufaishe wananchi, lakini mwisho wa siku inakuwa ni manufaa kwa wafanyabiashara na siyo wananchi tuliowalenga hapo mwanzo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali itengeneze chombo maalum cha kuangalia kila bidhaa tuliyoivekea msamaha wa kodi kinasimamia na kuhakikisha bidhaa hiyo inapatikana kwa bei iliyolengwa kwenye soko. Suala hilo pia linagusa mpaka maeneo ya dawa, kwamba dawa zimewekewa misamaha ya kodi, lakini ukienda madukani kwenye *private pharmacies* bei ni kubwa. Kwa hiyo, Serikali iliangalie hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala hilo hilo, tunasema kwamba Wizara hii ya jinsia iweke kipaumbele na kuhakikisha kwamba, sekta nyingine zote zinaangalia jinsia katika utekelezaji wa mambo yake. Katika kilimo, watu wote wanaofanya kilimo 80% ni wanawake. Usipowaangalia wanawake katika kilimo, maana yake ni kwamba kilimo lazima kife. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile katika elimu, ni vizuri sasa Wizara ya Afya kushirikiana na Wizara ya Elimu, ikatenga pesa, kama ni sh. 10,000/= kwa ajili ya Shule za Msingi kila mwanafunzi, basi kwa mtoto wa kike iwe ni sh. 12,000/= ama sh. 13,000/= ili ile sh. 3,000/= iweze kugharimia kwenda kulipia *sanitary towels*. Vile vile katika Vyuo Vikuu mkopo wa Chuo Kikuu uweze pia kugusa kuhakikisha kwamba wa msichana uwe juu zaidi ili kumsaidia asikose darasani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi sasa katika masuala yangu ya Mkoa wa Geita. Mkoa wa Geita tuna changamoto nyingi na tuna vijiji vingi ambavyo havina umeme. Naiomba Wizara ya Afya ishirikiane na Wizara ya TAMISEMI kuhakikisha kwamba, zahanati na vituo vya afya vinapatiwa umeme wa *solar* ama umeme kabisa kutoka gridi ya Taifa. Kwa sababu, mtu anaweza akajifungua usiku! Sasa mtu anazaaje gizani kwa kweli? Ni kitu kidogo ambacho kinakuwa kigumu! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi tuna tatizo hilo hilo la CHF ambapo wananchi hawapati dawa. Vile vile CHF mtu akitoka Geita akienda Chato hapatiwi huduma; akitoka Geita akaenda sehemu nyingine, hapatiwi huduma. Hili nalo muweze kuliangalia ili tuweze kuona ni namna gani tunaweza tukawasaidia wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kuiomba Serikali kwamba, ikumbuke Hospitali ya Mkoa wa Geita ambayo mmeifanya sasa imekuwa ni Hospitali ya Rufaa, lakini haifanani hasa na kuwa na sifa hiyo ili iweze kuwahudumia

wananchi wa Mkoa wa Geita. Pamoja na hilo, liangaliwe suala la kutafuta *fast ferry* kwa sababu, kutoka Geita kwenda Mwanza tuna maji pale katikati. Ukitegemea hizi *ferry* za kawaida, mgonjwa anaweza kufia ndani ya *ferry*. Kwa hiyo, *ferry* badala ya kwenda na mgonjwa inarudi na maiti. Kwa hiyo, tunaomba sasa tuweze kupatiwa pia *fast ferry* kwenye hilo ziwa kuhakikisha kwamba wagonjwa wanafikishwa *on time* katika hospitali zinazohusika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya, ahsante sana Mheshimiwa Upendo kwa mchango wako mzuri. Endelea hivyo hivyo, jenga hoja. (Kicheko/Makofi/Vigelegele)

Tunaendelea! Mheshimiwa Kunti Yusuph, kama nilivyosema atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii nami katika Bunge hili niweze kuchangia Wizara inayoamua Watanzania leo tuendeleo kuishi ama la. Wizara ya Afya ni Wizara nyeti sana, ndiyo inayosababisha sisi leo tuko humu ndani tukiwa na afya njema pamoja na Mwenyezi Mungu kutujalia. Wizara hii ni Wizara ambayo bado inachechemea. Wizara ambayo inakwenda kuamua hatima ya maisha ya Mtanzania, bado tunakwenda kuiletea mzaha na kufanya ushabiki kwenye maisha ya Watanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni takribani miaka 55 ya uhuru, hatuna Vituo vya Afya ndani ya Kata zetu 3,990. Tuna vituo vya afya ambavyo havifiki 500, halafu tuko humu ndani leo tunajisifu, tunapongezana kwa makofi eti kana kwamba tunakwenda kufaulu. Hatufaulu, tunarudi nyuma na tunaendelea kutokuwatendea haki Watanzania. Hali ya hospitali zetu kwenye maeneo yetu tunakotoka; tuachane na hospitali hizi za mjini, hebu twende kule vijijini. Mheshimiwa Waziri hotuba yake nikiiangalia na kuisoma imelenga maeneo ambayo yako hapa mbele yetu. Haijatugusa kule vijijini!

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijijini hospitali zetu zinasikitisha, zinatia huruma, wananchi wetu wanapata tabu. Hospitali zisizokuwa na maji! Hospitali zisizokuwa na umeme. Mbali na maji na umeme, lakini hospitali hizi hazina Wauguzi, hazina Madaktari, hazina madawa! Tunawatakia nini hawa Watanzania? Shida yetu ni nini? Si mtwambie Chama cha Mapinduzi miaka 55 mmeshindwa kuleta hoja ya msingi ya kuweza kuokoa maisha ya Watanzania! Tunabaki tunapigiana makofi humu ndani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuachane tu na suala zima la hali mbovu za hospitali, uwepo wa hizo hospitali zenyewe! Mkoa wangu wa Dodoma wenye Wilaya saba, tuna Wilaya nne tu ndiyo zina hospitali; Wilaya tatu hizi hazina

Hospitali za Wilaya. Mnaweza mkasema Wilaya ya Chemba ni mpya, Wilaya ya Bahi ni mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chamwino ambayo awali ilikuwa inaitwa Wilaya ya Dodoma Vijijini mpaka leo ambako Ikulu ipo ya Chama cha Mapinduzi, hawana hospitali wale wananchi! Wanatoka Vijiji vya Chamwino, Mtera huko imepakana na Iringa wanasafiri kuja Manispaa ya Dodoma kupata huduma. Hivi mnawatakiwa wema kweli hawa Watanzania wa Mkoa wa Dodoma? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambieni tu ndugu zangu, katika mikoa ambayo inawakoa, bado inasuasua ni Mkoa wa Dodoma ndiyo ambao angalau mnaambulia, lakini Waswahili wanasema usimwamshe aliyelala, utalala mwenyewe. Ipo siku wananchi hawa watakuja kuchoka na mateso na ahadi kila kunapokucha, mnaenda kuwaahidi kwamba tutawaleteni hospitali ambazo hamzipeleki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma zinazotolewa kwenye hospitali zetu, wenzangu wamesema, naomba niongezee. Niende huduma zinazotolewa kwenye huduma ya mama mjamzito. Huduma zinazotolewa kwenye hospitali zetu kwa mama mjamzito, zinawakatisha tamaa wanawake kwenda hospitalini ndiyo maana wengine wanaamua kuzalia majumbani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wa kike ambao hawajafikisha umri wa miaka 18 kwa Dini ya Kiislamu mtoto anaweza kuolewa hata miaka 14, 15, 16; mtoto huyu akiolewa akipata ujauzito akienda hospitalini kwa ajili ya kujifungua, hapewi huduma. Atapewa kashfa kibao, atapewa matusi ya kila aina na kumsababishia mtoto yule hata kukosa ujasiri wa kwenda kutimiza wajibu na jukumu lake katika Taifa lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lugha hizi zinatusababishia vifo vingi vinavyokwenda kuwapoteza akinamama, vinavyokwenda kuwapoteza watoto ambao tunahitaji kesho na wao waje watupokee mzigo huu tulionao katika Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wanawake ambao wana umri mkubwa kuanzia miaka 40, hawa nao imekuwa ni changamoto kwenye hospitali zetu. Wakifika Hospitalini, "limama jitu zima, limebebelea limimba mpaka leo linazaa! Hizo ni lugha ambazo zinatolewa na wafanyakazi wetu kwenye hospitali zetu. Mheshimiwa Waziri wewe ni mwanamke, unajua uchungu wa kuzaa...

MWENYEKITI: Siyo wote ni baadhi! Ni baadhi, siyo wote!

MHE. KUNTI Y. MAJALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni baadhi!

Mheshimiwa Waziri unajua jinsi wanawake tunavyopata tabu, lakini kuna mwanamke mwingine yawezekana kwenye usichana wake amehangaika kupata mtoto ameshindwa. Imefika umri wa miaka 40 huyu mtu kabahatika kupata hiyo mimba, asizae? Kwa nini baadhi ya hawa watumishi wasipewe onyo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona wiki iliyopita Mbeya, Muuguzi alichomtendea yule mama aliyekuwa anajifungua pale, Mkuu wa Mkoa alikwenda pale hospitalini. Yule mama anaeleza kwa uchungu namna alivyofanyiwa na mhudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tunataka kuwatendea haki hawa wanawake? Tunataka kweli wanawake hawa waendeleo kuja kwenye hospitali zetu kwa ajili ya kupokea kejeli, matusi na kashfa! Ya kazi gani? Vifo vya wanawake vinasababishwa na hizi kashfa; wanawake wengi wanashindwa kwenda hospitali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake pia tunashindwa kwenda Hospitali kujifungua mahali salama; siyo salama, pale napo tunakwenda kutafuta vifo vingine. Ukienda hospitalini, kaka yangu Mheshimiwa Kuchauka amesema, unaambiwa mwezi wako wa mwisho, mwezi wa Nane unaenda wa Tisa kwenda kujifungua, utaambiwa unapokuja njoo na ndoo; maeneo ambayo hayana maji, anaambiwa aende na maji mama mjamzito. Maeneo ambayo hayana umeme, mama anaambiwa aende na taa au mafuta ya taa ili aweze kupata huduma ya kuweza kutimiza wajibu wake na majukumu katika Taifa letu ya kuongeza Watanzania katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, CHF, janga la Taifa hili. Tunawatwisha Watanzania mzigo juu ya mzigo. Mmeshindwa kupeleka dawa; ili mjifiche kwenye kichaka, mmeamua kuwaundia mradi unaoitwa CHF mwendelee tena kukusanya fedha zao, wakienda hospitalini hakuna dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CHF hii watu wetu wamekwenda kujiunga; akienda hospitali na kadi ile akifika fursa pekee anayoipata kwenye ile kadi ama huduma pekee ni kwa ajili tu ya kumwona Daktari. Akitoka kwa Daktari, amepata dawa ni *paracetamol*. Awe anaumwa tumbo atapewa *paracetamol*, awe amevunjika mguu atapewa *paracetamol*, awe anaendesha atapewa *paracetamol*. Ugonjwa wowote huduma pekee atakayoipata ataambiwa *paracetamol* ndiyo dawa atakayoipata pale, akipata bahati sana ya kupata dawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huyu mwananchi anauliza, hivi nimeambiwa na Serikali yangu nijunge kwenye Mfuko huu ili niweze kuokoa maisha yangu. Hata pale ninapokuwa sina fedha nipate huduma, lakini leo hii wananchi wetu wametoa fedha zao na badala yake wanaenda kuambulia maneno ama kuoneshwa maduka ya kwenda kununua dawa. Mradi huu siyo rafiki kwa Watanzania. Mheshimiwa Waziri tunaomba aje na mbadala wa biashara hii ya CHF. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata miradi mingine ya Bima ya Afya, NHIF; ukienda na kadi ile, ukifika pale, kwanza kabla hata hujaitoa, unauliza jamani dirisha la Bima ya Afya liko wapi? Bima ya Afya? Eeh! Mhudumu anaweza akakukata kushoto akaendelea na safari zake. Kama uko kwenye foleni hujauliza chochote, unaulizwa; unatibiwa cash au una Bima? Ukimwambia una Bima, anakwambia subiri, kaa pale! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe Wabunge imetutokea, mimi nikiwa ni mhanga. Nimeenda Dar es Salaam Agakhan pale. Nimefika nikawaambia naumwa, nina Kadi ya Bima ya Afya – NHIF. Nikaambiwa, dada tunaomba usubiri pale. Nilisubiri zaidi ya dakika 45, nikaona haina sababu ni heri ninyanyuke nijiondokee zangu nikatafute hospitali nyingine nitoe fedha niweze kutibiwa. Sasa sisi kama tuko humu ndani yanakuwa namna hiyo na hizo kadi zenu mlizotupa, walioko kule nje hawa ambao mnawakatia hivi vikadi vyenu inakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaendelea! Mheshimiwa George Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Marwa na Mheshimiwa Godfrey Mjimwa ajiandae!

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Afya. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Wilaya yangu ya Mpwapwa. Wilaya ya Mpwapwa ina Hospitali ya Wilaya, lakini kuna upungufu mkubwa sana wa Madaktari na wafanyakazi wa kada nyingine. Mpwapwa kuna upungufu wa wafanyakazi 285 wa kada mbalimbali, ina Vituo vya Afya viwili, Rudi pamoja na

Kibakwe. Kwa utaratibu wa Wizara ya Afya Kituo cha Afya lazima kuwe na *Assistant Medical Officer* kwa ajili ya kufanya *minor surgeries*, kama kuna *complicated cases* pale, lakini pale kuna *Clinical Officer* na Kibakwe kuna *Clinical Officer*. Kwa hiyo, naomba watupelekee *Assistant Medical Officers* katika Vituo hivi vya Afya Kibakwe pamoja na Rudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Mwapwa ina Zahanati 50. Nusu ya Zahanati hizo zinahudumiwa na *Medical Attendant*. Nawapongeza *Medical Attendants*, wanafanya kazi vizuri, lakini ni kazi kubwa sana, kwa sababu mpango wa Wizara ya Afya ulikuwa ni ku-*train Clinical Assistants* wengi ili kuwasambaza kwenye zahanati, lakini huu mpango umeishia wapi? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba anieleze mpango huo umeishia wapi ili zahanati nyingi ziwe na *Clinical Assistant* au *Clinical Officers*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa madawa. Nimewahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya MSD, tatizo siyo MSD, tatizo MSD haina fedha. Kwa hiyo, upungufu wa fedha, uhaba wa fedha MSD ndiyo maana wanakosa madawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali itenge fedha za kutosha. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, tumeona kwamba hapa mmetenga shilingi bilioni 65, lakini umetoa taarifa kwamba kuna shilingi bilioni 251 kwa ajili ya kulipa deni la MSD na vile vile kununua madawa. Naomba fedha zote zipelekwa MSD, zisipelekwe shilingi bilioni moja mwezi huu, mwezi ujao shilingi bilioni mbili, hapana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MSD, Bodi yetu imewahi kutembelea *Sudan Medical Store* pamoja na *Uganda Medical Store*. *Medical stores* zao zinakuwa *full funded* na Serikali na wana *Vote* kabisa. Pesa inatoka Hazina, wanapelekwa *Medical Store*, lakini hapa imekua ni tatizo. Tumezungukia hospitali nyingi, hakuna madawa na tatizo la madawa wanasema labda MSD ndiyo hawasambazi madawa, lakini tatizo ni fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri, Wabunge wengi wamechangia suala hili, nadhani sasa MSD itapata fedha za kutosha ili wanunue madawa na kusambaza hospitali zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nizungumzie ugonjwa wa kipindupindu. Limekuwa ni tatizo katika nchi yetu. Kipindupindu ni ugonjwa mbaya, unaua watu wengi, lakini ni ugonjwa wa kujitakia, wala siyo ugonjwa wa bahati mbaya. Kwa sababu nakumbuka zamani kulikuwa hakuna ugonjwa wa kipindupindu. Nimewahi kuwa Bwana Afya; ilikuwa ikitokea kesi moja ya ugonjwa wa kipindupindu au mgojwa mmoja, lazima iwe *reported World Health*

Organization kwamba Tanzania kuna ugonjwa wa kipindupindu. Sasa imekuwa *cholera is endemic in Tanzania, why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, zamani kulikuwa na Mabwana Afya. Kazi ya Bwana Afya ni kukagua usafi, unakwenda vijijini unakagua usafi; kila kaya iwe na choo, iwe na shimo la taka, iwe na kibanda cha kuweka vyombo ambavyo vimesafishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi Wizara ya Afya ni mfumo. Bwana Afya hafanyi kazi alizosomea, Bwana Afya anakuwa mratibu wa UKIMWI, Mratibu wa Malaria, Mratibu wa Chanjo. Mabwana Afya wafanye kazi walizosomea. Naomba sana Mheshimiwa Waziri; na zamani kulikuwa na utaratibu wa kupeleka kila Zahanati *Health Assistant*, mkafuta utaratibu huo, mkasema hapana, kuna upungufu mkubwa sana, labda uhaba wa fedha. Najiuliza, mbona Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wameweza? Kila Kijiji kina Bwana Shamba, kila Kijiji kina Bwana Mifugo. Kwa nini Wizara ya Afya ninyi mnashindwa kupeleka Mabwana Afya Wasaidizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa kazi yao kubwa ni kukagua usafi kila Kijiji. Kila kijiji unakwenda unakagua usafi, haya magonjwa ya milipuko tungeyapunguza. Kinga ni bora kuliko tiba. Pale Muhimbili tulikuwa na Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma (*Health Education Unit*), kazi yake ilikuwa ni ku-*train* Mabwana Afya wengi Wasaidizi na wanasambazwa wilaya zote kwa ajili ya kukagua usafi katika vijiji. Siku hizi sijui kama kitengo kipo; kama kipo labda Mheshimiwa Waziri anielimishe, kimeimarishwaje kitengo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya afya kwa umma inasaidia sana. Lazima kwanza pale hospitalini wagonjwa wapewe elimu ya afya kabla ya kutibiwa. *Outpatient health education*. Tulikuwa na *outpatient health education*, *individual health education* na *public health education*. Kwa mfano Daktari anapomtibu mtu anayeharisha, Daktari anamwuliza kabisa kwa nini unaharisha? Anasema mimi naharisha kwa sababu labda sijui sikuchemsha maji au sina choo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *public health education*, lazima Mabwana Afya wasambae vijijini kutoa elimu ya afya, la sivyo kipindupindu kitatimaliza ndugu zangu. Naomba sana Wizara ya Afya itekeleze haya. Bwana Afya afanye kazi iliyokusudiwa na tu-*train* hawa *Medical Attendant* hao, au *Clinical Assistants* wengi kama ninavyosema. Upungufu wanao kama nilivyosema, MSD ni uhaba, kwa hiyo, ni vizuri MSD ikatengewa fedha za kutosha ili iweze kununua madawa mengi na kusambaza katika hospitali. Wananchi wengi wanapoteza maisha kwa sababu ya ukosefu wa madawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naunga mkono kwa asilimia mia moja kwa mia moja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje kwa kututunzia muda. Tunaendelea, Mheshimiwa Agnes Marwa atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah ajiandae.

MHE. AGNES M. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote namshukuru Mungu kwa kunijalia kuchangia siku ya leo katika Wizara ya Afya. Namshukuru kwa nafasi ya kipekee Mheshimiwa Rais Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya yeye na Serikali nzima, kwa kuonesha kwamba anaweza na kwa kuonesha kwamba sasa Tanzania mpya yenye matumaini inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani kwangu Mara kuna matatizo makubwa sana ya vituo vya afya, ukizingatia kwamba Mkoa wa Mara umepakana na mipaka mingi ambayo wenzetu wa nchi za jirani pia wanategemea huduma za afya kutokana na Mkoa wetu wa Mara. Kwa mfano, Wilaya ya Tarime kwa sasa imegawanyika katika sehemu mbili; tuna Halmashauri ya Mji na Halmashauri ya Wilaya. Hospitali tuliyonayo ni moja tu, ambayo haikidhi mahitaji kutokana na wingi wa watu waliopo Wilayani hapo Tarime. Kutokana na hali halisi ya matatizo hayo ya hospitali, Mgodi wa Acacia uliopo Wilayani Tarime, ambao uko chini ya North Mara wameamua kutujengea Kituo cha Afya katika Kijiji cha Nyamwaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mkuu wa Wilaya ya Tarime, kaka yangu Mheshimiwa Luoga, alikaa nao chini wakafanya maongezi, pamoja na Halmashauri ya Tarime. Wakaongea wakakubaliana kwamba badala ya kutengeneza au kujenga Kituo cha Afya, wakakubaliana kwa majengo yale yale na kwa gharama zile zile, tuiombe Serikali ikubali majengo yale baadaye yawe Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa dada yangu Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Kigwangalla bahati nzuri mpo hapa, nawaomba watukubalie Wilaya ya Tarime, yale majengo yatakayojengwa na Kampuni ya Acacia yawe ni Hospitali ya Wilaya kwa sababu wamejitolea wao wenyewe. Kwa hiyo, pia yanakuwa yametusaidia sisi kupunguza gharama ambazo tungezipata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee zaidi, kama mnakumbuka, naamini hata Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliopita wameiongelea sana Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ya Kwangwa. Hospitali ya Kwangwa ilikuwepo hata kabla hatujazaliwa, tunasikia historia yake. Kama mnavyojua, Mkoa wa Mara kuna matatizo mengi sana, ukizingatia kule

kwetu kulikuwa na mfumo dume ambao hadi sasa haujakwisha, kwa hiyo, kuna matukio mengi sana ambayo yanategemeana na Hospitali ya Rufaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma Hospitali ya Kwangwa, wanawake, watoto na wananchi wote wa Mkoa wa Mara kwa ujumla wanapata shida sana. Tangu mwaka 2012, mkoa ulikuwa unaomba shilingi bilioni mbili na *point*, lakini hizo fedha zilikuwa hazifiki kama zilivyokuwa zinaombwa. Toka kipindi cha mwaka 2012, mwisho imekuwa 2013; na mwaka 2014, Serikali imejitahidi kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Mara, wamejenga hospitali, imefikia ilipofikia, lakini mpaka sasa imekuwa kitendawili; na fedha ambayo imeshatoka ilikuwa ni sh. 3,334,967,000/= na fedha nyingine za kipindi hicho bado hazijatoka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu zaidi, wananchi wa Mkoa wa Mara, kwa kuiona Serikali ya Chama cha Mapinduzi ina umuhimu, pamoja na kuwa baadhi ya Majimbo wamewachagua Wabunge wa Upinzani, lakini Rais wetu aliongoza kwa kura za kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Rais aiangalie sasa hospitali ya Mkoa wa Mara ili sasa ifikie mwisho kwa sababu ni hospitali ambayo inaweza kutoa msaada mkubwa sana, lakini pia ikapunguza matatizo ya wananchi wa Mkoa wa Mara kutoka Mkoa wa Mara kwenda Mkoa wa Mwanza, wakati Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza pia inazidiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua, wananchi wa Mkoa wa Mara wengi wao akinamama ndiyo wanaotunza familia zao na akinamama hao hawana vipato vya kutosha; wanakosa hata nauli ya kuwatoa kutoka Mkoa wa Mara kwenda Mwanza. Kwa nini hili suala Serikali isiliangalie kwa nafasi ya kipekee zaidi ili hospitali hiyo itengewe sasa kiwango cha kutosha ili kuisaidia japo ianze kufanya kazi, hata kama majengo mengine yatakuwa bado, basi yatamaliziwa baadaye, lakini ianze kazi, iitwe Hospitali ya Rufaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana dada yangu, Mheshimiwa Ummy, baada ya Bunge, kama inawezekana twende wote Wilayani Tarime, aende akaangalie yale majengo ambayo *Acacia* imeshakubali kujenga ili muipe hadhi ya kuwa Hospitali ya Wilaya ya Tarime. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kwa nafasi ya kipekee sana, kuna wanawake wenzetu ambao ni *ma-nurse* mishahara yao ni midogo sana, haitoshi. Mwaangalie na mwaongezee mishahara. Pia Wizara ya Afya kwa ujumla muiangalie bajeti yake iongezwe kwani bajeti iliyopo ni ndogo sana, haitoshi kukidhi mahitaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi nyingine tena ya ziada, nasema MSD ni jipu kwa sababu, ni kweli kuna baadhi ya maeneo wanakosa pesa ya kuwalipa, lakini kwa mfano Wilayani Serengeti wametenga bajeti ya kuwalipa lakini wao madawa ndiyo hawana. Kwa hiyo, naomba kama inawezekana, urudishwe utaratibu wa zamani, twende tukanunue madawa au hospitali ziruhusiwe kununua madawa kwenye maduka makubwa ya wengine, ambapo madawa yanapatikana, kuliko wananchi wetu wanakufa wakati madawa hakuna MSD. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusiana na Bima ya Afya, wananchi wangu wa Mkoa wa Mara wanapata shida sana na wamekuwa mstari wa mbele kujiunga na Bima ya Afya. Katika mazingira ya kawaida, unapojikandikisha, kwa mfano umejiandikishia hapa hapa Bungeni, ukienda kituo kingine huwezi kutibiwa. Kwa hiyo, wananchi wangu wa Mkoa wa Mara wanapata shida. Mwanamke akijiandikishia Nyamongo mgodini au akijiandikishia Mtaa wa Mkendo, hawezi kwenda kutibiwa Mtaa wa Ilingo, kwa sababu Bima yake inaishia kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah na Mheshimiwa Halima Bulembo ajiandae.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo hotuba nzuri sana ambayo imewasilishwa na Waziri wa Afya, dada yangu Mheshimiwa Ummy. Vile vile nakushukuru sana kwa sababu nafasi hii niliyopewa ni nyeti lakini vile vile ni nafasi ambayo inaenda kuonesha kwamba Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi imejipanga vipi kwa ajili ya masuala mazima ya afya katika kipindi kinachofuata cha mwaka mmoja. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuweza kumshukuru sana Waziri wa Afya na msaidizi wake, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla. Nawashukuru sana kwa kazi nzuri mnazozifanya na sisi tuko nyuma yenu tukifanya kazi kwa ajili ya Taifa letu la Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza tu, napenda kugusia masuala muhimu ambayo wenzangu wengi wameshayaongelea, masuala ya Mfuko wa Jamii. Tukitaka kuangalia kiundani suala la Mfuko huu wa Jamii (CHF), bado una changamoto, tena kubwa sana, lakini naamini kabisa kwamba bajeti hii itakwenda kutibu maeneo mengi ambayo Mfuko huu una matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CHF kwa ujumla wake ukiangalia katika ile Act ya mwaka 2001 ya *Community Health Fund* utaona kwamba tatizo kubwa la

CHF ni mpangilio na namna gani huduma hii muhimu inatolewa kwa wananchi. Katika kuangalia hilo, utagundua kwamba katika Act ya mwaka 2001, suala la walemavu bado halijawekewa mkazo katika CHF. Namaanisha kwamba katika utaratibu huu wa CHF kuhakikisha kwamba wananchi wanachangia pesa kwa ajili ya kupata huduma za afya, watu wenye ulemavu hawajapa nafasi katika kupatiwa *exemption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu haujaleza ni namna gani ambavyo watu wenye ulemavu wanaweza wakapata huduma hii bure moja kwa moja kulinganisha na watu wenye uwezo au wale ambao wana uwezo wa kufanya kazi moja kwa moja ambao sio *disabled*. Kwa hiyo, Mfuko huu bado una changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiondoa hilo suala la walemavu, CHF bado utaona kwamba ina uhaba wa madawa. Watu wanachangia katika jamii, lakini madawa bado hayapatikani. Hii bado ni changamoto. Vile vile ukiangalia CHF pamoja na NHIF, *statistic* inaonesha kwamba mwaka 2012 ni asilimia 27 tu ya Watanzania wote ambao walikuwa wamejiunga na CHF pamoja na NHIF. Kwa hiyo, bado kuna idadi kubwa ya watu ambao aidha hawana elimu ya kutosha au imeonekana kwamba Mifuko hii bado haijawanufaisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Kalenga tatizo hili bado ni kubwa, nami nimejitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu kuongea na wananchi, lakini bado wananchi wanasuasua na bado hawana uhakika juu ya suala hili. Kwa hiyo, napenda sana kuona Serikali inakuja na mkakati maalum wa kuweza kuleta mabadiliko ili wananchi waweze kuwa na imani na Mfuko huu na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kuchangia, ni tatizo kubwa katika Hospitali ya Ipamba pale Jimboni Kalenga. Jimbo la Kalenga lina watu zaidi ya 200,000 lakini vile vile hospitali ya Ipamba inahudumia Wilaya nzima, nikimaanisha Jimbo la Kalenga na Jimbo la Isimani ambalo ni la Mheshimiwa Lukuvi, lakini bado hatuna gari la wagonjwa. Hili ni tatizo kubwa. Napenda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha, aweze kutoa majibu mahsusi ambayo yatakwenda kuwagusa wananchi wa Jimbo la Kalenga na Iringa Vijijini kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iringa Vijijini kama Wilaya yenye watu zaidi ya 300,000, hakuna gari la wagonjwa katika hospitali kubwa kama Ipamba. Hospitali hii inahudumia wananchi mpaka wa Manispaa ya Iringa Mjini, lakini vile vile inahudumia wananchi wanaosogea mpaka maeneo ya Mafinga kwa ndugu yangu Chumi. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kuangalia kwamba, akinamama ambao wanatoka maeneo ya milimani, maeneo ya mbali wanapata shida kubwa sana kuhakikisha kwamba wanafika katika hospitali

kubwa kama Ipamba kupata huduma kwa sababu tu ya kutokuwa na gari la wagonjwa. Kwa hiyo, napenda sana Serikali iweze kuja na majibu muhimu kuweza kuhakikisha kwamba hospitali hii inapatiwa gari la wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja kubwa ambalo nchi yetu ya Tanzania inalipata sasa hivi. Tuna tatizo moja katika masuala ya afya ya akili ya binadamu. Nchi yetu ya Tanzania kwa takwimu za haraka haraka inaonesha kwamba kuna watu zaidi ya 450,000 ambao wana matatizo ya afya ya akili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tatizo hili ni kubwa na *statistic* inaonesha kwamba miaka inavyozidi kuendelea kutakuwa kuna changamoto kubwa na watu wataendelea kupata matatizo haya kwa sababu mbalimbali hususan matumizi ya sigara, vile vile bangi, bila kusahau matatizo makubwa ya vileo. Kwa hiyo, napenda sana Serikali iweke umakini zaidi katika eneo hili kwa sababu idadi kubwa ya vijana au idadi kubwa ya watu wanaangamia kwa sababu ya kukosa elimu ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajaribu kugusia maeneo kadhaa. Hospitali yetu ya Milembe ambayo ndiyo hospitali kubwa ya Taifa ina changamoto kubwa. Leo hii hospitali ile inahudumia wagonjwa 250 mpaka 300 kwa siku, watu wenye matatizo ya afya ya akili. Tatizo hili bado ni kubwa katika nchi yetu ya Tanzania, ukienda pale utaona kwamba miundombinu haijakaa vizuri, utaona kwamba hakuna wahudumu wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile utaona kwamba, uwezo wenyewe wa hospitali katika kujiendesha nikiwa naamanisha masuala mazima ya kuletewa bajeti kwa muda hayafikiwi kwa muda. Kwa hiyo, unakuta hospitali inapata changamoto kubwa na inakosa namna ya kujiendesha yenyewe na hivyo basi, kuendelea kusuasua kuhakikisha kwamba ndugu zetu hawa wenye matatizo ya akili wanaweza kupata tiba kwa wakati. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kuona Serikali inakuja na majibu. Sehemu mojawapo ya kuweza kupata majibu haya ni kuhakikisha kwamba *referrals* zinatengenezwa, tunajenga vituo mbalimbali katika mikoa ili ndugu zetu hawa wasiweze moja kwa moja kutoka mikoani kuja Dodoma; kwa sababu kuna ndugu wanatoka Zanzibar, wanatoka Mwanza na Arusha wanakuja Dodoma kwa ajili ya huduma hii. Kwa hiyo, napenda *referrals* ziweze kutengenezwa, ziimarishwe katika mikoa yetu ili ndugu zetu wasiwe wanasafiri umbali mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukiangalia utaona kuna wale ambao wanakaa majumbani. Wanapokaa majumbani wanahudumiwa na familia zingine zenye uwezo mdogo sana kifedha. Akinamama wanahangaika kuwahudumia watoto wao wenye matatizo ya akili, wanashindwa kupata

nafasi ya kuweza kusafiri umbali mrefu kuwaleta Dodoma. Kwa hiyo, napenda sana hospitali hizi ziweze kuimarishwa kuhakikisha kwamba huduma hizi zinapatikana katika maeneo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kuangalia masuala ya UKIMWI. Nyanda za Juu Kusini tunaongoza katika tatizo hili kubwa la HIV. Naomba Serikali iweze kuja na mikakati maalum, kuweza kuangalia Mkoa kama Njombe wenye zaidi ya 14%; Mkoa wa Iringa wenye zaidi ya 9% ya maambukizi, Mkoa wa Ruvuma, yote ni Nyanda za Juu Kusini, napenda mikakati maalum iweze kuwekwa ili tuweze kupata majibu, namna gani tunaweza kuzuia tatizo hili la maambukizi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kuendelea zaidi, lakini napenda tu kuwasihia ndugu zangu wa upande wa pili kwamba tunavyochangia bajeti ya Serikali tuangalie kwa makini sana, kwa sababu Serikali inafanya kazi pande zote mbili. Ikiangalia masuala ya afya hakuna ambaye atasimama hapa na kusema kwamba hajatengenezewa mikakati maalum na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kumalizia kwa kusema kwamba, kama nitapata ruhusa yako nisome Mathayo 7:9 – 10 unasema hivi:

MBUNGE FULANI: Soma!

MHE. GODFREY W. MGIMWA: “Au kuna mtu yupi kwenu ambaye mwanaye akimwomba mkate atampa jiwe; au samaki akampa mkate?” (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nalisema kwa sababu kuna watu wako upande wa pili wanadhani Serikali haifanyi chochote. Serikali inawahudumia na nawaomba, kama wameshindwa kukaa upande wa pili, waje upande wetu, tutawaleta raha na hatutawaleta matatizo. Nawashukuru sana kwa kunisikiliza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Bulembo.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwa sababu nachangia kwa mara ya kwanza, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa

kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake lakini kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwapa moyo Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo pia kumpongeza Makamu wetu wa Rais Mheshimiwa Samia Hassan Suluhu, kwa kuwa Makamu wa Rais, mwanamke wa kwanza Tanzania kuwa nyadhifa kubwa katika nchi yetu na imeweza kutupa heshima kubwa wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu na Baraza lake Tukufu la Mawaziri kwa kuchaguliwa kwao lakini kwa kuthibitishwa kwake Waziri Mkuu katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nami naendelea kumwomba kwa Mwenyezi Mungu ili aendeleo kumwongoza aweze kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya kipekee kabisa niwashukuru wapiga kura wanawake wa Mkoa wa Lindi, UWT wa Chama cha Mapinduzi kwa kuniwezesha leo nikawa ndani ya Bunge lako Tukufu, nami nawaahidi kuwatumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nachukua nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba yake nzuri aliyotoa ambayo imeelekeza mipango ya utekelezaji wake kwa kipindi hiki kitakachoanzia 2016/2017, hotuba ambayo inatupa matumaini makubwa katika kuhakikisha afya za Watanzania zinaboreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kuboresha huduma ya afya nchini kwetu. Tunajua na tumeona mafanikio makubwa yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Nne, mafanikio hayo ndiyo ambayo yatazaa matunda mema katika kipindi hiki kinachokuja cha 2016/2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo makubwa tuliyoyaona, lakini bado tuna changamoto kubwa nyingi katika maeneo mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge wengi wameongelea changamoto mbalimbali zilizopo katika Majimbo yao lakini zilizopo ndani ya mikoa yetu. Napenda kuongelea changamoto kubwa ambazo zimo katika Mkoa wetu wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo hospitali ya Mkoa wa Lindi Manispaa inayoitwa Sokoine Hospital. Hospitali hii ina changamoto kubwa sana, changamoto kubwa tunajua kwamba Hospitali ya Mkoa wateja wake

wakubwa ni wagonjwa kutoka katika maeneo mbalimbali ya Wilaya mbalimbali zilizopo katika Mkoa wa Lindi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Sokoine, ina wagonjwa wengi sana, lakini Madaktari waliokuwepo ni wachache, kwa hiyo, inasababisha wagonjwa kushindwa kupata huduma kwa wakati kwa sababu tu ya mlundikano wa wagonjwa wengi kwa kukosa Madaktari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunalo tatizo kubwa la Madaktari Bingwa wa Wanawake. Wanawake tunapata matatizo makubwa sana na wengi wanapoteza maisha kwa sababu tu ya kukosa huduma iliyokuwa stahiki. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri alitazame kwa jicho la huruma suala ili Mkoa wa Lindi tuweze kupata Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokuwa na Daktari Bingwa katika Hospitali ya Mkoa itanusuru wanawake wengi kutoka wilaya mbalimbali. Kwa hiyo, tunaomba sana tuweze kupata Daktari Bingwa katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna changamoto nyingine kubwa ya kutokuwa na miundombinu iliyo kuwa mizuri ya majitaka na majisafi. Hospitali ile ya Mkoa wa Lindi tunajua ni hospitali kongwe, ni hospitali ya muda mrefu, miundombinu yake ya maji imekuwa michakavu sana na kusababisha katika wodi ya wazazi kukosa maji na Mheshimiwa Waziri ni mwanamke, anajua maji yalivyokuwa muhimu katika wodi ile ya wazazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kwa dhati kabisa suala hili la kufanya ukarabati wa miundombinu katika hospitali yetu ya mkoa, Serikali itusaidie kuhakikisha miundombinu ile inabadilishwa na kuwekwa miundombinu mingine. Katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi naisemea sana ile kwa sababu ndiyo inabeba wagonjwa wengi kutoka katika maeneo mbalimbali ya Wilaya za Mkoa wa Lindi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo mashine ya endoscopy, mashine ile inakosa mtaalam na kusababisha mashine ile kukaa muda mrefu bila kutumika lakini wagonjwa wanakosa tiba kwa kukosa mtaalam ambaye anaweza kutumia mashine ile. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri atutazame kwa jicho la huruma ili tuweze kupata mtaalam atakayeweza kuiendesha mashine ile ili wagonjwa wa magonjwa haya ya vidonda vya tumbo waweze kupata tiba kwa wakati muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya mbalimbali tumeona Wilaya nyingine zimekosa kuwa na Hospitali za Wilaya, ni pamoja na Lindi Manispaa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya hitimisho lake atueleze ni namna gani ataweza kuzisaidia Wilaya hizi ambazo hazina Hospitali za Wilaya ili Wilaya hizi ziweze kupata hospitali na wanawake na watoto waweze kupata huduma hizi za afya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo imeongelewa na Waheshimiwa Wabunge wengi ni ukosefu wa madawa katika hospitali zetu. Katika hospitali zetu za Mkoa wa Lindi zote zinakosa madawa. Tuna Wilaya sita katika Mkoa wa Lindi, ikiwepo Wilaya ya Liwale, Nachingwea, Lindi Vijijini, Kilwa, Lindi Manispaa pamoja na Ruangwa, tunakosa madawa ya kutosha na kufanya wagonjwa wakose madawa na hatimaye wengine kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba wananchi wetu wengi hawana uwezo wa kununua madawa katika maduka ya dawa. Wanapokosa dawa katika hospitali zetu za Serikali zinawafanya washindwe kupata tiba kwa wakati na kusababisha vifo vingi vya wanawake na watoto. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hili la upatikanaji wa madawa katika hospitali zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mfuko huu wa Bima ya Afya. Nchi yetu sasa hivi tumeingia katika Mfuko huu wa Bima ya Afya na wananchi wetu tunawahamisha kuingia katika Mfuko huu wa Bima ya Afya. Suala hili Waheshimiwa Wabunge wengi wameliongelea, tunapata tatizo kubwa kwa sababu wanapokwenda hospitali wanapata maandishi tu na badala yake dawa wanakosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawakatisha tamaa; na hata wale ambao wangependa kuingia katika mfumo huu wanapata hofu na kuacha kuingia katika mfumo huu wa Bima ya Afya. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye jitihada zaidi ya makusudi katika kuhakikisha hospitali zetu nchini kote zinakuwa na madawa ya kutosha na tutakapofanya kampeni hii ya kuingia katika Mfuko wa Bima ya Afya, wananchi wetu watakuwa na matumaini ya kupata dawa katika mahospitali yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala lingine la Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake katika Halmashauri zetu. Katika Halmashauri zetu tunatenga asilimia kumi; tano ya vijana na tano ya wanawake, lakini tumeona katika Halmashauri zetu nyingi hazina mapato ya kutosha na kupelekea pesa inayopatikana kuonekana kwamba ni kidogo haitoshelezi. Katika Majimbo mengine yana Kata zaidi ya 30. Majimbo mengine yana Kata 33, mengine yana Kata 30, na mengine Kata 35. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na mapato madogo, mathalan unapata shilingi milioni 10 ya vijana na shilingi milioni 10 ya wanawake...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wako ndiyo huo, tunakushukuru.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Kigwangalla kwa hotuba yao nzuri na kwa kazi nzuri ambazo wanakuwa wakiwafanyia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujielekeza moja kwa moja katika mchango wangu. Kwanza kabisa naomba kuzungumzia Bima ya Afya, nazungumzia Bima ya Afya kwa vijana wajasiriamali. Vijana ambao wanafanya kazi kwenye maafisi huwa wanawekewa ulazima wa kukatwa asilimia fulani katika mishahara yao ambayo inawapelekea kupata Bima ya Afya; lakini kwa vijana wajasiriamali hakuna kitu kama hiki, ni baadhi ambao wanakuwa na uelewa au wanakuwa na mwamko wa kujua nini faida ya Bima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nguvu kazi ya Tanzania ni vijana na wanaofanya kazi ni takriban milioni 23 ya Watanzania. Wajasiriamali ninaowazungumzia hapa ni wale madereva wa bodaboda, mama lishe, fundi ujenzi, mafundi vyerehani, ndiyo ninaowazungumzia hapa. Wengi hawajajiunga na Mifuko au Bima za Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumzia ni kwamba, naiomba Wizara iionbe Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ishuke chini kwa hawa vijana wajasiriamali, itoe elimu kubwa kuhusiana na Bima ya Afya, iwaambie faida ya Bima ya Afya ni nini? Leo dereva wa boda boda ukimwambia achange sh. 50,000/= kila mwezi anaona pesa yake inapotea, haelewi umuhimu ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Mifuko yetu ya hifadhi ikishuka chini kwa hawa vijana wajasiriamali ikawaelezea umuhimu, ikawaambia kwamba unapojiunga na Mfuko wa Hifadhi, *automatically* unapata Bima ya Afya, *NHIF*.

Hii itakuwa ni rahisi zaidi kwa wao kuelewa tofauti na kumwambia yeye achange kila mwezi sh. 50,000/= au sh. 100,000/= na kadhalika, inakuwa ni ngumu. (Makofi)

Ndugu zangu, tuelewe tu, tuwawezeshe wajasiriamali waelewe kwa sababu kijana wa leo mjasiriamali anapoumwa anapokwenda hospitali ndipo mtaji wake unapomalizika. Dereva boda boda anapata ajali, anavunjika mguu, anaambiwa kutibiwa kwake ni shilingi milioni tatu, nne mpaka tano, huo ndiyo mtaji wake aliutafuta kwa miezi kadhaa. Anapokuwa na Bima ya Afya inamsaidia yeye kupata matibabu bila kuumiza ule mtaji ambao alikuwa ameuweka kwa muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalotaka kuzungumzia ni mimba za utotoni. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kataja baadhi ya mikoa kama sita, kataja Mkoa wa Mara, Shinyanga, Geita, Singida na Dodoma kwamba ndiyo imeathirika kwa kiasi kikubwa na mimba ya utotoni. Naomba kumwambia dada yangu na kaka yangu, mimba za utotoni zimeathiri karibu Tanzania nzima. Suala hili lipo katika kila mkoa, linawagusa watu wengi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna adhabu zimekuwa zikitolewa kwamba ukimpa mimba mtoto wa kuanzia mwaka mmoja mpaka miaka nane, unafungwa maisha.

(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walinong'ona)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tisa mpaka kuendelea chini ya miaka 18, wengine wanaichukulia kama ubakaji wanasema au mapenzi. Unamkuta baba mwenye umri wa miaka 35, 40, 43 au 50 anakuja kumshawishi binti mdogo mwenye umri wa miaka 15, anampatia ujauzito. Kwa maisha yetu ya kawaida binti mwenye miaka 15 anakuwa bado ni mwanafunzi, kwa hiyo, anamwachisha shule kwa ajili ya ule ujauzito. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba adhabu kali itumike kukabiliana na hawa akinabab. Mara nyingi unamkuta mtu mwenye miaka 45, ni mfanyakazi TRA, ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, lakini anamharibia maisha huyu binti mwenye miaka kumi na tano. Tunajuaje huyu binti leo angekuwa Waziri kama dada yangu Mheshimiwa Ummu Mwalimu? Baadaye huko, tunajuaje labda leo angekuwa Makamu wa Rais kama Mheshimiwa Samia Suluhu? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba sana Wizara ya Afya ifikirie ni adhabu gani au mkakati gani itakuja nao kuweza kuwadhibiti hawa akina baba wanaotuharibia watoto wetu wadogo ambao hawajamaliza masomo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine na suala langu la mwisho, nataka kuzungumzia madawa ya kulevya. Tanzania yetu nikizungumzia Mkoa wa Dar es Salaam; kituo kinachotoa dawa kwa ambao wameathirika na madawa ya kulevya, ni Mwananyamala pekee. Hakuna kituo kingine! Ukienda pale Mwananyamala utalia, utasikitika, utawaonea huruma. Kama Mkoa wa Dar es Salaam ndiyo mkoa mkubwa ambao unaathirika; ndiyo kuna waathirika wakubwa wa madawa ya kulevya. Kuna kituo kimoja ambacho ndiyo cha Mwananyamala, foleni ni ya kufa mtu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Wizara ione itafanyaje kuunda mfumo katika kila Kanda kuweka hivi vituo vya kutoa huduma za hawa walioathirika na madawa ya kulevya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hiyo tu, naomba Wizara ije na mfumo wa *Rehabilitation Centers* kwa hawa ambao wameathirika na madawa ya kulevya. Siyo madawa ya kulevya tu, kuna wagonjwa wa akili, wavutaji sigara ambao ni walevi kupitiliza. Mtu mwenye madawa ya kulevya leo, anaenda Mwananyamala, anapewa pesa, anarudi Mtaani. Atarudi kila siku Mwananyamala kuomba pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute hizi *rehabilitation* ambazo mtu anakuwa anahudumiwa, akitoka pale anapelekwa kule anakaa kwa kipindi fulani, akija kutoka tayari ameshaachana na kile kitu ambacho kilikuwa kikimsumbua. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naomba Wizara itoe mwamko kwa hizi *rehabilitation centers* za watu binafsi. Kuna moja ipo Bagamoyo ambako amepelekwa Chid Benz, kuna moja ambayo ipo Kigamboni; basi tuwashike mkono, tuwatie moyo, tuweze kuwaongezea ili wawasaidie vijana wetu. Kama sisi wenyewe tumeshindwa kuanzisha, wamepatikana watu kama hao, wana moyo wa kusaidia vijana, tuwashike mkono, tuwape msaada waweze kuwasaidia vijana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri suala la madawa ya kulevya analifahamu, linaumiza sana vijana, linaumiza nguvu kazi ya Taifa na wote tunatambua kwamba vijana ni nguvu kazi ya Taifa. Naomba litiliwe sana mkazo, atakapokuja kutoa hitimisho lake na useme nia yenu ama mfumo wenu ni upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nakushukuru na naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Halima. Tunaendelea na mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Ndaki Mashimba.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kufanya na kwa *presentation* nzuri waliyofanya asubuhi ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie mambo mawili au matatu kama muda utatosha. La kwanza, ni majengo ya zahanati na vituo vya afya. Ilani ya Chama cha Mapinduzi imesema tunajenga Zahanati kila Kijiji na tunajenga Vituo vya Afya kwenye kila Kata. Maana yake, haya ni majengo ili huduma za afya ziweze kutolewa kwenye majengo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa najaribu kuangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona kiuwazi sana mpango mahsusi juu ya jambo hili la Vituo vya Afya kwenye Kata na Zahanati kwenye Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma pia hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, lakini na kwenyewe sikuona kwa uwazi sana. Jambo hili linazungumzwa vizuri na mkakati mahsusi umewekwa ili kuhakikisha kweli tuna zahanati kwenye kila kijiji na tuna vituo vya afya kwenye kila kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma hizi za afya zinatolewa kwenye majengo yenye viwango maalum; siyo kila jengo tu linaweza kuwa zahanati au kituo cha afya. Sasa kama hatujazungumza kwa uwazi hapa; na kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi jambo hili tulilizungumza sana kwa wapiga kura wetu na wengine tumehamasisha, wameanzisha maboma na mengine yamekwisha, yaliyofikia kwenye lenta, yapo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najiuliza, nikirudi naenda kuwaambia nini wananchi wangu sasa ambao tayari wana maboma yamekwisha, bado kuezekwa? Yapo maboma mengi kwenye Jimbo langu la Maswa Magharibi yamekwisha bado kuezekwa tu, lakini kwenye mpango wa Mheshimiwa Waziri wa Afya na hata kwenye mpango wa Waziri wa TAMISEMI sijaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuhitimisha, atuambie angalau mpango mkakati ni upi kuhusu zahanati kwa kila Kijiji na kituo cha afya kwa kila kata, vinginevyo, watu wetu tutawakatisha tamaa. Nina maboma mengi kwenye Jimbo langu na nilichokuwa nawaambia wapiga kura wangu ni kwamba Serikali watatusaidia kuyamaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko boma kwenye Kijiji cha Bukangilija, liko boma Kijiji cha Nyabubinza, liko boma Kijiji cha Mwanubi, liko boma Kijiji cha Mwang'anda; yako maboma mengi! Sasa kama hayapo kwenye mpango huu, kwa kweli nasikia baridi kwamba nitakapokutana na watu wangu itakuwaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akijumuisha hotuba yake, basi atuambie mpango mahsusi hasa kwa ajili ya kila kijiji kuwa na zahanati yake, kila kata kuwa na kituo cha afya, ni upi hasa ili tuweze na sisi kuwa na matumaini kwa wapiga kura wetu pia? Kwa hiyo, hilo ni jambo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni suala la ubora wa huduma za afya kwenye maeneo yetu. Nashukuru kwamba wamefanya uhakiki Wizara, kwenye hotuba ya Waziri ameelezea; wamefanya uhakiki na kutathmini na walikuwa wanavipa vituo vya afya au zahanati, zile zinazotoa huduma za afya alama za nyota ya kwanza mpaka ya tano. Sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukijaribu kuangalia, vituo hivi vinavyotoa huduma ya afya karibu asilimia 87 vilipata nyota kati ya sifuri (0) na moja (1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kuonesha kwamba huduma zinazotolewa kwenye vituo vya afya na kwenye zahanati bado ni duni sana. Ukweli tunaufahamu kwa sababu tunatoka kwenye maeneo hayo. Sasa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri sikuona pia mpango mkakati ni upi kuhakikisha kwamba hizi huduma zinakuwa bora kwenye hivyo vituo ambavyo wao wamevihakiki. Sijaona mpango mkakati ni upi ili kufanya huduma hizi ziwe bora kwenye maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake, huduma zinazopatikana kwenye zahanati au vituo vya afya, maana maeneo haya ndiyo yanayotoa huduma za msingi za afya kwenye maeneo yetu, siyo nzuri. Nina Kituo changu cha Afya cha Mwasai kinahudumia Kata tatu; Kata ya Masela, Kata ya Seng'wa na Kata ya Isanga. Kituo hiki cha Afya kina Nurse mmoja na *Clinical Officer* mmoja; watu wawili ndio wanaofanya kazi pale, vifaa tiba pale havitoshelezi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata mfadhili kwenye hicho Kituo cha Afya akatuletea vifaa vya upasuaji, viko kwenye *container* mpaka leo. Tukiuliza kwa nini havifanyiwi kazi, wataalam wanatuambia hakuna Daktari pale. Hii inaonekana kwamba watumishi kwenye zahanati na kwenye vituo vya afya ni pungufu sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri watutazame kwa jicho la pekee wa maeneo hasa ya vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu nina vituo vya afya viwili; Kituo kingine kinaitwa Malampaka na chenyewe ni hivyo hivyo, kina *container*

la upasuaji lakini limekaa tu, halifanyiwi kazi, vifaa vipo vimekaa tu. Tatizo ni kwamba hakuna mtaalam. Pia pale kuna tatizo la ziada kwamba hakuna jengo la upasuaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Serikali wakiwa wazi na kutuambia tunatatuaje haya matatizo ili huduma za afya kwenye maeneo yetu ziwe angalau bora? Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema, maeneo mengi yanayoonekana ni mazuri ni kuanzia kwenye wilaya, mkoa na kuendelea juu, lakini ukishuka chini huduma za afya siyo nzuri sana. Kwa hiyo, tunaomba Serikali itoe kipaumbele kwenye maeneo haya ili watu wetu pia ambao ndio wengi wapate huduma zinazotosheleza kwa ajili ya afya zao ili waweze kufanya na kujitafutia maendeleo yao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni huduma za ugonjwa wa saratani. Saratani imekuwa tatizo kwenye nchi yetu sasa hivi. Nilikuwa najaribu kuangalia takwimu sikuzipata vizuri, lakini inavyoelekea tatizo la saratani linaongezeka, maana watu wanaotoka kwenye maeneo yetu ni wengi; wanapochunguzwa wanakutwa na saratani, lakini huduma za matibabu au huduma za kupunguza ukali wa tatizo hili zipo tu Ocean Road, Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Serikali ifikirie ni kwa namna gani inaweza ikawa na huduma za matibabu kwenye Kanda au Mikoa ili kutuletea huduma hii ya matibabu kwa ugonjwa huu karibu na wananchi wetu? Vinginevyo ni ghali mtu wa kutoka kule Kijiji changu cha mwisho Jija atafute usafiri aende Maswa Shinyanga, baadaye apande basi mpaka Dar es Salaam akatafute matibabu, ni ghali sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Serikali inapojibu itueleze mpango wake ni upi hasa ili kuwapunguzia wananchi wake adha za kupata matibabu hasa kwa ugonjwa huu ambao sasa unakuja juu kwenye maeneo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo kwa siku ya leo, lakini nimalizie kwa kuwapongeza hawa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, muda wetu ndiyo huo.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, huyo ndio mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo. Nina matangazo.

Waheshimiwa Wabunge, nimejitahidi kutenda haki kama uwiano unavyotaka, lakini nimeulizwa kwa nini Chama cha CUF umewapatia nafasi nne? Siyo kweli. Ni kweli wazungumzaji ni wanne lakini walipatiana ndani ya muda ule ule wa dakika kumi, dakika tano tano. Kwa hiyo na wengine mkipenda kufuata nyayo hizo, fanyeni ndani ya muda huo huo, dakika tano tano, tutachangia wengi sana. Hilo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitekeleze kanuni. Wakati Bunge linataka kuahirishwa uliombwa Mwongozo wa kiti kutoka upande wa Serikali. Mheshimiwa Suzan Lyimo alipokuwa anachangia, alitoa katika maelezo yake kwamba kwa hali ya afya na nini na nini, lakini tungeweza kufanya vizuri zaidi kuliko kununua magari, akayataja; alitumia neno sijui washawasha. Serikali ilikuja ikasema, yawezekana yeye anajua zaidi, lakini upande wa Serikali unavyojua siyo hiyo aliyosema na takwimu alizotoa kwa magari na bei, Serikali imesema siyo sahihi.

Kwa hiyo, kiti kiliagiza Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Susan Lyimo athibitisha hayo na kama anaona hilo ni mbali sana kuthibitisha, basi afute tu kauli mambo yaishe. Bahati mbaya alikuwa hayumo ndani ya ukumbi, lakini bahati nzuri sasa hivi yupo. Kwa mujibu wa kanuni, nitampa heshima hiyo, ana *option* hiyo ya kusema yawezekana *it was a lapsus linguae*, ulimi uliteleza kwamba nilikuwa kwenye hali fulani; lakini kama atasema ushahidi ninao, nipeni muda niuweke mezani, nitatumia kanuni tu, tumpatie fursa hiyo aweze kufanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Lyimo!

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na ndiyo sababu nami nimeomba mwongozo kwa sababu nimepata taarifa hiyo kwamba mwongozo uliombwa kwa mujibu wa kanuni namba 63(1), cha (5) na cha (6) ambapo yeye alithibitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niseme yafuatayo kwamba kifungu cha (2) Mbunge yeyote anapokuwa akisema Bungeni hatachukuliwa kama amesema uongo iwapo atafanya rejea habari kuhusu jambo fulani lililotangazwa au lilioandikwa na vyombo vya habari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa siyo tu nina maelezo kutoka kwenye vyombo vya habari, vile vile nina *Hansard* ambayo Mheshimiwa huyu huyu aliyeomba mwongozo alinjibu tarehe 5 mwezi wa Pili na naomba niseme

kwenye hilo swali ambalo niliuliza la nyongeza ambapo swali la msingi lilikuwa limeulizwa na Mheshimiwa Nkamia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lyimo, nisaide...

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Eeh, nataka nijibu kwamba...

MWENYEKITI: Usitoe maelezo...

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Enhe!

MWENYEKITI: Wewe nenda *to the point* kwamba nitathibitisha niliyosema.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Nathibitisha.

MWENYEKITI: Haya.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Sawa sawa. Naomba nithibitishe niliyoyasema...
(Makofi)

MWENYEKITI: Hapana, siyo sasa hivi.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Sawa.

MWENYEKITI: Nakuomba, muda wetu siyo rafiki, tutakupatia nafasi. Kwa hali hiyo kwa sababu unaonekana upo tayari sana, tutashauriana ili upewe nafasi ya kutosha. Kesho utayawasilisha tu hapa na Serikali itayaona, Bunge na sisi tutapima kama yamekaa vizuri. Tunakwenda vizuri, nakushukuru sana Mheshimiwa Lyimo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, lingine, kanuni hizi maana yake ni kwamba, tunataka tufanye mambo yetu kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa ambao tumejiwekea sisi wenyewe.

Kanuni ya 60 ambao mna kanuni zetu, fasili ya 16, nimesikia tangu mchana, asubuhi, "dada yangu Ummy," "kaka yangu fulani," hizo lugha tunazivumilia tu, lakini haziruhusiwi humu. Dada yupo nyumbani. Hapa kanuni inatuambia hivi, katika mjadala wowote, Mawaziri watatajwa kwa majina ya nyadhifa zao. Huyu ni Waziri wa nini? Waziri wa Afya, siyo lazima ukasema yote ile, lakini siyo Dada Ummy. (Makofi)

Maana Waingereza wana kamsemo; *familiarity breeds contempt and sometimes it be gets children*. Kwa Wabunge watatajwa kwa kutumia neno "Mheshimiwa" kabla ya majina yao, naomba tuyazingatie haya, ndiyo maana

ya lugha ya Kibunge na ndiyo maana watu wanatushangaa *sometime* tunaporushiana maneno ambayo siyo ya Kibunge. Naombeni twende hivyo mtaona staha nzuri tu katika michango hii.

Mheshimiwa Upendo mmeona mchango wake, wala hakuwa anatukana mtu, *she was making point*. Tukifanya hivyo, ni vizuri tu. Mheshimiwa Bulembo umefanya vizuri tu na wengine. Mimi niseme tutafanya tu! Jenga hoja, siyo kupiga kelele na kumwagiana matusi. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, ya mwisho, ni mawili ya kiutawala. Kesho ni Alhamisi na kwa mujibu wa Kanuni ya 38(5) iko wazi, Mheshimiwa Waziri Mkuu hayupo na fasili ya (5) inasema kama hayupo Bungeni, siku hiyo hakuna kipindi cha maswali kwa Waziri Mkuu. Kwa hiyo, kesho hali ndiyo hiyo.

Lingine, Waheshimiwa Wabunge ambao hawana vitambulisho vya uraia; wafanyakazi wa NIDA wapo Dodoma, kuanzia leo wako hapa na watakuwa hapa kwa wiki moja. Wamepewa pale ukumbi wa Msekwa nyuma kule ambapo ilikuwa Zahanati. Unatakiwa sasa wewe uende na baadhi ya nyaraka muhimu ambazo watataka uwe nazo ambazo ni copy ya pasi ya kusafiria, copy ya leseni ya gari, copy ya Bima ya afya na copy ya vyeti vya kumalizia shule kama Sekondari au Chuo Kikuu. Lakini...

MBUNGE FULANI: Vyote au kimojawapo?

MWENYEKITI: Walivyoandika, ile “na” wameweka mwishoni huku, kwa hiyo, nadhani wanasema uwe navyo. Watakueleza huko. Nawaomba sana, kwani zoezi linatusaidia sana kwa wale ambao tupo hapa na hatujakamilisha hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yangu ambayo nimeletewa hapa. Baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(Saa 2.02 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 12 Mei, 2016 Saa Tatu Asubuhi)